

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 27 Aprili, 2017

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. RAMADHANI ABDALLAH ISSA - KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MHE. RITA E. KABATI (K.n.y. MHE. DKT. NORMAN A.S. KING - MWENYEKITI KAMATI YA MIUNDOMBINU):

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2017/2018.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. QAMBALO W. QULWI (K.n.y. MHE. JAMES F. MBATIA - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliiano juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Katibu.

NDG. RAMADHANI ABDALLAH ISSA - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali tutaanza na Ofisi na Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa John P. Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Constatine Kanyasu, Mbunge wa Geita.

Na. 105

**Ukiukwaji wa Sheria unaofanywa na
Makampuni ya Migodi**

MHE. CONSTATINE J. KANYASU (K.n.y JOHN P. KADUTU)
Aliuliza:-

Kampuni binafsi ya migodi zimekuwa zikikiuka mikataba ya kazi na pia zikikandamiza na kuwanyanyasa wafanyakazi:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya ukaguzi wa mikataba kwa kampuni zinazofamya kazi migodini?

(b) Je, kwa nini Serikali isiamue kuwaondoa nchini waajiri wakorofii kwa unyanyasaji wanaoufanya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA) Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, waajiri wote nchini yakiwemo na makampuni ya madini wanapaswa kutekeleza matakwa ya Sheria za Kazi kwa lengo la kulinda haki za wafanyakazi, kupunguza migogoro isyo ya lazima sehemu za kazi na kuongeza tija na uzalishaji mahala pa kazi. Ofisi yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa sheria kwa kufanya kaguzi sehemu za kazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa waajiri wanazingatia matakwa ya sheria. Pia elimu ya sheria za kazi zinatolewa kwa waajiri, wafanyakazi na vyama vyao ili kuongeza uelewa wao katika kutekeleza sheria. Aidha, hatua zinachukuliwa kwa kuwafikisha Mahakamani waajiri wanaokiuka masharti ya sheria za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi wa mikataba wa kampuni zinazofanya kazi migodini, Serikali iliunda kikosi kazi ambacho kilishirikisha Maafisa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, NSSF, SSRA, OSHA, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Wakala wa Ukaguzi wa Madini. Kikosi hiki kilipewa jukumu la kufanya ukaguzi wa kina kwenye migodi iliyopo kanda ya Ziwa na Kaskazini kwa lengo la kuangalia hali halisi ya utekelezaji wa sheria za kazi, afya na usalama mahali pa kazi, masuala ya hifadhi ya jamii, fedha na kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Serikali inatambua umuhimu wa uwekezaji katika kukuza fursa za ajira kwa Watanzania na kuchangia kukua kwa uchumi. Serikali itaendelea kusimamia sheria za kazi ili kuhakikisha kuwa waajiri wote nchini wanatimiza wajibu wao na wawekezaji wanapata nafasi ya kuwekezana kuchangia kukua kwa uchumi wa nchi yetu kwa kufuata sheria zilizoko nchini.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Constantine Kanyasu swali la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa pamekuwepo na unyanyasaji mkubwa sana wa wafanyakazi katika migodi, ikiwepo tabia ya ku-*blacklist* wafanyakazi na mfanyakazi anapokuwa *blacklisted* hawezi kuajiriwa sehemu yoyote katika mgodi, mara nydingi wanapokuwa *blacklisted* hawapewi nafasi ya kusikilizwa. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwa kiwango gani vyama vya vya wafanyakazi vina uwezo wa kuwatetea wafanyakazi linapoteka tukio kama hili? (*Makof*)

Swali langu la pili, migodi mingi imekuwa ikiwashirikisha wananchi wanaozunguka migodi kwa ajili ya ulinzi lakini wananchi hao wamekuwa wakipwewa mikataba ya mwaka mmoja na miezi sita, hawana bima na hawana mikataba ya aina yoyote, hili linafanyika ili kukwepa sheria ya kuwalipia NSSF na faida zao zingine. Je, ni lini migodi hii itaelekezwa kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapewa mikataba na wanalipwa haki zao kama wafanyakazi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwanza la unyanyashaji na *blacklisting* ambayo imekuwa ikifanyika, kama Wizara tumeshapata malalamiko hayo kutoka kwa wafanyakazi wengi walioko katika migodi, ambao wamekuwa wakilalamika kwamba waajiri wengi katika migodi hii hasa baada ya kuwa wafanyakazi hawa wametoka katika maeneo yao, wamekuwa wakiwa-*blacklist* ili wasipate nafasi yakuweza kuajiriwa katika migodi mingine na makampuni zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumeshachukua hatua na tayari katika ukaguzi wetu huu ambao tumeufanya

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

katika migodi yote, moja kati ya taarifa ambayo tunaisubiri ambayo itafanyiwa utekelezaji ni pamoja na jambo hilo na Serikali itatoa maelekezo kwa waajiri wote kwamba wanachokifanya ni kinyume na utaratibu wa sheria za nchi na hairuhuswi kwa mwajiri yeyote kum-*blacklist* mfanyakazi. Kwa hiyo, tutaendelea kuwachukulia hatua kwa wale wote watakaoendelea kufanya jambo hili, ambalo linawaondolea haki ya kimsingi kabisa wafanyakazi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusu mikataba, kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya mwaka 2004 imeanisha vema katika Kifungu Na. 14 aina ya mikataba ambayo mwajiri anapaswa kumpatia mfanyakazi. Kama Mwajiri anakiuka katika eneo hilo, anashindwa kutoa mikataba kwa mujibu wa sheria inavyosema, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba kwa sababu umeleta lalamiko hili rasmi tutalifanyia kazi na tutachukua dhidi ya wale waajiri wote ambao wanashindwa kukidhi matakwa ya Kifungu Na. 14 cha Sheria za Kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mukya, swali la nyongeza.

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kumekuwa na tabia mbaya na chafu ya udhalilishaji wa hawa waajiri wa madini ya kuwapekua wafanyakazi sehemu za siri. Hii imefanyika katika Kampuni ya *Tanzanite one* kule wanapovuna madini ya *Tanzanite*, wanawapekua sehemu za siri hasa sehemu za kujisaidia haja kubwa. Je, hakuna njia mbadala ya kufanya zoezi hilo zaidi ya kuwdhalilisha hawa wafanyakazi (*Makofit*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, anachokisema Mheshimiwa Mbunge, mimi mwenyewe nilikwenda pale *Tanzanite one* katika mgodi huo, nilikutana na changamoto hiyo kubwa ambayo wafanyakazi walieleza mbele yangu.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara ile nilitoa maelekezo na taratibu zote za namna ya ukaguzi unavyopaswa kufanyika ili usidhalilishe utu wa wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika migodi hiyo. Maelekezo yalitolewa ya kwamba zipo taratibu za kufuata katika ukaguzi lakini siyo za kumdhalilisha mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuondoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maelekezo tayari yapo, kama vitendo hivi vinaendelea basi niwaombe wafanyakazi wale waripoti tuchukue hatua stahiki zaidi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rita Kabati, swali la nyongeza.

MHE. RITA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niullize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa huu udhalilishaji ambao umekuwa ukifanyika na hao wawekezaji siyo katika migodi tu, upo hata katika viwanda vyetu. Nimeshuhudia mara nyingi sana Mheshimiwa Naibu Waziri akienda kusuluhiha migogoro hasa ikihusiana na unyanyasaji wa wafanyakazi. Je, ni adhabu gani kubwa kabisa ambao wamekuwa wakipatiwa hawa waajiri au wawekezaji ambao wamekuwa wakiwanyanya hawa wafanyakazi. Kwa sababu nimeona jambo hili limekuwa likijirudia mara kwa mara. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Antony Mavunde majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwekezaji anayekuja kuwekeza hapa nchini hasa wale ambao wanapitia *TIC* na wale ambao wamejisajili katika Vyama vya Waajiri. Wamekuwa wakipewa sheria za nchi hii na utaratibu ambao unapaswa kufuatwa na jambo lolote linalojitokeza kinyume chake hapo sisi kama Serikali tumeendelea kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto kubwa sana kwa wawekezaji raia wa China ambao wengi

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wamekuwa wakiingia nchini na taratibu za kisheria zimekuwa hazifuatwi, lakini wale ambao wamesajiliwa wako chini ya *ATE*. *ATE* wamefanya kazi kubwa ya tafsiri sheria za kazi za nchi yetu kwenda katika lugha ya Kichina. Maana mwanzoni wao walikuwa wanatumia *excuse* ya kutofahamu sheria, ingawa katika *principle* zile za sheria katika ile *maxim* inayosema *ignorantia juris non excusat*, ambayo inasema muhimu kabisa kwamba hakuna *excuse* kwa mtu ambaye hafahamu sheria. Kwa hiyo walichokifanya hawa waajiri wametafsiri sheria zile, lakini bado kuna watu ambao wanakiuka taratibu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tamko tu mbele ya Bunge hili kwamba wale waajiri wote hasa wawekezaji ambao wanafahamu sheria za nchi zetu, wanapaswa kufuata utaratibu ambao wanaendelea na unyanyasaji, tutaendelea kuwachukulia hatua stahiki ili kuhakikisha kwamba, tunaondoa dhana hii ya udhalilishaji na unyanyasaji wa wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia adhabu kubwa ambayo tumekuwa tukiichukua ni kwamba, tumekuwa tukiwandoa nchini mara moja wale wote ambao tunawabaini ni wageni wanawadhalilisha Watanzania katika nchi yetu ili tutengeneze kitu kinaitwa *deterrance*, mtu mwingine yejote asiweze kurudia kosa hilo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando, sasa aulize swalı lake.

Na. 106

Serikali Kulitumia Jeshi la Polisi Nchini

MHE. OTHMAN OMAR HAJI Aliuliza:-

Moja kati ya kazi za Polisi ni ulinzi na usalama wa raia na mahali zao, usoefu unaonesha kila zinapotokea kampeni za Uchaguzi Jeshi la Polisi hutumika kama Taasisi ya

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Chama Tawala hivyo husababisha ulinzi na usalama (hasa Wapinzani) kutoweka mikononi mwa Polisi:-

Je, Serikali haioni kwamba inalitumia Jeshi la Polisi kwa lengo la kudhoofisha Upinzani na kurahisisha kukipatia ushindi Chama chake cha CCM?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi (*PGO*) ambazo zinatoa mwongozo kwa shughuli za Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ifahamike kwamba Jeshi la Polisi lipo kwa ajili ya Ulinzi wa raia na mali zao na siyo kwa ajili ya chama fulani cha siasa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anasema. Ni Jeshi linalowatumikia Watanzania wote pasipo kujali vyama vyao, kabilzaao, dini zao ama rangi zao. Hata hivyo, ikitokea Askari wamekiuka taratibu za kiutendaji tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali za kinidhamu dhidi ya wale ambaao Wizara yangu inapata malalamiko rasmi kuititia dawati la malalamiko.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Othman Omar Haji, swalii la nyongeza.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza madogo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tarehe 20 Machi, 2016 ambapo vyombo vya dola vilikamilisha kusimamia zoezi la uchaguzi wa Zanzibar, ambaao uliiweka madarakani Serikali

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

haramu inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein jambo ambalo wakati huo palitokea tuhuma dhidi ya wafuasi wa *CUF* kwamba wanapita wakiharibu mali za wafuasi wa CCM, shutuma ambazo ziliwapelekewa wafuasi wa *CUF* kukamatwa, kupigwa, kuwekwa mahabusu.....

MBUNGE FULANI: Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa naomba ukae tafadhalii. Mheshimiwa Omar naomba uulize swalii maana umeshazungumza kwa muda kidogo naomba uulize swalii lako.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na matokeo hayo ambayo yalitokea katika Kisiwa cha Pemba, katika Kisiwa cha Unguja maeneo ya Tumbatu kulitokea nyumba za wafuasi.....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge naomba uulize swalii.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, najenga hoja.

NAIBU SPIKA: Umejenga hoja kwa muda mrefu, sasa ultakiwa uwe umejitayarisha tagu mwanzo, uliza swalii.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Nyumba za wafuasi wa *CUF* kuchomwa moto na wafuasi wa CCM, kwa kuthibitisha majibu ya Mheshimiwa Waziri Je, kwa nini wafuasi hawa walioshutumia na *CUF* katika Kisiwa cha Tumbatu, kwa nini mpaka leo hawajakamatwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, inapotokea Wapinzani wanataka kufanya mikutano, Jeshi la Polisi wanasema wana taarifa za kiintelijensia kwamba hakuna usalama. CCM wanapofanya mikutano yao, Jeshi la Polisi linakusanyika pote ili kulinda mikutano hiyo. Je, kwa nini Jeshi la Polisi linailinda mikutano ya CCM lakini pale ambapo Upinzani wanafanya mikutano hawataki kuilinda?

MBUNGE FLANI: Kuhusu utaratibu

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka nimthibitishie pamoja na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein ni halali ambayo imechaguliwa na wananchi kuititia Uchaguzi Mkuu halali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kauli kama hizi katika Bunge lako Tukufu ambazo zinapotosha umma siyo tu kupotosha na kudhalilisha Serikali halali na maamuzi sahihi ya wananchi ziendelee kupingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili anauliza swalii kwamba baada ya uchaguzi kuna wafuasi wa *CUF* ambao walishutumiwa kwa tuhuma mbalimbali ambao walikamatwa na akatolea mfano wa Kisiwa cha Tumbatu kuna wafuasi ambao hawakuchukuliwa hatua nadhani alikusudia wa vyama vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Uchaguzi Mkuu baadhi ya Vyama vya Upinzani ikiwemo chama chake, viongozi walijitokeza kuhamasisha wananchi kufanya mambo ambayo yanakiuka sheria za nchi yetu. Kuna matukio mbalimbali ambayo yamejitokeza ikiwemo kuchomwa moto kwa nyumba, kuchomwa mashamba, kurusha mabomu ikiwemo nyumba ya Kamishna Mkuu wa Polisi wa Zanzibar ambayo kwa uchunguzi uliofanyika mpaka sasa hivi tunavyozungumza watu ambao wamekamatwa kuhusika na urushaji bomu katika nyumba ya Kamishna ni Viongozi Waandamizi wa Chama cha *CUF*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi imeshakamilisha uchunguzi wake na suala lipo kwa *DPP* na linahitajika kupelekwa Mahakamani ili hatua za kisheria zichukuliwe. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, watu hawa ambao

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wamefanya matukio ya ukiukwaji wa sheria wapo wengi, mpaka sasa hivi zaidi ya watu 24 wameshapelekwa katika vyombo vyta sheria na wengine wapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi. Kwa hiyo, siyo sahihi kwamba Jeshi la Polisi linafumbia macho uvunjifu wa sheria. Iwe Tumbaktu, Pemba, Unguja ama sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ye yoyote ambaye anakiuka sheria za nchi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kuhusiana na hoja ya kwamba mikutano ya CCM inaruhusiwa na Polisi lakini mikutano ya *CUF* hairuhusiwi. Naomba nikuthibitishie pamoja na Wabunge na wananchi wote kwa ujumla, kwamba hakuna ubaguzi kama nilivyojibu katika swali langu la msingi katika kuhakikisha kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi yake kwa mujibu wa sheria, halibagui chama cha siasa. Tunapozungumza sasa hivi mikutano ya hadhara imezuilliwa kwa vyama vyote ikiwemo Chama cha Mapinduzi. Hakuna sehemu yoyote ambayo Chama cha Mapinduzi kinaruhusu mikutano ya hadhara zaidi ya Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa katika Majimbo yao. Mikutano ya ndani inaruhusiwa kwa vyama vyote na hajjawahi kuzuiliwa kwa chama chochote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge kama ana uthibitisho wa mikutano halali ya chama chake ambayo imezuilliwa basi atuletee taarifa ili tufuatilie tuweze kuchukua hatua stahiki. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Martha Umbulla, swali la nyongeza.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mara nyingi Jeshi la Polisi linapohitajika kuwahi kwenye matukio ya kuwalinda raia na mali zao wanapata shida sana ya kuwahi kwenye matukio hayo kutokana na matatizo waliyonayo kwenye magari yao, magari mengi yanakosa matairi, mafuta na ni mabovu, tatizo hilo ni karibia nchi nzima lakini nazungumzia katika Mkoa wangu wa Manyara. Je, Serikali ina mpango gani mahsus kabisa wa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kuhakikisha kwamba magari ya Jeshi la Polisi yanakuwa na vifaa hivyo muhimu ili kuhakikisha kwamba ulinzi wa raia na mali zao unakuwa wa uhakika? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba tuna changamoto ya upungufu wa vitendea kazi kwa ujumla katika Jeshi letu la Polisi na hii inatokana na ufinyu wa bajeti tulionao. Tutajitahidi katika bajeti ya mwaka huu kuongeza fedha kwa ajili ya matumizi kwa Jeshi la Polisi ili tuweze kukidhi mahitaji hayo, siyo tu kwa Mkoa wa Manyara pia kwa nchi nzima kwa ujumla wake. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Peter Lijualikali, swali la nyongeza.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Juzi hapa tumetoka kwenye Uchaguzi Mdogo Ifakara tarehe 23 ambapo kwanza Mwandishi wa Mwananchi Juma Mtanda alitekwa na wanachama na wafiasi wa CCM, wakampora *iPad*, simu na Kamera, akaenda Polisi akalalamika. Matokeo yake Polisi wakawatafuta watu wa CCM na wakamrudishia. Maana yake ni kwamba Polisi wanawajua wanaofanya uhalifu huu, mpaka leo hakuna ambacho kimefanyika, hakuna kesi wala chochote, hiyo ni moja. (*Makofii*)

Pili, kwenye uchaguzi ule kuna Askari WP Huruma alipigwa na jiwe na tofali akapasuka, ameshonwa nyuzi tano na amepigwa na wanachama wa CCM, lakini Polisi wanamuachia anatembea, anafanya chochote taarifa ipo. Namwomba Mheshimiwa Waziri anaiambie kama CCM wanaruhusiwa kufanya vurugu mpaka kujeruhi Askari wetu halafu wakaachiwa huru? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lijualikali anazungumzia tuhuma za wanachama wa CCM kuwajeruhi Askari Polisi, pia kupora Waandishi wa Habari. Kwanza kabisa nashindwa kulijibu swali hili moja kwa moja kwa sababu unapozungumzia tuhuma kwamba hawa ni wafuasi wa chama fulani inahitaji uthibitisho.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowenza kusema...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib na Wabunge wenzako tumsikilize Waziri ameulizwa swali. Mheshimiwa Esther Matiko, tafadhali. Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowenza kusema ni kwamba uhalifu wa aina yoyote utakaofanywa na mtu yoyote wa chama chochote, dhidi ya raia yoyote ikiwemo Waandishi wa Habari na Jeshi la Polisi ndiyo kabisa. Jeshi la Polisi liko hapa kwa ajili ya kulinda usalama wetu, hatutakubali kamwe mtu ye yoyoteacheze na Jeshi la Polisi na siyo tu Jeshi la Polisi hata Waandishi wa Habari wamekuwa wakifanya kazi vizuri sana ya kuelimisha jamii na kutoa taarifa nzuri kwa umma. Hatuwezi kukubali Waandishi wa Habari au Jeshi la Polisi kufanyiwa matukio yoyote ya kihalifu na raia mwingine yeyote, tutachukua hatua kali za kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge kama ana ushahidi wa hilo jambo alete, lakini siwezi nikasema hapa kwamba chama fulani kimefanya jambo fulani bila uthibitisho. (*Makofii*)

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali fupi la nyongeza. Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mkuranga, Kibiti na Rufiji ningemba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie sawa na jibu lake la msingi ya kwamba kazi mojawapo ya

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Polisi ni ulinzi wa raia na mali zao. Je, Serikali inawahakikishajie wananchi wa Wilaya hii ya Mkuranga, Kibiti na Rufiji juu ya usalama wao na wa mali zao kipindi hiki cha operesheni ya kutafuta wahalifu ili waweze kufanya kazi zao kwa uhuru bila ya kubigudhiwa? Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mkuranga, Kibiti na Rufiji kama ambavyo kila mmoja anafahamu kwamba limekuwa na changamoto ya matukio mbalimbali ya uvunjifu wa amani ambapo mpaka sasa hivi kuna raia wengi wamepoteza maisha, pia mnakumbuka hivi karibuni Askari wetu takribani nane walipoteza maisha kwa mpigo. Mimi binafsi nilifanya ziara katika maeneo hayo ambayo nimeyazungumza na kufanya mukutano wa hadhara na wananchi. Katika mambo ambayo tumeyazungumza alifanya ziara Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; kuna mambo makubwa matatu ambayo tumeyasisitiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tumeendelea kuwasitisiza wananchi kulisaidia Jeshi la Polisi kutoa taarifa juu ya matukio ya uhalifu na wahalifu ambao wanawashuku katika maeneo yao ili kazi ya Jeshi la Polisi iweze kuwa rahisi. Pili, tumeendelea kuwahakikishia wananchi wa Mkoa huo kwamba Serikali itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba kwamba amani na usalama wa wananchi wa maeneo hayo linakuwa ni jambo la kipaumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya hivyo ni lazima Jeshi la Polisi liwe karibu na wananchi vilevile, wananchi wawe karibu na Jeshi la Polisi na Jeshi la Polisi liwe karibu na wananchi, kwa maana ya kujenga mahusiano mazuri kati ya pande hizi mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kukiomba kwa Mheshimiwa Mbunge akiwa Mwakilishi wa wananchi wa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Jimbo la Mkuranga pamoja na Wabunge wengine wa maeneo yale, kuhakikisha kwamba wanaendelea kuwaelimisha wananchi waendelee kuwa karibu na Jeshi la Polisi, kuwasaidia kupata taarifa mbalimbali za uhalifu wakati huu ambapo Jeshi la Polisi na Serikali kwa ujumla inafanya jitihada kuhakikisha kwamba maisha ya wananchi wa maeneo hayo yanalindwa pamoja na mali zao, pamoja na maisha, usalama wa Askari wenyewe ambao wanalinda usalama huo wa raia. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 107

**Changamoto ya Upatikanaji wa Leseni za
Udereva Tarime/Rorya**

MHE. ESTHER N. MATIKO Aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa leseni za udereva katika Mkao wa Polisi Tarime/Rorya kutokana na kutokuwepo kwa huduma hiyo. Hali hiyo inapelekea wananchi kupata adha kubwa ya kufuata huduma za leseni Musoma Mjini ambao ni Mkao mwingine wa Polisi; kutokana na adha hiyo wananchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali waliamua kujenga na kukamilisha jengo la usalama barabarani:-

(a) Je, ni lini Mkao wa Polisi Tarime/Rorya utafungiwa mitambo ya kutoa leseni za udereva ili kuondoa usumbufo uliopo sasa wa kutumia gharama na muda kufuata huduma hiyo Musoma Mjini?

(b) Je, ni lini Ofisi za Mkao wa Polisi Tarime/Rorya zitajengwa ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania na Jeshi la Polisi Usalama Barabarani imekuwa ikiboresha huduma za utoaji leseni za udereva na ukusanyaji wa ada za leseni ili kuhakikisha kuwa huduma hizi zinawafikia wananchi bila usumbufu. Serikali kupitia taasisi hizi imefunga mitambo ya kutoa leseni za udereva kila Makao Makuu ya Mkoa ambapo wananchi wote wanaohitaji huduma hizi hufika Mkoani na kuhudumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, illi kufunga mitambo hii kunahitajika maandalizi makubwa ya kifedha na uandaaji wa miundombinu ya mtandao, majengo na rasilimali watu. Kwa sasa, mitambo hiyo imefikishwa hadi kwenye Mikoa ya kikodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Serikali ingependa kufunga mitambo ya kutoa leseni za udereva katika ngazi za Wilaya ikiwemo Wilaya ya Tarime/Rorya. Hata hivyo, kwani gharama za kufunga mitambo hii katika Wilaya zote nchini ni kubwa mno. Serikali inao mkakati wa kufikisha huduma hizi Wilayani ikiwemo Wilaya ya Tarime/Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya ni mionganoni mwa Mikoa mipyä ambayo bado haijajengewa ofisi mpya za kisasa ikiwemo Songwe, Katavi, Simiyu na Geita. Serikali inatambua uhaba huo wa ofisi katika mikoa hiyo na kuna mkakati wa ndani wa kujenga ofisi hizo kwa kutumia rasilimali zilizopo kama nguvu kazi ya wafungwa na kutengeneza matofali ya kujengea ofisi hizo muhimu kwa huduma ya Kipolisi na Idara zingine za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nasikitika kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani leo hii inaita kwamba ni Wilaya ya Tarime/Rorya haijui kwamba ni Mkoa wa Kipolisi wa Tarime/Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya masikitiko yangu, nipende kumwambia Naibu Waziri kwamba tayari tuna miuondombinu kwa maana ya mtandao wa *TRA* pale, tayari wananchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamejenga hilo jengo na tuna rasilimali watu. Sasa nataka kujua ni lini sasa baada ya kutambua kwamba Tarime/Rorya ni Mkoa wa Kipolisi na hivyo ni Makao Makuu ya Mkoa wa Kipolisi, ni lini mtakuja kufunga huo mtambo ili kupunguza adha ya wananchi kwenda kwenye Mkoa wa Polisi wa Mara kutafuta huduma? (*Makofi*)

Swali la pili ni kuhusiana na kujenga ofisi ya Mkoa wa Polisi Tarime/Rorya ambao Mheshimiwa Waziri amesema ni mkoa mpya. Mkoa wa Polisi Tarime/Rorya ni wa siku nyingi ukilinganisha na Katavi, Simiyu na Geita. Kwa mikakati yenu ya ndani ningependa kujua ni lini mtakuja kujenga jengo zuri lenye hadhi ya Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya ili kuondokana na kukaa kwenye magodauni ambayo wanakaa sasa hivi na kushusha hadhi ya Kipolisi Mkoa wa Tarime/Rorya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nirudie majibu yangu ya msingi ambayo nimejibu kwamba, changamoto kubwa ambayo inakabili kutokukamilisha ujenzi wa vituo vya Polisi na miundombinu mingine ikiwemo hii miundombinu ya utoaji wa leseni ni ufinyu wa kibajeti. Azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba mikoa na wilaya zote nchini zinapata huduma hizo muhimu. Changamoto nyingine kubwa ambayo nimezungumza ni katika mikoa ile mipyä.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue fursa hii kumhamasisha Mheshimiwa Mbunge, nimefanya ziara katika maeneo mbalimbali ikiwemo hii mikoa mipyä na nimeona jitihada mbalimbali ambazo viongozi wa maeneo hayo wamekuwa wakifanya ili kuhamasisha wananchi, pamoja na sisi tupo tayari kuweza kuwasaidia nguvu kazi kupitia Jeshi la Magereza kuanza mchakato wa ujenzi wa vituo vyä kisasa kwa mikoa mipyä hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hayo yakiendelea tutaendelea kuhakikisha kwamba tunajitahidi itakavyowezekana kadri ya bajeti itakavyoruhusu kwa upande wetu kujenga vituo hiyo vyä Polisi, wakati huo huo kuzungumza na mamlaka ya TRA kuhakikisha kwamba huduma za utoaji leseni zinapatikana katika mikoa na wilaya zote nchini Tanzania, ikiwemo sehemu ambayo Mheshimiwa Mbunge anatoka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kuna changamoto kubwa sana ya vijana wa Lushoto hasa wa bodaboda kupata leseni; Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi Wilaya ya Kipolisi Lushoto ili vijana wa Lushoto waweze kupata leseni bila kutumia gharama kubwa za kwenda hadi mkoani? (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wilaya iweze kupandishwa hadhi, iwe Kanda Maalum ama Mkoa wa Kipolisi kuna utaratibu ambao unatakiwa ufuatwe kabla ya kutoa maamuzi. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Lushoto siyo katika maeneo ambayo mpaka sasa tumeweza kupata maombi rasmi ya mchakato wa kuongeza hadhi ya Kipolisi, ikiwa kuna vigezo vinakidhi basi Mheshimiwa Mbunge

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kwa kushirikiana na Viongozi wa Jeshi la Polisi katika eneo lake waanze mchakato huo ili tuweze kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pascal Haonga, swali la nyongeza.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, kumekuwa na vijana wengi sana wa bodaboda nchini maeneo mbalimbali wamejiajiri kwa kubeba abiria, lakini bodaboda hao wengi hawana leseni. Je, Serikali ipo tayari kuwasaidia bodaboda kuwapatia leseni, kwa kuwa wengi walikuwa wanajihuisha na matukio ambayo siyo mazuri sasa wameamua kujiajiri. Sasa Serikali ipo tayari kuwapatia leseni bodaboda ili kuwasaidia? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kuendesha bodaboda au chombo chochote cha usafiri bila leseni ni uvunjifu wa sheria. Hatutakuwa tayari kuendelea kulea uvunjifu wa sheria. Hatuwezi kuwapa leseni watu kwa kisingizio kwamba walikuwa wanaendesha bila leseni kuhalalisha uvunjifu wa sheria.

Tunachokisisitiza hapa ni kwamba Mheshimiwa Mbunge uendelee kuhamasisha wananchi wote kufuata sheria ikiwemo hao vijana ambao wanaendesha bodaboda bila leseni. Wafuate utaratibu wa kupata leseni kwa kufanya *test* ili waweze kupata leseni kisheria, siyo kupata leseni kwa sababu wamekiuka sheria. Sisi tutawachukulia hatua za kisheria wale wote ambao tutawabaini kwamba wanaendesha gari na pikipiki kinyume na sheria. Tunaomba ili sheria isiweze kuwakumba basi wafuate sheria kwanza.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 108

Serikali Kujiimarisha Katika Kukabiliana na Majanga Mbalimbali Nchini

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA Aliuliza:-

Majanga ni mambo yasiyotarajiwa ila huwa yanatokea tu, majanga kama ajali za baharini, ziwani, barabarani, matetemeko, vimbunga, majanga ya njaa na kadhalika yamekuwa yakitokea:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha na kuimarisha nyenzo na ujuzi kwa Kikosi cha Uokoaji wa Majini kinacho julikana kama *Coast Guard* kwa ajili ya uokoaji?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina utaratibu wa namna ya kushughulikia masuala ya utafutaji na uokoaji majini. Kituo maalum kijulikanacho kama *Dar es Salaam Maritime Rescue Coordination Center (MRCC)* kimeanzishwa na kimekuwa kikitoa huduma kwa saa 24 kila siku. Kituo hiki kinasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*). Aidha, kwa kuzingatia ukubwa wa shughuli za usafiri, uvuvi na nyinginezo katika maziwa, kituo kidogo cha Uratibu wa Utafutaji na Uokoaji (*MRCC*) kimeanzishwa Jijini Mwanza.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha utaratibu wa utafutaji na uokoaji, Wizara yangu imeandaa rasimu ya sheria ya utafutaji na uokoaji (*search and rescue*) inayozingatia miongozo ya Kimataifa ya Utafutaji na Uokoaji (*International Air and Maritime Search and Rescue Guidelines*) na wadau mbalimbali wametoa maoni yao kuhusu rasimu hiyo na sasa kazi ya kurekebisha rasimu ya sheria hiyo ili kuzingatia maoni ya wataalam mbalimbali inaendelea ili kuruhusu hatua zaidi za kupitisha sheria hiyo kuendelea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swalilala nyongeza.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ila nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa nyendo zimekuwa nydingi, watu wanakwenda sana kutoka sehemu moja kwenda nydingine kwa ajili ya kiuchumi na mengineyo, kwa hiyo ajali za majini, baharini na kwenye maziwa yawezekana zikatokea. Serikali imejipanga hivi ilivyojipanga; Je, Serikali inaonesha vipi shughuli zinazofanywa na *SUMATRA* na kule Zanzibar, kwa sababu bado ajali zitakuwa zikatokea tunafanyaje?

Swali la pili; Serikali ina mpango gani kwa wale waliopatwa na msiba na kupoteza ndugu zao wakati ilipopata tatizo *MVBukoba, MV Spice Islander* iliyozama kule Nungwi na ajali nydingine. Je, watu wote hawa wameshalipwa fidia zao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mahusiano ya *MRCC* na upande wa Zanzibar, naomba nimhakikishie kwamba *MRCC* ni ya masuala ya Muungano na yanasmamiwa na *SUMATRA*, kwa hiyo *Zanzibar Maritime*

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Authority watashirikiana na taasisi yetu katika kusimamia hii MRCC iweze kuhudumia pande zote za Muungano mara ajali inapotekeea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili nimuombe tu Mheshimiwa Asha Juma kwamba ajali ya *MV Bukoba* na ajali nyingine zote zimeshughulikiwa na Serikali kwa kiwango kikubwa sana, maadam sina takwimu hapa nisingeweza kumpa undani wa nini kilifanyika, lakini ni masula ambayo yalishughulikiwa na Idara yetu ya maafa iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ukamilifu kabisa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yussuf, swali la nyongeza.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza. Ni dhahiri kwamba Watanzania wengi wanapoteza maisha katika bahari au katika maziwa zinapotokea ajali na ni ukweli uliowazi kwamba hatuna wataalam wa uokozi wa kutosha kama *divers* ndani ya nchi yetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kikosi kazi chenye wataalam kama *divers* na wakiwi na zana za kisasa za uokoaji ili kuepusha ajali zinazotokea na kuokoa maisha ya watu wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna kikosi maalum kwa ajili ya uokoaji kama kumetokea ajali, kikosi hicho kinashirikisha pamoja na Jeshi la Wananchi, *Marine Police*, *SUMATRA* na wadau wengine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kawaida ajali ikitokea baharini chombo kinatakiwa kipeleke *signal* maalum ambayo tunaita *distressing signals*, *signals*/hiyo ikipelekwa meli zote zilizopo zinakwenda kusaidia kuokoa kwa sababu ukisubiri wewe mpaka wataalam watoke Dar es Salaam na

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

meli imetokea pengine kilometra 200 ulipo itakuwa ni *too late*. Kwa ufupi tu tuna vikosi maalum ambavyo ikitokea tu vikosi hivyo vinakwenda na vinafanya kazi hiyo. Kwanza Polisi, Jeshi la Wanamaji na Zanzibar kuna KMKM na wataalam wengine wapo ili kuhakikisha kwamba tunawasaidia wale wanaopata ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kama Serikali kuwaimarisha hawa kiutaalam ili waweze kufanya kazi na teknolojia za kisasa za uokoaji. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, swali la nyongeza, majibu.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ziwa Victoria kumekuwa na meli nydingi ambazo zimekuwa zikisaidla wananchi kubeba mizigo na abiria kwenda Ukerewe na nchi za jirani. Hivi sasa ni meli moja tu inayotembea *MV Umoja* imepaki, *MV Serengeti* imepaki, inayotembea ni *MV Clarias* peke yake. Wananchi wanaoenda visiwani hasa Ukerewe wanatumia feri za mizigo, sasa za kwetu zimeharibika, sina hakika kama Wizara imeshindwa kukarabati zile feri ama watumishi walioko kule wanafanya mipango na wale watu wenye maferi. Nataka kujua kwa Waziri ni lini feri hizi zitaanza ku-*operate* kwa muda muafaka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tunazo meli ambazo zimesimama kwa sababu ya kuharibika ikiwa ni pamoja na *MV Umoja* na *MV Serengeti* na hata hii *MV Clarias* siyo muda mrefu sana imekarabatiwa ni karibuni tu imeanza kutoa hiyo huduma, nayo ilikuwa imeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti iliyopita ya 2016/2017, tulitenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa meli za Ziwa Victoria, nimhakikishie pamoja na kwamba taratibu za

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kumpata mtu wa kuweza kufanya hiyo kazi zimeshakamilika, muda siyo mrefu kazi hiyo itaanza na kazi hiyo itakapokamilika meli hizo zitarudi majini. Aidha, tuna mpango wa muda mrefu wa kujenga meli mpya itakayohudumia Ziwa Victoria na maziwa mengine Tanganyika na Nyasa, kwa Nyasa tumeshakamilisha ili kuhakikisha kwamba meli hizo ambazo zimefanya kazi muda mrefu sana katika maziwa hayo zinapunguziwa uzito na meli mpya zitakazokuwa zimejengwa. Utaratibu wa kujenga meli hiyo bado tunaendelea nao na muda si mrefu tunatarajia kupata mkandarasi wa kujenga meli hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, swalil nyongeza.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Swalil langu ni dogo tu, majanga ya moto katika Jiji la Mbeya yamekuwa yanajitokeza mara kwa mara hususan Soko la *SIDO* Mwanjelwa, Uhindini na sababu kubwa ni uchakavu na ubovu wa miundombinu. Naomba Serikali iniambie ina mkakati gani katika kuondoa tatizo hili kwa kushirikiana na Halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, swalililoulizwa ni kama ni la Mambo ya Ndani lakini kama unaweza kulijibu naomba utusaidie. Naibu Waziri sijui kama ulilisikia, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, *emphasis* ya swalilake ipo katika miundombinu na ndiyo maana nilikuwa nadhani nilijibu na kama kutahitajika maelezo ya ziada yataweza kutolewa, *emphasis* yake ameitoa kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie muda si mrefu hapa tutasoma bajeti yetu ataona ni kwa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

namna gani Wizara yetu imezingatia haya ambayo ameyauliza, vilevile wakati tunapitisha Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI unafahamu kuna baadhi ya fedha zimetengwa kwa ajili ya kushughulikia miundombinu katika Jiji la Mbeya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, majibu ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ameyatoa kuhusiana na vifaa vya Zimamoto siyo tu kwa Mkoa wa Mbeya lakini nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Mbeya binafsi nillifanya ziara katika Mkoa wa Mbeya na nataka nipongeze sana uongozi wa Jeshi la Zimamoto, Mkoa wa Mbeya kwamba umefanya ubunifu wa hali ya juu kwa kuhakikisha kwamba unapanua huduma za zimamoto katika Wilaya nyingine za Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwaunga mkono tuliweza kuhakikisha kwamba tunafanya mambo makubwa matatu. Moja, tumewapatia gari ambayo itakuwepo katika Wilaya ya Rungwe, pili kulikuwa kuna changamoto ya gari ya zimamoto ya Mkoa wa Mbeya ambayo tumefanya jitihada ya kukamilisha matengenezo yake na sasa inaendelea kutoa huduma katika Mkoa wa Mbeya, pamoja na mambo mengine ambayo zaidi yanalenga katika kuongeza utoaji wa elimu ya uokoaji katika Mkoa mzima wa Mbeya na Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba katika bajeti inayofuata na katika bajeti zilizopita tumetoa kipaumbele sana katika kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya ziada ya zimamoto. Hizo ni kati ya jitihada ambazo tunachukua ukiachilia mbali mchakato ambao unaendelea sasa hivi wa mazungumzo

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na kampuni ya Ubelgiji pamoja na Austria kuweza kupata mkopo wa vifaa vya zimamoto na uokoaji kwa Tanzania nzima.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga sasa aulize swali lake.

Na. 109

Kupeleka Minara ya Simu – Jimbo la Kalenga

MHE. GODFREY W. MGIMWA Aliuliza:-

Tatizo la mawasiliano ya simu katika Jimbo la Kalenga bado ni kubwa:-

Je, ni lini Serikali itapeleka minara ya simu kwenye vijiji vya Kanning'ombe, Ikungwe, Lyamgungwe, Igunda na Ikuvilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ilainisha maeneo mbalimbali katika Jimbo la Kalenga na kuyaingiza katika miradi mbalimbali ya utekelezaji. Vijiji vya Igunda na Lyamgungwe kutoka katika Kata ya Lyamgungwe vimo katika utekelezaji wa mradi wa *Viettel*. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba 2017. Aidha, Vijiji vya Ikungwe na Kanning'ombe vimeingizwa katika orodha ya miradi inayosubiri fedha ili kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/2018. (*Makofii*)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, swali la nyongeza.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya kupeleka mawasiliano katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, swali hili nimeuliza mwaka 2014 nikajibiwa kwamba 2015 nitapata majibu ya uhakika, sikupata majibu. 2015 nikapata nafasi ya kuuliza nikaambiwa 2016, leo hii ni 2017 naambiwa ni 2018. Naomba niweze kupata majibu ya uhakika leo kwamba ni lini sasa vijiji hivi vilivyoorodheshwa vitapata minara ya simu na wananchi wangu waweze kupata mawasiliano hayo ya simu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika minara ya simu ambayo inajengwa katika maeneo mbalimbali katika Jimbo langu la Kalenga *service levy* *hailipwi* moja kwa moja kwenye Halmashauri, inaenda kulipwa kwenye makampuni yenye ambayo mengi yapo Dar es Salaam. Wananchi katika Jimbo langu wanakosa mapato ya ndani kutokana na minara hiyo ya simu. Ningependa kujuua kutoka Wizarani, je, ni namna gani sasa wanawenza kuwapelekea fedha hizi wananchi ambao nao wanatakiwa kwa namna moja au nyingine waweze kupata faida kutokana na minara hii ya simu, kwa sababu inayotumika pale ni ardhi?

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba fedha ambazo yanapata makampuni haya au faida ambazo zinapata kampuni hizi zinakwenda pia kuwasaidia wananchi katika maeneo husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, tunapojojbu maswali hapa huwa tuna dhamira ya dhati ya kutekeleza kile tunachokijibu na kwa kawaida Wizara huwa tunajiaandaa kujipanga kutekeleza kile ambacho tunakijibu hapa. Inapofika wakati wa bajeti inaweza ikatokea kama ilivyotokea kwa eneo hili kwamba Mfuko wetu wa Mawasiliano kwa Wote huwa unakosa fedha, unapokosa fedha tunatarajia tuifanye hiyo kazi mwaka unaofuata, hiyo inabakia dhamira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba dhamira yetu ni kuhakikisha vijiji hivi kama tulivyosema katika jibu la msingi, tunavitekeleza katika mwaka huu wa 2017/2018 na fedha tunatarajia kuziomba na tunaamini mtazipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii la pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ile minara ya simu pale inapoengwa kwa kawaida yale makampuni yanaingia mikataba na ama vijiji au mwenye ardhi husika, kwa kawaida Wizara hatuingilii sana katika mikataba hii ya kulipa gharama za ardhi inayotumika na wawekezaji katika minara ya simu. Hata hivyo, nalichukua wazo lake au pendekero lake ili tuangalie namna gani Wizara inaweza kusaidia katika kuhakikisha minara hii ambayo imewekwa katika Jimbo hili la Kalenga inatumika na inawanufaisha wananchi kupitia mikataba yao ambayo wameweka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucia Mlowe, swalii la nyongeza.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa, katika Mkoa wa Njombe kuna matatizo makubwa sana ya mawasiliano hasa maeneo ya mwambao katika Wilaya ya Ludewa kama Rupingu, Ibumi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea minara watu wa maeneo hayo? (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyoshirikiana na Mbunge wa Jimbo la Ludewa katika kuhakikisha kwamba eneo la Mwambao linashughulikiwa kikamilifu. Kwa sababu swali hilo limeulizwa muda siyo mrefu na tumelijibu hapa liliulizwa na Mheshimiwa Deo Ngalawa na leo linaulizwa na Mheshimiwa Lucia Mlowe nawashukuruni sana kwa ushirikiano wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekuwa nikilijibu kuititia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo kwamba eneo hilo tutahakikisha tunajenga minara katika kipindi hiki na itakapofika mwaka 2020 tatizo hilo tutakuwa tumelitatu. Siyo hilo tu na lile lingine la kutoboa barabara katika ukanda ule wa Ziwa, tutakuwa tumeshashughulikia hayo matatizo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mmesimama wengi sana sasa, Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo linalolikabili Jimbo la Kalenga linafanana vilevile na Kijiji cha Ruvuma chini, Kijiji cha Kihungu, Kijiji cha Mpepai, hao nao wanapata shida kubwa ya mawasiliano. Je, ni lini Serikali itahakikisha vijiji hivi navyo vinawekwa katika mpango na mwaka huu usipite wapate mawasiliano kama wanavyopata Watanzania wengine? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji hivyo alivyovitaja vyta Ruvuma chini, Mpepai na eneo lote lile la ukanda wa Ziwa Nyasa pamoja na Mto Ruvuma, maeneo

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

hayo yameingizwa katika mpango wa UCSAF, tunachohitaji ni kupata fedha ili tuweze kuyatekeleza hayo maeneo na nimhakikishie tutaendelea kufuatilia kama ambavyo Waziri wangu alimuahidi ofisini wakati alipokuwa akifuatilia hili suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba tutalifuatilia hadi tunakamilisha mawasiliano katika maeneo hayo ili watu wetu wasiwe wanapata matatizo na mawasiliano ya nchi jirani na wakashindwa kuwasiliana kwa upande wa Tanzania.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza linahusu wageni waliotufikia Bungeni leo. Wapo wageni Wanne wa Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambaao ni Injinia Joseph Nyamhanga ambaye ni Katibu Mkuu Ujenzi, Dkt. Leonard Chamuriho ambaye ni Katibu Mkuu - Uchukuzi, Dkt. Mary Sasabo ambaye ni Katibu Mkuu-Mawasiliano na Ndugu Angelina Madete ni Naibu Katibu Mkuu-Mawasiliano. (*Makofi*)

Pia wameambatana na Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa mbalimbali kutoka Wizara hiyo. Pia wapo Mameneja wa Mikoa (*TANROADS*) pamoja na wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Usafirishaji (*NIT*), karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wawakilishi wawili kutoka Jumuiya ya Ulaya (*European Union*) ambaao ni Ndugu Fabio Di Stephano ambaye ni Mkuu wa kitengo cha miundombinu na ushirikiano wa kikanda, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Ally Mwichande ambaye ni Meneja wa mipango na miundombinu, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe Waziri wa habari, Utamaduni, Sanaa na

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Michezo, ambaye ni Mwanariadha na mshindi wa medali ya dhahabu katika mbio za Mumbai za mwaka 2017 Ndugu Alphonse Simbu. Karibu sana kijana wetu, tumefurahi sana maana Watanzania umetutoa kimasomaso. (*Makofi/Vigelegele*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

MBUNGE FULANI: Hawachangi wanajua kupiga makofi tu, wapuuzi kweli. Mumchangie.

MHE. ESTER A. BULAYA: Makofi na michango.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo. Sawa, ndugu yetu Alphonse Simbu ameongozana na, hiki cheo cha Kijeshi sjui kinaitwaje lakini ni Kanali K. J. Mziray ambaye ni Mkuu wa Utawala wa Mafunzo JKT, ameongozana pia na Luteni Kanali Meidini ambaye ni Mkurugenzi wa Elimu, Michezo na Utamaduni JKT. Pia ameongoza na Mejja Mvula ambaye ni Mkuu wa Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Makuyuni, Ndugu John Mshana ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano (*Multi Choice-Tanzania*). (*Makofi*)

Kwa nafasi ya kipekee kabisa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Harrison Mwakyembe anawashukuru sana watu wa *Multi Choice-Tanzania* kwa ufadhili wao kwa Ndugu yetu Alphonse Simbu, pia anawashukuru sana watu wa JKT kwa kumpa hiyo fursa ya kufanya vizuri kijana wetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Ndugu Benjamin Sitta ambaye ni Meya wa Manispaa ya Kinondoni, ambaye ni mgeni wa Wabunge wa Manispaa ya Kinondoni na huyu ameongozana na msaidizi wake. (*Makofi*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

MBUNGE FULANI: Mwizi huyo.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naona leo tuna wageni wa aina nyingi humu ndani. Tunaendelea, tunao wageni 100 wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Mwigulu Nchemba amba ni Askari kutoka Jeshi la Magereza wakiongozwa na SP Magreth Simba, karibuni sana wageni wetu kutoka Jeshi la Magereza. (*Makofii*)

Pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni, karibuni sana wageni wetu, naamini mtajifunza hayo ambayo mtayaona leo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na matangazo, lipo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wanawake Tanzania (*TWPG*), anawatangazia Wabunge wanawake wote kuwa leo tarehe 27 Aprili, 2017, kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wanawake wote itakayofanyika katika ukumbi wa zahanati ya zamani ya Bunge. Semina itafanyika mara tu baada ya kuahirisha kikao cha Bunge saa saba mchana. Kwa hiyo mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka utawala, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba leo tarehe 27 Aprili, 2017 na kesho tarehe 28 Aprili, 2017 wataalam wa Benki ya *Bank ADC* watakuwepo kwenye viwanja vyta Bunge kuelekea Idara ya Habari kwa ajili ya kutangaza bidhaa na huduma za kibenki zinazotolewa na benki hiyo kwenye matawi yake kote nchini. Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kuwatembelea ili muweze kupata fursa ya kufahamu bidhaa na huduma mbalimbali zitolewazo na benki hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo pia tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge matokeo ya mechi zilizochezwa jana kwenye sherehe za maadhimisho ya miaka 53 ya Muungano. Mpira wa miguu (*Football*), timu ya *Bunge Sports Club* ilitoa fundisho kwa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wenzao wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwafunga magoli 4-0. Wafungaji magoli hayo walikuwa ni Mheshimiwa Cosato Chumi magoli mawili; Mheshimiwa Sixtus Mapunda goli moja na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa goli moja. Nyota wa mchezo huo alikuwa ni Mheshimiwa Mussa Sima. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, mpira wa pete (*Netball*), timu ilitoa matokeo ya kuwashangaza watazamaji kwa kuwafunga Baraza la Wawakilishi mabao 32-2. Nyota wa mchezo huo ni Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk na Mheshimiwa Angelina Mabula. Sasa hapa Waheshimiwa Wabunge na mimi nimetajwa ndiyo maana naona uvivu kutaja lakini wacha nisome na Mheshimiwa Tulia Ackson, Naibu Spika. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa Mheshimiwa Ngeleja anasema Mheshimiwa Spika alikuwa chachu kubwa ya ushindi kwa aina ya ushangiliaji wake akiwa karibu na Spika mwenzake wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa kumwambia bado moja kila linapoingia goli. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika alitoa changamoto jana ilibidi timu zote tucheze kwa bidii sana ili tusimuaibishe maana jana alikuwepo uwanjani. (*Makofi/Kicheko*)

TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, niwasomee taarifa ya Spika kwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba kufuatia mwongozo ulioombwa tarehe 18 Aprili, 2017 na Mheshimiwa Doto M. Biteko, alielekeza Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kukutana na kufanya kazi tukio la mauaji ya Askari Polisi nane yaliyotokea katika Wilaya ya Kibiti Mkoani Pwani, tarehe 13 Aprili, 2017.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika anawajulisha kwamba, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikutana tarehe 18 Aprili, 2017 kama alivyoelekeza

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na baada ya kukutana walitathmini tukio hilo na kumwita mbele ya Kamati Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Mwigulu L. Nchomba na kupokea taarifa yake.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati imempelekea Mheshimiwa Spika taarifa yake yenye tathmini ya kina kuhusu tukio hilo pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati. Baada ya kupitia taarifa hiyo na kwa mamlaka aliyonayo Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 117(17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2016, ameiwasilisha taarifa hiyo Serikalini ili mapendekezo ya Kamati yaweze kufanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo taarifa ya Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kidogo kuhusu maswali ya nyongeza kwa sababu nadhani yanaleta taabu napata ujumbe hapa mbele. Kwanza kabisa maswali ya nyongeza kwa mujibu wa Kanuni zetu yanapaswa kutokana na swali la msingi.

Jambo la pili, fursa ya kupata kuuliza swali la nyongeza pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Spika kwa sababu ya haya malalamiko, ameagiza hapa mbele kutakuwa na karatasi inayooonesha Wabunge wameshauliza maswali ya nyongeza mangapi ili kutoa fursa kwa Wabunge wote iliyo sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, anafahamu kwamba ziko nyakati ama yako mazingira ambayo mmoja anaweza kupata maswali zaidi ya mwingine, lakini ili kuweza kuweka uwiano siyo kwamba atatafutwa mtu hata kama hayupo, lakini kama yupo anayehitaji kuuliza swali la nyongeza na hajawahi kuuliza, atapewa kipaumbele kuliko ambaye ana maswali mengi zaidi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nimelisema hilo ili usije ukawa unaandika ujumbe wa kulalamika lakini huenda kwenye karatasi iko hapa mbele, wewe ndiye una maswali mengi zaidi kuliko watu wengine wote. Kwa hiyo twende hivyo Waheshimiwa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wabunge, yako mazingira mwagine atapewa nafasi kwa sababu maswali mengine mwagine hasimami ama haombi, lakini pale ambapo anakuwa ameomba ambaye karatasi hii inaonekana ana maswali machache ama hana kabisa, atapewa kipaumbele.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo yanayohusu maswali ya nyongeza pia lingine ni kwamba aliyewahi zaidi ya mwagine anaweza akapewa kipaumbele kuliko aliyejuja baadaye, msijisikie vibaya nafasi isipopatikana. Nafasi ni chache lakini hata hizo chache Mheshimiwa Spika ameamua kuwiwekea huo utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, tunaendelea.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bilago

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7).....

MBUNGE FULANI: Bado anaorodhesha.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Nimeshatajwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimemtaja Mheshimiwa Bilago naona bado mmesimama, naomba mkae. Mheshimiwa Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) jambo lilitotokea hivi karibuni.

Hoja yangu ni juu ya maswali ya Waziri Mkuu, maswali ya Waziri Mkuu leo hayakuwepo na mimi namwona yupo, nahisi kwamba labda imetokana na jana kuwa sikukuu kwamba hatukujiteza kupeleka maswali ya Waziri Mkuu jana. Hili suala nalionna kama sikukuu zitafululiza siku ya

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Jumatano huenda tukapoteza hii nafasi muhimu sana ya kumuuliza Waziri Mkuu maswali ya papo kwa papo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, kama inawezekana, sikukuu ikiwa inaangukia siku ya Jumatano au mapumziko siku hiyo na hatuwezi kupata nafasi ya kupeleka maswali kwa Waziri Mkuu, basi maswali hayo yaweze kupelekwa siku ya Jumanne, majina ya watakaouliza maswali akae nayo tu akijua siku ya Alhamis hiyo shughuli itakuwepo. Naomba mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Na mimi nasimama kwa Kanuni ya 68 nitasoma na 64 (1)(d) na (g).

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kauli za kudhalilisha Viongozi wetu Wakuu, kinyume na Kanuni yetu ya 64 kama ilivyotaja (d) na (g). Wapinzani hasa kutoka Zanzibar kila wakiuliza maswali wanatia vijembe vyatutambua Mheshimiwa Dkt. Shein na sisi Bungeni humu...*(Makofi)*

Mnapiga makofi ya nini si msikilize? Bungeni tumejiwekea sheria zetu kwa ajili ya heshima ya Bunge, kitie chako kinaruhusu mambo haya yanaendelea kufanyika. Nini mwongozo wako ili haya maneno ya kupiga vijembe Viongozi wetu Wakuu yafanyike wakiwa nje ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.*(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda kuomba mwongozo kwa Kanuni ya 68 (7).

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bungeni kwetu leo tumetembelewa na Askari Magereza, nimesimama kutaka kuwasemea na kutaka kujua hatma yao kwa sababu wamekuwa wakilalamika kuhusiana na *package allowance* ambayo tuliiiondoa tukasema watakuwa wanalipwa kila baada ya miezi mitatu sh. 300,000. Kuna Majeshi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi, Askari wa Uhamiaji na Askari wa Zimamoto. Wakati wa Bajeti ya Waziri Mkuu, mimi na Mheshimiwa Mchengerwa na Mheshimiwa Ridhiwani tulizungumzia hili na wakaahidi kwamba Serikali itawalipa. Ajabu baada ya hapo wamelipwa Askari wa Jeshi la Wananchi kwa mara ya pili, wenzetu wa Magereza, Uhamiaji na wale wa Zimamoto hawajalipwa hata mara moja.

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu.

MH: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupata mwongozo wako kwa nini Serikali inawabagua Jeshi la Magereza, Uhamiaji na wale wa Jeshi la Zimamoto na zaidi....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Matiko, umesema unahitaji Mwongozo wangu, ngoja kwanza, wewe ni Mbunge mzoefu, unafahamu Kanuni unaweza kuombea mwongozo kwenye jambo gani. Sasa unasema unataka kuwasemea Askari Magereza kwa kuwa wapo hapa ndani, kuwasemea Askari Magereza siyo mwongozo. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. (*Makofii*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7). Kumekuwa na kawaida ya Mawaziri wanapotujibu maswali Wabunge, kawaida hii ni pale tunapowauliza maswali halafu wanayajibu kisiasa. Nitatolea mfano leo, swali Namba 106 lilitolizwa na Ndugu Othman Omar Haji, Mheshimiwa Waziri akalijibu, akaeleza akasema tatizo la Zanzibar ni Viongozi wa *CUF* walienda kuvunja Ofisi. Mheshimiwa Lijualikali akauliza swali linalohusu viongozi wa CCM kule Kilombero, Waziri huyo akasema siwezi kuzungumzia tu kwa sababu ni viongozi wa CCM.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, tazito hili limekuwa mara nyingi na *double standard* kwa Mawaziri wa Chama cha Mapinduzi dhidi ya maswali ya Wabunge wa Upinzani wanafanya siasa. Tumeona hata Mheshimiwa Lucia Mlowe ameuliza swali hapa, Waziri anasema Mbunge wa Jimbo anataja wa Mbunge wa CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sisi ni Wabunge tunapouliza maswali majukwaa yetu tunayaacha nje ya ukumbi wa Bunge hili, naomba mwongozo wako, Je, ni halali, ni haki ni kama wanatudhalilisha tunapouliza haya maswali na kuonekana ni wahalifu wakati tunauliza kwa niaba ya wananchi waliotutuma katika jengo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mlongozo imekuwa mingi sana, mwongozo wa mwisho utatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Suleiman.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama hapa kwa Kanuni ya 68(7), kuhusu jambo liliotokea hapa Bungeni leo. Wakati Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani akijibu suala la Mheshimiwa Othman Omar Haji, amesema uwongo kwa kutoa tuhuma nzito sana kwa Viongozi Waandamizi wa *CUF*. Amesema kwamba Viongozi Waandamizi wa *CUF* ndiyo wanaohusika na ulipuaji wa nyumba ya Mkuu wa Polisi Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hilo ni la uwongo na halipo. Sasa naomba mwongozo wako juu ya suala hili. Je, anao ushahidi wa kutuletea hapa Bungeni wa kuturidhisha kwamba ni kweli ni Viongozi Waandamizi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa pili ninaouomba.....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suleiman, mwongozo mmoja umetosha ndiyo maana wengine imebidi niwakatishe hapo, mlongozo imekuwa mingi sana leo.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo kadhaa hapa na Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa kuwa hili jambo huwa tunalirudia mara kwa mara, nami sitachoka kwa sababu ndiyo sehemu ya kazi yangu.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(7) inasema hivi:

"Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambako hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba "*mwongozo wa Spika*" kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaluhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yataolewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa."

Waheshimiwa Wabunge, tunaposimama kwa wingi kuomba miongozo, maana yake ni kwamba mambo yaliyotokea kipindi cha maswali na majibu mengi yanaenda kinyume na utaratibu na mnataka kujiridhisha, ndiyo maana yake. Sasa niwaombe sana, mambo yale ambayo si kwamba yamefanyika hapa na hayahitaji kuzungumziwa kama Kanuni yetu inavyosema, tuache basi kutumia kipindi hiki kwa sababu tunakuwa tunapoteza wakati wetu muhimu sana wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nianze na mwongozo wa Mheshimiwa Bilago ambaye ameuliza kuhusu maswali ya Waziri Mkuu na kwamba leo yupo lakinijaujilizwa maswali. Ameendelea kwa kusema kwamba ana wasiwasi sikukuu zikiendelea kuwa Jumatano maswali haya yatakuwa jaujilizwi.

Waheshimiwa Wabunge, namna alivyoomba huu mwongozo ameonesha kabisa hana uhakika ni sikukuu ngapi katika wakati wa Bunge zitatokea siku ya Jumatano. Kwa sababu hiyo sina sababu ya kulitolea mwongozo suala hili, kwa sababu angetoa mfano wa siku ngapi zitaangukia

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Jumatano ningeweza kusema kwamba tutalitafutia utaratibu. Kwa kuwa, haipo na imetokea jana hili jambo Mheshimiwa Bilago halihitaji mwongozo siku ya jana ilikuwa sikukuu ndiyo maana leo maswali hakuna.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo pia na Mheshimiwa Musukuma kufuatia swali lilloulizwa na Mheshimiwa Omar, kuhusu maneno ambayo ameyatumia wakati akiuliza maswali yake na kwamba yanadhalilisha viongozi kwa mujibu wa Kanuni ya 64.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 64, wote tunaifahamu naomba tuifuatilie, tuisitumie lugha humu ndani ambazo zinatuweka matatani mpaka baadaye tunajikuta katika maeneo ambayo tusingependa kuwa huko. Kwa hivyo, Mheshimiwa Musukuma jambo lako limesikika na Wabunge wapo humu ndani wamelisikia naamini kwamba watazingatia Kanuni ya 64.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Esther Matiko pia alisimama yeye nilikwisha kumjibu. Jambo hilo halijatokea hapa ndani, kwa hivyo haliwezi kuzungumziwa katika mwongozo.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ameomba mwongozo kuhusu kawaida ya Mawaziri namna wanavyojibu maswali. Ametoa mifano miwili kwamba yako majibu ambayo yanajibiwa kana kwamba maswali yameulizwa kisiasa wakati maswali yameulizwa na watu ambao wanawakilisha wananchi na wanataka maswali yao yajibiwe kikamilifu. Ametoa mfano mwingine kwamba majibu yanayotolewa Mbunge wa Upinzani akiuliza yanatolewa kana kwamba na Mbunge wa CCM ni lazima atajwe.

Waheshimiwa Wabunge, haya mambo mawili yote yametokea leo, kama ambavyo nimetoka kueleza hapo mwanzo, niwaombe upande wa Mawaziri, upande wa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Serikali, tunapo jibu majibu tuzingatia pia utaratibu wa kujibu haya maswali. Mbunge aliyeuliza swali ajibiwe swali lake kikamilifu kama vile ambavyo Kanuni zinataka.

Waheshimiwa Wabunge, suala hili kwa sababu limeulizwa kwa ujumla sina sababu ya kusema nikaangalie *Hansard* nilisikia kwa ujumla wake, nadhani Mbunge mwenye swali lake ajibiwe yeye aliyeuliza. Haya yapo kwenye haya masuala yote mawili ambayo yameletwa, kuhusu maswali kujibu kisiasa na maswali kujibu kwa kutaja Wabunge wa vyama tofauti. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Dkt. Suleiman akisema kuhusu majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kwamba ametoa tuhuma nzito kwa Viongozi Waandamiziwa *CUF*, kwa mujibu wa maelezo yake anasema majibu aliyotoa ama tuhuma alizotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni za uwongo na hakuna ukweli wowote.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili Mheshimiwa Suleiman kwa sababu tupo pamoja na mambo mengine bado tupo katika kujifunza, jambo hili alilozungumza Mheshimiwa Suleiman na akasema hapa kwamba je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatoa ushahidi. Kwa sababu nimesema tupo katika kujifunza Mheshimiwa Suleiman Kanuni ya 63....

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo ili hizi Kanuni tusiwe tunarudia kila wakati. Kanuni ya 63(1), (2), (3) na (4) zinamtaka Mbunge anayesema kwamba mwingine anasema uwongo ndiye anayetakiwa kuthibitisha. Mbunge anayemwambia Mbunge mwingine kwamba anasema uwongo ndiye anayepaswa kuthibitisha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tupo katika kujifunza jambo hili, Mheshimiwa Dkt. Suleiman, Waziri hata leta hapa ndani huo ushahidi kwa sababu Kanuni hii

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

inakutaka wewe ndio ulete, lakini Kiti leo kitaamua siyo wewe ulete ila unapotaka kutoa hayo maelezo tutumie Kanuni mahsusili ili tuweze kwenda sawasawa. Kwa hivyo, ushauri wa jumla nimeshawapa upande wa Serikali na naamini watazingatia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo tunaendelea. Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

MHE. KHATIB SAID HAJI: Hoja ya kuahirisha Bunge kujadili jambo la dharura.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haji ulisimama kwenye miongozo nimekukatalia, kwa hiyo hata hilo unalosimama nalo sasa naamini unataka kufanya hilo ambalo ultaka kufanya mwanzo. Tafadhali naomba utulie tuendelee.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na jambo lililopo mbele yetu, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali na kupokea na kujadili, taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2017/2018.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutuwezesha sote kukutana leo kujadili maendeleo ya Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Napenda nimpongeze kwa namna ya kipekee, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa umahiri mkubwa na kudumisha umoja, amani, upendo na utulivu.

Mheshimiwa Rais, ameendelea kusimamia utekelezaji wa llani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2015 na kutekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi za Serikali kwa wananchi. Ama kwa hakika uongozi wake mahiri umekuwa dira sahihi katika kuleta mabadiliko ya kweli ambayo Watanzania wameyasubiri kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu, kwa jinsi ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais, kusimamia na kuiongoza shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu hili Tukufu kwa hekima na busara kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu mmoja tangu Bunge la Bajeti liliopita, Bunge lako Tukufu limepata pigo kubwa kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha, Mbunge wa Viti Maalum. Naomba kutoa salamu zangu za pole na kumwombwa Mwenyezi Mungu aendelee kutupa subira katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mheshimiwa Alhaji Abdallah Bulembo, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete na Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare kwa kuteuliwa kuwa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wabunge wa Bunge hili. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Juma Ally Juma kwa kuchaguliwa kwa kura nydingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King Mbunge wa Jimbo la Makete na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuongoza Wizara yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa hotuba yake iliyotoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na mwelekeo wa kazi za mwaka wa fedha 2017/2018.

Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao katika Bunge lako la Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi; katika mwaka wa fedha 2016/2017, sekta ya ujenzi ilitengewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 35.941 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hadi kufikia Machi mwaka huu shilingi bilioni 25.786 zilikuwa zimetolewa na Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, sekta ya ujenzi ilitengewa shilingi triliioni 2.176 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni shilingi triliioni 1.248 na shilingi bilioni 344.838 zilikuwa fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za Mfuko wa Barabara zilitengwa shilingi bilioni 582.644. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu fedha zilizotolewa ni shilingi trilioni 1.171. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 958.528 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 212.793 ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 555.215 za Mfuko wa Barabara. Kwa ujumla, kiasi kilichotolewa ni sawa na asilimia 53.8 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara na madaraja. Serikali imeendelea kutekeleza sera ya kuunganisha mikoa yote na nchi zote jirani kwa barabara za lami. Miradi ya barabara yenye jumla ya kilomita 987 na madaraja makubwa mawili imekamilika kujengwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2016/2017. Miradi hiyo iliyokamilika ni pamoja na ujenzi wa kiwango cha lami ya barabara ya Namtumbo - Kilimasera - Matemanga - Tunduru yenye urefu wa kilomita 187.9; Tunduru – Nakapanya - Mangaka yenye urefu wa kilometra 137.3 na Mangaka - Mtambaswala yenye urefu wa kilomita 65.5, hizi zote ni Ukanda wa Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ukanda wa Kaskazini miradi iliyokamilika ni ukarabati wa barabara ya Mkumbala - Same yenye urefu wa kilometra 96 na ujenzi wa barabara Dodoma - Babati, sehemu ya Dodoma - Mayamaya yenye urefu wa kilometra 43.65. Kwa upande wa Ukanda wa Kati Magharibi na Ukanda wa Ziwa, miradi iliyokamilika ni ujenzi wa barabara ya Mbeya - Lwanjilo - Chunya yenye urefu wa kilomita 72; barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi sehemu ya Bariadi - Lamadi yenye urefu wa kilomita 71.8; barabara ya Nzega - Puge yenye urefu wa kilomita 58.8; barabara ya Sitalike - Mpanda yenye urefu wa kilomita 36.9; barabara ya Tabora - Urambo - Ndono yenye urefu wa kilomita 94 na barabara ya Kyaka - Bugene - Kasulo sehemu ya Kyaka - Bugene yenye urefu wa kilomita 59.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ukanda wa Mashariki ujenzi wa barabara ya Bagamoyo - Msata yenye urefu wa kilomita 64 umekamilika kwa kiwango cha lami. Madaraja makubwa yaliyokamilika ni Daraja la Kilombero na Daraja la Ruvu Chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2016/2017, hadi kufikia mwezi Machi, 2017 kilomita 433 za barabara kuu zilikamilika kujengwa kwa kiwango cha lami katи ya lengo la kilomita 992. Aidha, ukarabati wa jumla ya kilomita jumla 77 katи ya lengo la kilomita 146.5 za barabara kuu za kiwango cha lami zilikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa matengenezo ya barabara, matengenezo ya barabara kuu na za mikoa yalihusisha matengenezo ya kawaida kilomita 22,839, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi kilomita 4,749 na matengenezo ya madaraja 2,821. Hadi kufikia Machi, 2017 kwa ujumla utekelezaji wa mpango wa matengenezo ya barabara ulikuwa umefika asilimia 67 ya malengo ya mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo katika barabara kuu jumla ya kilomita 5,895.31 zilifanyiwa matengenezo ya kawaida, kilomita 1,074.5 zilifanyiwa matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi na madaraja 998 yalifanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa barabara za mikoa jumla ya kilomita 12,746.9 zilifanyiwa matengenezo ya kawaida, kilomita 1,745.2 zilifanyiwa matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi na madaraja 1,032 yalifanyiwa matengenezo. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja katika mwaka wa fedha 2016/2017 yamo katika ukurasa wa 9 - 49 wa kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi zilizo chini ya sekta ya ujenzi. Maelezo kuhusu utendaji wa taasisi zilizo chini ya sekta ya ujenzi yameoneshwa kwa kina katika kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 49 - 67.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, sekta ya uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 2.587. Kati ya pesa hizo shilingi trilioni 2.495 ni fedha za maendeleo na shilingi bilioni 91.519 ni fedha za matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2017 fedha za miradi ya maendeleo shilingi bilioni 825.858 sawa na asilimia 33.1 zilikuwa zimetolewa na fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 58.739 sawa na asilimia 69.18 zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri kwa njia ya barabara. Wizara kuititia *SUMATRA* imeendelea kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma za uchukuzi mijini na vijijini kwa kufanya ukaguzi wa kushtukiza wa vyombo vyia usafiri, utoaji nauli elekezi, elimu na mafunzo na ushauri kwa watumiaji na watoaji wa huduma za usafiri wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam. Huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam zimeendelea kutolewa na *TAZARA* na *TRL*. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 idadi ya watumiaji wa usafiri wa treni katika Jiji la Dar es Salaam ilikuwa ni abiria 5,762,555 ikililinganishwa na abiria 1,771,188 waliosafiri katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hili ni ongezeko la asilimia 225. Maelezo zaidi kuhusu usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam yapo kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 73 - 74.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni Hodhi ya Rasilimali ya Reli (*RAHCO*), Kampuni ya Reli Tanzania na *TAZARA*. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, kazi za kuboresha, kujenga, kukarabati miundombinu ya reli na upembuzi yakinifu zimeendelea kutekelezwa na *RAHCO*, *TRL* na *TAZARA* kwa niaba ya Serikali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kusaini mkataba wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro. Mkataba huu ulisainiwa tarehe 3 Februari, 2017. Aidha, tarehe 12 Aprili, 2017, Rais wa Jamhuri ya Muungano

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wa Tanzania, Mheshimiwa Dk John Pombe Joseph Magufuli aliweka jiwe la msingi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli hiyo.

(ii) Zabuni ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Morogoro - Makutopora zimefunguliwa na sasa *evaluation* inafanyika.

(iii) Zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Makutopora - Tabora, Tabora - Isaka, Isaka - Mwanza zitafunguliwa mwisho wa mwezi huu.

(iv) Kwa upande wa *TAZARA* matengenezo makubwa ya njia ya reli yamefanyika ili kupunguza maeneo korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu kazi zilizotekelizwa na *RAHCO*, *TRL* na *TAZARA* yapo katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 74 - 79.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri na uchukuzi majini. Huduma za uchukuzi katika Ziwa. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilitenga fedha shilingi bilioni 50.5 kwa ajili ya kununua meli moja katika Ziwa Victoria na kukarabati meli tatu. Kuhusu ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria, taratibu za kumpata mkandarasi zinatarajiwaa kukamilika Mei mwaka huu. Kuhusu mradi wa ukarabati wa *MVLiemba* mkandarasi amepatikana na kazi hii inatarajiwaa kuanza Mei, 2017. Maelezo zaidi kuhusu kazi zilizotekelizwa yapo katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 81 - 83.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za bandari. Katika mwaka wa fedha 2016/2016, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi za huduma za bandari katika miji ya Lubumbashi huko Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Lusaka huko Zambia, Kigali huko Rwanda na Bujumbura huko Burundi; kuanzisha Wakala wa Mamlaka huko Kampala (Uganda); kuimarisha usalama wa mizigo bandarini na kutoa huduma za bandari kwa saa 24 kwa siku na siku saba kwa wiki.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya kuboresha utendaji wa bandari za mwambao na maziwa makuu iliyotekelizwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukamilika kwa jengo la ghorofa 35 la kuwaweka pamoja watoa huduma muhimu wanaotoa huduma katika bandari ya Dar es Salaam yaani *One Stop Center*. Jengo hilo lilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Mheshimiwa Joseph Kabila tarehe 4 Oktoba, 2016.

(ii) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa uboreshaji wa bandari ya Dar es Salaam. Kazi hiyo ilikamilika Machi, 2017. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza Juni, 2017.

(iii) Ujenzi wa gati la Kagunga katika Ziwa Tanganyika ulikamilika Januari, 2017.

(iv) Ujenzi wa gati la Ntama katika Ziwa Victoria ulikamilika Agosti, 2016.

(v) Ujenzi wa gati la Lushamba ulikamilika Julai, 2016.

(vi) Ujenzi wa meli yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo katika Ziwa Nyasa ulianza Juni, 2016 na unatarajiwa kukamilika Agosti, 2017.

(vii) Ukarabati wa gati la Lindi umekamilika kwa asilimia 50. Kazi inatarajiwa kukamilika yote ifikapo Agosti, 2017.

(viii) Ujenzi wa gati la Pangani umekamilika Septemba, 2016 na kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Karema (Kigoma) ili kuunganishwa na bandari ya Kalemia (DRC) inaendelea. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza Septemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na maandalizi ya msingi ya ujenzi wa bandari ya Mbegani (Bagamoyo). Kwa sasa majadiliano na kampuni ya *China Merchants Port Limited* kuhusu vipengele vya mkataba yanakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa bandari ya Mwambani (Tanga), *TPA* inaendelea na maandalizi ya makabrasha kwa ajili ya marejeo ya upembuzi yakinifu na zabuni hiyo inatarajiwa kutangazwa kabla ya Juni, 2017. Aidha, maandalizi kwa ajili ya kujenga gati la Chongoleani (Tanga) kwa ajili ya kupokelea mafuta kutoka Uganda yanaendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upanuzi wa bandari ya Mtwara, awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa gati moja ambapo kampuni ya *China Railway Construction Company* ilisaini mkataba wa ujenzi tarehe 4 Machi, 2017. Gati hilo lenye urefu wa mita 350 ni kwa ajili ya kuhudumia shehena mchanganyiko. Ujenzi wa gati hili utakamilika ndani ya miezi 21. Maelezo zaidi kuhusu miradi na huduma za bandari yapo katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 83 - 94.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri na uchukuzi kwa njia ya anga. Udhibiti wa usafiri wa anga. Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCCAA*) iko katika hatua ya mwisho ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya ununuzi wa rada nne kwa ajili ya viwanja vya ndege vya *JNIA*, Mwanza, *KIA* na *SONGWE*. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2017, Tanzania imeingia mikataba na *BASA* na jumla ya nchi 68 ikilinganishwa na nchi 60 zilizokuwa zimesaini makubaliano hayo mwaka 2015/2016. Maelezo zaidi kuhusu udhibiti wa usafiri wa anga yapo katika kitabu changu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 94 - 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za viwanja vya ndege. Wizara kupitia Mamlaka za Viwanja vya Ndege inaendelea kuboresha miundombinu na huduma za viwanja vya ndege nchini ili kuwezesha ndege kubwa na ndogo kutua na kuruka kwa usalama. Miradi iliyotekelawa ni pamoja na:-

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(i) Ujenzi wa jengo la abiria (*Terminal III*) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere unaendelea kutekelezwa na unatarajiwu kukamilika Desemba, 2017. Kukamilika kwa jengo hilo kutaongeza uwezo wa kiwanja kuhudumia abiria hadi kufikia milioni nane na nusu kwa mwaka kutoka kiwango cha sasa cha milioni mbili na nusu.

(ii) Ukarabati wa Kiwanja cha *KIA* umekamilika kwa asilimia 70 na ujenzi unatarajiwu kukamilika Mei, 2017.

(iii) Kukamilika kwa kazi ya kurefusha barabara za kurukia na kutua ndege kwa mita 500 katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, ujenzi wa jengo la mizigo na maegesho ya ndege.

(iv) Awamu ya pili ya ukarabati na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora ambao unaendelea. Kazi za ukarabati wa kiwanja hiki zilianza Septemba, 2017 na zinatarajiwu kukamilika Juni, 2017.

(v) Kukamilika kwa ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba na kuanza kutumika. Aidha, ujenzi wa shule ya msingi kwa ajili ya kupisha mradi huu umekamilika mwezi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu huduma za viwanja vya ndege yapo katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 100 - 103.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za usafiri wa anga. Huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Ndege ya Tanzania (*ATCL*) pamoja na kampuni za sekta binafsi. Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kufufua na kuboresha huduma za Kampuni ya Ndege Tanzania ili kusaidia kukuza sekta nyingine za kiuchumi ikiwa ni pamoja na utalii, biashara, madini na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali iliingia mikataba ya ununuzi wa ndege sita, ndege mbili aina ya *Bombardier Dash 8 – Q400* zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja ziliwasili Septemba, 2016 na Oktoba, 2016 ndege hizo zilianza kazi na sisi sote tumefurahia usafiri huo. Ndege moja aina ya *Bombardier Dash 8 – Q400* itawasili nchini Julai, 2017. Ndege mbili aina ya *Bombardier CS 300* zenye uwezo wa kubeba abiria 127 kila moja zitawasili nchini Juni, 2018 na ndege moja ya masafa marefu ya aina ya *Boeing 787 Dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262 itawasili nchini mwaka 2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu huduma za usafiri wa anga yapo katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 104 - 106.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mawasiliano. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Aprili, 2017, Wizara iliweza kukusanya kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 6.577 sawa na Shilingi bilioni 14.260 kutokana na mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo fedha hizo ni maalum kwa ajili ya urejeshaji wa deni la ujenzi wa mradi huo kwa Benki ya EXIM ya China na pia kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa mkongo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa kiasi cha Shilingi bilioni 3.073 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2017, Shilingi bilioni 2.262 zilikuwa zimetolewa na Hazina. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 92.73 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni Shilingi bilioni tano na fedha shilingi bilioni 87.73 zilikuwa fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2017 fedha zilizotolewa ni Shilingi bilioni 37.295.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Sekta ya mawasiliano inaratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa

Taifa wa Mawasiliano nchini ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ilifika Awamu ya III sehemu ya kwanza na Awamu ya IV ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya III sehemu ya kwanza ilihusisha uunganishaji wa Zanzibar kwenye Mkongo wa Taifa wa mawasiliano; ujenzi wa mtandao wa miundombinu ya Itifaki yaani *Internet Protocol Multilayer Label Switching* na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (*National Internet Data Centre*). Awamu hiyo ilikamilika Julai, 2016 na kuanza kufanya kazi ya kutoa huduma. Hadi sasa kuna wateja 27 ambao wameanza kutumia kituo hicho. Awamu ya IV ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa ni Mikongo ya Mijini (*Metro Networks*) unatekelezwa kwa kushirikiana kati ya Serikali na watoa huduma wa mawasiliano yaani Kampuni za *Tigo, Airtel* na *Zantel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudzi za Serikali kufikisha huduma za mawasiliano vijiji. Sekta ya Mawasiliano kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano katika mwaka wa fedha 2016/2017, imeendelea na ufikishaji wa huduma za mawasiliano vijiji ambapo kwa sasa jumla ya kata 382 kati ya kata 443 zenyet vijiji 1,825 na wakazi 2,891,731 zimekwishapata huduma za mawasiliano. Serikali inawahimiza watoa huduma wote ambao hawajakamilisha miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijiji kufanya hivyo mara moja bila kuchelewa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Miundombinu ya TEHAMA ya Kikanda. Sekta ya mawasiliano inatekeleza Programu ya Miundombinu ya TEHEMA ya Kikanda kwa kutumia fedha za nje. Miradi inayotekelizwa ni pamoja na mradi wa Shule Mtandao yaani *E-school*/unaohusisha ununuzi, usimikaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA katika shule 80 za sekondari na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu walioeteuliwa kwa kazi hiyo katika shule hizo. Pia mradi wa *Video Conference* unaohusisha ununuzi, ufungaji na usimikaji wa mitambo *Video Conference* katika Makao Makuu ya Mikoa 26 na baadhi ya taasisi za Serikali unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, program nyingine za *RCIP* zinatekelezwa kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali. Utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya sekta ya mawasiliano yaani *UCSAF*, *TCRA Posta*, *TTCL* na Tume ya TEHAMA umeoneshwa kwa kina kwenye ukurasa wa 117 - 125 wa kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango na makadirio ya mapato ya matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018. Sekta ya Ujenzi, bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara - Fungu 98, Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni shilingi bilioni 34.123. Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya shilingi triliioni 1.895 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi triliioni 1.350 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 545.582 ni fedha za nje. Aidha, kati ya fedha za ndani shilingi bilioni 642.284 ni fedha zilitengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara. Mgawanyo huo umeoneshwa kwenye kiambatanisho Na.3 ukurasa 214 - 250 katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu miradi ya maendeleo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya barabara na madaraja. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi triliioni 1.052 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kuu, zenye urefu wa kilomita 720 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja 13 pamoja na ukarabati wa kilomita 150 kwa kiwango cha lami. Aidha, shilingi bilioni 30 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara za mikoa zenye urefu wa kilomita 58.4 na madaraja 12 pamoja na ukarabati wa kiwango cha changarawe wa kilomita 469.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya miradi ya barabara kuu inayoendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami itakayotekeliza katika mwaka wa fedha 2017/2018 itahusisha barabara ya Mayamaya – Mela – Bonga, yenye urefu wa kilomita 188.2; Sumbawanga – Matai - Kasanga Port yenye urefu wa kilomita 112; Sumbawanga - Kanazi yenye

urefu wa kilomita 75, Kanazi – Kizi - Kibaoni yenze urefu wa kilomita 76.6; Kidahwe - Kasulu yenze urefu wa kilomita 50; Kibondo - Nyakanazi yenze urefu wa kilomita 50; Mafinga - Igawa yenze urefu wa kilomita 137.9; Arusha - Tengeru pamoja na barabara mchepuo ya Arusha yenze urefu wa kilomita 56.5; Makutano – Natta - Mugumu yenze urefu wa kilomita 50; Mwigumbi – Maswa yenze urefu wa kilomita 50; Bulamba - Kisorya yenze urefu wa kilomita 51; Sanya Juu - Alerai yenze urefu wa kilomita 32; Mtwara - Mnivata yenze urefu wa kilomita 50 na Mpanda - Ifukutwa - Vikonge yenze urefu wa kilomita 35. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha zege wa barabara ya Itoni - Ludewa - Manda sehemu ya Lusitu - Mawengi yenze urefu wa kilomita 50 utaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaanza pia utekelezaji wa miradi mingine ya barabara na madaraja ambayo inajumuisha barabara ya Tabora - Koga -Mpanda yenze urefu wa kilomita 343; Mbinga - Mbamba-Bay yenze urefu wa kilomita 66; Masasi - Nachingwea - Nanganga yenze urefu wa kilomita 61; Chaya - Nyahua yenze urefu wa kilomita 85.4; Uvinza - Malagalasi yenze urefu wa kilomita 51.1; Njombe - Ndulamo - Makete yenze urefu wa kilomita 109; Mto wa Mbu - Loliondo sehemu ya Waso - Sale yenze urefu wa kilomita 49; Natta - Mugumu yenze urefu wa kilomita 41.6; Urambo - Kaliua yenze urefu wa kilomita 28; Kidatu - Ifakara yenze urefu wa kilomita 68 na Kibaoni - Sitalike yenze urefu wa kilomita 71.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ni barabara ya Nyamuswa - Bunda - Bulamba yenze urefu wa kilomita 55; Mpemba - Isongole yenze urefu wa kilomita 51.2; Rujewa - Madibila - Mafinga yenze urefu wa kilomita 152; Njombe – Lupembe - Madeke yenze urefu wa kilomita 125, Chunya - Makongorosi yenze urefu wa kilomita 43; Makongorosi - Rungwa - Itigi - Mkiwa sehemu ya Noranga – Itigi - Mkiwa yenze urefu wa kilomita 56.9 na Maswa - Bariadi yenze urefu wa kilomita 49.7. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali itaanza ujenzi wa madaraja mapya ya Wami huko Mkoa wa Pwani, Selander huko Dar es Salaam, Magara huko Mkoa wa Manyara, ukarabati wa daraja la

Kirumi huko Mkoa wa Mara pamoja na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja la Simiyu, daraja la Kigongo/Busisi huko Mwanza na daraja la Mtera hapa Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara itaendelea na ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya *TAZARA* pamoja na ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam - Chalinze kwa kiwango cha *expressway*. Aidha, kufuatia kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (*BRT*), Serikali itaanza ujenzi wa awamu zinazofuata za miundombinu ya *BRT*. Katika awamu ya pili ujenzi utahusisha barabara ya Kilwa, Kawawa na Chang'ombe zenye urefu wa kilomita 20.3 na ujenzi wa *flyovers* katika makutano ya Chang'ombe na Uhasibu chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa usafiri katika Jiji la Dar es Salaam. Mradi huu utahusisha ujenzi wa barabara za juu (*interchange*) kwenye makutano ya Ubungo; ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (*BRT*) Awamu ya III na Awamu ya IV. Awamu ya III itahusisha barabara za Azikiwe, Bibi Titi, Uhuru na Nyerere zenye urefu wa kilomita 23.6 kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto. Awamu ya IV itahusisha barabara za Ali Hassan Mwinyi, Samu Nujoma na Bagamoyo kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Tegeta.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu miradi ya barabara na madaraja itakayotekelozwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 yameoneshwa katika ukurasa 146 – 166 katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti. Aidha, orodha ya miradi ya barabara za mikoa itakayotekelozwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika kiambatisho Na.2 ukurasa 251 – 271.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya viwanja vyta ndege. Katika mwaka wa fedha 2017/2018,

Wizara imepanga kujenga na kukarabati miundombinu ya viwanja vya ndege nchini, ambapo jumla ya shilingi bilioni 176.368 zimetengwa. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali itaendelea na ujenzi wa Jengo la III la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza, ukarabati wa Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Geita. Aidha, Serikali itaanza upanuzi wa ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya Tabora, Kigoma, Sumbawanga na Shinyanga. Vilevile Serikali itaanza ukarabati na ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya Mtwara, Musoma, Iringa na Songea. Maelezo ya kina kuhusu kazi zitakazofanyika yapo katika ukurasa wa 168 – 174 wa kitabu cha hotuba ya bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mfuko wa Barabara. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mfuko wa Barabara unatarajiwu kukusanya jumla ya shilingi bilioni 917.548 zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabaranchini. Kati ya fedha hizo, sekta ya ujenzi na taasisi zake imetengewa shilingi bilioni 642.284 na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetengewa shilingi bilioni 275.264.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya shilingi bilioni 642.284 zilizotengwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, imetengwa shilingi bilioni 66.676 kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara na ukarabati na ununuzi wa vivuko. Mchanganuo wa miradi hiyo imeoneshwa katika kiambatanisho Na.3 kuanzia ukurasa 272 – 282 wa kitabu cha hotuba ya bajeti. Aidha, miradi ya barabara mikoa itakayoteklezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, imeoneshwa katika kiambatanisho Na.4 ukurasa 283 – 298 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Barabara umetengewa shilingi bilioni 573.084 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa. Muhtasari na

maelezo ya kina ya mpango wa matengenezo ya barabara na madaraja kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara yapo katika viambatanisho Na.5(A - E) ukurasa 299 – 280 katika kitabu cha hotuba ya bajeti. Maelezo ya kina kuhusu mpango wa utekelezaji kazi katika taasisi hizo chini ya sekta ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2017/2018 yametolewa katika hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 177 – 182.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi. Makadirio ya matumizi ya kawaida na bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2017/2018. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Sekta ya Uchukuzi ni bilioni 91.142. Aidha, sekta ya uchukuzi imetengewa jumla ya shilingi trillioni 2.477 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa kwenye kiambatanisho Na.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu miradi ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Uchukuzi imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Dodoma kwa kiwango cha *standard gauge* ambapo shilingi bilioni 900 zimetengwa.

(ii) Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa njia ya reli kati ya Mtwara na Mbamba-Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga ambapo shilingi bilioni mbili zimetengwa. Shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli kati ya Arusha na Musoma.

(iii) Kukarabati njia ya reli kutoka Dar es Salaam – Isaka. Kazi hizi zinaghari miwa na Benki ya Dunia ambapo shilingi bilioni 200 zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga shilingi bilioni

24.496 kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo. Kuhusu miradi ya miundombinu ya bandari, Serikali kuititia *TPA* imetenga shilingi bilioni 487.281 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kampuni ya Ndege ya Tanzania (*ATCL*) imetengewa shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege tatu, ambapo ndege mbili ni za aina ya *CS 300* na ndege kubwa moja ya masafa marefu ya aina *Boeing 787-8 Dreamliner*. Fedha hizo pia zitatumika kwa ajili ya gharama ya bima, mafunzo ya Marubani Wahandisi na Wahudumu, gharama za kuanzia (*start up cost*) pamoja na malipo ya awali ya ndege nyingine mpya ya *Boeing 787 Dreamliner*. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kufanya matengenezo ndege nne za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Uchukuzi kuititia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetengewa shilingi bilioni tano kwa ajili ya ununuzi na usimikaji wa vifaa vya usalama viwanjani. Aidha, Mamlaka ya Hali ya Hewa imetengewa shilingi bilioni 6.2 kwa ajili ya ununzi wa rada na vifaa vya hali ya hewa na *TCAA* itagharamia ununuzi na ufungaji wa rada nne za kuongozea ndege za kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea kuboresha miundombinu ya Mamlaka ya reli Tanzania na Zambia jumla ya shilingi bilioni 26 zimetengwa. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha huduma zinazotolewa na Kampuni ya Reli Tanzania (*TRL*) ambapo shilingi bilioni 30.8 zimetengwa. Kazi zitakazotekelawa na *TRL* na *TAZARA* zimeoneshwa kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 195 – 196. Mgawanyo wa fedha za bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa miradi ya Sekta ya Uchukuzi umeoneshwa katika kiambatanisho Na. 6 cha kitabu cha hotuba ya bajeti.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mawasiliano - Fungu 68. Jumla ya shilingi bilioni 18.104 za Sekta ya Mawasiliano zinajumuisha shilingi bilioni 4.104 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 2.267 ni za mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 1.837 ni za matumizi mengineyo. Shilingi bilioni 14 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani. Sekta ya Mawasiliano imepanga kutekeleza mpango wa muda wa kati na muda mrefu na utatilia mkazo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la TEHAMA:-

(i) Utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano na kufikisha huduma zake katika Makao Makuu ya Wilaya zote nchini na ujenzi wa vituo viwili va kutunza *data* yaani *data centre* hapa Dodoma na Zanzibar;

(ii) Ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano na mitandao yaani *Public Key Infrastructure – PKI*;

(iii) Kuratibu matumizi ya huduma za TEHEMA nchini;

(iv) Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa Kitaifa wa usalama mitandao; na

(v) Kusimamia uanzishwaji wa mkakati wa mtandao wa TEHAMA wenye kasi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mawasiliano.

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016;

(ii) Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 na mpango mkakati wake wa utekelezaji;

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(iii) Kukamilisha mpango mkakati wa utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA nchini na kusimamia utekelezaji wake; na

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa mpango wa anuani za makazi na misimbo ya posta katika Miji Mikuu ya mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa utekelezaji kazi katika taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018, umeainishwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu kuanzia ukurasa 198 – 205.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Napenda kuwashukuru sana viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mheshimiwa Injinia Edwin Ngonyani, Naibu Waziri; Mhandisi Joseph Nyamhanga, Katibu Mkuu Sekta ya Ujenzi; Mhandisi Dkt. Leonard Chamuriho, Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi; Mhandisi Dkt. Maria Sasabo, Katibu Mkuu Mawasiliano; Mhandisi Anjelina Madete, Naibu Katibu Mkuu Mawasiliano, Wakuu wa Vitengo, Idara mbalimbali, Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara, Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Naomba kuwaambia kwamba sitawaangusha na nawashukuru sana kwa kazi kubwa wanayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru washirika mbalimbali wa maendeleo ambao wametoa michango yao kwa namna moja au nyiningine katika kuendeleza Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hapa nchini. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, *JICA* ya Japan, *KOICA* ya Korea Kusini, Abu Dhabi *Fund*, Ujerumani *KfW*, Uingereza *DFID*, Uhlanzi *ORIO*, Jumuia ya Nchi za Ulaya (*EU*), Benki ya Utekelezaji ya Ulaya (*EIB*), Shirika la Maendeleo ya Marekani (*USAID*), KUWAIT *Fund*, Uturuki, *OPEC Fund*, BADEA, HSBC TMEA, Sekretarieti ya Jumuia ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuia ya SADC, CRDB, TIB, Asasi Zisizo za Kiserikali pamoja na sekta binafsi. (*Makofii*)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, muhtasari wa maombi ya fedha ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika mwaka wa Fedha 2017/2018. Katika mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 4,516,885,061,000. Kati ya fedha hizo Sh.1,929,705,714,000 ni kwa ajili ya Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi; Sh.2,569,073,208,000 ni kwa ajili ya Fungu 62 - Sekta ya Uchukuzi; na Sh.18,104,139,000 ni kwa ajili ya Fungu 68 - Sekta ya Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zilizoombwu umeoneshwa kwa kina katika kitabu cha hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu kuanzia ukurasa wa 212 - 213.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha miradi ya Wizara itakayotekelawa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuanzia kiambatanisho Na.1-7 ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengewa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatanisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda nitoe shukrani zangu tena za dhati kwako wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba yangu inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni www.mc.tc.go.tz na kupitia kwenye *blog* ambayo ni wizarauumtanzania.blogspot.com.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makof)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, ahsante Mheshimiwa Waziri.

**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO MHESHIMIWA PROF. MAKAME M. MBARAWA
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWAMWAKA WA FEDHA
2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuweka mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

2. *Mheshimiwa Spika*, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutuwezesha sote kukutana tena leo kujadili maendeleo ya sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

3. *Mheshimiwa Spika*, kipekee naomba kuwapongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Raís wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza vema nchi yetu.

4. *Mheshimiwa Spika*, napenda nimpongeze kwa namna ya pekee Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa umahiri mkubwa na kudumisha umoja, amani na utulivu. Mheshimiwa Rais ameendelea kusimamia utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na kutekeleza kwa kiwango kikubwa

ahadi za Serikali kwa wananchi. Ama kwa hakika uongozi wake mahiri umekuwa dira sahihi katika kuleta **mabadiliko ya kweli** ambayo Watanzania wameyasubiri kwa muda mrefu. Hili limejidhihirisha kipekee katika Wizara ninayoiongoza ambapo kwa kipindi kifupi, kumekuwa na mabadiliko makubwa na ya kujivunia, hususan kuanza kwa ujenzi wa barabara za juu katika maeneo ya TAZARA na Ubungo, kufanikiwa kufufua Shirika la Ndege (ATC) na kuweka mkazo katika kufufua reli ya Kati ili itumiwe kwa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kiwango cha kisasa (standard gauge) na hivyo kuokoa barabara zetu. Aidha, napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumsaidia na kumshauri Rais kwa hekima katika utekelezaji wa majukumu mazito aliyonayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema, hekima na busara ili waendelee kuliongoza Taifa letu kwa amani na utulivu.

5. *Mheshimiwa Spika*, naomba pia kumpongeza Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), kwa kuendelea kuongoza vema shughuli za Serikali bungeni na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, nikupongeze wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa hekima na busara. Uongozi wako umewezesha Bunge kutimiza kikamilifu jukumu lake la kusimamia na kuishauri Serikali.

6. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka huu mmoja tangu Bunge la Bajeti liliopita, Bunge lako Tukufu limepata pigo kubwa kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mhe. Hafidh Ally Tahir, Mbunge wa Dimani na Mhe. Dkt. Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalum. Naomba kutoa salamu zangu za pole na kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutupa sote moyo wa subira. Aidha, natoa pole kwa wananchi wote waliojeruhiwa na waliopoteza ndugu, marafiki na mali kutokana na ajali zitokanazo na vyombo vyaa usafirishaji. Wizara inaahidi kuendelea kuboresha udhibiti na usimamizi wa shughuli na huduma za usafirishaji ili kupunguza ajali hizo.

7. *Mheshimiwa Spika*, ninapenda pia kuwapongeza Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mhe. Anne Killango Malecela, Mhe. Alhaj Abdallah Majura Bulembo, Mhe. Salma Rashid Kikwete na Mhe. Mch. Dkt. Getrude Rwakatare kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili. Aidha, nimpongeze Mhe. Juma Ali Juma kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani. Vilevile, nawapongeza Wabunge wateule wa Bunge la Afrika Mashariki kwa ushindi wao. Nawatachia wote kila la kheri katika majukumu yao mapya katika kuwatumikia wananchi.

8. *Mheshimiwa Spika*, sina budi kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mbunge wa Jimbo la Makete na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijiini kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza Wizara yangu. Ushauri na maelekezo yao mazuri yaliwezesha Wizara kusahihisha dosari mbalimbali na kuboresha utendaji wake.

9. *Mheshimiwa Spika*, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango (Mb) kwa hotuba zao zilizotoa mwelekeo wa jumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018. Hotuba hizo pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge zimesaidia katika kuandaa mawasilisho yangu.

B. MAJUKUMU YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

10. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

11. *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya msingi ya Sekta ya Ujenzi ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ujenzi (2003) pamoja na Sera ya Taifa ya Usalama Barabaran (2009); ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege; ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali; usimamizi wa masuala ya ufundi na umeme; usimamizi wa shughuli za ukandarasi, uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi; usimamizi wa maabara na vifaa vya ujenzi; usimamizi wa masuala ya mazingira katika Sekta; uboreshaji, utendaji na uendelezaji wa watumishi wa Sekta na usimamizi wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Sekta.

12. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Uchukuzi ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya reli na bandari; usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga, reli na bandari; utoaji wa leseni za usafirishaji; usalama katika usafirishaji; usimamizi wa huduma za hali ya hewa; kuendeleza rasilimali watu na kusimamia Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Sekta ya Uchukuzi.

13. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Sekta ya Mawasiliano, majukumu yake ni pamoja na kusimamia Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003; Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997; na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2016 na utekelezaji wake. Aidha, Sekta ya Mawasiliano ina dhamana ya kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vinachangia katika maendeleo ya nchi yetu, pamoja na usimamizi wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano.

14. *Mheshimiwa Spika*, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Mpango na Bajeti ya Wizara

hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kila sekta kwa mtiririko wa Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Uchukuzi na hatimaye Sekta ya Mawasiliano.

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA 2016/2017

15. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021), Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka wa 2015, Malengo Endelevu ya Maendeleo, Ahadi na Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Sera nyinginezo za Kisekta, Kitifa na Kimataifa.

C.1 UTENDAJI WA SEKTA ZILIZO CHINI YA WIZARA KATIKA MWAKA 2016/2017

**C.1.1 SEKTA YA UJENZI
Ukusanyaji wa Mapato**

16. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Ujenzi ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 58,004,000** kuititia Idara na Vitengo vyenye vyanzo vya mapato. Idara hizo ni Utawala na Rasilimali Watu, Huduma za Ufundu na Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi. Hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya **Shilingi 30,820,000** ziliikuwa zimekusanywa.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

17. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Ujenzi ilitengewa kiasi cha **Shilingi 35,941,266,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 34,287,474,500** ni Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 1,653,791,500** ni Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi 25,786,058,298.19** ziliikuwa zimetolewa na HAZINA. Kati ya fedha hizo, **Shilingi**

24,244,612,600 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 1,541,445,698.19** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Bajeti ya Maendeleo

18. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 2,176,204,557,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 1,248,721,422,000** na **Shilingi 344,838,635,000** zilikuwa fedha za nje. Kwa upande wa fedha za Mfuko wa Barabara zilitengewa **Shilingi 582,644,500,000**.

Hadi Aprili, 2017 fedha zilizotolewa ni **Shilingi 1,171,321,144,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 958,528,028,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 212,793,116,000** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizotolewa zinajumuisha **Shilingi 455,215,636,000** za Mfuko wa Barabara. Kwa ujumla, kiasi kilichotolewa ni sawa na asilimia 53.8 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Utekelezaji wa Miradi ya Barabara na Madaraja

19. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza sera ya kuunganisha mikoa yote na nchi zote jirani kwa barabara za lami. Miradi ya barabara yenye jumla ya takriban kilometra 987 na madaraja makubwa mawili ilikamilika kujengwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2016/2017. Miradi hiyo iliyokamilika ni pamoja na ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Namtumbo – Kilimasera – Matemanga - Tunduru (km 187.9); Tunduru – Nakapanya – Mangaka (km 137.3) na Mangaka – Mtambaswala (km 65.5) katika Ukanda wa Kusini. Kwa upande wa Ukanda wa Kaskazini, miradi iliyokamika ni ukarabati wa barabara ya Mkumbara – Same (km 96) na ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati (sehemu ya Dodoma – Mayamaya - km 43.65). Kwa upande wa Ukanda wa Kati na Magharibi miradi iliyokamilika ni ujenzi wa barabara ya

Mbeya – Lwanjilo – Chunya (km 72), barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (sehemu ya Bariadi – Lamadi - km 71.8), barabara ya Nzega – Puge (km 58.8), barabara ya Sitalike – Mpanda (km 36.9), barabara ya Tabora– Urambo - Ndono (km 94) na barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (sehemu ya Kyaka - Bugene (km 59.1). Kwa upande wa Ukanda wa Mashariki, ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Msata (km 64) umekamilika kwa kiwango cha lami. Madaraja makubwa yaliyokamilika ni Daraja la Kilombero na Daraja la Ruvu Chini.

20. *Mheshimiwa Spika*, baadhi ya miradi ya barabara kuu inayoendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami inahusisha barabara za Mayamaya – Mela – Bonga (km 188.2), Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112), Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Kidahwe- Kasulu (km 50), Kibondo – Nyakanazi (km 50), Mafinga – Igawa (137.9), Arusha – Tengeru pamoja na barabara ya mchepuo ya Arusha (km 56.5), Makutano – Natta – Mugumu (km 50), Mwigumbi – Maswa (km 50), Bulamba – Kisorya (km 51), Sanya Juu – Alerai (km 32), Mtwara – Mnivata (km 50) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 35). Aidha, ujenzi kwa kiwango cha zege wa barabara ya Itoni- Ludewa – Manda sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) unaendelea.

21. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017 ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya TAZARA uliendelea ambapo ujenzi umefikia asilimia 32, maandalizi kwa ajili ya kuitisha zabuni za ujenzi wa Daraja Jipya la Selander na ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze kwa kiwango cha Expressway yaliyendelea. Aidha, kufuatia kukamilika kwa Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT). Serikali imeanza maandalizi ya Awamu ya Pili ya ujenzi wa miundombinu ya BRT itakayohusisha barabara za Kilwa, Kawawa na Chang'ombe zenyе urefu wa kilometra 20.3 na ujenzi wa *flyovers* katika makutano ya Chang'ombe na Uhasibu chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Vilevile, tarehe 20 Machi, 2017 Serikali iltililiana saini na

Benki ya Dunia mkataba wa mkopo wa kugharamia mradi wa uboreshaji wa usafiri katika Jiji la Dar es Salaam (*Dares Salaam Urban Transport Improvement Project*). Mradi huo utahusisha ujenzi wa barabara za juu (*Interchange*) kwenye makutano ya Ubungo, ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne. Awamu ya Tatu itahusisha barabara za Azikiwe, Bibi Titi, Uhuru na Nyerere zenyе urefu wa kilometra 23.6 kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto. Awamu ya Nne itahusisha barabara za Ali Hassan Mwinyi, Sam Nujoma na Bagamoyo kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Tegeta.

22. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuititia Wakala wa Barabara (TANROADS) ilipanga kusimamia kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya mtandao wa barabara kuu na za mikoa wenye urefu wa **kilometra 35,000**. Hadi kufikia Machi, 2017, **kilometra 433** za barabara kuu zilikamilika kujengwa kwa kiwango cha lami, sawa na **asilimia 72** ya lengo la **kilometra 592** kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, ukarabati wa jumla ya **kilometra 77** za barabara kuu kwa kiwango cha lami ulikuwa umekamilika ni sawa na **asilimia 52.56** ya lengo la **kilometra 146.5** kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa upande wa barabara za mikoa, jumla ya **kilometra 45.52** zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami, sawa na **asilimia 45.2** ya lengo la **kilometra 100.7** kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Vilevile, jumla ya **kilometra 520.2** za barabara za mikoa zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe ukilinganisha na malengo ya **kilometra 1,296.70** ya mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, Serikali imeendelea na ujenzi wa madaraja makubwa **14** ambapo madaraja ya Kilombero na Ruvu Chini yamekamilika pamoja na ukarabati wa **madaraja 29**.

23. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa matengenezo ya barabara, matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa yalihusisha matengenezo ya kawaida (*routine and recurrent maintenance*) **kilometra 22,839**,

matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi **kilometa 4,749** na matengenezo ya madaraja **2,821**. Hadi kufikia Machi, 2017, katika barabara kuu, jumla ya **kilometa 5,895.31** zilifanyiwa matengenezo ya kawaida, **kilometa 1,074.5** zilifanyiwa matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi na madaraja **998** yalifanyiwa matengenezo. Kwa upande wa barabara za mikoa, jumla ya **kilometa 12,746.90** zilifanyiwa matengenezo ya kawaida, **kilometa 1,745.2** zilifanyiwa matengenezo ya mudamaalumnasehemukorofinadaraja **1,032** yalifanyiwa matengenezo. Kwa ujumla, utekelezaji wa mpango wa matengenezo ya barabara ulikuwa umefikia **asilimia 67** ya malengo ya mwaka wa fedha 2016/2017.

24. *Mheshimiwa Spika*, kazi ya kudhibiti uzito wa magari katika mwaka wa fedha 2016/2017 iliendelea kwa kutumia mizani **39** ya kudumu na **22** inayohamishika katika barabara kuu za lami. Hadi Machi, 2017 magari 2,602,400 yalipimwa ambapo kati ya hayo 684,952, sawa na asilimia 30.84, yaliikuwa yamezidisha uzito. Jumla ya fedha iliyokusanya kutokana na tozo ya uharibifu wa barabara na malipo ya kuitisha mizigo mipana na isiyo ya kawaida hadi Machi, 2017 ilikuwa ni **Shilingi 4,107,740,624.00**.

25. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200)** sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 144) kwa kiwango cha "Expressway" utatekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi "*Public Private Partnership (PPP)*". Aidha mradi huu unahusisha ukarabati (overlay) kwa kiwango cha lami sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44). Hadi kufikia Machi, 2017, Mtaalam Mwelekezi (Transaction Advisor) alikuwa amewasilisha taarifa ya mwisho ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali pamoja na nyaraka za zabuni kulingana na taratibu za miradi ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership*). Taratibu za kutangaza zabuni ili kumpata mbia (*Concessionnaire*) zinaendelea. Aidha, kilometa mbili (2) za sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44) ziliikuwa zimekarabatiwa.

26. Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa **barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Makofia – Msata (km 107)** kwa sehemu ya Bagamoyo – Msata (km 64) zimekamilika. Aidha, ujenzi wa Daraja la Ruvu Chini pamoja na tuta la barabara lenye urefu wa kilometra 4.16 umekamilika.

Kazi ya usanifu wa kina wa barabara ya **Bagamoyo-Saadani – Tanga (km 178)** imekamilika. Taratibu za kupata fedha za ujenzi kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mashirika mengine ya fedha duniani zinaendelea chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

27. Mheshimiwa Spika, mradi wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya **Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa** (km 422) umegawanywa katika awamu tatu na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

i. Kyamyorwa – Buzirayombo (km 120)

Kazi za ujenzi wa barabara hii zilikamilika Februari, 2008. Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii aliagizwa na Wizara kurudia kwa gharama zake mwenyewe ujenzi wa sehemu zilizoharibika kutoptaka na mashimo kujitokeza katika baadhi ya maeneo ya barabara hii. Kazi za kurudia sehemu hiyo zinaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 76.

ii. Usagara – Geita (km 90) (Lot 1 na Lot 2) Kazi za

ujenzi wa barabara hii zimekamilika na kupokelewa na Serikali. Fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/2017 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi kwa sehemu ya Geita – Usagara (Lot 1 na 2) na kulipa fidia ya mali zilizoathiriwa na ujenzi wa barabara ya Buzirayombo – Geita (km 100).

iii. Uyovu – Bwanga - Biharamulo (km 112) Kazi

za ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea. Hadi kufikia Machi, 2017, maendeleo ya mradi kwa sehemu ya Uyovu – Bwanga (km 45) ni asilimia 58 ambapo jumla ya kilometra 21 zimeshajengwa kwa kiwango cha lami. Aidha,

kilometra 14.5 zimeshajengwa kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Bwanga – Biharamulo (km 67).

28. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mradi wa barabara ya **Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 353.7)**, ujenzi wa sehemu ya *Uvinza – Kidahwe (km 76.6)*, *Daraja la Kikwete katika Mto Malagarasi na Barabara Unganishi (km 48)*, *Tabora – Ndono (km 42)* na *Ndono – Urambo (km 52)* umekamilika. Kwa sehemu ya *Kaliua – Kazilambwa (km 56)* hadi kufikia Machi, 2017 utekelezaji umefikia asilimia 90.4 ambapo kilometra 48.4 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

Kuhusu sehemu ya *Uvinza – Malagarasi (km 51.1)*, Mfuko wa ABU-DHABI na Mfuko wa OPEC umekubali kutoa fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya *Kazilambwa – Chagu (km 40)*. Kwa sehemu ya *Urambo – Kaliua (km 28)* hadi kufikia Machi, 2017, Serikali inakamilisha taratibu za kusaini mkataba na mzabuni aliyeshinda.

29. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mradi wa barabara ya **Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga na Bomang'ombe – Sanya Juu (km 173)**, ujenzi umekamilika katika sehemu za Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 32); Tarakea – Rombo Mkuu (km 32) na Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika (km 32). Aidha, kwa sehemu ya Bomang'ombe – Sanya Juu – Kamwanga (km 100), hadi kufikia Machi, 2017 mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Sanya Juu – Elerai (km 32.2) ulikuwa umesainiwa na Mkandarasi alikuwa kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara hii.

30. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Machi, 2017 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa njia nne barabara ya **Arusha – Moshi – Holili (km 140) sehemu ya Arusha (Sakina) – Tengeru (km 14.1) na pamoja na Arusha Bypass (km 42.4)** zinaendelea na zimefikia asilimia 46.64. Aidha, kuhusu ujenzi wa barabara ya **KIA – Mererani (km 26)**, kazi za ujenzi

zinaendelea na zimefikia asilimia 94 ambapo km 25 za lami zilikuwa zimekamilika.

31. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya **Kwa Sadala – Masama - Machame Junction (km 16)**, hadi kufikia Machi, 2017 kilometra 12.5 za tabaka la lami zilikuwa zimekamilika. Aidha, usanifu wa kina wa kilometra 3.5 kwa sehemu ya Masama – Machame Junction umekamilika na kazi za ujenzi wa sehemu hii zitaanza baada ya kupata fedha za ujenzi.

32. *Mheshimiwa Spika*, usanifu wa kina wa mradi wa barabara ya **Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8)** umekamilika na ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza baada ya kupata fedha za ujenzi.

33. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa barabara ya **Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95)** ulikamilika mwaka 2008. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi

34. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa barabara ya **Dodoma- Manyoni(km 127)** ulikamilika Novemba, 2009. Aidha, mradi huu unahusisha ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini (km 4.8) pamoja na ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Muhalala (Manyoni) – “One Stop Inspection Station” (OSIS). Hadi Machi, 2017, ujenzi wa barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini ulikuwa umekamilika. Aidha, kazi ya ujenzi wa OSIS upo katika hatua ya maandalizi ya kuanza ujenzi ikiwa ni pamoja na ufungaji wa mizani inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) eneo la Nala Mkoani Dodoma.

35. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Nelson Mandela (km 15.6)** ulikamilika Juni, 2011. Maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Dar Port hadi TAZARA (km 6.0) yanashubiri upatikanaji wa fedha.

36. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mradi wa barabara ya **Dumila – Kilosa (km 63)**, kazi za ujenzi

zimekamilika Desemba, 2013 kwa sehemu ya **Dumila – Rudewa (km 45)**. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi. Kwa sehemu ya **Rudewa – Kilosa (km 18)** hadi Machi, 2017 taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu hii zilikuwa zinaendelea. Aidha, kuhusu ujenzi wa mizani ya kisasa (Weigh in Motion - WIM) eneo la Dakawa, taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea.

37. Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya **Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112)** umefikia asilimia 74.5 ambapo kilometra 71.5 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami hadi kufikia Machi, 2017. Aidha, kwa sehemu ya **Matai – Kasesya (km 50)** taratibu za kumtafuta Mkandarasi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zinaendelea.

38. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa madaraja makubwa hadi kufikia Machi, 2017 ni kama ifuatavyo:

i. Daraja la Kirumi kwenye barabara ya Makutano – Sirari:

Mtaalam wa kuchunguza hali ya *cables* na kupendekeza jinsi ya kuzifanya ukarabati amekamilisha kazi hiyo na kwa sasa anaandaa taarifa itakayotumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

ii. Daraja la Sibiti na Barabara Unganishi kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti:

Kazi za ujenzi zimefikia asilimia 38.7.

iii. Daraja la Mto Kilombero na Barabara Unganishi kwenye barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge:

Ujenzi wa Daraja umekamilika na ujenzi wa barabara unganishi umefikia asilimia 90.

iv. Daraja la Kavuu na Barabara Unganishi

kwenye barabara ya Majimoto – Inyonga:

Ujenzi wa daraja upo katika hatua za mwisho. Kazi zilizobakia ni pamoja na kukamilisha kilometa 10 za barabara unganishi.

v. Daraja la Mbutu kwenye barabara ya Igunga– Manonga:

Ujenzi wa Daraja la Mbutu umekamilika. Fedha iliyotengwa kwa mwaka 2016/2017 ni kwa ajili ya sehemu ya malipo kwa Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

vi. Ununuzi wa Mabey Compact Emergency Bridge Parts na Crane Lorry

Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata mtoaji wa huduma (supplier) wa vyuma (*Mabey Compact Emergency Bridge Parts*) zinaendelea.

vii. Daraja la Ruhuhu kwenye barabara ya Kitai-Lituhi:

Ujenzi wa daraja la Ruhuhu umeanza na umefikia asilimia 25.

viii. Daraja la Momba katika barabara ya Sitalike - Kibaoni – Kilyamatundu/Kamsamba – Mlowo:

Uchambuzi wa Zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi umekamilika. Majadiliano ya kimkataba yanaendelea ili kusaini mkataba kabla ya mwisho wa Mei, 2017.

ix. Daraja la Lukuledi II kwenye barabara ya Mtama – Kitangali – Newala:

Kazi za ujenzi wa daraja hili zimekamilika. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

x. Daraja la Selander

Mhandisi Mshauri anaendelea na usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni.

xi. Daraja la Sukuma katika barabara ya Magu-Kabila - Mahaha:

Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa daraja hili zinaendelea.

xii. Daraja Jipy la Wami kwenye barabara ya Chalinze – Segera:

Taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa daraja jipya la Wami zinaendelea.

xiii. Daraja la Simiyu kwenye barabara ya Mwanza – Musoma:

Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu.

xiv. Daraja la Mlalakuwa

Kazi za ujenzi wa daraja hili zinaendelea na zimefikia asilimia 10.

xv. Daraja la Mara

Mkandarasi wa ujenzi wa daraja hili amepatikana na anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

39. *Mheshimiwa Spika*, kazi za ujenzi na upanuzi wa barabara ya **New Bagamoyo (Morocco JCT - Mwenge – Tegeta: km 17.2)**; sehemu ya Mwenge – Tegeta (km 12.9) zimekamilika na mradi huu upo katika kipindi cha uangalizi kinachotarajiwa kukamilika tarehe 30 Julai, 2017. Aidha, kazi

ya upanuzi wa dharura sehemu ya Mwenge – Morocco (km 4.3) toka njia tatu kuwa njia tano zimekamilika Julai, 2016. Upanuzi na ukarabati kwa kiwango cha *dual carriageway* wa sehemu hii ya Morocco – Mwenge utafanyika mara baada ya kupata msaada wa fedha kutoka Serikali ya Japan kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani (JICA).

40. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara ya **Kyaka – Bugene (km 59.1)** ikijumuisha ujenzi wa daraja la **Mwisa** pamoja na makalavati, hadi kufikia Machi, 2017 kazi za ujenzi zilikuwa zimekamilika.

41. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Machi, 2017 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kuhusu barabara ya **Isaka – Lusahunga – Rusumo (km 392)**, ni kama ifuatavyo:

i. Sehemu ya Isaka – Lusahunga (km 242)

Ukarabati wa sehemu ya **Isaka – Ushirombo (km 132)** ulikamilika Machi, 2013 na kwa sehemu ya **Ushirombo – Lusahunga (km 110)** maendeleo ya kazi yalikuwa asilimia 51.8 ambapo kilometra 54 zimekamilika kufanyiwa ukarabati kwa kiwango cha lami.

ii. Sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 91) na Nyakasanza – Kobero (km 59)

Kazi za usanifu wa kina zimekamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kupitia Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 91) na kazi ya kufanya mapitio ya usanifu wa kina ili kukidhi viwango vinavyotakiwa na AfDB inaendelea. Vilevile, Serikali imeanza mazungumzo na Benki ya Dunia ambayo imeonesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara za Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero.

iii. Mizani ya Mwendakulima (Kahama)

Serikali haina tena mpango wa kufunga mizani inaopima magari yakiwa kwenye mwendo eneo la

Mwendakulima (Kahama), badala yake mpango huo utatekelezwa katika maeneo ya Manyoni na Nyakanazi.

iv. Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) cha Rusumo

Ujenzi wa Kituo hiki umekamilika.

42. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7)**, hadi kufikia Machi, 2017 ujenzi wa sehemu ya **Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35)** umekamilika, kazi za ujenzi kwa sehemu ya **Tabora – Nyahua (km 85)** zilikuwa zimefikia asilimia 95 ambapo kilometra 78.33 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na kwa sehemu ya **Chaya – Nyahua (km 85.4)** taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kusimamia kazi pamoja na Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea.

43. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya **Korogwe – Handeni (km 65)** na barabara ya **Handeni – Mkata (km 54)** umekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi.

44. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **barabara za mikoa**, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 ni ukarabati wa jumla ya kilometra **712.40** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometra **63.75** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja **15**. Hadi kufikia Machi, 2017, kilometra **284.96** za barabara za mikoa zilikuwa zimekarabatiwa kwa kiwango cha changarawe na kilometra **20.1** zimejengwa kwa kiwango cha lami.

45. Mheshimiwa Spika, kazi za ukarabati wa sehemu zilizoharibika yenye urefu wa kilometra 10 katika **Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza** zinaendelea.

46. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami, upanuzi na ukarabati wa **barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam (km 124.75)**; kazi za ujenzi zimekamilika kwa

barabara za Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley – Jangwani/Twiga Jct (km 2.7); Ubungo Bus Terminal – Kigogo Round About (km 6.4); Jet Corner – Vituka – Davis Corner (km 10.3); Tangi Bovu – Goba (km 9) na Tabata Dampo – Kigogo na Ubungo Maziwa – External (km 2.25). Aidha, hadi Machi, 2017, kazi za ujenzi wa barabara ya Kimara – Kilungule – External/Mandela Road (km 9), sehemu ya kwanza (External/ Mandala Road – Maji Chumvi yenyе urefu wa kilometra 3 zilikuwa zimekamilika. Kwa upande wa barabara ya **Mbezi (Morogoro Road) – Malamba Mawili – Kinyerezi – Banana (km 14)**, kazi za ujenzi wa sehemu ya Kifuru – Kinyerezi zimekamilika ambapo kilometra 4.0 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kazi za ujenzi wa sehemu ya Mbezi (Morogoro Road) – Malamba Mawili – Kinyerezi zilikuwa zinaendelea.

Kuhusu barabara ya **Tegeta Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi Mwisho (km 20)**, hadi Machi, 2017, kazi za ujenzi sehemu ya Goba – Mbezi Mwisho (km 7) zilikuwa zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kuhusu sehemu ya Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba (km 13) taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya sehemu ya Madale – Goba (km 5) zinaendelea.

47. *Mheshimiwa Spika*, hadi Machi, 2017, utekelezaji wa ujenzi wa barabara zingine za kupunguza msongamano ni kama ifuatavyo: **Kimara Baruti – Msewe (km 2.6)**, kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia asilimia 45; **Kibamba – Kisopwa (km 12.0)**, kazi za ujenzi wa sehemu ya Kibamba hadi Mlongazila (km 4) zimekamilika; **Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7)**; mradi upo katika hatua za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi; **Ardhi-Makongo – Goba (km 4.0)**, kazi za ujenzi zinaendelea na kwa barabara ya **Maji Chumvi – Chang’ombe – Barakuda (km 2.5)**, tathmini ya mali zitakazoathiriwa na mradi inaendelea.

Vilevile, awamu ya kwanza ya ujenzi wa **Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Bus Rapid Transit Infrastructure)** na vituo vyake imekamilika. Mradi huu umefunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 25 Januari, 2017.

48. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa ujenzi wa barabara ya **Ndundu – Somanga (km 60)** umekamilika. Fedha zilizotengwa mwaka 2016/2017 ni kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi huu.

49. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya **Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/ Songea (km 396)**, hadi kufikia Machi, 2017, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Ifakara hadi Lumecha/ Songea zilikuwa zimekamilika. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara ulikuwa katika hatua za mwisho chini ya ufadhili wa EU.

50. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mradi wa barabara ya **Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 373)**, hadi kufikia Machi, 2017, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Tabora – Usesula (km 30)** zilikuwa zimefikia asilimia 35 ambapo kilomita 9.4 zimekamilika. Aidha, kwa sehemu ya **Sikonge (Usesula) – Ipole – Koga – Mpanda (km 343)** fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zilikuwa zimepatikana kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Zabuni za ujenzi zimetangazwa ili kupata Makandarasi wa ujenzi.

51. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya **Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo (km 239) na Loliondo – Mto wa Mbu (km 213)**, hadi kufikia Machi, 2017 ujenzi wa sehemu ya **Makutano – Sanzate (km 50)** umefikia asilimia 42 na zabuni za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya **Natta – Mugumu (km 41.6)** zimetangazwa na uchambuzi wa zabuni hizo unaendelea. Aidha, majadiliano ya kimkataba (negotiations) wa ujenzi wa barabara ya **Loliondo – Mto wa Mbu** (sehemu ya Waso – Sale: km 49) na Mkandarasi aliyeshinda zabuni ya ujenzi yanaendelea.

52. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya **Ibanda – Itungi/Kiwira (km 26)**, hadi Machi, 2016 taratibu za kumpata Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa sehemu za Kajunjumele –

Kiwira Port na Ibanda – Itungi Port zinaendelea. Aidha, kwa upande wa barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach, sehemu ya Tenende – Matema, kazi zimekamilika kwa asilimia 33.5.

53. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara ya **Nzega – Tabora (km 115)**, ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika kwa sehemu ya **Nzega – Puge (km 58.8)** na **Puge – Tabora (km 56.10)** ikiwa ni pamoja na barabara ya mchepuo ya Nzega (Nzega Bypass – km 7). Fedha zilizotengwa katika mwaka 2016/2017 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri.

54. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya **Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Nyakanazi (km 768)**, hadi kufikia Machi, 2017 maendeleo ya ujenzi wa sehemu ya **Sumbawanga – Kanazi (km 75)** yamefikia asilimia 81.2, ambapo kilometra 53.3 zimejengwa kwa kiwango cha lami; kwa sehemu ya **Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6)** ujenzi umekamilika kwa asilimia 91.6 ambapo kilometra 64.4 zimejengwa kwa kiwango cha lami na mradi wa **Sitalike – Mpanda (km 36.9)** umekamilika. Kuhusu sehemu ya **Mpanda – Mishamo (km 100); Sehemu ya Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 30)**, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zimekamilika. Kwa sasa Mkandarasi ameanza ujenzi wa barabara hiyo.

55. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Nyanguge – Musoma (km 185.5)** unahuishisha pia ujenzi wa barabara ya Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass: km 17), Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55), Bulamba - Kisorya (km 51) na barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92). Mradi huu unahuishisha pia ukarabati wa barabara ya Makutano – Sirari (km 83).

Hadi kufikia Machi, 2017 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo: -

Ukarabati wa barabara ya **Mpakani mwa Simiyu/Mara - Musoma (km 85.5)** ulikamilika Novemba, 2014 na kazi za ujenzi wa barabara ya **Mchepuo wa Usagara - Kisesa (km 17)** inayojumuisha pia ujenzi wa daraja kubwa moja la Nyashishi na madaraja madogo manne (4) inaendelea na imefikia asilimia 72. Aidha, utekelezaji wa mradi wa **Nansio - Kisorya - Bunda (Sehemu ya Bulamba - Kisorya: km 51)** umekamilika kwa asilimia 24.

Taratibu za kumpata Makandarasi wa ujenzi wa barabara za **Nyamuswa - Bunda - Bulamba (km 55)** na **Musoma - Makojo - Busekela (km 92)** na ukarabati wa barabara ya **Makutano - Sirari (km 83)** zinasubiri upatikanaji wa fedha.

56. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Magole - Turiani - Mziha (km 83.8)**, hadi kufikia Machi, 2017, maendeleo ya mradi kwa sehemu ya Magole - Turiani (km 48.8) ni asilimia 86.3 ambapo kilometra 36 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Kwa sehemu ya Turiani - Mziha (km 35), usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

57. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa barabara za juu (*flyovers*) na maboresho ya makutano ya barabara katika jiji la Dar es Salaam umelenga kujenga 'Flyover' ya TAZARA, "Interchange" ya Ubungo na maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu (Kurasini) na Morocco. Hadi Machi, 2017 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

(i) Barabara ya Juu (*Flyover*) ya TAZARA

Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 32 na kazi za ujenzi zinaendelea.

(ii) Barabara za Juu (*Interchange*) Ubungo

Mkandarasi wa ujenzi wa barabara za juu (*Interchange*) katika makutano ya Ubungo alikuwa

amepatikana na anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Aidha, uzinduzi wa ujenzi wa mradi huu umefanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 20 Machi, 2017.

(iii) Barabara za Juu (Flyovers) za Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu na Morocco

Taratibu za ununuzi wa Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika makutano ya barabara maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata na Morocco ziliikuwa zinaendelea. Kwa upande wa makutano ya Uhasibu na Chang'ombe, barabara zake za juu zimejumuishwa kwenye miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya II (BRT Phase II).

58. *Mheshimiwa Spika*, barabara ya **Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (km 171.8) imekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kwa sehemu ya **Mwigumbi - Maswa (km 50.3)** hadi kufikia Machi, 2017 mradi huu ulikuwa umekamilika kwa asilimia 65.10 na kazi zinaendelea. Vilevile, Serikali inaendelea na taratibu za kumtafuta Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Maswa - Bariadi (km 49.7).**

59. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya **Tabora - Ipole - Rungwa (km 172), hadi kufikia Machi, 2017, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ilikuwa katika hatua za mwisho.**

60. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya **Kidahwe - Kasulu - Kibondo - Nyakanazi (km 350), hadi kufikia Machi, 2017 ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Kidahwe - Kasulu (km 50)** ulikuwa umefikia asilimia 30 na kwa sehemu ya **Nyakanazi - Kibondo (km 50)** ujenzi ulifikia asilimia 28.2. Aidha, kazi ya mapitio ya usanifu wa kina wa sehemu iliyobaki ya **Nyakanazi - Kasulu/Manyovu (km 250)** ilikuwa inaendelea chini ya ufadhilli wa Benki ya Maendeleo ya Afrika chini ya Mpango wa NEPAD kupitia Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.**

61. *Mheshimiwa Spika*, barabara ya kwenda Uwanja wa Ndege wa Mafia (**Mafia Airport Access Road - km 14**) ilikamilika Januari, 2015. Fedha zilizotengwa mwaka 2016/2017 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

62. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa barabara ya **Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12)** una lengo la kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Machi, 2017 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hii zilikuwa zimefikia asilimia 60.

63. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa **Daraja la Nyerere (Kigamboni) (mita 680)** na barabara unganishi umekamilika. Fedha iliyotengwa ni malipo ya sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa daraja pamoja na kuanza ujenzi wa barabara unganishi. Hadi Machi, 2017, Mkandarasi alikuwa anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara unganishi kutoka Daraja la Nyerere (Kigamboni) hadi Vijibweni (km 1.5) pamoja na barabara ya Tungi – Kibada (km 3.8) na Kibada – Mjmwema (km 1.6).

64. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa ujenzi wa **njia za magari mazito na maegesho ya dharura katika Ukanda wa Kati** una lengo la kuimarisha na kuboresha barabara pamoja na kuongeza usalama kwa watumiaji barabara katika ukanda huo. Hadi Machi, 2017 taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulikuwa unaendelea.

65. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi wa barabara ya **Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) hadi Pugu (km 8.0)** ni kuipanua barabara hii kuwa njia sita. Utekelezaji wa mradi huu umesitishwa ili kupisha mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya tatu utakaotekelzwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

66. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa barabara ya **Kimara – Kibaha (km 25.7)** unahusisha upanuzi wa barabara

hii kuwa njia sita ikijumuisha **upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**. Hadi Machi, 2017 taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi huu zimesitishwa kwa kuwa utajumuishwa kwenye awamu ya pili ya mradi wa *Dar es Salaam Maritime Gateway* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

67. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mradi wa barabara ya **Kisarawe - Maneromango – Mlandizi (km 119)** ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hadi Machi, 2017, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mlandizi – Mzenga - Maneromango (km 65) na usanifu wa barabara ya Kisarawe – Maneromango (km 54) ulikuwa umekamilika. Barabara hizi ni sehemu ya barabara ya Kisarawe – Maneromango – Mlandizi (km 119).

68. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imepanga kupanua sehemu ya **barabara ya Bandari (km 1.2), barabara ya Dockyard (km 0.7) na barabara ya Mivinjeni (km 1.0)** ili kukidhi mahitaji ya magari makubwa yanayoingia na kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam. Hadi Machi, 2017, kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea chini ya ufadhili wa *TradeMark East Africa (TMEA)* na inasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

69. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu kuijenga kuwa njia sita barabara ya pete ya **Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**, hadi Machi, 2017, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa njia sita zinaendelea.

70. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa ujenzi wa **mizani mpya karibu na bandari ya Dar es Salaam**, unatekelezwa ili madereva wa magari makubwa wapime uzito wa mizigo waliyobeba kabla ya kuanza safari na hivyo kudhibiti uzidishaji wa mizigo kwenye malori. Hadi Machi, 2017

majadiliano na Mkandarasi aliyependekezwa kupewa kazi ya ujenzi yanaendelea kabla ya kusaini ya mkataba.

71. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya **Tunduma – Sumbawanga (km 223.21)** umegawanywa katika sehemu tatu ili kurahisisha utekelezaji. Ujenzi kwa sehemu ya Tunduma - Ikana (km 63.7); Ikana - Laela (64.2) na Laela - Sumbawanga (km 95.31) umekamilika. Kuhusu barabara ya Tunduma – Ikana (eneo la Tunduma mjini - km 1.6) kazi za ujenzi zinaendelea. Aidha, kwa upande wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2) taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea.

72. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mradi wa barabara ya **Kagoma – Lusahunga (km 154)**, ujenzi ulikamilika Desemba, 2013. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

73. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya **Arusha – Namanga (km 105)** ulikamilika Desemba, 2012. Aidha, kazi ya ujenzi wa Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani (One Stop Border Post - OSBP) imekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

74. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi na ukarabati wa **barabara ya Arusha – Minjingu – Babati – Singida (km 327.5)** umekamilika. Fedha zilizotengwa kwenye mradi huu kwa mwaka 2016/2017 ni za kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi.

75. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya **Dares Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani**, lengo ni kukarabati na kupanua barabara ya lami sehemu ya Gerezani kutoka njia mbili za sasa hadi nne pamoja na ujenzi wa Daraja la Gerezani chini ya msaada wa fedha kutoka Serikali ya Japan na kuchangiwa na Serikali ya Tanzania. Aidha, mradi huu unahuishwa usanifu wa kina na utayarishaji

wa Nyaraka za Zabuni kwa ujenzi wa kiwango cha lami sehemu ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe na daraja la Mzinga. Hadi Machi, 2017 taratibu za ununuzi wa Mhandisi Mshauri kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na utayarishaji wa Nyaraka za Zabuni kwa sehemu ya **Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8)** pamoja na **Daraja la Mzinga** zilikuwa zinaendelea. Kwa sehemu ya **Bendera Tatu – KAMATA (km 1.3)**, taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya upanuzi wa barabara hii kuitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA) zinaendelea.

76. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya **Msimba – Ruaha/Ikokoto – Mafinga – Igawa (km 356.6)** kazi za ukarabati zimekamilika kwa sehemu ya Iringa – Mafinga (km 68.9); Iyovi – Kitonga Gorge (km 86.3); Ikokoto – Iringa (km 60.9) na barabara ya mchepuo kuingia Iringa Mjini (km 2.1). Aidha, kwa barabara ya Mafinga – Igawa (km 137.9) hadi Machi, 2017, kazi za ukarabati kwa sehemu ya Mafinga – Nyigo zilikuwa zimefikia asilimia 41.5 na kwa sehemu ya Nyigo - Igawa, kazi za ukarabati zimefikia asilimia 43.

77. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya **Rujewa- Madibira-Mafinga (km 152)** hadi Machi, 2017, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami zilikuwa zinaendelea. Kazi za ujenzi zinaendelea kwa sehemu ya **Igawa - Mbarali - Ubaruku sehemu ya Mbarali - Ubaruku (km 8.9)** na kwa sehemu ya **Njombe - Ndulamo - Makete (km 109)** majadiliano na Makandarasi wa ujenzi waliopendekezwa yanaendelea kabla ya kusaini mkataba. Aidha, kwa barabara ya **Njombe – Lupembe – Madeke (km 125)** taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea.

78. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Korogwe – Mkumbara – Same (km 172)** umegawanyika katika sehemu mbili: Korogwe – Mkumbara (km 76) na Mkumbara – Same (km 96). Mradi umekamilika kwa sehemu zote mbili. Fedha zilizotengwa mwaka 2016/2017 ni kwa ajili ya sehemu ya malipo ya Mkandarasi.

79. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya Mbeya – Makongolosi (**km 115**), ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo (km 36) na Lwanjilo – Chunya (km 36) umekamilika. Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kuwapata Makandarasi wa ujenzi kwa sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 43) na Mkiwa – Itigi - Noranga (km 56.9) zilikuwa zinaendelea.

80. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mradi wa barabara ya Chalinze – Segera – Tanga (**km 245**), kazi za ukarabati wa barabara yote zimekamilika. Aidha, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass: km 10) zimekamilika. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi.

81. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (**km 211**) unalenga kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami na
zege. Hadi kufikia Machi, 2017, mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) ulikuwa umesainiwa na kazi za ujenzi zinaendelea.

82. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma – Mtera – Iringa (**km 260**), sehemu zote tatu ambazo ni Iringa – Migori (km 95.2); Migori – Fufu Escapment (km 93.8) na Fufu Escapment – Dodoma (km 70.9) umekamilika. Fedha zilizotengwa mwaka 2016/2017 ni kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi. Kuhusu barabara ya mchepuo wa Iringa (km 7.3) ili kupunguza msongamano wa magari katika mji wa Iringa, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo.

83. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Dodoma – Babati (**km 261**), umegawanywa katika sehemu nne. Ujenzi umekamilika kwa sehemu za Dodoma – Mayamaya (km 43.65) na Bonga – Babati (km 19.2). Aidha, hadi Machi, 2017 utekelezaji wa mradi

kwa sehemu ya Mayamaya – Mela (km 99.35) ulikuwa umefikia asilimia 82.23 ambapo kilometra 79.5 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kwa sehemu ya Mela - Bonga (km 88.8) utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 75.81 ambapo kilometra 67.5 zimejengwa kwa kiwango cha lami.

84. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa barabara ya **Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 659.7)** na **Masasi – Newala – Mtware (km 209)** unatekelezwa kwa awamu. Hadi Aprili, 2017, utekelezaji umekamilika kwa barabara za **Masasi – Mangaka (km 54)**, **Mangaka – Nakapanya (km 70.50)**, **Nakapanya – Tunduru (km 66.50)**, **Mangaka – Mtambaswala (km 65.50)**, **Tunduru – Matemanga (km 58.7)**, **Matemanga – Kilimasera (km 68.2)** na **Kilimasera – Namtumbo (km 60.7)**. Aidha, usanifu wa kina wa sehemu ya **Mbinga – Mbamba Bay (km 66)** na **Masasi – Nachingwea – Nanganga (km 91)** umekamilika. Serikali inatafuta fedha za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hizi. Kuhusu barabara ya **Mtware – Newala – Masasi (km 209.00)**, hadi Machi, 2017, mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Mtware – Mnivata (km 50) ulikuwa umesainiwa na maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea.

85. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia kwenye **Chuo cha Uongozi cha Bagamoyo** pamoja na barabara za ndani ya Chuo hicho, hadi Machi, 2017 ujenzi ulikuwa haujaanza.

86. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, fedha za Mfuko wa Barabara zimeendelea kutumika katika miradi mbalimbali ikiwemo **kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, ukarabati wa barabara kwa kiwango cha changarawe na kujenga uwezo. Hadi kufikia Machi, 2017 utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:

*i. Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo/
Benaco (km 183.1) – Sehemu ya Bugene – Kasulo/Benaco
(km 124)*

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

*ii. Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu –
Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha –
Chambalo – Chemba – Kwamtoro – Singida (km 460)*

Kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

*iii. Kufanya Mapitio na Kuandaa Miongozo
(Standards and Specifications)*

Mwongozo wa Uendelezaji wa Barabara Zenye Idadi Ndogo ya Magari (Manual for Low Volume Roads) pamoja na Mwongozo wa Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Barabara ilizinduliwa. Aidha, maandalizi ya Mwongozo wa Usanifu, Ujenzi na Matengenezo ya Madaraja yaliendelea. Vilevile, maandalizi ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayepitia na kuboresha miongozo mitatu ya usanifu na ujenzi wa barabara "The Standard Specifications for Road Works 2000; Pavement and Materials Design Manual 1999; na CML Laboratory Testing Manual 2000" yalikuwa yanaendelea.

iv. Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

v. Barabara za Juu na Malipo ya Fidia- TAZARA na Ubungo

Serikali inaendelea na malipo ya fidia kwa mradi wa TAZARA Flyoverna mradi wa Ubungo *Interchange*.

vi. Barabara ya Kolandoto - Lalago - Mwanhuzi - Matala -Oldeani Jct (km 328)

Upembuzi yakinifu umekamilika. Aidha, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

vii. Barabara ya Karatu - Mbulu - Haydom - Mto Sibiti - Lalago -Maswa (km 389)

Mkataba wa kazi ya upembuzi yakinifu wa barabara hii umesainiwa na tayari kazi zimeanza chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Ujeruman (KfW).

viii. Barabara ya Isyonje - Kikondo - Makete (km 96.2)

Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

ix. Barabara ya Nyamirembe Port - Katoke

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea.

x. Daraja la Kigongo/Busisi katika Barabara ya Usagara - Geita:

Kazi ya upembuzi yakinifu inaendelea.

xii. Barabara ya Tarime – Mugumu (km 86)

Kazi ya upembuzi yakinifu inaendelea

xii. Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu – Kahama (km 457)

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri zinaendelea.

xiii. Kupunguza Msongamano wa Magari katika Barabara za Jiji la Dar es Salaam (Decongestion Of Dsm Roads)

Hatua za utekelezaji wa mradi wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara sita za kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara za katikati ya Jiji la Dar es Salaam ni kama ifuatavyo: Barabara ya Goba – Mbezi Mwisho (km 1.01 zilikamilika); barabara ya Tangi Bovu – Goba (km 2.82 zilikamilika); barabara ya Kimara Baruti – Msewe (km 0.3 zilikamilika); barabara ya Kifuru – Kinyerezi (taratibu za ununuzi zinaendelea); na barabara ya Tabata Dampo – Kigogo (imekamilika). Aidha, mradi wa ujenzi wa barabara ya Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda kwa kiwango cha lami upo katika hatua za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

xiv. Barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi (km 96.7)

Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xv. Barabara ya Tegeta – Bagamoyo (km 43.2)

Kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza upanuzi wa barabara hii.

*xvi. Barabara ya Makofia - Mlandizi
(km 36.7)*

Kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zilikamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

xvii. Barabara ya Mbegani - Bagamoyo (km 7.2)

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

*xviii. Barabara ya Omugakorongo - Kigarama -
Murongo (km 105)*

Kazi ya upembuzi yakinifu ilikuwaimekamilika na usanifu wa kina unaendelea.

*xix. Barabara ya Mtwara Pachani - Lusewa -
Lingusenguse - Nalasi (km 211)*

Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xx. Barabara ya Kibondo - Mabamba (km 45)

Kazi ya upembuzi yakinifu ilikuwaimekamilika na usanifu wa kina ulikuwa unaendelea.

*xxi. Kupunguza Msongamano - Jiji la Mwanza
(Daraja la Waenda kwa Miguu la Furahisha)*

Ujenzi wa daraja la Furahisha umekamilika.

xxii. Barabara ya Arusha - Kibaya - Kongwa (km 430)

Taratibu za kutia saini mkataba wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

*xxiii. Barabara ya Kibada – Mwasonga – Kimbiji
(km 19.2)*

Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

xxiv. Barabaraya Kimbiji-Tundwisorogani (km 30.5)

Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa kina zinaendelea.

*xxv. Barabara ya Nanganga – Ruangwa –
Nachingwea (km 91):*

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

xxvi. Daraja la Mlalakuwa

Mkataba wa ujenzi umesainiwa na kazi ya ujenzi inaendelea.

*xxvii. Barabara ya Kwa Mathias
– Msangani*

Kazi za ukarabati wa barabara hii zimefanyika.

xxviii. Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Mikoa

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni ukarabati wa jumla ya kilometra **584.30** kwa kiwango cha changarawe; ujenzi wa kilometra **36.9** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja **14** katika Mikoa mbalimbali nchini.

Hadi Machi, 2017 kazi zilizotekelzwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa jumla ya kilometra **235.24**,

ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa **25.44** na daraja moja limekamilika na ujenzi wa madaraja mengine uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko, Maegesho ya Vivuko na Matengenezo ya Magari

87. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kuititia Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA) ilipanga kuendelea na ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo, upanuzi wa maegesho ya Kigamboni, ujenzi wa maegesho ya Bwina mkoani Geita na ujenzi wa maegesho ya Lindi – Kitunda. Aidha, Wizara ilipanga kukamilisha ujenzi wa vivuko vypa vya Pangani – Bweni, Kigongo - Busisi na Magogoni – Kigamboni; ununuzi wa vitendea kazi na ukarabati wa karakana za TEMESA; ununuzi wa boti ya abiria ya kivuko cha Kilambo – Namoto na Mkongo – Utete pamoja na ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II na MV Sengerema. Kazi nyingine zilizopangwa kufanya ni kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali pamoja na kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali.

88. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Machi, 2017 ununuzi wa kivuko kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Magogoni – Kigamboni umekamilika na kimeanza kutumika; mkataba ujenzi wa kivuko cha Kigongo – Busisi umesainiwa Januari, 2017 na mradi uko katika hatua ya usanifu wa kina; ununuzi wa boti ndogo za abiria kwa ajili ya kivuko cha Kilambo – Namoto (Mtwara) na kivuko cha Mkongo – Utete (Pwani) unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2017 na ujenzi wa kivuko kipyä cha Pangani ulikamilika mwezi Agosti, 2016 na tayari kivuko kinatoa huduma.

89. *Mheshimiwa Spika*, kuhusumiradiyaujenzi wa maegesho ya vivuko, usanifu wa maegesho ya kivuko cha

Dar es Salaam – Bagamoyo ulikamilika na zabuni kutangazwa. Hata hivyo, Mkandarasi hakuweza kupatikana kutokana na gharama za zabuni kuwa kubwa kuliko bajeti iliyotengwa. Aidha, upanuzi wa maegesho ya Kigamboni upo katika hatua za kumpata Mkandarasi na ufungaji wa mashine za kielektroniki za kukata tiketi za kivuko unaendelea. Vilevile, ujenzi wa maegesho ya Bwina katika mkoa wa Geita upo katika hatua za kumpata Mkandarasi. Kuhusu ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Lindi – Kitunda mkoani Lindi, mradi upo kwenye hatua za kusaini mkataba.

90. *Mheshimiwa Spika*, ukarabati wa kivuko cha MV Magogoni umekamilika na tayari kivuko kinatoa huduma; ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II upo katika hatua za mwisho unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2017 na ukarabati wa kivuko cha MV Sengerema upo katika hatua za maandalizi ya zabuni.

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

91. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Wakala wa Majengo ya Serikali ilipanga kukamilisha ujenzi wa nyumba za Makazi za Majaji mikoani; ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Urambo; kujenga nyumba za makazi ikulu – Dar es Salaam; ujenzi wa Jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya Bariadi na kufanya matengenezo ya nyumba za makazi ya Viongozi. Aidha, Wizara ilipanga kuanza ujenzi wa nyumba 644 za wakazi wa Magomeni *Quarters*.

92. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Machi, 2017, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania imeendelea kutekeleza miradi ifuatayo; ujenzi wa nyumba za Viongozi; ujenzi wa nyumba 13 za Majaji na ukarabati wa nyumba za viongozi na majengo ya Serikali ambapo jumla ya nyumba 31 zilikamilika. Aidha, Wizara imeanza ujenzi wa nyumba 644 za wakazi wa Magomeni *Quarters* ambapo ujenzi ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 15 Aprili, 2017.

Usalama Barabarani na Mazingira

93. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inaratibu shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilipanga kuanzisha Mamlaka ya Usalama Barabarani nchini, kufanya mapitio ya Sheria ya Usalama Barabarani, ukaguzi wa usalama wa barabara, uendeshaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani, kuanzisha mfumo wa kudhibiti mwendokasi wa vyombo vya usafiri barabarani, ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi na ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo. Aidha, Wizara ilipanga kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kutoa elimu ya usalama barabarani kwenye shule za msingi na kwa umma. Kuhusu Utunzaji wa Mazingira, Wizara ilipanga kutoa mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na hifadhi ya mazingira katika Sekta ya Ujenzi kwa wataalam mbalimbali kutoka Taasisi za Wizara. Kazi zingine ni kuandaa Mfumo wa Kusimamia Mazingira, kutoa elimu ya usimamizi wa mazingira na kuandaa program za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira.

94. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Machi, 2017 Wizara imekamilisha maandalizi ya Nyaraka zote za uanzishwaji wa Mamlaka ya Usalama Barabarani na kuwasilisha kwenye mamlaka husika kwa ajili ya maamuzi. Sambamba na hilo, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ambayo itahusisha uanzishwaji wa Mamlaka ya Usalama Barabarani. Wizara pia imekamilisha maandalizi ya utekelezaji wa kazi ya Ukaguzi wa Usalama wa Barabara (Road Safety Audit) ambao hufanyika wakati wa usanifu, ujenzi na baada ya ujenzi ili kubaini kama Sheria, Kanuni na Mwongozo wa Usalama umezingatiwa. Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani umekamilika na unafanya kazi kwa mikoa yote nchini. Wizara imekamilisha utoaji wa elimu juu ya mfumo huu kwa awamu ya kwanza na maandalizi ya utoaji wa elimu kwa awamu ya pili yameanza. Vilevile, Wizara imekamilisha maandalizi ya kumpata Mtaalamu Mshauri kwa ajili ya

kuanzisha Mfumo wa kudhibiti Mwendo kwa vyombo vyua usafiri barabarani. Kazi ya kuanzisha mfumo huu itaanza mwezi Mei, 2017.

Kuhusu ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (*One Stop Inspection Station – OSIS*), Wizara imekamilisha malipo ya fidia katika Ukanda wa Kati (Central Corridor) katika maeneo ya Manyoni na Nyakanazi. Aidha, mkataba wa ujenzi katika vituo hivi umesainiwa. Usanifu katika Ukanda wa Dar es Salaam (Dar es Salaam Corridor) katika maeneo ya Vigwaza, Mikumi, Makambako na Mpemba unaendelea.

95. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu masuala ya usimamizi wa mazingira, katika mwaka 2016/2017, Wizara imekamilisha maandalizi ya hadidu za rejea kwa ajili ya kumpata Mtaalam Mwelekezi wa kuandaa Programu za Udhhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira katika Sekta (*Pollution Control Programme*). Vilevile, maandalizi ya hadidu za rejea kwa ajili ya kumuajiri Mtaalam Mwelekezi wa Kuandaa Mfumo wa Kusimamia Mazingira (*Environmental Management System*) yamekamilika.

UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI

Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)

96. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mfuko wa Barabara ulipanga kukusanya jumla ya Shilingi **832,349,290,000.00** ili zitumike katika matengenezo ya barabara nchini. Katи ya fedha hizo, Shilingi **582,644,500,000.00** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na mikoa zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Shilingi **249,704,790,000.00** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia barabara za Wilaya na Vijijini ambazo zinasimamiwa na Ofisi ya Raїs – TAMISEMI.

97. *Mheshimiwa Spika*, Bodi pia ilipanga kuimarisha na kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Mfuko kuwa ya kielektroniki na kushirikiana na TANROADS na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuweka mfumo

wa pamoja wa kielektroniki na kamera za CCTV kwenye vituo vya mizani. Aidha, Bodi ilipanga kuendelea na ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote nchini. Vilevile, Bodi ilipanga kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi ya Bodi na kuhamia Dodoma ifikapo Desemba, 2016.

98. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Bodi ilikuwa imegawa jumla ya **Shilingi 628,189,431,702.00** sawa na asilimia **75.47** ya bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17. Kati ya hizo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilipokea Shilingi 455,215,636,000.00 na Ofisi ya Rais- TAMISEMI ilipokea Shilingi 172,973,795,702.00.

99. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu kuimarisha na kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Mfuko kuwa ya kielektroniki, katika mwaka 2016/2017, Bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imekamilisha kuweka Mfumo wa kielektroniki wa kutoa vibali na malipo ya kusafirisha mizigo yenye vipimo visivyo vya kawaida kisheria (Abnormal Load Permit Fees – e- permit). Aidha, mfumo wa kielektroniki wa malipo kwa magari yanayozidisha uzito (e - payment) uko kwenye hatua za mwisho za majaribio na uwekaji wa kamera za CCTV kwenye vituo vya mizani unaendelea. Bodi pia imeendelea kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara kwa kutumia wataalam washauri na wafanyakazi wa Bodi. Vilevile, ujenzi wa jengo la ofisi mjini Dodoma umekamilika na Bodi imehamishia shughuli zake katika jengo hilo.

Wakala wa Majengo ya Serikali

100. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wakala wa Majengo ulipanga kuendelea kukamilisha ujenzi wa jengo lenye Ghorofa 5 (Mtaa wa Moshi Plot Na.5) – Dodoma; kununua viwanja mikoani; kufuatilia upatikanaji wa hati za viwanja vya Wakala mikoani na Makao Makuu; kufanya upembuzi yakinifu kwenye viwanja vya TBA kwa ajili ya miradi ya uwekezaji pamoja na kumalizia ujenzi wa jengo la TBA Makao Makuu na Ofisi ya TBA Mkoa wa Manyara. Kazi

nyingine ni kukarabati majengo mbalimbali nchini; kuanza ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa yenyе flat 8 kila moja katika eneo la iliyokuwa NMC Mbezi Beach – Dar es Salaam na majengo mawili ya ghorofa katika kiwanja Na. 276-Ukonga, Dar es Salaam; kumalizia nyumba 57 daraja 'B' mikoani; ujenzi wa nyumba 100 za Watumishi mikoani pamoja na upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuendeleza karakana za samani mikoani; ujenzi wa nyumba 256 kati ya nyumba 851 zitakazojengwa Bunju Dar es Salaam na nyumba 300 kati ya nyumba 600 eneo la Gezaulole, Dar es Salaam pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la kibiashara, Goliondoi – Arusha.

101. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wakala wa Majengo umeendelea kuimarisha Kikosi chake cha ujenzi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya "Tunnel Formwork System" ili kuongeza kasi ya ujenzi na kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma. Katika kutimiza azma hiyo, Wakala umenunua vifaa mbalimbali kama vile *tunnel formwork*, mtambo wa kisasa wa kuchanganya zege (Batching Plant) na mtambo wa kuinua vitu vizito wakati wa ujenzi (Tower Crane) kwa ajili ya kutumika katika ujenzi wa nyumba zake katika maeneo mbalimbali nchini. Wakala umeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 851 Bunju "B" Dar es Salaam (Program Maalum); ujenzi wa Ikulu – Chamwino Dodoma; ujenzi wa nyumba 149 za Viongozi chini ya TAMISEMI katika mikoa 20 ya Tanzania Bara; ukarabati wa Ikulu Ndogo-Chamwino Dodoma na Arusha; ukarabati wa majengo ya Wakala katika nchi nzima; kumalizia ujenzi wa majengo ya uwekezaji ya Wakala yenyе ghorofa 4 hadi 10 kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Arusha; ujenzi wa majengo 20 ya ghorofa 3 kila moja kwa ajili ya mabweni ya wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; matengenezo ya nyumba 31 za Mawaziri; ujenzi wa makazi ya Waziri Mkuu – Dodoma; ujenzi wa nyumba za askari Magereza Ukonga – DSM, ujenzi wa shule ya Ihungo - Kagera pamoja na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Uchaguzi (NEC)- Dodoma. Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa nyumba 57 za Daraja 'B' katika mikoa 19 nchini; kuendelea na ujenzi wa jengo la Kitega

uchumi lililopo barabara ya Simioni/Goliondoi (Arusha) na kukamilisha Jengo la Ghorofa 5 lililopo Mtaa wa Moshi (Dodoma).

Aidha, Wakala umeendelea na mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 za Watumishi wa umma ambapo umekamilisha ujenzi wa nyumba 315 na zimeanza kuuzwa na kukabidhiwa kwa wahusika. Awamu ya tatu ya ujenzi wa nyumba 320 inaendelea katika eneo la Bunju B, Dar es Salaam. Aidha, Wakala umeendelea na kununua viwanja katika sehemu mbalimbali nchini na kufanya Wakala kuwa na jumla ya viwanja 2,947 na maeneo 9 yenye jumla ekari 2,489.5 kwa ajili ya mradi maalum wa ujenzi wa nyumba 10,000 za watumishi wa umma.

Vilevile, Wakala umesimamia jumla ya miradi 232 ya Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Umma ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Usanifu wa miradi hii umezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Wakala wa Ufundu na Umeme

102. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wakala ulipanga kuendelea na matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; ukarabati na ujenzi wa karakana mpya mikoani na kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali.

103. *Mheshimiwa Spika*, hadi Machi, 2017, mradi wa ukarabati wa karakana ya mkoa wa Dar es Salaam (Vingunguti) unaendelea na awamu ya tatu ya ujenzi wa karakana mpya ya mkoa wa Manyara imekamilika na Wakala umekamilisha taratibu za kuanza utekelezaji wa awamu ya nne. Kuhusu matengenezo ya magari, hadi Machi, 2017, TEMESA imefanya matengenezo jumla ya magari 10,835 katika karakana zake.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

104. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Bodi ya Usajili wa wa Wahandisi (ERB) iliweka malengo ya kusajili wahandisi **950**, mafundi sanifu **150**, Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **20**, kusimamia mafunzo ya kuijiendezea kitaaluma kwa wahandisi wataalam na wahandisi washauri (CPD), kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu (SEAP) **1,133** pamoa na kukagua shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa wenye kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi.

105. *Mheshimiwa Spika*, hadi Machi, 2017, Bodi imesajili wahandisi **1,403** na kampuni za ushauri wa kihandisi **11** na kufanya jumla ya wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali kuwa **18,443** na kampuni za ushauri wa kihandisi kuwa **302**. Kat i ya jumla ya wahandisi waliosajiliwa, wahandisi **16,756** ni wazalendo na **1,687** ni wageni. Kampuni za ushauri wa kihandisi za wazawa ni **219** na za kigeni ni **90**. Katika kipindi hicho, Bodi ilifuta usajili kwa wahandisi watalaamu **336**, wahandisi washauri **27** na kampuni za ushauri wa kihandisi **39** kwa kukiuka Sheria ya usajili wa wahandisi. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya miradi **157** ilikaguliwa. Wahandisi wa kigeni **300** walibainika kufanya kazi bila usajili ambapo kati yao **172** walikuwa na sifa na hivyo walisajiliwa, na **128** walikuwa hawana sifa hivyo walikataliwa usajili na hivyo kurejeshwa kwao.

106. *Mheshimiwa Spika*, Bodi pia iliandaa warsha **4** katika Kanda **4** kati ya kanda **5** kwa Wahandisi Wataalam wanaosimamia mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu. Vilevile, Bodi iliendelea kuwaapisha wahandisi wataalam Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo jumla ya wahandisi **2,576** waliapishwa. Aidha, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa wahandisi wahitimu **1,200**.

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

107. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilipanga kusajili Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi **95**, na kufanikiwa kusajili wataalam **88**; ikiwa ni asilimia **96** ya malengo. Vilevile, Bodi ilipanga kusajili Kampuni **34** za Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ambapo, hadi Machi, 2017 Bodi ilisajili kampuni **21**, ikiwa ni asilimia **62** ya malengo. Aidha, Bodi ilipanga kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu **64** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo, ambapo wahitimu **61** walipata mafunzo, sawa na asilimia **95** ya lengo.

108. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza mkakati wa kuboresha ukaguzi wa miradi ya ujenzi, Bodi ililmashira ofisi zake za kanda, ambazo ziko Mwanza, Arusha, Dar es Salaam, Mbeya na Dodoma. Vilevile, Bodi ilifanya ukaguzi wa shughuli za wataalam kwenye miradi ya ujenzi **2010**, sawa na asilimia **112** ya lengo la kukagua miradi **1800**.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

109. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilipanga kusajili Makandarasi wapya **900** wa fani mbalimbali na kukagua miradi ya ujenzi **2,800** ambayo ina thamani ya kuanzia Shilingi milioni 10 na kuendelea. Bodi pia ilipanga kuendesha kozi tano za mafunzo katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dar es Salaam.

110. *Mheshimiwa Spika*, hadi Machi, 2017 Bodi ilisajili Makandarasi wapya **574** na hivyo kufanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa kufikia **8,475**. Aidha, Bodi ilikagua miradi ya ujenzi **1,942**, ambapo miradi **610** ilikutwa na mapungufu mbalimbali ikiwemo kutozingatia afya na usalama kazini, kutosajili miradi na kufanya kazi za thamani inayozidi kiwango kinachoruhusiwa. Makandarasi katika miradi yenye upungufu walichukuliwa hatua kwa mujibu wa

sheria. Vilevile, Bodi iliendesha kozi **4** za mafunzo kupitia Mpango Maalum wa Mafunzo Endelevu kwa Makandarasi ambapo jumla ya makandarasi **297** walishiriki mafunzo hayo.

111. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Bodi iliendelea kuendesha mfuko wa kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund- CAF) unaotoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa makandarasi wadogo na wa kati ili kuwezesha ushiriki wa makandarasi wazalendo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mfuko huu ulifikisha mtaji wa Shilingi Bilioni 2.4 katika mwaka 2016/2017. Aidha, idadi ya wanachama wa Mfuko iliongezeka kutoka 1,366 mwaka 2015/16 hadi 1,510 mwaka 2016/2017.

Baraza la Taifa la Ujenzi

112. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Baraza lilipanga kuendelea kuratibu mfumo wa majaribio wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi ili kukuza uwazi wa uwajibikaji (Construction Sector Transparency Initiative - CoST) katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi; kuboresha ukusanyaji, uwekaji na utoaji wa takwimu na taarifa za sekta ya ujenzi kwa kuboresha kituo cha rasilimali ya habari na kukipatia nyaraka muhimu pamoja na kutathmini, kuhuisha na kuchapisha nyaraka zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi; kuimarisha mipango ya tafiti na maendeleo katika Sekta ya Ujenzi itakayohusisha kutambua maeneo ambayo yatapewa kipaumbele katika kufanya utafiti kwa maendeleo ya Sekta ya Ujenzi, kuchapisha matokeo ya tafiti zikiwemo bei za vifaa vya ujenzi na ukokotoaji wa bei kwa kipimo cha mraba; kuanzisha *database* ya ghamra za ujenzi pamoja na kuchambua upya kanuni za ukokotoaji wa mabadiliko ya bei za ujenzi.

Vilevile, Baraza lilipanga kufanya jitihada za kujiimarisha kifedha kwa kufanya upembuzi yakinifu ili kuendeleza viwanja vilivyopo mtaa wa Migombani - Regent na Mbezi jijini Dar es Salaam na kiwanja kilichopo Dodoma. Baraza pia lilipanga kuendelea na jitihada za kutunisha/ kuanza kazi kwa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi

(Construction Industry Development Fund - CIDF) kwa kushirikiana na TPSF (Tanzania Private Sector Foundation) na wadau wengine wa maendeleo pamoja na kuendelea kusaidia wajenzi katika sekta isiyo rasmi kwa kusaidia utekelezaji wa kazi wa Chama cha Wajenzi wa Sekta isiyo Rasmi (Tanzania Association of Informal Construction Workers - TAICO) na kuwashawishi wajenzi wa sekta isiyo rasmi waliopo Dar es Salaam na mikoani kujunga na chama chao.

113. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Machi, 2017, Baraza lilitkeleza kazi zifuatazo:- kushiriki katika kufanya mapitio na maboresho ya Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003 na kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Sera hiyo (*Implementation Action Plan*): kuandaa hadidu za rejea ili kuwezesha Wataalam Washauri kufanya utafiti wa mabadiliko ya Sheria (Cap 162, Revised Edition (R.E.) 2008); kutoa mafunzo ya usuluhishi wa migogoro ya ujenzi, usimamizi wa mikataba (*Contract Administration*) na ununuzi wa huduma ya ushauri wa kitaalam; kufanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi 150 chini ya Mfuko wa Barabara (Road Funds Board) kwenye Halmashauri za Wilaya na TANROADS zilizo kwenye mikoa mitatu ya Iringa, Katavi na Rukwa pamoja na kuendelea kufanya usuluhishi wa migogoro ya kimkataba ya sekta ya ujenzi Tanzania. Jumla ya migogoro mipyäiliyosajiliwa ni 23 na tayari iko katika hatua mbalimbali za usuluhishi.

114. *Mheshimiwa Spika*, Baraza pia liliendelea kukusanya na kuandaa bei za vifaa vyatya ujenzi na "Indices" kwa ajili ya matumizi ya "Price Fluctuation Formula". Vilevile, Baraza limeendelea na taratibu za kukusanya taarifa muhimu ili kuwezesha uchapishaji wa Jarida la "Construction Business Journal" na "Directory of Construction Materials". Aidha, Baraza limeendelea kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania katika kuandaa viwango (standards) mbalimbali vyatya sekta ya ujenzi kwenye mbao, zege, udongo, misingi na miamba.

Kuhusu uanzaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund - CIDF*),

Baraza liliendelea na ufuatiliaji wa kupatikana fedha ili kuwezesha kazi hiyo kuititia mradi wa “*Private Sector Competitiveness Project - PSCP*” unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Vilevile, Baraza limeendelea kuratibu utekelezaji wa majaribio wa mfumo wa kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma ujulikanao kwa jina la “Construction Sector Transparency Initiative (CoST)”. Majaribio haya yanafadhiliwa na kuratibiwa katika ngazi ya kimataifa na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID).

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

115. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kituo kilipanga kuendelea na jukumu lake la kusambaza teknolojia katika sekta ya ujenzi na uchukuzi hapa nchini kwa kusambaza taarifa zinazohusu teknolojia mbalimbali katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na kuendelea kutoa huduma ya maktaba ya Kituo. Aidha, Kituo kilipanga kuandaa na kuendesha mafunzo kuititia warsha na semina kwa wadau yanayolenga kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi, na kuendelea kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na usafirishaji hapa nchini.

116. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Machi, 2017, Kituo kiliendelea kutoa huduma za maktaba ya Kituo kuhusu Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji na kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo na njia za Kituo za utunzaji wa kumbukumbu na upashanaji wa habari. Vilevile Kituo kilishiriki katika mradi unaotekelizwa na Umoja wa Mamlaka za Barabara katika nchi za SADC (Association of Southern African National Road Agencies – ASANRA) unaolenga kutambua mapungufu ya ujuzi na hivyo kutoa mapendekezo ya kujenga uwezo kwa watendaji wa Mamlaka za Barabara. Aidha, Kituo kilianza utekelezaji wa mradi unaolenga kuboresha mifumo

ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na uchukuzi hapa nchini Tanzania.

Vilevile, Kituo kiliandaa Mkutano wa Kimataifa wa Kikanda Barani Afrika kuhusu utumiaji wa kandarasi za muda mrefu za usimamizi na matengenezo ya barabara ambapo mkandarasi hupimwa na kulipwa kwa matokeo ya ubora wa barabara badala ya kupimwa na kulipwa kwa kazi alizozifanya. Mkutano ulihudhuriwa na washiriki **193** kutoka nchi **17** za Afrika, Asia, Ulaya na Amerika. Kituo pia kiliandaa Mkutano wa Kimataifa wa Kikanda Barani Afrika kuhusu mikakati ya kuongeza kasi kwa utekelezaji wa miradi ya usalama barabarani Barani Afrika. Mkutano ulihudhuriwa na washiriki wapatao **200** kutoka nchi **11** za Afrika, Asia, Ulaya na Amerika.

C.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

117. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Uchukuzi ilitengewa kiasi cha **Shilingi 91,519,632,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 52,430,658,000** ni Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 39,088,974,000** ni Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2017 **Shilingi 65,809,714,764.31** zilikuwa zimetolewa na HAZINA. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 39,415,167,846** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Fungu 62 na Taasisi na **Shilingi 26,394,546,918.31** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Bajeti ya Maendeleo

118. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Uchukuzi ilitengewa **Shilingi 2,495,814,130,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 2,322,603,400,000** na **Shilingi 173,210,730,000** zilikuwa fedha za nje. Kati ya fedha za ndani zilizotengwa, **Shilingi 161,426,400,000** ni fedha za Mfuko wa Reli.

Hadi Aprili, 2017 fedha zilizotolewa ni **Shilingi 825,858,477,991.57**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 694,180,788,701.65** ni fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 131,677,689,289.92** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizotolewa zinahusisha **Shilingi 111,669,711,654** za Mfuko wa Reli. Kwa ujumla, kiasi Kilichotolewa ni sawa na **asilimia 33.1** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

HALI YA UTENDAJI WA SEKTA YA UCHUKUZI

119. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Sekta ya Uchukuzi ilitekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

HUDUMA ZA USAFIRI MIJINI NA VIJJINI

Usafiri kwa Njia ya Barabara

120. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia SUMATRA imendelea kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma za uchukuzi vijijini. Aidha, ukaguzi wa kushtukiza wa vyombo vya usafiri; utoaji nauli elekezi, elimu na mafunzo; na ushauri kwa watumiaji na watoaji wa huduma za usafiri wa barabara mijini na vijijini umesaidia kupunguza kero zinazotokana na watoa huduma za usafiri vijijini. Pamoja na uboreshaji wa huduma unaoendelea, huduma za usafiri vijijini zimeendelea kukabiliwa na changamoto zinazotokana na kutokuwepo kwa miundombinu thabiti na hivyo kusababisha gharama za usafiri kuwa kubwa. Aidha, baadhi ya mabasi yanayotoa huduma vijijini yapo katika hali duni ya ubora na hivyo mtumiaji wa huduma hiyo kukosa njia mbadala ya kupata huduma hiyo. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI pamoja na sekta binafsi tumeendelea kuboresha huduma za usafiri ili kuboresha hali ya usafiri katika ngazi zote kuanzia mikoani hadi vijijini.

121. *Mheshimiwa Spika*, mara nyingi Serikali imekuwa inasilitiza juu ya utunzaji wa mazingira na afya ya watumiaji wa usafiri wa barabara ikiwemo kutumia maeneo

maalum kwa ajili ya kujisitiri wakati wa safari. Katika utekelezaji wa agizo hilo, mwaka 2016/2017, SUMATRA kwa kushirkiana na wataalam wa Afya ilifanya ukaguzi wa vituo vya abiria wanaosafiri katika njia kuu za Dar es Salaam hadi Mtwara na Dar es salaam kuelekea Mbeya. Zoezi hilo liliweza kubaini vituo vilivypo na kuhakikisha kuwa zinazingatia utunzaji wa mazingira na salama kiafya.

Huduma za Usafiri Mijini

122. *Mheshimiwa Spika*, huduma za usafiri kwenye Majiji na Mijini hususan usafiri wa barabara kwa kiasi kikubwa zimeendelea kutolewa na sekta binafsi. Ongezeko la ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma limesababisha kuwepo kwa ushindani wa utoaji huduma ya usafiri katika majiji na miji hapa nchini. Ushindani huu umesababisha wananchi wa mijini kupata huduma ya usafiri kwa urahisi zaidi na gharama nafuu. Pamoja na urahisi wa upatikanaji, utoaji wa huduma hii unakabiliwa na tatizo la msongamano wa magari hasa katika Miji mikubwa ya nchi yetu na hivyo kuwafanya wananchi kushindwa kufika katika shughuli zao kwa wakati. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali iliendelea kuboresha huduma hizo kwa kukarabati barabara mbalimbali zinazopunguza msongamano, kuboresha usafiri wa abiria Jijini Dar es Salaam na kuendelea kuhamasisha utekelezaji wa Mradi wa mabasi yaendayo haraka (BRT). Jitihada nyininge zilizofanyika ili kukabiliana na tatizo la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam ni kuhimiza matumizi ya mabasi makubwa kutoa huduma katikati ya Jiji, kuainisha njia za magari makubwa kupita na hasa malori kuingia mjini pamoja na muda wa malori kuingia na kutoka jijini Dar es Salaam. Aidha, juhudhi zinaendelea kujenga barabara za pete (ring roads), makutano ya barabara (flyovers) ya TAZARA na Ubungo.

Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa Njia ya Barabara

123. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuboresha udhibiti na mahusiano ya kitaasisi ili kuimarisha

utoaji wa huduma za usafiri. Agosti 2016, SUMATRA ilianza kusimika mfumo wa ufuatiliaji mwenendo wa mabasi ya masafa marefu (Vehicle Tracking System- VTS) kwa kutumia TEHAMA. Mfumo huu una uwezo wa kulifuatilia basi muda wote na popote linapokuwa na kurekodi mwendokasi wa basi husika. Mwendokasi wa basi unapokuwa umezidi kikomo kilichokubaliwa, kengele hulia ndani ya basi. Mfumo huu pia husaidia Jeshi la Polisi na wamiliki wa mabasi kufuatilia mwenendo wa mabasi yao kutoka katika ofisi zao. Jumla ya mabasi 150 yamefungwa mfumo huu kama sehemu ya majaribio ya utendaji wa Mfumo. Mpaka sasa majaribio yanaonesha matokeo mazuri na kuanzia Aprili, 2017 Mfumo huu utasambazwa katika mabasi mengine yaendayo masafa marefu.

124. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, SUMATRA ilianza kutekeleza maagizo ya Serikali ya kufanya utafiti kuhusu vyanzo, madhara na namna bora ya kukabiliana na msongamano wa magari katika miji na majiji nchini hususan mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza. Utafiti huu unaendelea na unatarajiwa kukamilika Juni, 2017. SUMATRA pia ilifanya utafiti kuhusu hali ya usalama barabarani. Utafiti huo umebainisha maeneo yanayohitaji uboreshaji ili kuimarisha usalama wa usafiri barabarani; maeneo yaliyobainishwa ni pamoja na Menejimenti ya usalama barabarani; Usalama wa miundombinu ya barabara; Usalama wa watumiaji wa barabara; Usalama wa vyombo vya usafiri; na Huduma kwa waathirika (victims) wa ajali. Baada ya tafiti hizo kukamilika, Serikali kupitia SUMATRA itaandaa Mikakati ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tafiti hizo.

125. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, SUMATRA iliendelea kuimarisha udhibiti wa huduma za usafiri wa barabarani ili kuruhusu ushindani ulio sawa. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya leseni 26,018 za usafirishaji abiria zilitolewa ikilinganishwa na leseni 22,422 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 16. Kuhusu leseni za magari ya mizigo, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017,

jumla ya leseni 41,918 zilitolewa ikilinganishwa na leseni 38,178 zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2015/2016. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 9.8.

USAFIGI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA RELI

Usafiri wa Reli Jijini Dar es Salaam

126. *Mheshimiwa Spika*, huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam zimeendelea kuboreshwa ili kukidhi matarajio na mahitaji ya wananchi. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, idadi ya watumiaji wa usafiri wa treni ya TAZARA kutoka Mwakanga hadi stesheni kuu ya Dar es Salaam ilikuwa abiria 2,516,202 ikilinganishwa na abiria 1,384,086 waliosafiri katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hili ni ongezeko la asilimia 81.8. Kwa upande wa TRL, huduma za usafiri wa treni Jijini Dar es salaam ziliendelea kutolewa kutoka stesheni ya Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa na kutoka Stesheni za Dar es Salaam na Pugu. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya abiria 3,246,353 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 387,102 waliosafiri katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 739. Ongezeko hili lilitokana na TRL kukarabati mabehewa 8 na kuanzisha safari kati ya Stesheni za Dar es Salaam na Pugu. Hii imesaidia kupunguza tatizo la msongamano wa magari katika maeneo hayo. Wizara kuititia RAHCO inaendelea kufanya upembuzi yakiniwa wa ujenzi wa njia mpya za reli kwenda maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Kerege. Upembuzi huu unatarajiwaa kukamilika Juni, 2017.

Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO)

127. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, kazi za kuboresha, kujenga na kukarabati miundombinu ya reli zimeendelea kutekelezwa na RAHCO kwa niaba ya Serikali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:

i. Kusaini mkataba wa ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Dar es salaam hadi

Morogoro (Km 205 au Km 300 ikijumuisha njia za kupishana). Mkataba huo ulisainiwa tarehe 3 Februari 2017 na hatua mbalimbali za ujenzi zimeanza Aprili, 2017. Aidha, tarehe 12 Aprili, 2017, Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli aliweka jiwe la msingi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli hiyo;

ii. Kuandaa makabrasha na kutangaza zabuni kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* katika maeneo ya Morogoro na Makutupora (Km 336); Makutupora hadi Tabora (km 294); Tabora hadi Isaka (km 133); na Isaka hadi Mwanza (km 249). Zabuni hizo zilitangazwa Novemba, 2016 na kufunguliwa tarehe 19 Aprili, 2017;

iii. Kukarabati reli ya kutoka Mpanda eneo la kutoka stesheni ya Ugalla River hadi stesheni ya Katumba yenye umbali wa kilometra 15 kwa kuondoa reli za ratili 45 na 50 kwa yadi na kuweka reli za ratili 60 kwa yadi;

iv. Ujenzi wa madaraja 10 katи ya 38 yaliyo katika hali mbaya katи ya Tabora – Kigoma;

v. Kazi ya kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata mshauri mwelekezi wa ujenzi wa mabwawa mawili (2) katika eneo la Godegode - Gulwe na Msagali katika eneo la km 384;

vi. Usanifu wa madaraja 38 yaliyo katika hali mbaya katи ya Dar es Salaam na Isaka. Aidha, makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kukarabati madaraja hayo yamewasilishwa Benki ya Dunia ili kupata ridhaa (No objection); na

vii. Kazi ya kuondoa mchanga unaoziba madaraja na makalvati katika eneo la Kilosa – Gulwe imeendelea kufanyika katika kipindi chote cha mvua. Hii imesaidia kupunguza mafuriko ya mara kwa mara katika eneo hilo.

128. *Mheshimiwa Spika*, kazi zinazoendelea kutekelezwa katika mwaka 2016/2017 ni pamoja na:

- (i) Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Arusha hadi Musoma (Km 600) kwa *Standard gauge* na matawi ya Engaruka (km 53), Minjingu (km 35) na tawi kuelekea Dutwa (km 2.8) pamoja na reli ya Tabora - Mwanza (km 120). Taarifa ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Tanga- Arusha ilijadiliwa na wadau Machi, 2017;
- (ii) Usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Uvinza – Musongati na Mpanda – Karema (Km 150) na Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Kaliua – Mpanda na Tabora – Kigoma (Km 411). Kazi hizi zinatarajiwa kukamilika Desemba, 2017;
- (iii) Kuendelea na kazi ya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha njia ya reli kati ya Tabora - Kigoma na Kaliua – Mpanda. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Juni, 2017;
- (iv) Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Mtwara – Mbambabay na matawi yake kwenda kwenye machimbo ya Mchuchuma na Liganga. Kazi ya kumpata Mshauri wa uwekezaji (Transaction advisor) atakayenadi mradi kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi zinaendelea.

Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)

129. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2016/2017, hadi Machi, 2017, TRL ilisafirisha tani 214,923 za mizigo ikilinganishwa na tani 143,276 katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hili ni ongezeko la asilimia 50. Ongezeko hili limechangiwa na ukarabati wa baadhi ya maeneo korofii ya reli na madaraja; ukarabati wa mabehewa ya mizigo na kukamilika kwa uundwaji upya wa awamu ya pili ya vichwa 8 vya treni vya njia kuu. Kuhusu usafirishaji wa abiria, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, abiria wa masafa marefu 537,934 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 502,096 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016.

Hili ni ongezeko la asilimia 7. Ongezeko hili limechangiwa pia na kuongezeka kwa safari za treni ya abiria za masafa mrefu kutoka safari 3 hadi safari 4 kwa wiki.

130. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine zilizotekelezwa katika mwaka 2016/2017 ni pamoja na:

i. Kukamilisha ujenzi wa njia ya Stesheni ya Karakata – Dar es Salaam (mita 400) eneo la llala (llala Block Post) ili kuepusha mwingiliano wa treni za abiria kutoka Stesheni hadi Pugu/ Ubungo na treni za mizigo kutoka Bandari ya Dar es salaam kuelekea Ubungo;

ii. Kukamilisha ukarabati wa mahebewa 124 ya mizigo na mabehewa 28 ya abiria;

iii. Kuanzisha huduma ya usafiri wa treni ya Jiji Dar es Salaam kutoka Stesheni hadi Pugu; na

iv. Kukamilisha utandikaji wa reli yenye urefu wa mita 600 kwenda kiwanda cha mbolea cha YARA kilichopo Mlandizi, Pwani. Ujenzi wa reli hii utarahisisha upakiaji na usafirishaji wa mbolea.

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

131. *Mheshimiwa Spika*, Serikali za Tanzania na Zambia zimeendelea na juhudini za uendelezaji wa miundombinu na uboreshaji wa huduma za Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA). Utendaji wa TAZARA umeanza kuonesha mafanikio baada ya kufanya mabadiliko ya uongozi ndani ya Mamlaka na kuendelea kulipa malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya tani 93,688 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 79,119 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Utendaji huu ni ongezeko la asilimia 18. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, TAZARA ilisafirisha abiria 338,014 ikilinganishwa na abiria 262,448 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Utendaji huu ni ongezeko la asilimia 29.

132. *Mheshimiwa Spika*, miradi iliyoetekelezwa ni pamoja na kufanya matengenezo makubwa ya njia ya reli ili kupunguza maeneo korofi yanayolazimu kupunguza mwendokasi wa treni kutoka maeneo 48 hadi maeneo 12; na kukamilisha ukarabati wa mabehewa ya mizigo 170 kati ya 400 na mabehewa 11 ya abiria. Kwa ujumla TAZARA imeweza kupunguza muda wa kusafirisha mizigo kati ya Dar es Salaam, Tanzania na New Kapiri Mposhi, Zambia kutoka wastani wa siku 30 hadi siku 6.

USAFIRI NA UCHUKUZI MAJINI

133. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za usafiri na uchukuzi majini kuititia taasisi zake za Kampuni inayomilikiwa kwa pamoja kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP), Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) pamoja na sekta binafsi. Aidha, huduma za bandari zimeendelea kutolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) pamoja na sekta binafsi.

Huduma za Uchukuzi Baharini

134. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, uchukuzi wa masafa marefu baharini umeendelea kutolewa na SINOTASHIP. Kampuni hii imeendelea kutoa huduma zake kwa kutumia meli kubwa moja yenye uwezo wa kubeba tani 57,000 kwa wakati mmoja. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, SINOTASHIP ilisafirisha tani 410,000 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na tani 380,000 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2015/2016. Hili ni ongezeko la asilimia 7.9 ya mizigo iliyo safirishwa. Aidha, kuhusu ununuvi wa meli nyingine, SINOTASHIP inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kununua au kukodi meli za mizigo ili kushiriki kikamilifu katika fursa zinazojitokeza ikiwa ni pamoja na kusafirishia gesi (LNG) kutoka Tanzania kwenda kwenye soko la ndani au nje ya nchi.

Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa

135. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kuititia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imeendelea kutoa huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Kampuni ya MSCL ilisafirisha abiria 37,671 ikilinganishwa na abiria 84,173 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Huu ni upungufu wa asilimia 55.24. Kuhusu usafirishaji wa mizigo, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Januari, 2017, Kampuni ya MSCL ilisafirisha mizigo tani 11,199 ikilinganishwa na tani 33,015 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2015/2016. Huu ni upungufu wa asilimia 66.1. Sababu za upungufu ni kusimama kwa meli za MV Clarias; MV Liemba; MV Serengeti na MT Sangara kutokana na ubovu. Manunuzi ya makandarasi kwa ajili ya kukarabati meli za MV Liemba na MV Serengeti yamekamilika na kazi hii inatarajiwaa kuanza Mei 2017. Aidha, ukarabati wa Meli ya MV Clarias ulianza Septemba, 2016 na kukamilika Februari, 2017. Meli hiyo imeanza kufanya kazi.

136. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Serikali ilitenga fedha Shilingi bilioni 50.5 kwa ajili ya kununua meli moja (1) katika ziwa Victoria na kukarabati meli tatu (3). Kuhusu ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria, taratibu za kumpata Mkandarasi zinatarajiwaa kukamilika Mei 2017. Zoezi hili limechukua muda baada ya Mzabuni aliyepatikana kushindwa kukidhi matakwa ya zabuni za taarifa za ufundu na fedha (Financial and Technical proposals). Kampuni ya MSCL inaendelea na taratibu za manunuzi kwa kutumia utaratibu wa *restricted tendering* ambapo kampuni zinazosifika kwa ujenzi wa meli Duniani zinafanyiwa upekuzi (due diligence) ili kujirithisha na uwezo wao kabla ya kuwapelekea nyaraka za zabuni. Mkandarasi wa ujenzi wa meli hiyo anatarajiwaa kupatikana kabla ya Juni 2017. Kuhusu Mradi wa ukarabati wa meli za MV. Victoria, MV. Butiama na MV. Liemba ni kuwa ukarabati wa meli ya MV Liemba utaanza Mei, 2017. Kwa sasa mkandarasi wa kukarabati meli ya MV Liemba amepatikana na majadiliano yanaendelea kabla ya kusaini mkataba.

137. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine zilizotekelزوا katika mwaka 2016/2017 ni pamoja na:

i. Kukamilisha matengenezo ya meli ya MV Umoja Julai, 2016. Meli hii inaendelea kutoa huduma za usafiri kati ya Mwanza na Portbell-Uganda;

ii. Kukamilisha matengenezo ya meli ya MV Songea Julai, 2016;

iii. Kuendelea na manunuzi ya mkandarasi wa kufunga Mfumo wa Kielektroniki kwa ajili ya Ukataji Tiketi. Kazi ya kufunga mfumo huu inatarajiwa kuanza Juni, 2017; na

iv. Kuendelea na manunuzi ya mkandarasi wa kufunga vifaa vya kudhibiti matumizi ya mafuta melini. Ufungaji wa vifaa hivyo unatarajiwa kuanza Mei, 2017.

Huduma za Bandari

138. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kusimamia Bandari kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara; bandari ndogo zilizoko katika mwambao wa bahari ya Hindi za Kilwa, Lindi, Mafia, Pangani na Bagamoyo; bandari za Maziwa Makuu za Mwanza, Bukoba, Kemondo Bay na Musoma zilizopo katika Ziwa Victoria; Kigoma na Kasanga zilizopo katika Ziwa Tanganyika; na Mbamba Bay na Itungi/ Kiwira zilizopo katika Ziwa Nyasa.

139. *Mheshimiwa Spika*, katikakipindicha Julai, 2016 hadi Februari, 2017, TPA ilihudumia jumla ya tani milioni 8.572 za shehena ikilinganishwa na tani milioni 8.640 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Utendaji huu ni pungufu kwa asilimia 1.0. Katika shehena hiyo, bandari ya Dar es Salaam ilihudumia jumla ya tani milioni 7.683 za shehena na bandari nyingine tani milioni 0.957. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Februari, 2017, Kitengo cha Makasha (General Cargo) cha bandari ya Dar es Salaam kilihudumia makasha 106,448 ikilinganishwa na makasha

101,540 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 4.8.

140. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Februari, 2017, Kitengo cha Makasha (TICTS) kilihudumia makasha **301,555** ikilinganishwa na makasha **317,507** yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Huu ni upungufu wa asilimia5. Sababu za kushuka kwa utendaji huo ni pamoja na:

- i. Kuzorota kwa huduma za reli ya TAZARA kati ya Dar es Salaam na ukanda wa shaba (Copper Belt);
- ii. Utendaji usioridhisha wa reli ya Kati;
- iii. M dororo wa biashara na shughuli za usafirishaji wa majini, hasa katika ukanda wa Asia unaohudumia meli nyingi zinazokuja ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika;
- iv. Ushindani kutoka Bandari nyingine unaotokana na kuimarika kwa miundombinu ya reli na bandari za Beira na Nacala nchini Msumbiji, hivyo kuvutia baadhi ya wateja kutoka nchi za Zambia na Malawi;
- v. Usumbu na udanganyifu kwa wateja kutoka kwa Wakala wa Forodha na uondoshaji shehena; na
- vi. Kuanzishwa kwa Himaya Moja ya Forodha (Single Customs Territory) kwa nchi zisizo wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati Bandari shindani kama Mombasa, Beira, Nacala na Durban hawatumii mfumo huu. Hali hii imepunguza sana kiasi cha shehena inayohudumiwa kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC); na
- vii. Sheria kutoruhusu matumizi ya magari makubwa ya inter-links katika barabara zetu tofauti na nchi nyingine shindani.

141. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Februari, 2017, shehena ya mizigo iliyohudumiwa kwenda na kutoka katika nchi jirani za Burundi, Jamhuri ya

Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia ilikuwa tani milioni 3.143 ikilinganishwa na tani milioni 3.624 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Upungufu huu ni sawa na asilimia 13.3. Sababu za upungufu huo ni pamoja na malalamiko ya wateja wa nchi hizo juu ya kuwepo kwa tozo la ongezeko la thamani kwenye huduma (VAT on auxiliary services) kwa mizigo ya nchi jirani; kuanzishwa kwa dirisha moja la forodha (Single Customs Territory) kwa mizigo ya nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC); na ushindani kutoka bandari za Mombasa, Kenya; Beira na Maputo, Msumbuji; Walvis Bay, Namibia; na Lobito, Angola.

142. *Mheshimiwa Spika*, ili kukabiliana na upungufu wa shehena za mizigo, Mamlaka ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi za huduma za bandari (Liaison offices) katika miji ya Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DR Congo), Lusaka (Zambia), Kigali (Rwanda) na Bujumbura (Burundi); kuanzisha wakala wa Mamlaka huko Kampala, Uganda; kuimarisha usalama wa mizigo bandarini na kutoa huduma za bandari kwa saa 24 kwa siku kwa wiki.

143. *Mheshimiwa Spika*, miradi ya kuboresha utendaji wa bandari za Mwambao na Maziwa Makuu iliyotekelzeza katika mwaka 2016/2017 ni pamoja na:

i. Kukamilika kwa jengo la kuwaweka pamoja wadau muhimu wanaotoa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam (One Stop Center). Jengo hilo la ghorofa 35 lilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mheshimiwa Joseph Kabila Kabange tarehe 4 Oktoba, 2016. Jengo hili litaanza kutumika Mei, 2017;

ii. Upembuzi Yakinifu wa uboreshaji wa bandari ya Dar es ulikamilika Machi, 2017. Kazi za usanifu na ujenzi zinatarajiwa kuanza Juni, 2017 na kukamilika ndani ya miezi 36;

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- iii. Kukamilika kwa upanuzi wa barabara ya kuingia lango Na. 4 katika Bandari ya Dar es Salaam Oktoba, 2016; barabara ya kuingia lango Na. 8 Desemba, 2016; ukarabati na upanuzi wa barabara ya kuingia lango Na. 5 Aprili, 2017; na ujenzi wa barabara ya kutoka Karakana ya meli (Dock Yard) ili kuunganishwa na barabara ya Nelson Mandera ilikamilika Septemba, 2016;
- iv. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa bandari kavu ya Ruvu ulianza Januari, 2017. Lengo la mradi huu ni kuongeza uwezo wa bandari ya Dar es Salaam kuhudumia mizigo na kupunguza msongamano wa mizigo na malori bandarini na Jijini Dar es Salaam;
- v. Ujenzi wa gati la Kagunga katika Ziwa Tanganyika ulikamilika Januari, 2017;
- vi. Ujenzi wa gati la Ntama katika Ziwa Victoria ulikamilika Agosti, 2016;
- vii. Ujenzi wa gati la Lushamba ulikamilika Julai 2016;
- viii. Kazi ya kufanya upembusi yakinifu ili kubaini mahitaji ya namna bora ya kuendeleza Bandari ya Kigoma ilikamilika Julai, 2016;
- ix. Kazi ya kufanya upembusi yakinifu wa kuboresha miundombinu katika bandari za Ziwa Victoria (Mwanza, Musoma na Bukoba) ilikamilika Aprili, 2017;
- x. Ujenzi wa matishari mawili (Self- Propelled Cargo Barges) yenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja katika Ziwa Nyasa ulikamilika Februari, 2017. Matishari hayo yanaendelea kufanyiwa majaribio kabla ya kuanza kutumika rasmi mwezi Mei, 2017;
- xi. Ujenzi wa Meli yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo katika Ziwa Nyasa ulianza Juni, 2016

na unatarajiwa kukamilika Agosti 2017. Kazi za ujenzi zinafanyika katika chelezo lilojengwa katika bandari ya Itungi (Kyela) mwaka 2015;

xii. Kukamilika kwa maandalizi ya ujenzi wa gati za Nyamisati, katika bahari ya Hindi; Ndumbi katika Ziwa Nyasa; Lagosa, Kibirizi na Kabwe katika Ziwa Tanganyika. Ujenzi huu unatarajiwa kuanza Juni 2017 na kukamilika Juni 2019;

xiii. Ukarabati wa gati la Lindi unaoteklezwa na Mkandarasi *M/s Comfix& Engineering Ltd* umekamilika kwa asilimia 50. Ujenzi unatarajiwa kukamilika Agosti, 2017;

xiv. Ujenzi wa gati la Pangani chini ya Mkandarasi *M/s Alpha Logistics Tz Ltd* ulikamilika Septemba, 2016. Mradi huo uko katika kipindi cha uangalizi hadi Septemba, 2017

xv. Ujenzi wa gati la Kalya/Sibwesa umekamilika kwa asilimia 50. Ujenzi

huo unatarajiwa kukamilika Juni, 2017;

xvi. Kazi ya kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Karema, Kigoma ili kuunganishwa na Bandari ya Kalemie, DRC unaendelea. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza Septemba 2017;

xvii. Ujenzi wa gati la Ndumbi ulianza Machi 2017 kwa kutumia wataalam wa ndani ya Mamlaka na unatarajiwa kukamilika Desemba 2017.

144. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari inaendelea na kazi ya uboreshaji na uongezaji wa kina katika gati Na. 1 hadi 7, ujenzi wa gati jipya la kushushia magari eneo la Gerezani Creek katika bandari ya Dar es salaam na kupanua na kuongeza kina cha lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli. Benki ya Dunia ambayo inagharamia mradi huu imetoa idhini (*No Objection*) kwa ajili ya kumwajiri Mkandarasi Kampuni ya *China Harbour Engineering and Construction Company (CRCC)*. Mradi huu unatarajiwa kuanza Juni, 2017.

145. *Mheshimiwa Spika*, Serikali inatambua umuhimu wa kupanua Bandari ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kujenga gati Na. 13 & 14 ili kuhudumia mizigo mingi kwa ufanisi zaidi. Awali mradi wa ujenzi wa gati Na. 13 na 14 ulikuwa utekelezwe na sekta binafsi kwa utaratibu wa Sanifu, Jenga, Endesha na Rejesha (Design, Build, Operate and Transfer - DBOT). Utaratibu wa kutumia sekta binafsi ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na gharama za ujenzi kuwa kubwa; Wazabuni kutojumuisha uhamishaji wa kituo cha kupokelea mafuta cha Kurasini (KOJ) na uondoshaji wa mabomba ya mafuta yanayopita chini katika eneo la mradi. Hivyo, Serikali itaanza kutekeleza mradi huu katika hatua ya pili (phase II) baada ya kukamilika miradi ya awamu ya kwanza ya uboreshaji na uongezaji wa kina cha Bandari ya Dar es Salaam.

146. *Mheshimiwa Spika*, Serikali inaendelea na maandalizi ya msingi ya ujenzi wa bandari ya Mbegani, Bagamoyo. Kukamilika kwa ujenzi wa bandari hii kutaongeza uwezo wa kuhudumia shehena ziingiazo nchini na ziendazo nchi jirani za Burundi, DR Congo, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia. Kwa sasa majadiliano na Kampuni ya China Merchants Port Limited (CMPort) kuhusu vipengele vya Mikataba yanakamilishwa. Aidha, zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaoathirika limefanyika kwa jumla ya wananchi 2,188 sawa na asilimia 98.96 ya wadai wote. Jumla ya shilingi billioni 47.584 zimelipwa hadi Machi, 2017. Zoezi la ulipaji wa fidia linatarajiwa kukamilika Juni 2017.

147. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu ujenzi wa bandari ya Mwambani, Tanga, TPA inaendelea na jitihada za kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kuzingatia ujenzi wa reli mpya (Tanga – Arusha – Musoma). Mradi huu ulifanyiwa upembuzi yakinifu wa mara ya kwanza ambapo haukutoa taarifa zenye kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi na kufanya upembuzi huo kurejewa upya. Maandalizi ya makabasha kwa ajili ya marejeo ya upembuzi yakinifu yamekamilika na zabuni hiyo inatarajiwa kutangazwa kabla ya Juni 2017. Aidha, maandalizi kwa ajili ya kujenga gati la Chongoleani (Tanga) kwa ajili ya kupokelea mafuta kutoka

Uganda yanaendelea kwa kufanya upembuzi yakinifu. Meli zenye uwezo wa kubeba hadi tani 250,000 (Suezmax) zinatarajiwa kuhudumiwa katika gati jipya litakalojengwa eneo la Chongoleani. TPA imeainisha eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 2,400 kwa ajili ya kuhifadhi kwa muda vifaa vya ujenzi.

148. *Mheshimiwa Spika*, ni muhimu kupanua Bandari ya Mtwara ili kuifanya kuwa ya kisasa kwa ajili ya kuhudumia shehena za gesi; mafuta; madini na mazao ya kilimo kutoka katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara (Mtwara Development Corridor) unaojumuisha mikoa ya kusini na nchi za Malawi na Zambia. Upanuzi wa Bandari hii utahusu ujenzi wa magati manne (4) ambayo yatajengwa kwa awamu. Awamu ya kwanza itahusu ujenzi wa gati moja ambapo Kampuni ya *China Railway Construction Company (CRCC)* ilisaini Mkataba wa ujenzi tarehe 4 Machi, 2017. Gati hilo lenye urefu wa mita 350 ni kwa ajili ya kuhudumia shehena mchanganyiko. Ujenzi wa gati hili utakamilika ndani ya miezi 21.

149. *Mheshimiwa Spika*, Mfumo wa TANCIS wa Mamlaka ya Mapato umeanza kutoa huduma ambapo makusanyo yote ya tozo za huduma za bandari (wharfage) kwa mizigo inayoingia nchini (Local and transit goods) kwa bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara zimeanza kukusanywa tangu Agosti, 2016. Mizigo inayosafirishwa nje ambayo bado inatumia mfumo wa *billing system* kama mizigo ya Zanzibar, mizigo inayopita nchini (transhipment), mizigo inayozidi (overloaded), makasha matupu, mizigo ya nchi za Afrika Mashariki (single custom territory), mizigo ya bandari za maziwa na mizigo yenye malipo maalum (concession rates) itahamishiwa katika Mfumo wa TANCIS katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi.

Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Majini

150. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia SUMATRA imendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 2003 (Merchant Shipping Act, 2003). Aidha, kwa

kushirikiana na Mamlaka ya Bahari Zanzibar (Zanzibar Maritime Authority - ZMA), huduma na usalama wa usafiri majini umeendelea kusimamiwa katika eneo lote la maji ya Tanzania kwa kuzingatia matakwa ya Shirika la Bahari Duniani (IMO).

151. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeanza kutekeleza matakwa ya Shirika la Bahari Duniani (IMO) kwa Kusimamia upimaji uzito wa makasha yanayosafirishwa nje ya nchi kupitia bandari zetu (IMO SOLAS Requirements on Gross Mass Verification of a Container Carrying Cargo) kuanzia Julai, 2016. Hadi Machi, 2017, jumla ya watoa huduma ya upimaji uzito wa makasha (Container Gross Mass verifiers) 70 walikuwa wamesajiliwa. Upimaji huu utaimarisha usalama wa vyombo vyta usafiri majini kwa kujuza uzito sahihi wa mizigo inayosafirishwa kwenye meli. Aidha, usalama wa shughuli za upakuaji na upakiaji bandarini utaimarika.

152. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia SUMATRA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuzitambua bandari bubu ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi na kuweka mikakati ya kuainisha bandari bubu zote zilizo katika mwambao wa bahari ya Hindi na katika Maziwa Makuu. Lengo ni kurasimisha baadhi ya bandari hizo, kuboresha na kuzidhibiti. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, ukaguzi ulifanyika katika mwambao wa Ziwa Tanganyika katika mikoa ya Rukwa na Katavi. Katika ukaguzi huu, jumla ya bandari bubu 12 zilibainika. SUMATRA inaendelea kufanya mawasiliano na Halmashauri zinazomiliki maeneo yasiyo rasmi kwa matumizi ya vyombo vyta majini ili kuweka utaratibu bora na salama wa matumizi ya maeneo hayo.

153. *Mheshimiwa Spika*, moja ya kasoro zinazotolewa na wadau wa bandari kuhusu utendaji wa sekta ndogo ya bandari ni suala la usalama hususan mizigo inayoingia na kutoka katika bandari zetu. Kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha utendaji wa bandari zetu, katika mwaka 2016/2017, SUMATRA iliratibu mikutano 64 ya wadau kuhusu usalama na ulinzi wa bandari. Mikutano hiyo ilifanyika

katika mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Kagera, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Pwani na Tanga.

USAFIGI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

Udhhibitit wa Usalama wa Usafiri wa Anga

154. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuzingatia vigezo na kanuni za usalama wa usafiri wa anga kama inavyoshauriwa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (The International Civil Aviation Organisation-ICAO). Kwa lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za usafiri wa anga nchini. Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imeendelea kusajili ndege kulingana na masharti ya usajili ambapo katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017, ndege 14 zilisajiliwa kwa mara ya kwanza hapa nchini na ndege 79 zilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora wa kuendelea kufanya kazi. Lengo ni kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kanuni za Usalama wa Usafiri wa Anga zinafuatwa.

155. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TCAA imeendelea kudhibiti ajali za vyombo vya usafiri wa anga. Katika mwaka 2016/2017, hakuna ajali ya usafiri wa anga iliyotokea isipokuwa yalikuwepo matukio saba (7) ya vyombo vya usafiri wa anga. Aidha, Mamlaka imeendelea kuimarisha usalama katika viwanja vyote vya ndege ili kuhakikisha kwamba viwanja hivyo havitumiki katika matukio ya uhalifu yakiwemo ya kupitisha madawa ya kulevyta na nyara za Umma. Pia, Mamlaka imeendelea kuhakikisha kwamba maafisa wa usalama katika viwanja vya ndege wanapatiwa mafunzo stahiki na kupewa leseni. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya maafisa usalama 35 walipatiwa mafunzo. Kati yao, maafisa 25 walihitimu na kupewa leseni.

156. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Mamlaka ya Usafiri wa Anga ilieendelea kufanya kaguzi za viwanja vyote vya ndege nchini ili kuhakikisha kuwa viwanja hivi vinakidhi vigezo, masharti na kanuni zilizowekwa na Mamlaka. Viwanja vya ndege vilivyokaguliwa na kupewa

vyeti vya ubora baada ya kukidhi vigezo vya kimataifa kwa ajili ya kupokea ndege kubwa ni pamoja na Julius Nyerere, Amani Abedi Karume na Kilimanjaro. Aidha, uimarishaji na uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Pemba, Geita, Matemanga na Jengo la Tatu la Abiria katika kiwanja cha Julius Nyerere uliendelea kudhibitiwa ili kukidhi viwango vya usalama.

157. *Mheshimiwa Spika*, Ili kudhibiti na kuimarisha usalama wa usafiri wa anga nchini, TCAA inatarajia kununua rada 4 za kuongozea ndege za kiraia. Majadiliano ya mkataba baina ya TCAA na Mkandarasi (M/s Thares Air Systems) kutoka Ufaransa yanakamilishwa na mkataba unatarajiwa kusainiwa wakati wowote. Rada hizi ambazo zitakamilika usimikaji wake Aprili, 2018 zitafungwa katika viwanja vya ndege vya JNIA, Mwanza, Kilimanjaro na Songwe kwa gharama ya Shilingi bilioni 61.3.

158. *Mheshimiwa Spika*, utendaji wa sekta ya usafiri wa anga nchini umeendelea kukua. Katika mwaka 2016/2017, idadi ya abiria wanaotumia usafiri wa anga imefikia abiria 5,057,180 ikilinganishwa na abiria 4,861,277 waliosafiri mwaka 2015/2016. Hili ni ongezeko la asilimia 4. Kwa abiria wanaosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi, katika mwaka 2016/2017, jumla ya abiria 2,238,653 wanatarajiwa kusafiri ikilinganishwa na abiria 2,146,360 waliosafiri katika mwaka 2015/2016. Sababu za ongezeko hili ni pamoja na kusainiwa kwa mikataba ya usafiri wa anga kati ya Tanzania na nchi zingine (Bilateral Air Services Agreements - BASA); uimarishaji wa miundombinu na huduma za viwanja vya ndege; uboreshaji wa uwanja wa ndege wa Julius Nyerere (JNIA); ukuaji wa uchumi na shughuli za utalii nchini. Aidha, idadi ya abiria waliosafiri ndani ya nchi imeongezeka kutoka abiria 2,910,820 mwaka 2015/2016 hadi abiria 3,056,361 katika mwaka 2016/2017. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 5. Sababu ya ongezeko la abiria wa ndani ni pamoja Serikali kutekeleza azma yake ya kuimarisha na kuendeleza Kampuni ya Ndege Tanzania, kukua kwa shughuli za kiuchumi,

kuongezeka kwa utalii nchini na kuanzishwa kwa safari za ndege katika maeneo mapya ya Dodoma, Bukoba na Songea.

159. *Mheshimiwa Spika*, utoaji wa huduma za kusafirisha mizigo katika viwanja mbalimbali vya ndege nchini umeendelea kukua. Hadi Aprili, 2017, mizigo ya kwenda na kutoka nchini ilifikia tani 32,773.6 kutoka tani 31,425.2 zilizosafirisha katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Ongezeko hili lilichangiwa na kukua kwa shughuli za kibashara na kiuchumi ndani na nje ya nchi na jitihada za kuboresha miundombinu ya huduma za usafirishaji wa mizigo kupitia usafiri wa anga.

160. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya kampuni 59 zilipewa leseni kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali katika viwanja vya ndege. Kati ya hizo, Kampuni 25 zilipewa leseni ya kutoa huduma mbalimbali kwa kampuni nyengine za ndege (Third Party Ground Handling Services Providers); Kampuni 14 kutoa huduma kwenye ndege zake zenyewe (self handling); Kampuni 8 kutoa huduma za vyakula kwa kampuni za ndege na Kampuni 12 kutoa huduma ya ugavi wa mafuta ya ndege. Aidha, hadi Machi, 2017, jumla ya kampuni za usafiri wa ndege 61 zilikuwa zinatoa huduma za usafiri wa anga wa ratiba (scheduled) na usiokuwa wa ratiba (non-scheduled air services). Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika mwaka 2015/2016.

161. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania imeendelea kuingia makubaliano ya huduma za usafiri wa anga na nchi mbalimbali (BASA) kwa lengo la kukidhi mahitaji ya soko na kurahisisha usafiri katika sekta hii muhimu. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017, jumla ya makubaliano mapya kumi (10) yaliingiwa baina ya Tanzania na nchi za Israel, Ureno, Guyana, Canada, Norway, Sweden, Morocco, Falme za nchi za Kiarabu, Denmark na Uganda. Aidha, mikataba ya nchi nne (4) za Malawi, Kenya, Oman na Uturuki ilipitiwa upya. Makubaliano haya yanafanya hadi Aprili, 2017, Tanzania kuwa imeingia mikataba ya BASA na jumla ya nchi 68

ikilinganishwa na nchi 60 zilizokuwa zimesaini makubaliano hayo mwaka 2015/2016. Hadi Aprili, 2017, Mashirika ya ndege ya kimataifa ya ndani na nje ya nchi 29 yalikuwa yanatoa huduma za usafiri wa anga kwa utaratibu wa BASA. Aidha, safari za ndege kati ya nchi hizo na Tanzania ziliikuwa 193 kwa juma.

162. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa gharama za mawasiliano ya ndege kati ya kituo na kituo zinapungua na zinakuwa za uhakika. Moja ya uboreshaji huo ni kubadilisha mfumo wa mawasiliano ya anga kutoka mfumo unaotumika sasa wa analogia kwenda mfumo wa digitali. Kazi ya kuboresha mawasiliano kati ya waongoza ndege na marubani wakiwa angani (VHF area cover relay station) huko Lokisale, Arusha na Changarawe, Iringa zimekamilika. Aidha, zabuni ya kuboresha mfumo wa mawasiliano kwenda mfumo wa digitali wa ufuatillaji wa safari za ndege katika kituo cha Pemba ilitangazwa Februari, 2017.

Kuhusu kufanya ukarabati wa mnara wa kuongozea ndege katika kituo cha Pemba, zabuni ya kumpata mkandarasi wa kufanya ukarabati wa mnara huo zilifunguliwa tarehe 2 Februari, 2017. Kazi za ukarabati zinaendelea na zinatarajija kukamilika Juni, 2017.

163. *Mheshimiwa Spika* kuhusu mfuko wa mafunzo kwa marubani na wahandisi wa ndege, Mamlaka ya TCAA inaendelea na juhudzi za kutafuta fedha ili kuweza kufadhili wanafunzi wengi zaidi kwenye mafunzo ya urubani na wahandisi wa ndege. Hata hivyo, Mamlaka inaendelea kushirikiana na vyuo vingine hapa nchini kikiwemo Chuo cha Usafirishaji (NIT) ili kuhakikisha kwamba mafunzo hayo yanatolewa hapa nchini.

Huduma za Viwanja vya Ndege

164. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imeendelea kuboresha miundombinu na huduma za viwanja vya ndege nchini ili

kuwezesha ndege kubwa na ndogo kutua na kuruka kwa usalama. Uboreshaji huo unalenga kuvivezesha viwanja vya ndege nchini kutumika kwa majira yote ya mwaka na kuvutia mashirika mengi zaidi ya ndege nchini ili kuongeza ushindani na hivyo kupunguza gharama za usafiri wa Anga.

165. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa jengo la tatu la abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) unaendelea kutekelezwa na unatarajiwa kukamilika Desemba 2017. Jengo hilo limeezekwa na kazi zinazoendelea ni ujenzi wa kuta za ndani ya jengo, usimikaji wa madaraja ya abiria kupandia/kushukia kwenye ndege, mifumo ya viyoyozi, miundombinu ya umeme, mifumo ya maji safi na maji taka pamoja na mifumo ya zimamoto. Aidha, ujenzi wa maegesho ya ndege umefikia hatua ya matabaka ya lami. Kukamilika kwa jengo hilo kutaongeza uwezo wa kiwanja kuhudumia hadi abiria milioni 8.5 kwa mwaka kutoka abiria milioni 2.5.

166. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kusimamia uendeshaji na uboreshaji wa Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ili kuhakikisha kinakuwa bora na kuchangia katika ukuaji wa biashara za maua, mbogamboga, matunda na utalii. Kazi za ukarabati wa kiwanja hiki zimekamilika kwa asilimia 70 na ujenzi unatarajiwa kukamilika Mei, 2017. Aidha, magari mawili mapya, makubwa na ya kisasa ya zimamoto yalinunuliwa. Kukamilika kwa ukarabati wa KIA kutaongeza uwezo wa barabara ya kuruka na kutua ndege kuhudumia ndege nyngi na jengo la abiria kuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 1.2 kwa mwaka kutoka abiria 500,000 wa sasa.

167. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, mradi wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza uliendelea kutekelezwa. Hadi kufikia Machi, 2017 hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa kazi za kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa mita 500. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, ujenzi wa jengo la mizigo na maegesho ya ndege.

168. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia TAA inaendelea na awamu ya pili ya ukarabati na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora. Kazi zinazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya pili ya kutua na kuruka ndege (secondary runway), eneo la maegesha ya ndege (apron), barabara ya maungio (taxiway) kwa kiwango cha lami, usimikaji wa mitambo ya kuongozea ndege (NavAids, DME na VOR) na taa za barabara ya kurukia ndege (AGL). Kazi za ukarabati wa Kiwanja hiki zilanza Septemba, 2016 na zinatarajiwaa kukamilika Juni, 2017.

169. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Kigoma, Benki ya EIB ilitoa kibali (No Objection) cha kutangaza upya zabuni ya ukarabati Machi, 2017 kufuatia gharama za wazabuni kutokuwa shindani. Zabuni ya marejeo inatarajiwaa kutangazwa Mei, 2017. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake (maegesha ya ndege, maegesha ya magari na barabara ya kuingia na kutoka), usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa uzio wa usalama na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa (OBS).

170. *Mheshimiwa Spika*, baada ya kukamilika kwa ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba na kuanza kutumika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekamilisha ujenzi wa shule mpya ya msingi katika eneo la Mafumbo. Madhumuni ya ujenzi wa Shule hii ni kuweka mazingira mazuri ya utoaji wa huduma za usafiri wa anga bila kuathiri utoaji elimu. Ujenzi wa shule hii ulikamilika Aprili, 2017.

171. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine zilizoendelea kutekelezwaa katika mwaka 2016/17 ni pamoja na:

i. Usimikaji wa taa za kuongozea ndege wakati wa kutua (PAPI) katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe ulikamilika Novemba, 2016;

ii. Kazi ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya kuanza kazi za ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga zilikamilika Machi, 2017. Ukarabati wa viwanja hivyo utaanza Mei, 2017;

iii. Nyaraka za manunuzi ya Mtaalam Mwelekezi wa kazi ya kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa miundombinu ya Kiwanja kipycha cha Ndege cha Msalato zimewasilishwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ili kupata "No Objection". Kazi hii inatarajiwa kuanza Agosti 2017;

iv. Kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege kumi na moja (11) vya Lake Manyara, Musoma, Iringa, Tanga, Songea, Kilwa Masoko, Lindi, Moshi, Njombe, Simiyu na Singida kwa kiwango cha lami. Kazi hizo zitakamilika Mei, 2017;

v. Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Jengo la pili la abiria (TBII) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere imekamilika. Serikali inaendelea na majadiliano na Serikali ya Ufaransa kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji wa mradi huo.

Huduma za Usafiri wa Anga

172. *Mheshimiwa Spika*, huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) pamoja na Kampuni za sekta binafsi zikiwemo Precision Air, Fastjet, Auric na Coastal Air.

173. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kufufua na kuboresha huduma za Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) ili kusaidia kukuza sekta nyngine za kiuchumi ikiwa ni pamoja na utalii, biashara, madini na kilimo. Katika mwaka 2016/2017, Serikali iliingia mikataba ya ununuzi wa ndege sita. Ndege mbili (2) aina ya *Bombardier Dash 8 – Q400* zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja ziliwasili nchini Septemba, 2016 na kuanza kazi

Oktoba 2016. Ndege moja (1) aina ya *Bombardier Dash 8 – Q400* itawasili nchini Julai, 2017; ndege mbili (2) aina ya *Bombardier CS 300* zenyé uwezo wa kubeba abiria 127 kila moja zitawasili nchini Juni, 2018 na ndege moja (1) ya masafa marefu aina ya *Boeing 787 Dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262 itawasili nchini Julai, 2018.

174. *Mheshimiwa Spika*, ujio wa ndege hizo mbili aina ya *Bombardier Dash 8 – Q400* pamoja na ile iliyokuwepo aina ya *Dash 8 - Q300* umeiwezesha ATCL kutoa huduma za uhakika za usafiri wa anga katika maeneo ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Bukoba, Mbeya, Dodoma, Zanzibar na Moroni (Comoro). Kwa kutumia ndege hizo tatu, ATCL inatarajia kupanua huduma zake katika maeneo ya Mtwara, Mpanda, Songea na Tabora kuanzia mwezi Juni 2017. Safari za nchi jirani za Entebbe (Uganda), Nairobi (Kenya), Bujumbura (Burundi) na Kigali (Rwanda) zitaanza baada ya kupata ndege ya tatu ya aina ya *Bombardier Dash 8 – Q400* Julai 2017. Aidha, mara baada ya ndege aina ya *Bombardier CS 300* kuwasili nchini, ATCL itaanza safari za kwenda Afrika ya Magharibi, Afrika ya Kati, Afrika ya Kusini, Mashariki ya Kati na India; na baadae kufanya safari za masafa marefu kwenda China, Ulaya, na Marekani baada ya ndege ya *Boeing 787* kuwasili.

175. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, ATCL ilisafirisha abiria 47,510 ikilinganishwa na abiria 32,434 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 46. Ukuaji huu ulitokea kati ya Oktoba, 2016 na Machi, 2017 baada ya upatikanaji wa ndege mbili mpya. Katika mwaka 2016/2017, mifumo mipyä na ya kisasa ya ukatishaji wa tiketi (reservation system), udhibiti wa mapato (Revenue management system) na uhudumiaji wasafiri uwanjani (Departure Control System) imefungwa. Aidha, ATCL imefungua kituo cha kisasa cha huduma kwa wateja (call centre) ili kuondoa kero zitokanazo na matumizi ya simu za kawaida katika kuhudumia wateja. Lengo ni kuongeza ubora wa huduma zake kwa wateja. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja kuendelea na hatua za kusafisha

mizania ya ATCL; kuimarisha mifumo mbalimbali ya kielectroniki kwa ajili ya uuzwaji wa tiketi za ndege na udhibiti wa mapato ya Kampuni; na kuendeleza raslimali watu ili kuongeza ufanisi.

HUDUMA ZA HALI YA HEWA

176. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea kuboresha huduma na miundombinu ya hali hewa. Hii ni pamoja na kuboresha mbinu za utabiri na utoaji wa huduma pamoja na tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa. Aidha, TMA iliendelea kutoa utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku kumi, mwezi na msimu. Utabiri huu ulichangia katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kijamii. Lengo ni kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa data na taarifa za hali ya hewa na hilyo kuboresha utabiri wa hali ya hewa.

177. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Mamlaka imeendelea kutoa huduma za hali ya hewa kwa vyombo vinavyosafiri Angani, Baharini na kwenye Maziwa. Taarifa za hali ya hewa kwa vyombo vya usafiri majini zinapatikana katika ofisi zilizopo katika Bandari za Zanzibar, Dar es salaam, Kigoma na Mwanza. Aidha, huduma za hali ya hewa zimeendelea kutolewa katika viwanja vyote vya ndege vinavyotoa safari za ratiba. Taarifa hizi zimesaldia kuimarisha usalama wa vyombo vya usafiri wa anga na majini ili kuhakikisha usalama.

178. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa huduma za hali ya hewa zitaanza kutolewa katika Ziwa Tanganyika. Napenda kutoa taarifa kuwa, TMA ilianza kutoa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa Ziwa Tanganyika vikiwemo vyombo vya usafiri Septemba, 2016. Ili kuhakikisha kuwa huduma hizi zinakuwa endelevu, mtambo wa kupima hali ya hewa unaojiendesha wenyeje ulifungwa katika Bandari ya Kigoma. Kazi nyingine zilizoteklezwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa ofisi zilizo katika uwanja wa ndege wa Chakechake, Pemba; Bandari

ya Mkoani na vituo vya hali ya hewa vya Same, Ukitriguru (Mwanza) na Igeri (Njombe).

179. *Mheshimiwa Spika*, usalama wa binadamu na mazingira umekuwa katika mashaka kutoptana na matumizi ya kemikali ya zebaki (mercury). Kufuatia hatari hiyo, mwaka 2013, Umoja wa Mataifa ulipitisha azimio la kupiga marufuku matumizi ya zebaki Duniani ifikapo mwaka 2020. Hivyo, Shirika la Hali ya Hewa Duniani liliazimia kuwa ifikapo 2020, vifaa vyote vya hali ya hewa vinavyotumia zebaki viondolewe katika matumizi. Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imeanza kubadilisha vifaa vinavyotumia zebaki ambapo mpaka sasa imefanikiwa kubadilisha vifaa vinavyopima mgandamizo wa hewa (barometers). Aidha, Mamlaka inaendelea kutekeleza mpango wa kubadilisha vifaa vinavyopima hali ya joto (thermometers).

C.1.3 SEKTA YA MAWASILIANO

Ukusanyaji wa Mapato

180. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/17, Sekta ya Mawasiliano ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 11,011,000** kutoptana na mauzo ya nyaraka za zabuni mbalimbali. Hadi kufikia Aprili, 2017 Sekta bado haijokusanya kiasi chochote kutoptana na taratibu za zabuni kuahirishwa katika kipindi hicho. Taratibu hizo zinatarajija kuanza Mei, 2017.

181. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi mwezi Aprili, 2017, Wizara iliweza kukusanya kiasi cha Dola za Marekani **6,577,916.08** (sawa na **Shilingi 14,260,922,061.44**) kutoptana na Mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ambapo fedha hizo ni maalum kwa ajili ya urejeshaji/ulipaji wa deni la ujenzi wa mradi huo kwa Benki ya EXIM ya China na pia kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Mkongo huo.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

182. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa kiasi cha **Shilingi 3,073,949,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,161,623,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Sekta ya Mawasiliano na **Shilingi 912,326,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 **Shilingi 2,262,734,571** zilikuwa zimetolewa na HAZINA. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,374,703,138** zimetolewa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Sekta ya Mawasiliano na **Shilingi 888,031,433** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Bajeti ya Maendeleo

183. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa jumla ya **Shilingi 92,730,110,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 5,000,000,000** na **Shilingi 87,730,110,000** zilikuwa fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 37,295,532,723**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 190,309,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 37,105,223,723** ni fedha za nje.

Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano

184. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Mawasiliano imekuwa moja ya nguzo muhimu ya kukuza uchumi kwa Taifa letu. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la uchangiaji katika uchumi kutoka asilimia 12.1 mwaka 2015 hadikufikiaasilimia 14.3 mwaka 2016. Pia, mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali yameonesha matokeo chanya kufuatia ongezeko la watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini ambapo idadi imeongezeka kutoka laini za simu za kiganjani 39,808,419 mwezi Desemba, 2015 hadi kufikia laini 40,173,783 mwezi Desemba, 2016. Aidha, kuna ongezeko kubwa la huduma zinazotolewa na Serikali na pia sekta binafsi kuititia mawasiliano ya simu za kiganjani kama vile kutuma/

kupokea pesa, kulipia ankara za maji, umeme, kununua hisa, kulipia ving'amuzi, kulipia huduma za elimu, kulipia tozo za Mamlaka ya Mapato, kulipia huduma za usafiri n.k. Hali hii imechangia kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali na kuboresha maisha ya wananchi.

185. *Mheshimiwa Spika*, idadi ya watumiaji wa intaneti waliongezeka kutoka 17,263,623 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 19,862,525 kwa mwaka 2016. Aidha, vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 118 mwaka 2015 hadi kufikia vituo 148 mwaka 2016 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga viliongezeka kutoka vituo 26 mwaka 2015 na hadi kufikia vituo 30 mwaka 2016. Pia watoa huduma za mawasiliano ya simu na posta wameongezeka na kuleta ushindani wenye tija na ufanisi nchini kwa sekta zote.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

186. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Mawasiliano inaratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchini, ambao kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilifikia Awamu ya III sehemu ya kwanza na IV ya utekelezaji. Awamu ya III sehemu ya kwanza ilihuisha uunganishaji wa Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ujenzi wa mtandao wa miundombinu ya Itifaki (Internet Protocol-Multilayer Label Switching yaani IP- MPLS Network) na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (National Internet Data Centre) Dar es Salaam; awamu hiyo ilikamilika mwezi Julai, 2016 na kuanza kufanya kazi ya kutoa huduma. Awamu ya IV ni ujenzi wa mikongo ya mijini (Metro Networks) na unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Watoa Huduma za Mawasiliano (Tigo, Airtel na Zantel). Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 ujenzi umekamilika katika miji ya Dar es Salaam (kilomita 300), Mwanza (kilomita 36), Arusha (kilomita 58), Tanga (kilomita 43.28), Moshi (kilomita 35.08), Mbeya (kilomita 6.9), Shinyanga (kilomita 2.3), Musoma (kilomita 2.1) na Biharamulo (kilomita 0.2), Morogoro (kilomita

18) na Dodoma (kilomita 42). Kukamilika kwa ujenzi huu kumesaidia kuboresha utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wateja kwa kutumia Mkongo huo.

Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kutunza Data

187. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Kutunza Data cha Taifa (National Data Centre-NDC) ulikamilika mwezi Julai, 2016 na kilianza rasmi kutoa huduma mwezi Septemba, 2016. Huduma zinazotolewa na kituo hicho ni pamoja na: (a) kupangisha mfumo, vifaa/mitambo (Co-location), (b) kuhifadhi "Data" (Data Storage and Back-up), (c) kupangisha mtambo mtandaoni (Dedicated and Virtual Server), (d) mifumo mtandaoni (Software as a Service – SaaS). Watumiaji wa kituo hiki ni; Serikali, Watoa Huduma za Mawasiliano, Taasisi za Fedha, Taasisi za Elimu, Afya, Utalii, Killimo na Utafiti, Wafanyabiashara, Ofisi za Diplomasia na Watu Binafsi. Kituo kinawezesha utunzaji wa Data hapa nchini, usalama na usiri wa data, mwingiliano wa mifumo ya data (intergration). Aidha, hadi sasa kuna wateja 27 ambaao wameanza kutumia kituo hicho.

Juhudi za Serikali Kufikisha Huduma ya Mawasiliano Vijijini

188. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano katika mwaka wa fedha 2016/2017, imeendelea na ufikishaji wa huduma ya mawasiliano vijijini ambapo mpaka sasa jumla ya kata 382 kati ya kata 443 zenye viji 1,825 na wakazi 2,891,731 zimekwisha pata huduma ya mawasiliano. Serikali inawahimiza watoa huduma wote ambaao hawajakamilisha miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini kufanya hivyo mara moja bila ucheleweshaji zaidi.

Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi

189. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi

ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 inayoelekeza kuwepo kwa Anwani za Kitaifa zitakazowezesha ufkishaji wa barua, nyaraka na vipeto nyumbani, mahali pa biashara na ofisini. Azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kunakuwepo na Anwani za Kitaifa ambazo zitaainisha makazi, mahali pa kazi au pa biashara. Anwani hizi pia zitarahisisha na kuboresha utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi, kwa mfano: Afya, Elimu, Sensa, Uokoaji, Biashara Mtandao na Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali. Utekelezaji wa mradi huu unaendelea ambapo Mitaa na barabara ambazo hazikuwa na majina zimepewa majina katika Kata 18 za manispaa ya Dodoma na barabara 18 zilizochongwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino. Marekebisho yanafanywa na uwekaji miundombinu unaendelea katika baadhi ya nguzo na majina ya mitaa katika Kata nane za Manispaa ya Dodoma. Aidha, watendaji na viongozi wameendelea kujengewa uwezo ili washiriki katika utekelezaji wa mradi huu.

Programu ya Miundombinu ya TEHAMA ya Kikanda (RCIP)

190. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Mawasiliano inatekeleza Programu ya Miundombinu ya TEHAMA ya Kikanda (RCIP) kwa kutumia fedha za nje. Miradi inayotekelzeza ni pamoja na:- Mradi wa shule mtandao (e-school) unaohusisha ununuvi, usimikaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA katika Shule 80 za Sekondari na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu walioteuliwa kwa kazi hiyo katika shule hizo. Mradi wa *Video Conference*: unaohusisha ununuvi, ufungaji na usimikaji wa mitambo ya video conference katika Makao Makuu ya Mikoa 26 na baadhi ya Taasisi za Serikali unaendelea.

191. *Mheshimiwa Spika*, taratibu za ukamilishaji wa mahitaji ya miundombinu na fedha kwa ajili ya ufungaji wa *video conference* katika mikoa mipya ya Geita, Simiyu, Songwe na Njombe zimefanyika. Kazi nyingine inayofanyika ni marekebisho ya Sheria za Usalama Mtandao (Cyber Laws), ambapo Rasimu ya Mswada wa Sheria ya Kulinda Taarifa

Binafsi (The Personal Data Protection Bill) na rasimu ya Mpango Mkakati wa Kitaifa wa usalama wa mtandao zimeandaliwa. Aidha, uratibu na ukamilishwaji wa upembuzi yakinifu wa kuainisha mahitaji ya muundombinu wa matumizi salama ya Miamala ya Kielektroniki (Public Key Infrastructure – PKI) unaendelea.

192. *Mheshimiwa Spika*, Programu ya RCIP inatelekelezwa kwa kushirikisha taasisi nyingine kupitia miradi ifuatayo:- Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali-Govnet (e-GA); Mfumo wa Wakala wa Usajili, Vizazi na Vifo kupitia RITA; Mfumo wa Taarifa za Biashara kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara; Mfumo wa Taarifa za Kitabibu (Telemedicine system) kupitia Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; Mfumo wa Taarifa za Ununuzi (e-Procurement System); na Mradi wa *Electronic Records* kupitia Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Mradi wa *Govnet* umekamilika na umeunganisha taasisi 72 kwenye mtandao mmoja wa serikali kwa lengo la kuboresha mawasiliano ya maongezi, *data na video* na hivyo kudhitibiti na kuimarisha usalama. Aidha, awamu ya pili ya *Govnet* inaendelea na itaunganisha mamlaka za serikali za mitaa 77 na inatarajia kukamilika mwezi Juni, 2017. Miradi ya mfumo wa taarifa za biashara na mfumo wa taarifa za kitabibu imekamilika na inatarajia kuanza kazi mwezi Mei, 2017. Pia, mifumo iliobakia inatarajia kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2017.

Ofisi Mtandao (e-Office)

193. *Mheshimiwa Spika*, mfumo wa Ofisi Mtandao utawezesha serikali kuwa na mfumo utakaorahisisha utendaji wa shughuli zote za kila siku za ofisi ili kurahisisha utendaji kazi serikalini kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na kuboresha utendaji. Kuanzia Februari 2017 mfumo umeanza kufanya kazi kwa majaribio kwa baadhi ya Ofisi ambazo ni Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (POPSM), Ofisi ya Waziri Mkuu (PMO), Ofisi ya Nyaraka, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA).

UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA MAWASILIANO

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

194. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imetekeleza mradi wa kuunganisha mtandao wa intaneti katika shule za umma 250 kwa kuendelea kutoa huduma ya intaneti na mafunzo katika shule hizo. Aidha, Mfuko uko katika mazungumzo na kampuni ya mawasiliano kwa njia ya Satelite ya Avanti kwa ajili ya uunganishwaji wa shule zingine 50 kupitia awamu ya pili ya mradi huu. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2017 shule zaidi ya 80 zilikuwa zkipata huduma ya mtandao wa intaneti kutokana na ufadhilli mbalimbali ikiwemo Viettel na RCIP.

195. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, iliendelea na utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya TEHAMA kwa upande wa Zanzibar, ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 ujenzi wa vituo 7 katи ya vituo 10 upo katika hatua za mwisho. Aidha, vituo vitatu (3) vya Mahonda, Kitogani na Manispaa Mjini ujenzi wake umekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upanuzi wa kiwanda cha sukari kilichopo Mahonda, Wilaya ya Kaskazini B mkoa wa Kaskazini Unguja, pamoja na upatikanaji wa eneo la ujenzi wa kituo (Kitogani) na ukarabati wa jengo (Manispaa Mjini).

196. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote inatekeleza mradi wa kufikisha huduma za matangazo ya runinga ya kidigitali katika mkoa wa Songwe. Hadi sasa mtoa huduma amekwisha patikana na taratibu za manunuvi zimekamilika ikiwemo kutiwa saini mkataba wa manunuvi ya ving'amuvi hivyo baina ya Mfuko na *Star Times*. Aidha, Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017 ambapo jumla ya ving'amuvi 500 vitauzwa kwa wananchi kwa bei ya ruzuku kutoka katika Mfuko.

197. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, imetekeleza mradi wa wasichana

na TEHAMA ambapo wanafunzi 240 wa kidato cha III walikusanyika katika kanda sita na kupewa mafunzo mbalimbali yahusuyo TEHAMA na uandishi wa programu za kompyuta. Washindi watano kutoka katika kila kanda walikusanyika Dar es Salaam katika shindano la Taifa lililowapata washindi watano wengine watakaoshiriki katika mkutano wa ITU utakaofanya Addis Ababa, Ethiopia tarehe 27 Aprili, 2017. Dhumuni kubwa la mashindano hayo ni kuwapa motisha wasichana kupenda masomo ya sayansi na TEHAMA.

198. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeendelea na utekelezaji wa mradi wa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu kutoka shule mbalimbali zilizonufaika na miradi ya kuunganishwa na mtandao wa intaneti. Jumla ya walimu 300 wanategemewa kupewa mafunzo haya kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT).

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano (TTMS)

199. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kusimamia uendeshaji kwa ufanisi mtambo wa TTMS ili kuwezesha mifumo ambatanishi iliyowekwa kufanya kazi zake vizuri. Mifumo hiyo ni pamoja na; Mfumo wa Usimamizi wa mawasiliano ya simu za Ndani (Local Off-net and On-net Traffic Monitoring) na zile za Kimataifa (International Traffic Monitoring); Mfumo wa Usimamizi wa ubora wa huduma (Quality of Service (QoS) Platform); Mfumo wa Kubaini Simu za Ulaghai (Antifraud Management System); na Mfumo wa Miamala ya Fedha (Mobile Money Transactions Monitoring).

200. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai – Septemba, 2016 TCRA iliweza kukamilisha utekelezaji wa

mfumo wa kutambua takwimu za mawasiliano ya simu za ndani ya kila mtandao wa kampuni (On-net traffic). Aidha, kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Februari, 2017 Mamlaka imeweza kufanya matengenezo ya kawaida (preventive maintenance) ya vifaa vilivyofungwa katika maeneo ya watoa huduma na vifaa vilivyopo katika chumba cha usimamizi wa mawasiliano (NOC). Vilevile, TCRA inaendelea na utekelezaji wa mfumo wa usimamizi wa mawasiliano ya simu za ndani (on-net traffic), idadi ya miamala ya fedha, tozo za TRA, fedha zilizopo kwenye mzunguko wa simu za mkononi pamoja na taarifa za mfumo wa rajisi (CEIR) zipatikane kwa wakati "on real time".

201. *Mheshimiwa Spika*, sambamba na kazi hizo TCRA imeendelea na zoezi la kufanya vipimo katika mitandao ya makampuni ya simu (quality of service measurements) kwa ajili ya kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na makampuni ya simu. Vipimo hivyo vilifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Iringa, Tanga na Mtwara. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa mteja anapata huduma zenye ubora.

202. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka imeweza pia kufanya malipo ya kila mwezi kwa Serikali (Hazina na COSTECH) pamoja na mkandarasi yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa zinazoingia na kuishia hapa nchini kama ilivyoelekezwa na Kanuni ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (TTMS) ya mwaka 2013 na maboresho yake. Kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2016 TCRA imeweza kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (HAZINA) kiasi cha **Shilingi 13,214,914,648.67** na **Shilingi 5,170,133,295.76** ziliwasilishwa katika Mfuko wa NFAST COSTECH, ikilinganishwa na **Shilingi 20,520,017,341.46** kwa kipindi cha Januari-Desemba, 2015 kilichowasilishwa HAZINA. Kupungua kwa makusanyo kunatokana na kuongezeka kwa matumizi ya data ambazo bei zake ni nafuu ikilinganishwa na simu za maongezi (voice).

Mfumo wa Kumbukumbu za Simu za Kiganjani kwa Kushirikiana na Watoa Huduma wa Simu za Kiganjani (CEIR).

203. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Februari 2017 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliendelea na usimamizi wa uendeshaji wa mfumo wa Rajisi ya namba tambulishi za simu za Kiganjani kwa ufanisi. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ushirikishwaji wa watoa huduma hasa kuhakikisha kuwa namba tambulishi mpya (IMEI) zinazotumwa na Shirikisho la makampuni ya simu duniani (GSMA) zinaakisiwa katika mifumo ya CEIR na EIR na kuwezesha uendeshaji mzuri wa mfumo.

204. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka pia imeweza kufanya matengenezo ya kawaida ya vifaa viliviyofungwa katika maeneo ya watoa huduma na vifaa viliviyopo katika chumba cha Usimamizi wa mawasiliano (Network Observation Center- NOC). Katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Februari, 2017 TCRA iliweza kuzifungia simu zisizo na ubora zipatazo 1,580,333. Simu zilizofungwa haziwezi kutumika tena katika mtandao wowote hapa nchini. TCRA inaendelea kutoa elimu pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuondoa tatizo la simu zisizo na viwango hapa nchini.

Usalama wa Mitando ya Mawasiliano - Tanzania Computer Emergency Response Team (TZ-CERT)

205. *Mheshimiwa Spika*, ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) umekuja na fursa nyngi na unakabiliwa na changamoto nyngi ambazo zinaathiri maendeleo ya TEHAMA. Athari hizo ni pamoja na uhalifu kmtandao (cyber Crime), ugaidi kwenye mifumo ya mitando (Cyber terrorism) na Uharibifu wa mila na desturi (mfano picha zisizo na maadili kwenye mitando). Mamlaka ya Mawasiliano kuititia kituo cha TZ-CERT imeendelea kusimamia usalama wa mitando nchini kwa kuhakikisha uwezo wa wataalamu wa serikali na taasisi binafsi unaboreshwu ili kulinda usalama wa Mitando na huduma

zake pamoja na kuwa na vifaa muhimu vyatia kugundua matatizo ya usalama na kuyatatu mapema iwezekanavyo.

Utekelezaji wa Mobile Number Portability (MNP)

206. *Mheshimiwa Spika*, huduma hii imeanza rasmi tarehe 1 Machi 2017. Huduma ya hiari inayompa uhuru mtumiaji wa simu wa kuhama toka mtandao mmoja wa huduma za mawasiliano ya simu za kiganjani kwenda mtandao mwingine wowote anaoutaka na kuendelea kupata mawasiliano bila kubadili namba yake ya simu. Lengo ni kuongeza ushindani kwenye sekta ya mawasiliano na hivyo kuwa kichocheo cha utoaji huduma bora na zenye gharama nafuu maana kama huduma haziridishi, basi wateja watahama na namba zao toka mtoa huduma mmoja kwenda mwingine.

Shirika la Posta Tanzania (TPC)

207. *Mheshimiwa Spika*, Shirika limeendelea kutoa huduma ya kusambaza barua, nyaraka, vipeto na vifurushi kwa kupitia mfumo wa kawaida wa masanduku na mifuko ya kupokelea barua iliyoko katika ofisi za posta nchini pamoja na mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi ambao huwafikia wateja hadi majumbani/ ofisini kwao. Shirika limeendelea kuimarisha huduma ya "Posta Mlangoni" ambapo huduma zimetolewa katika Kata ambazo miundombinu ya Anwani za Makazi imekamilika ambazo ni kata 8 mkoani Arusha; kata 32 jijini Dar es Salaam na kata 8 zilizoko Dodoma. Utoaji wa huduma kwa Zanzibar utaanza kabla ya mwisho wa mwaka huu 2016/2017 ambako wadi 2 Unguja na wadi 4 Pemba zenye miundombinu zitahusika.

208. *Mheshimiwa Spika*, Shirika lina mtandao wa Ofisi 110 zilizounganishwa katika mtandao wa *Postglobal NetSmart*. Ofisi hizi zinaweza kufuatilia (Track and Trace) nyaraka, vifurushi na vipeto vinavyotumwa kupitia mtandao wa Posta. Huduma nyingine zinazo patikana kupitia mtandao ni za Mfumo wa kifedha. Jitihada zinaendelea kuunganisha Ofisi nyingine 30 kadiri ya mtiririko wa fedha

utakavyoruhusu ili kufikia Ofisi 140 kabla ya mwisho wa mwaka 2016/2017. Shirika pia linakamilisha uanzishwaji wa huduma ya Biashara Mtandao itakayoliwezesha kuuza bidhaa zake zikiwemo Stempu na bidhaa nyingine kuititia tovuti ya Duka Mtandao: <http://www.stamps.tz.post>

Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)

209. *Mheshimiwa Spika*, TTCL inaendelea na utekelezaji wa mpango mahsus wa kusimika mtandao wa kisasa wa 3G/4G LTE. Katika kipindi hiki cha mwaka 2016/2017 TTCL ilifanya uzinduzi wa Nembo Mpya (new Corporate Image). Uzinduzi wa nembo mpya ya TTCL ni sehemu ya utekelezaji wa mkakatiwa mabadiliko ya kibiashara unaolenga katika kuifanya TTCL kushindana kwa mafanikio katika soko la mawasiliano ya simu na huduma za data. Mpaka sasa TTCL imesimika mtandao wa 3G na 4G kwenye miji mikuu 10 ya mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Zanzibar, Morogoro, Pwani, Mbeya, Arusha, Tanga, Pemba na 2G katika maeneo ya vijijini chini ya mradi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF). Kabla ya mwisho wa mwaka 2017 itakuwa imefikia miji yote mikuu ya mikoa.

210. *Mheshimiwa Spika*, sambamba na hilo TTCL pia imekamilisha usimikaji wa mitambo mipy ya kutoa huduma za ziada (value added service) kwa ajili ya kutoa huduma za ujumbe mfupi na pia mitambo ya kutoa huduma za kupokea na kutuma miamala ya fedha (mobile money platform). Huduma za kupokea na kutuma miamala ya fedha zitaanza kutumika mara tu taratibu za kupata leseni ya kutoa huduma kutoka Benki kuu zitakapokamilika ikiwa ni pamoja na kukamilisha usajili wa Kampuni tanzu *Mobile Moneykama* ilivyo kwenye kanuni mpya ya Benki Kuu.

Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

211. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kuititia Tume ya TEHAMA imeanza kutekeleza mpango wa kutambua na kuendeleza wataalam wa TEHAMA nchini. Hadi kufikia Machi

2017, zaidi ya wataalam wa TEHAMA 700 wameitikia wito wa kuanza kwa zoezi hilo na kurejesha fomu za kuomba kutambuliwa. Zoezi la utambuzi linakwenda sambamba na kubaini fani za TEHAMA zisizo na wataalam au zenyé wataalam wachache ukilinganisha na mahitaji ya soko la ndani na kimataifa. Aidha, Mpango huu utasaidia taifa kuwa na wataalam walio na ubora uliothibitishwa na kuzingatia miiko ya utaalam inayotambulika kimataifa.

TAASISI ZA MAFUNZO

212. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inasimamia vyuo vya mafunzo vifuatavyo:

Chuo cha Ujenzi Morogoro

213. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Chuo kilipanga kufundisha jumla ya wanafunzi **945** katika fani za ufundi stadi wa kazi za barabara, majengo pamoja na udereva. Chuo pia kilipanga kujenga karakana mpya ya Ufundji Bomba; kununua gari moja (1) kwa ajili ya kufundishia madereva; kununua kifaa cha kielektroniki cha kukagulia magari pamoja na kukarabati majengo matatu na mitambo mitatu (3) ya kufundishia.

Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya wanafunzi **909** wa fani za ufundi stadi wa kazi za barabara, majengo pamoja na udereva walipata mafunzo. Aidha, Chuo kiliendelea na ukarabati wa majengo matatu (3) ya chuo na kumbi mbili (2) za mikutano pamoja na kununua vifaa vya kufundishia ikiwemo viyoyozи vipya na kukarabati vilivyopo sita (6). Chuo pia kilifanikiwa kununua gari jipya *TOYOTA Hilux Double Cabin* pamoja na kununua kifaa cha kielektroniki cha kukagulia magari (vehicle diagnostic machine).

Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute - ATTI)

214. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Chuo kilipanga kuendesha mafunzo ya ukarabati

na matengenezo ya barabara za changarawe; mafunzo ya uwekaji tabaka la lami (*Surface Dressing*) kwa Wahandisi (10), Mafundi Sanifu (30) na wasimamizi wa barabara (30); kuboresha mitaala ya Chuo ya utoaji wa mafunzo ya teknolojia stahiki ya nguvukazi pamoja na kuendelea kutoa mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa vitendo. Aidha, Chuo kitaendelea na utoaji wa mafunzo na kuhamasisha matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa umma kwa njia ya makongamano na kuendelea kutoa ushauri wa matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa wadau mbalimbali.

215. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Machi, 2017, Chuo kimetoa mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa wasimamizi wa barabara kutoka Halmashauri za Wilaya na sekta binafsi; kimetoa mafunzo ya uwekaji wa tabaka la lami kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kwa Wahandisi na Mafundi sanifu kutoka Halmashauri za Wilaya na sekta binafsi; kimetoa mafunzo ya awali kwa wasimamizi wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na kuendesha mafunzo yaliyoratibiwa na Wizara ya kuwajengea uwezo wanawake katika kushiriki kazi za barabara nchini. Wanawake hamsini (50) walipata mafunzo yaliyofanyika chini ya kitengo cha kushirikisha wanawake katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara.

Vilevile, Chuo kimeendelea kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kwa wadau wa sekta ya ujenzi katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Morogoro, Singida, Dodoma, Tabora, Mbeya na Rukwa pamoja na kutoa mafunzo kwa njia ya vitendo kupitia barabara za mafunzo na kuweza kuzifanya matengenezo na ukarabati jumla ya kilomita 1.13 katika Halmashauri ya Rungwe na barabara za mafunzo kilomita 21 chini ya Wakala wa Barabara (TANROADS) Mbeya zilitengenezwa na kufanya matengenezo ya mara kwa mara. Katika kazi hizi za matengenezo ya barabara wananchi wapatao 105

wamenufaika pamoja na kupata ujuzi wa kukarabati na kutengeneza barabara zao kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

216. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kimeendelea kutoa huduma za mafunzo, utafiti, ukarabati wa vifaa vya kuokolea maisha majini na uwakala wa ajira kwa wafanyakazi melini. Mafunzo yaliyotolewa yalilenga kuendeleza rasilimali watu na kuboresha utendaji wao katika sekta ya usafiri majini. Aidha, Chuo kilendelea kutoa mafunzo ya *refresherili* kukidhi vigezo na masharti ya Mkataba wa Kimataifa wa mafunzo ya mabaharia (STCW 1978 Manila Amendment). Katika mwaka 2016/2017, Chuo kilidahili wanafunzi 509 katika kozi ndefu. Kati yao, wanafunzi 25 ni wanawake na wanafunzi 31 walitoka nje ya Tanzania. Chuo pia kilidahili wanafunzi 5,109 wa kozi fupi ambapo kati ya hao wanafunzi 512 walitoka nje ya Tanzania.

217. Mheshimiwa Spika, Chuo kimeendelea kupata ithibati katika fani mbalimbali ili kutoa huduma bora na zenye tija. Jumla ya mitaala 9 katika fani za uhandisi wa meli na usafirishaji majini illihuishwa. Aidha, mitaala mipyä 5 katika fani ya *Shipping and logistics Management* itaanza kutumika Septemba, 2017. Kuanza kutumika kwa mitaala hii kutafanya Chuo kuwa na jumla ya ithibati 14 za *National Technical Award* (NTA) kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (National Council for Technical Education – NACTE). Vilevile, Chuo kina jumla ya ithibati 37 za kutoka SUMATRA. Ithibati hizi zinahusu kozi fupi za ujuzi na usalama melini.

218. Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu wa eneo kilipo Chuo kwa sasa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma zake ilikamilika Novemba, 2016. Kazi zinazoendelea ni pamoja na kutafuta mbia kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ujenzi wa Chuo kwa utaratibu wa kuishirikisha Sekta Binafsi na Sekta ya Umma; kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga uazio katika eneo la Chuo Wilayani Mkuranga na kukamilisha mitaala ya kozi mipyä za sheria za

masuala ya bahari na bima za uchukuaji na usafirishaji wa mizigo (Maritime Law & Insurance) inayotarajiwa kukamilika Mei, 2017.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

219. *Mheshimiwa Spika*, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kimeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika nyanja za lojistiki, menejimenti na teknolojia ya usafirishaji. Katika mwaka 2016/2017, Chuo kilidahili wanafunzi 2,910 ikilinganishwa na wanafunzi 2,516 waliodahiliwa mwaka 2015/2016. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 16. Aidha, mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Uzamili ya Lojistiki na Menejimenti ya Ushafirishaji yalianza kutolewa. Mitaala ya shahada ya uzamili katika menejimenti ya bandari na usafiri wa majini na menejimenti ya usafiri wa anga inaendelea kupitiwa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu kwa ajili ya kupata ithibati.

220. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017 nililitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya kuanza rasmi kwa kozi ya Stashahada na Shahada ya Kwanza ya Uhndisi wa Matengenezo ya Ndege (Aircraft Maintenance Engineering). Napenda kulitaarifu Bunge lako kuwa kozi hizi zimepokelewa vizuri ambapo jumla ya wanafunzi 40 walidahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 38 walidahiliwa katika mwaka 2015/2016. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 5. Aidha, ili kuendelea kuboresha huduma za elimu zinazotolewa, Chuo kimenunua *simulator* ya kufundishia marubani katika ngazi ya awali (CR-12 Pro Panel Flight Simulator) na kupata msaada wa ndege moja kutoka Shirika la *Tropical Airya* Zanzibar kwa ajili ya mafunzo ya marubani ya kuruka na kutua ndege.

221. *Mheshimiwa Spika*, Chuo cha NIT kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imeendelea kutoa elimu ya mazingira na kukagua magari yaliyotumika na kuingizwa nchini kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Magari haya hukaguliwa katika Kituo Cha Kisasa Cha Ukaguzi wa Magari kilichoko katika maeneo ya Chuo. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya magari 679 yalikaguliwa ikilinganishwa

na magari 544 yaliyokaguliwa katika mwaka 2015/2016. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 25 na limetokana na kuongezeka kwa uzoefu wa wafanyakazi katika kufanya kazi hiyo.

Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC)

222. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (Civil Aviation Training Centre - CATC) kinaendelea kutoa mfunzo kwa wanafunzi wa ndani na nje ya nchi. Nchi ambazo zimekuwa zikitoa wanafunzi kujiunga na Chuo hiki ni pamoja na Uganda, Burundi, Rwanda Zambia, Botswana, Swaziland, Namibia, Somalia, Kenya, Ghana, Nigeria na Liberia. Mafunzo hayo yanahusu taaluma za uongozaji ndege; mafundi wa mitambo ya kuongozea ndege; wataalam wa mawasiliano ya urukaji; usalama na upekuzi; safari za ndege na usimamizi wa viwanja vya ndege.

223. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Mamlaka ilipanga kununua mashine ya *Simulator* ya kufundishia wanafunzi. Uthamini wa zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mashine hii ulikamilika Februari, 2017. Kazi inayoendelea ni majadiliano na mzabuni ili kusaini mkataba ifikapo Julai, 2017. Aidha, katika mwaka 2016/2017, jumla ya wanafunzi 700 walihitimu mafunzo mbalimbali kutoka katika Chuo hiki.

Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma

224. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kukiboresha Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ili kiweze kutoa mafunzo yenye tija. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya wanafunzi 57 walihitimu mafunzo ya hali ya hewa. Kati yao, wanafunzi 33 walihitimu katika ngazi ya mafunzo ya Cheti na wanafunzi 24 katika ngazi ya Stashahada. Aidha, Chuo kiliweza kutoa mafunzo ya hali ya hewa mahsus kwa sekta ya Usafiri wa Anga ambapo jumla ya wanafunzi 19 walihitimu mafunzo hayo. Katika kipindi hicho, wanafunzi 57 walidahiliwa ili kujiunga na masomo katika ngazi ya Cheti na Stashahada.

MASUALA MTAMBUKA

Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara

225. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa wanawake wanashirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilizindua rasmi Mwongozo wa Ushirikishwaji wa Wanawake katika kazi za barabara ambapo nakala 550 za Mwongozo huo zimechapishwa na kugawanywa pamoja na kutoa elimu kwa wadau kuhusu matumizi ya miongozo hiyo kupitia Warsha. Vilevile, mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu (Database) kwa wanawake wanaoshiriki kazi za barabara umezinduliwa na unatumika. Wizara pia iliendelea kutoa mafunzo kwa Makandarasi wanawake kuhusu kutumia teknolojia ya nguvukazi pamoja na namna ya kuandaa zabuni ambapo wanawake hamsini (50) walishiriki.

Ushiriki wa Wizara Katika Jumuiya Mbalimbali za Kimataifa

226. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kushiriki katika masuala yanayohusu Sekta ya Ujenzi katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda na hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

227. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara kupitia Sekta ya Ujenzi imeendelea na utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya barabara iliyoidhinishwa mwaka 2012 na Wakuu wa Nchi za EAC ambayo itawezesha kuboresha huduma za bandari na reli zinazohudumia Tanzania na nchi jirani. Kazi zilizofanyika ni; kuendelea na mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya Nyakanazi -Kasulu - Manyovu (km 250) inayoungana na barabara ya Rumonge - Bujumbura kwa upande wa Burundi na barabara ya Lusahunga - Rusumo (km 91) inayoungana na barabara ya Kayonza - Kigali kwa upande wa Rwanda chini ya uratibu wa Sekretariati ya

Jumuia ya Afrika Mashariki; Maandalizi ya Awamu ya Pili ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT II) katika barabara ya Kilwa ambao utajumuisha maboresho ya makutano ya Uhasibu, KAMATA na Chang'ombe yanaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Aidha, ujenzi wa TAZARA *Flyover* unaofadhiliwa na Serikali ya Japan unaendelea.

Mkataba wa ujenzi wa Ubungo *Interchange* umesainiwa mwezi Februari 2017 na ujenzi kuzinduliwa Machi, 2017; Upanuzi wa barabara ya Arusha (Sakina) – Tengeru (km 14.1) na ujenzi wa Arusha Bypass (km 42.4) unaendelea. Kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni wa barabara ya Bagamoyo (Makurunge) – Saadani – Tanga (km 178) imekamilika na taratibu za kupata fedha za ujenzi kutoka AfDB zinaendelea.

228. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Ujenzi pia imeendelea kushiriki kikamilifu katika mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu masuala ya mtangamano. Baadhi ya masula muhimu yanayoendelea kujadiliwa ni: Uwianishaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango kuhusu usafirishaji wa mizigo mizito kwa magari makubwa kwa njia ya barabara pamoja na Majadiliano ya Biashara ya Huduma (Trade In Service) kwa nchi wanachama wa SADC ambayo yamelenga kufungua na kupanua fursa za utoaji huduma kwa Sekta ya Ujenzi zikiwemo kazi za ujenzi, huduma za kihandisi pamoja na huduma za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya barabara katika Mpango Kamambe ni kama ifuatavyo: Upembuzi yakinifu umekamilika kwa ajili ya ujenzi wa Dar es Salaam – Chalinze *Expressway* (km124) itakayotumiwa na wasafirishaji wa nchi za Burundi, DR Congo, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia; taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Mtwara – Mbamba Bay sehemu ya barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) inayounganisha Tanzania na nchi za Malawi na Zambia zinaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Kwa upande wa Umoja wa Afrika, Wizara ilishiriki katika mukutano wa Kamati Maalum ya Ufundu (*African Union Specialized Committee on Transport, Transcontinental and Interregional Infrastructure, Energy and Tourism*) uliofanyika Lome, Togo kuanzia tarehe 13 – 17 Machi, 2017. Mukutano huo uliandaliwa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika (African Union Commission – AUC) kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Togo, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na *United Nations Economic Commission for Africa (UNECA)*.

Masuala Mengine Yaliyotekelawa na Wizara

229. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Ujenzi imeendelea kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka watumishi 5 katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi kumi na wawili (12) walihudhuria mafunzo ya muda mfupi.

Aidha, Wizara imeendelea kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuongeza ufanisi na kutoa huduma kwa wakati. Mfumo wa utoaji wa vibali vyta mizigo inayozidi uzito barabarani kwa njia ya kielektroniki unaendelea kutoa huduma kwa wasafirishaji ndani na nje ya nchi. Tovuti ya Wizara imboreshwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata taarifa mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi. Wizara pia imeshiriki katika mikutano na mafunzo yanayolenga matumizi ya TEHAMA ili kuboresha utendaji wa kila siku. Wizara imeendelea na zoezi la kuweka takwimu katika *Database* ya Wizara inayotoa taarifa kuhusu maendeleo ya ujenzi wa barabara, vivuko, nyumba na majengo ya Serikali.

230. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sera na mipango inayosimamiwa na Wizara pamoja na kuzitunza na kuhifadhi barabara zetu, kuzingatia sheria na kanuni za matumizi ya barabara. Vilevile, Wizara kupitia Kitengo cha Huduma za Kisheria imeendelea kushiriki katika ukamilishaji

wa rasimu ya kanuni za Usajili wa Makandarasi (The Contractors Registration Board Regulations) chini ya Sheria ya Usajili wa Makandarasi ya mwaka 1997 na kufuatilia mashauri mbalimbali yanayohusu Wizara mahakamani.

231. *Mheshimiwa Spika*, majukumu mengine yaliyotekelawa na Wizara ni pamoja na; kuandaa na kuwasilisha Taarifa ya Hesabu ya Mwaka 2016/2017 kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wizara ya Fedha na Mipango; kuandaa taarifa za takwimu za Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2016; kuandaa na kupitia Sheria, Kanuni na Sera zinazohusu Sekta ya Ujenzi; kupitia na kushauri kuhusu mikataba inayohusu Sekta ya Ujenzi; pamoja na ufanya mapitio ya Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003 (Construction Industry Policy, 2003) na maandalizi ya mkakati wa utekelezaji.

D. CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

232. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na:

233. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, **mtiririko hafifu wa fedha za maendeleo** ulisababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na hivyo kuathiri malengo yaliyowekwa. Ili kukabiliana na changamoto hii, Wizara iliendelea kufuatilia fedha za maendeleo kutoka HAZINA kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyopangwa;

234. *Mheshimiwa Spika*, Wizara pia ilikabiliwa na changamoto ya **makandarasi kusimamisha kazi za ujenzi mara kwa mara kutokana na kutolipwa malimbikizo ya madai yao**. Mkakati uliopo ni pamoja na kuendelea kuwashawishi makandarasi na watoa huduma kuendelea na utekelezaji wamiradiwakati Serikali ikishughulikia madai yao.

235. *Mheshimiwa Spika*, kuna changamoto ya **uchakavu wa miundombinu ya reli na bandari** kutokana na kukosa matengenezo kingamizi. Changamoto hii imeendelea kukabiliwa kwa kuandaa mipango ya biashara (business plan) ya mashirika ya reli na bandari ili kusaidia ushawishi wa kutafutia fedha za kuboresha utendaji na kuleta tija ikiwa ni pamoja na kushirikisha sekta binafsi.

236. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu changamoto ya **uchakavu na uchache wa vitendea kazi** kama vichwa vya treni na mabehewa, Wizara imeendelea kujenga uelewa kwa wawekezaji na wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi ili wazione fursa zilizopo na hivyo kuwekeza kwenye sekta ya Uchukuzi kupitia mpango wa ubia wa sekta ya umma na binafsi (PPP).

237. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa changamoto inayokabili huduma za reli ya **uharibifu/hujuma zinazofanywa na wananchi katika miundombinu ya reli** pamoja na **mafuriko na wizi wa vyuma chakavu**, Wizara imeendelea kusimamia Sheria zilizopo kuhusu uharibifu huo pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kutunza miundombinu ya uchukuzi kwa lengo la kupunguza hujuma ya miundombinu hiyo. Aidha, mikakati ya kukabiliana na mafuriko yanayoweza kuharibu miundombinu ya reli, Wizara kupitia TRL/RAHCO imeendelea kufanya matengenezo kingamizi (preventive maintenance). Vilevile Serikali imeendelea na juhudzi za kushirikisha jamii inayokaa pembeni ya miundombinu ya reli katika kuilinda. Lengo ni kupunguza au kuondokana na vitendo vya kuihujumu miundombinu hiyo.

238. *Mheshimiwa Spika*, changamoto nydingine ni **madai ya fidia** katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia ya mali za wananchi wanaotakiwa kupisha utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya uchukuzi.

E. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

239. *Mheshimiwa Spika*, vipaumbele veya miradi ya Wizara itakayotekelawa katika mwaka 2017/2018 ni miradi inayoendelea kutekelezwa, miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo na miradi iliyoinishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021), Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2015 na Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali.

E.1 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA SEKTA ZILIZO CHINI YA WIZARA

E.1.1 SEKTA YA UJENZI

Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato, Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

240. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano(Sekta ya Ujenzi) inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 62,004,000.00** kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Kiufundi na Kitengo cha Menejimenti ya Huduma za Ununuzi na Ugavi.

241. *Mheshimiwa Spika*, bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara kwa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni Shilingi **34,123,282,000.00**. Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi 1,895,582,432,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kama inavyooneshwaa katika **Kiambatisho Na.1**. Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

MRADI WA KUJENGA UWEZO (INSTITUTIONAL SUPPORT)

242. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 250.00** fedha za ndani. Fedha hizo zitatumika kuwapatia Watumishi wa Sekta ya Ujenzi mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali kwa lengo la kuwaimarisha kitaaluma. Aidha, fedha hizo zitatumika kununua vitendea kazi na vifaa vya ofisi.

MIRADI YA VIVUKO, UJENZI WA NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI 0755951992

Vivuko na Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko

243. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 10,000.00** kwa ajili ya miradi ya vivuko kama ifuatavyo:

i) Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko

244. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu una lengo la kujenga maegesho ili vivuko viweze kuegeshwa na kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye vivuko kwa urahisi nyakati zote za mwaka. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 1,361.00** kwa ajili ya upanuzi wa maegesho ya Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bwina, Bukondo na Zumacheli mkoani Geita; ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Lindi – Kitunda pamoja na kazi ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hii.

ii) Ununuzi wa Vivuko Vipyta

245. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 6,683.00** kwa ajili ya malipo ya mwisho ya ununuzi wa kivuko kipyta cha Magogoni – Kigamboni; kukamilisha ununuzi wa kivuko

kipya cha Kigongo – Busisi; ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA pamoja na kazi za ufuatiliaji wa miradi hii.

iii) Ukarabati wa Vivuko

246. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka w a fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni **1,956.00** kwa ajili ya kukarabati vivuko vya MV Pangani II; MV Sengerema; MV Kigamboni; MV Misungwi pamoja na kazi ya ufuatiliaji wa miradi hii.

Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

247. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 12,450.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatavyo:

i) Ujenzi wa Nyumba za Viongozi na Ofisi za Serikali

248. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 10,795.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za viongozi wa Serikali. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 10,000.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 50 za Viongozi Dodoma na **Shilingi milioni 795.00** ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba 5 za Majaji katika Mikoa ya Dar es Salaam (1), Kilimanjaro (1), Kagera (1), Mtwara (1) na Shinyanga (1).

ii) Ujenzi wa Nyumba za Makazi Magomeni Quarters

249. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 100.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba za Magomeni Quarters.

iii) Huduma za Ushauri, Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Majengo na Nyumba za Serikali

250. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 205** zimetengwa kwa ajili ya huduma za ushauri, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Serikali.

iv) Ukarabati wa Nyumba, Ofisi, Karakana, na Ununuzi wa Samani kwa Nyumba za Viongozi

251. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 800.00** zimetengwa kwa ajili ya kukarabati nyumba za viongozi na ununuzi wa samani kwenye lkulu Ndogo za Serikali na Viongozi wa Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano – Sekta ya Ujenzi wenye stahili ya kupewa samani.

v) Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

252. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 50** zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors) kupitia Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB).

vi) Ujenzi wa Karakana za TEMESA

253. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Karakana za TEMESA katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi.

MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA

254. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara itaendelea kutekeleza sera ya kuunganisha mikoa yote kwa barabara za lami pamoja na kupunguza msongamano wa magari katika majiji na miji mikubwa

hususan katika jiji la Dar es Salaam. Maelezo ya kina ya miradi itakayotekelawa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni kama ifuatavyo:

Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 200) sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 144)

255. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 12,771.00** kwa ajili ya kulipa fidia ili kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze (km 144) kwa kiwango cha "Expressway" kwa utaratibu wa kushirikisha Serikali na Sekta Binafsi (Public Private Partnership - PPP). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na ukarabati wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44.2) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6).

Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata

256. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 25,912.00** kwa ajili ya sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Bagamoyo – Msata (km 64); maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara za Bagamoyo (Makurunge) – Saadan – Tanga (km 178), Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (sehemu ya Tegeta – Bagamoyo: km 46.9), Mbegani – Bagamoyo (km 7.2) na Makofia – Mlandizi (km 36.7). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24) na Kisarawe – Maneromango (km 54).

Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo - Kyamyorwa (km 352)

257. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 35,379.00** fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Uyovu – Bwanga – Biharamulo (km 112) na ukarabati wa barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo

(km120). Aidha, kazi nyingine kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3) na Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7).

Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 353.7)

258. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 47,858.00** kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya malipo ya mwisho ya Makandarasi waliojenga miradi ya Daraja la Kikwete katika Mto Malagarasi, barabara ya Kidahwe – Uvinza (km 76.6), Tabora – Ndono (km 42) na Ndono – Urambo (km 52). Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa sehemu ya Kaliua – Kazilambwa (km 56) pamoja na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Uvinza – Malagarasi (km 51.1) na Urambo – Kaliua (km 28).

Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai - Kamwanga/Bomang'ombe – Sanya Juu (km 171)

259. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 33,932.70** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya mwisho ya Makandarasi wa barabara ya Rombo Mkuu – Tarakea (km 32), Marangu – Rombo Mkuu/Mwika – Kilacha (km 32) na KIA – Mererani (km 26). Aidha, sehemu ya fedha hizo itatumika kuendelea na ujenzi wa njia nne kutoka njia mbili za sasa wa barabara ya Arusha – Moshi – Holili/Taveta – Voi sehemu ya Sakina – Tengeru (km 14.1), njia mbili kwa barabara ya Mchepuo ya Arusha (Arusha Bypass: km 42.4), Kwa Sadala – Masama – Machame Jct (km 16.0), Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Sanya Juu – Alerai: km 30) na Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST – km 14). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kiboroloni – Kikarara – Tsuduni – Kidia (km 10.8), na kuanza maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105) pamoja na ujenzi wa mizani ya Himo.

Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara ya Mchepuo kuingia Manyoni Mjini (km 4.8)

260. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,036.00** kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini na malipo ya sehemu ya gharama za usuluhishi (Arbitration) kwa sehemu ya Dodoma – Manyoni. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni) na kujenga mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion – WIM) eneo la Nala (Dodoma).

Ukarabati wa Barabara ya Port Access (Nelson Mandela) (km 6)

261. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 308.00** kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa barabara sehemu ya Dar es Salaam Port – TAZARA (km 6) chini ya awamu ya pili ya mradi wa *Dar es Salaam Maritime Gateway* utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Barabara ya Dumila – Kilosa - Mikumi (km 141)

262. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,207.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi aliyejenga sehemu ya Dumila – Rudewa (km 45), kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 18) pamoja na maandalizi ya ujenzi wa mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion - WIM) eneo la Dakawa.

Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112)

263. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 20,957.00** zimetengwa

kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai –Kasanga Port (km 112) na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50).

Ujenzi wa Madaraja Makubwa

264. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 36,301.00** kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Makandarasi waliojenga Daraja la Kilombero (Morogoro) na Daraja la Kavuu (Katavi); kuanza ukarabati wa Daraja la Kirumi (Mara); kuendelea na ujenzi wa Daraja la Sibiti (Singida), Daraja la Ruhuhu (Ruvuma), Daraja la Momba (Rukwa/Songwe), Daraja la Sukuma (Mwanza), Daraja la Mlalakuwa (Dar es Salaam) na Daraja la Mara (Mara). Kazi zingine ni kuanza ujenzi wa Daraja la Wami (Pwani), Daraja Jipya la Selander (Dar es Salaam), Daraja la Magara (Manyara); kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Simiyu (Mwanza), Daraja la Kigongo/Busisi (Mwanza), Daraja la Muhimbili (Dar es Salaam), Daraja la Mtera (Dodoma) na kununua vyuma vya Daraja la Dharura (*Emergency Bridge Parts*).

Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta: km 17)

265. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya **Shilingi milioni 318.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.2) na uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua kwenye barabara ya Mwenge – Tegeta (km 12.8).

Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 170)

266. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 7,830.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1) pamoja na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa sehemu ya Bugene – Kasulo (km 124) na Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105).

Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242)

267. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 18,768.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi wa barabara ya Isaka – Ushirombo (km 132), kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110) na ukarabati wa dharura wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 92). Kazi nyingine ni maandalizi ya ujenzi wa mizani inayopima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion – WIM) ya Nyakanazi (Kagera).

Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7)

268. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 45,864.25** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Tabora – Nyahua (km 85), kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.3) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85.4). Mradi huu utagharamiwa kwa fedha za mkopo nafuu kutoka KUWAIT Fund.

Barabara ya Korogwe – Handeni (km 65)

269. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 4,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara hii.

Barabara za Mikoa

270. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 30,000.00** zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya kilometra **469.5** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometra **58.4** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja **12**. Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa

itakayotekelawa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)

271. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya **Shilingi milioni 342.00** zitatumika kuanza kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuifanya ukarabati barabara hii.

Barabara ya Handeni – Mkata (km 54)

272. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, barabara ya Handeni – Mkata (km 54) imetengewa **Shilingi milioni 1,458.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

Mradi wa Kuondoa Msongamano Barabara za Dar es Salaam (km 156.7)

273. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 12,409.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara za Kimara – Kilungule – External (km 9.0) na Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi Mwisho (sehemu ya Goba - Mbezi Mwisho: km 7.0); Tangi Bovu – Goba (km 9.0); kuendelea na ujenzi wa barabara za Mbezi – Malambbamawili – Kinyerezi – Banana (km 14.0); Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6); Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.7); Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7); Ardhi – Makongo – Goba (km 9.0); sehemu ya Goba –Makongo (km 4.0); Maji ya Chumvi – Chang'ombe – Barakuda (km 2.5); kuanza ujenzi barabara za Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (*One Lane Widening*) (km 25.1); Mwai Kibaki (km 9.1); Mjimwema – Kimbiji (km 27.0) na Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba (km 13.0); sehemu ya Madale – Goba (km 5.0).

Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)

274. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya Shilingi milioni **626.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii.

Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/ Songea (km 464)

275. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni **20,256.867** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu za Kidatu – Ifakara (km 68) na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396).

Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 359)

276. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni **69,273.938** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara sehemu ya Mpanda – Koga – Ipole – Usesula (km 343) pamoja na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tabora – Sikonge (Usesula) (km 30).

Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/ Loliondo – Mto wa Mbu (km 338)

277. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni **17,397.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano – Natta (Sanzate) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu za Natta (Sanzate) – Mugumu na Mto wa Mbu – Loliondo sehemu ya Waso – Sale (km 49).

Barabara ya Ibanda – Itungi/Kajunjumele – Kiwira Port (km 26)

278. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,465.00** kwa ajili ya kuendelea na upembizi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara za Ibanda – Kiwira Port sehemu ya Kajunjumele – Kiwira Port na Ibanda – Itungi Port. Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach (sehemu ya Tenende – Matema: km 34.6) na Tukuyu – Mbambo –Katumba sehemu ya Bujesi – Mbambo (km 15) pamoja na kuanza ujenzi wa barabara ya Tukuyu – Mbambo-Katumba sehemu ya Tukuyu – Mbambo (km 15).

Barabara ya Tanga – Horohoro (km 65)

279. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 865.00** kwa ajili ya kukamilisha malipo ya fidia.

Barabara ya Nzega – Tabora (km 114.7)

280. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 23,736.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Nzega – Puge na Puge – Tabora.

Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 768)

281. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 31,000.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Sitalike – Mpanda (km 36.5) na kuendelea na kazi za ujenzi wa sehemu za Sumbawanga – Kanazi (km 75.0), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 35.0).

Aidha, kazi zingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Kibaoni – Sitalike (km 71.0).

Barabara ya Nyanguge – Musoma (km 183) na Mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17)

282. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 30,332.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 80.0), malipo ya madai ya Mkandarasi wa mradi wa Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5), kuendelea na kazi ya ujenzi wa sehemu ya barabara ya Usagara – Kisesa Bypass (km 17.0), Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba (km 51.0), upanuzi wa barabara ya kwenda uwanja wa ndege wa Mwanza (km 12.0) na Daraja la Waenda kwa Miguu la Furahisha. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara za Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55.0) na Musoma – Makojo – Busekela (km 92.0). Aidha, fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kazi za ukarabati (*overlay*) wa barabara ya Makutano – Sirari (km 83.0).

Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 152.8)

283. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,704.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi sehemu ya Magole – Turiani (km 48.8) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Turiani – Mziha – Handeni (km 104).

Ujenzi wa Flyovers Jijini Dar es Salaam na Barabara Unganishi

284. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 46,890.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa ‘Flyover’ ya TAZARA; *Interchange* ya Ubungo pamoja na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, makutano

ya barabara za Kinondoni/Ally Hassan Mwinyi na Kenyatta na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct).

Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 171.8)

285. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 25,188.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya sehemu ya malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Bariadi – Lamadi (km 71.8), kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Mwigumbi – Maswa (km 50.3) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Maswa – Bariadi (km 49.7).

Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa - km 172)

286. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 435.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii.

Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 358)

287. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 19,284.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidahwe – Kasulu (km 50.0) na Nyakanazi – Kibondo (km 50.0) pamoja na kukamilisha mapitio ya usanifu wa kina wa sehemu ya Kibondo – Kasulu na usanifu wa kina wa sehemu ya Kasulu- Manyovu na kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Kibondo – Kasulu - Manyovu (km 258).

Barabara ya Kwenda Uwanja wa Ndege wa Mafia (Mafia Airport Access Road, km 16)

288. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni**

1,006.00 kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara hii.

Barabara ya Dodoma University (km 12.0)

289. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,852.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii.

Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Uganishi

290. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,231.00** ikiwa ni sehemu ya mchango wa Serikali katika gharama za ujenzi wa daraja hilo na kuanza ujenzi wa barabara unganishi ya Daraja la Nyerere (Kigamboni) – Vijibweni (km 1.5) na barabara za Tungi – Kibada (km 3.8) na Kibada – Mjimwema (km 1.6).

291. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara pia itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu za Ukanda wa Kati umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 359.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuanza kazi ya usanifu wa kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika barabara kuu ya Ukanda wa Kati.

Upanuzi wa Barabara ya JNIA – Pugu (km 8) kuwa njia sita umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 122.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa miundombini ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu (*BRT Phase III*) kwa kuwa barabara hii ni sehemu ya mradi huo.

Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na

Mpiji umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 122.00** kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa barabara na madaraja hayo. Miradi huu utatekelezwa kwenye awamu ya pili ya mradi wa *Dar es Salaam Maritime Gateway* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Ujenzi wa Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119) umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 100.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Maneromango - Mzenga - Mlandizi (km 65).

Ujenzi wa Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34.0) umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 436.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya mapitio ya upembusi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu za Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7) na Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 21.3) illi kujengwa kwa njia sita.

Ujenzi wa Mizani Karibu na Bandari ya Dar es Salaam umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 218.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mizani ya kupima uzito wa magari karibu na Bandari ya Dar es Salaam.

292. Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya maendeleo ya barabara itakayotekelawa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni:

Barabara ya Tunduma – Sumbawanga (km 276.01) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,215.00** katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Tunduma Mjini (km 1.6) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mpemba – Isongole (km 51.2).

Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 154) imetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 10,826.000** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara hii pamoja na kuanza ujenzi wa barabara ya Muleba-Kanyambogo – Hospitali ya Rubya (km 18.5).

Barabara ya Arusha - Namanga (km 105) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,218.00** kwa ajili ya kulipa fidia ya mali zilizoathirika na utekelezaji wa mradi huu.

Barabara ya Singida - Babati - Minjingu (km 223.5) imetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 2,855.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Singida - Kateshi (km 65.1), Kateshi - Dareda (km 73.8) na Dareda-Babati - Minjingu (km 84.6).

Barabara ya Dar es Salaam - Mbagala (Kilwa Road)- Gerezani (sehemu ya KAMATA - Bendera Tatu, km 1.3) imetengewa **Shilingi milioni 12,132.91** kwa ajili ya kuanza kazi za ukarabati na upanuzi wa sehemu ya Gerezani - Bendera Tatu (km 1.3) pamoja na maandalizi ya upanuzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu - Kongowe (km 3.8) pamoja na Daraja la Mzinga.

Barabara ya Msimba - Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 445.8) imetengewa **Shilingi milioni 104,772.84** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi aliyekarabati barabara ya Iringa-Mafinga (km 68.9), kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Mafinga - Igawa (km 137.9), kuendelea na ujenzi wa barabara za Njombe - Ndulamo -Makete (km 109.4), Igawa - Mbarali - Ubaruku (sehemu ya Mbarali - Ubaruku: km 8.0) na Iringa-Ruaha National Park (km 104) pamoja na kuanza ujenzi wa barabara za Rujewa - Madibira - Mafinga (km 152.0) na Njombe - Lupembe - Madeke (km 125.0) .

Barabara ya Korogwe - Mkumbara - Same (km 172) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 535.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya mwisho ya Mkandarasi wa sehemu ya Korogwe - Mkumbara (km 76).

Barabara ya Mbeya - Makongolosi - Mkiwa (km 528) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 22,038.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Mbeya - Lwanjilo (km 36.0) na Lwanjilo - Chunya (km 36.0). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu za Chunya -

Makongolosi (km 43.0) na Makongolosi – Rungwa–Itigi – Mkiwa (sehemu ya Noranga – Itigi – Mkiwa: km 56.9).

Barabara ya Chalinze – Segera – Tanga (km 248) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Amani – Muheza (km 36.0).

Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,465.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50.0).

Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kibaya - Singida (km 460) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Handeni-Kibereshi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba-Kwa Mtoro – Singida (km 460.0).

Barabara ya Dodoma – Iringa (km 267.1) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,452.01** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara za Iringa – Migori (km 95.1), Migori – Fufu *Escarptment* (km 93.8) na Fufu *Escarptment* – Dodoma (km 70.9). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass: km 7.3).

Barabara ya Dodoma – Babati (km 251.4) imetengewajumlaya **Shilingimilioni116,724.137** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa sehemu za Mayamaya – Mela (km 99.4) na Mela – Bonga (km 88.8). Aidha, Makandarasi wa sehemu za Dodoma – Mayamaya (km 43.7) na Bonga – Babati (km 19.6) watalipwa sehemu ya madai yao.

Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 623.3) imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 64,516.144** kwa ajili ya kulipa malipo ya mwisho ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Mangaka – Nakapanya

(km 70.5), Nakapanya – Tunduru (km 66.5), Mangaka – Mtambaswala (km 65.5), Tunduru – Matemanga (km 59.0), Matemanga – Kilimasera (km 68.2) na Kilimasera – Namtumbo (km 60.0). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Masasi – Newala – Mtwara (sehemu ya Mtwara – Mnivata: km 50) na kuanza ujenzi wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) na Masasi – Nachingwea – Nanganga (km 91.0).

Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na Ofisi za Mikoa umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,280.00** kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara (TANROADS) pamoja na Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

Ujenzi wa Barabara ya Kwenda Chuo cha Uongozi (km 8.8) umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 50.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo.

Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili Hadi ya Nne imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 25,100.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi ya Nne (*BRT Phase II- IV*).

MIRADI YA USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA

293. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi wa **Usalama Barabarani** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,193.84** kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi, uanzishwaji wa Mamlaka ya Usalama Barabarani nichini, ukaguzi wa usalama wa barabara pamoja na mapitio ya Sera na Sheria ya Usalama Barabarani. Aidha, mradi wa **Kujenga Uwezo na Marekebisho ya Mfumo wa Usalama na Mazingira** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 151.50** kwa ajili ya kutoa elimu ya usalama barabarani kwa umma, utoaji wa elimu ya usalama barabarani mashulenii pamoja na uendeshaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani.

294. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa **Menejimenti ya Utunzaji wa Mazingira** katika mwaka wa fedha 2017/2018, umetengewa **Shilingi milioni 154.66** kwa ajili ya kutoa Mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na hifadhi ya mazingira katika sekta ya Ujenzi kwa wahandisi na mafundi sanifu, kuandaa mfumo wa kusimamia mazingira (Environmental Management System) kwa mikoa miwili, kutoa elimu ya weledi wa usimamizi wa mazingira hususan utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 kwa menejimenti ya Wizara na kuandaa program za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika sekta (Pollution Control Programme) ikihusisha kuandaa machapisho na matangazo yanayohusu utunzaji na kuhifadhi mazingira kwa umma kwa njia ya redio, luninga, vipeperushi na magazeti.

MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE

295. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Ujenzi imekabidhiwa jukumu la kusimamia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Viwanja vya Ndege nchini. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, miradi ya viwanja vya ndege itakayotekelzwa ni kama ifuatavyo:

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma

296. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,250.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 1,050.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 6,200.00** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB). Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka), usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, kujenga uzio, na ujenzi wa jengo kwa ajili ya huduma za hali ya hewa.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mpanda

297. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni**

700.00 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya mkandarasi.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora

298. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 11,050.00**. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 2,450** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 8,600.00** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake (barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari), ukarabati wa njia ya pili ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, jengo kwa ajili ya huduma ya hali ya hewa (OBS), maegesho ya ndege pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe

299. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,530.00** fedha za ndani kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake, usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na matengenezo ya tabaka la mwisho la njia ya kutua na kuruka ndege.

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza

300. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 23,580.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 18,580** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,000.00** ni fedha za nje kutoka Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi kwa Afrika (BADEA). Kazi zitakazotekelزوا ni pamoja na kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria na kuendelea na kazi za kuongeza urefu wa barabara ya kuruka na kutua ndege (runway), ujenzi wa jengo la mizigo (Cargo Terminal), maegesho ya ndege na viungio vyake, mnara wa kuongoza ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua.

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha

301. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 700.00** fedha za ndani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na upanuzi wa jengo la abiria na kazi za kuongeza urefu wa barabara ya kuruka na kutua ndege (runway) kwa meta 200 pamoja na ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege (Turning Pad).

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara

302. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 4,550.00** fedha za ndani kwa ajili ya kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongoza ndege. Fedha hizi pia zitatumika kulipia madai ya Wahandisi Washauri pamoja na ujenzi wa barabara mchepuo inayoingia kiwanja cha ndege (access road).

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga

303. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 18,400.00**. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 5,200** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 13,200.00** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, mnara wa kuongoza ndege, jengo kwa ajili ya huduma ya hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga

304. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 15,600.00**. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 1,800.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 13,800.00** ni fedha za nje kutoka Benki

ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB). Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, mnara wa kuongoza ndege, jengo kwa ajili ya huduma za hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Kati ya fedha za ndani, **Shilingi milioni 600** zitatumika kulipa fidia na **Shilingi milioni 1,200** ni mchango wa Serikali katika mradi.

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro

305. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 32,568.64**. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 5,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 27,568.64** ni fedha za nje kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Uhlanzi (ORIO) kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, barabara za viungio, jengo la abiria, ujenzi wa barabara mpya ya kiungio, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ujenzi wa mfumo mpya wa majitaka.

Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa

306. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 17,390.00** fedha za ndani. Kati ya fedha hizo **Shilingi milioni 15,270.00** ni kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Geita, Iringa, Ruvuma na Mara. Aidha, kiasi cha **Shilingi milioni 1,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kugharamia maandalizi ya ujenzi wa viwanja vya ndege nane (8) ambavyo ni Lake Manyara, Moshi, Tanga, Kilwa Masoko, Lindi, Njombe, Singida na Simiyu. Vilevile, kiasi cha **Shilingi milioni 1,120.00** zitatumika kukarabati uwanja wa ndege wa Dodoma.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato

307. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,500.00**. Kati

ya hizo, **Shilingi milioni 3,500.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,000.00** ni fedha za nje kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya usanifu wa kina wa ujenzi wa kiwanja hicho pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa kiwanja kipywa cha Msalato.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba

308. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 2,550.00** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo la watu mashuhuri (VIP Lounge) pamoja na ulipaji wa fidia eneo la Omukajunguti.

Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha JNIA

309. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 35,000** fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) pamoja na miundombinu yake.

FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA

310. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 917,548,000,000** zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, Sekta ya Ujenzi na Taasisi zake imetengewa **Shilingi 642,284,000,000** na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetengewa **Shilingi 275,264,000,000**.

311. Mheshimiwa Spika, kati ya **Shilingi 642,284,000,000.00** zilizotengwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), TANROADS imetengewa **Shilingi 573,084,321,840.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara (Sekta ya Ujenzi) imetengewa **Shilingi 63,676,035,760.00** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu

wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi 5,523,642,400.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Mchanganuo wa miradi itakayotekelawa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3 - 5.**

Miradi ya Barabara Kuu

312. *Mheshimiwa Spika*, fedha zilizotengwa kwa mwaka 2017/2018 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya barabara kuu ni **Shilingi 16,314,580,000**. Kazi zilizopangwa kutekelezwawatika Barabara Kuu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kilometa **3,624.80**. Orodha ya miradi ya barabara kuu itakayotekelawa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3.**

Miradi ya Barabara za Mikoa

313. *Mheshimiwa Spika*, miradi ya barabara za mikoa imetengewa **Shilingi 33,907,137,900.00** fedha za Mfuko wa Barabara katika mwaka 2017/2018. Kazi zilizopangwa kutekelezwawitni kufanya ukarabati wa jumla ya **kilometra 688.28** kwa kiwango cha changarawe na kujenga **kilometra 40.6** kwa kiwango cha lami. Aidha, **madaraja 12** yatakarabatiwa katika Mikoa mbalimbali nchini. Orodha ya miradi ya barabara za mikoa itakayotekelawa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4.**

Miradi ya Vivuko

314. *Mheshimiwa Spika*, fedha zilizotengwa kwa mwaka wa 2017/2018 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya miradi ya vivuko ni **Shilingi 5,180,816,900.00**. Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 3.**

Miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira

315. *Mheshimiwa Spika*, fedha zilizotengwa kwa mwaka wa 2017/2018 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira ni **Shilingi 2,827,894,800.00**. Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.3**

Kazi zinazohusu Shughuli za Barabara

316. *Mheshimiwa Spika*, usimamizi na ufuutiliaji wa kazi zinazohusu shughuli za barabara pamoja na ujenzi wa jengo la Wizara umetengewa **Shilingi 5,445,606,160.00**. Mchanganuo wa kazi hizo umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 3.**

MPANGO WA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

317. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi 573,084,321,840.00** fedha za Mfuko wa Barabara zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja, uendeshaji wa mizani, gharama za usimamizi na uendeshaji wa Wakala wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mchanganuo wa mpango huo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A hadi 5E.**

MPANGO WA UTEKELEZAJI KAZI KATIKA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Wakala wa Barabara

318. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wakala umepanga kujenga barabara zenyet urefu wa **kilometra 720** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **13** pamoja na ukarabati wa **kilometra 150** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Aidha, Wakala umepanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa

ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometra 32,642.82**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofii ya **kilometra 5,883.98** na matengenezo ya madaraja **2,786**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu (Performance Based Management and Maintenance of Roads).

319. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa barabara za mikoa, Wakala utajenga kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa **kilometa 99** ambapo **kilometa 58.4** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 40.6** zitajengwa kwa fedha kutoka Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometa 1,157.78** zitakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo **kilometa 469.50** zitatumia fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 688.3** zitatumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, **madaraja 24** yatajengwa ambapo **madaraja 12** yatatumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **madaraja 12** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Wakala wa Majengo (TBA)

320. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wakala wa Majengo umepanga kununua viwanja mikoani na Makao Makuu; kufuatilia upatikanaji wa hati za viwanja vya Wakala mikoani na Makao Makuu; ununuzi wa samani kwenye majengo ya ubia yaliyoko barabara ya Chimara na Chole; kufanya upembuzi yakinifu kwenye viwanja vitatu vya TBA kwa ajili ya miradi ya uwekezaji pamoja na kumalizia ujenzi wa jengo la TBA Makao Makuu kwa kuweka lifti. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa majengo mawili yenye ghorofa 8 kila moja katika eneo la iliyokuwa NMC, Mbezi Beach – Dar es Salaam na majengo mawili ya ghorofa katika kiwanja Na. 176 - Ukonga, Dar es Salaam. Aidha, Wakala utafanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuendeleza karakana za samani mikoani pamoja na ukarabati wa majengo mbalimbali mikoani. Wakala pia utaendelea na

ujenzi wa nyumba 200 za watumishi wa Serikali kama sehemu ya programu ya ujenzi wa nyumba 2500 Dar es Salaam.

Wakala wa Ufundu na Umeme

321. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA) utaendelea na kazi ya upanuzi wa maegesho ya Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; kuendelea na ujenzi wa maegesho ya Bwina mkoani Geita na ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Lindi – Kitunda. Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa kivuko kipyaa cha Kigongo – Busisi; ununuzi wa vitendea kazi; ukarabati wa karakana za TEMESA pamoja na kukamilisha ukarabati wa vivuko vya MV Sengerema na MV Kigamboni. Aidha, TEMESA itaendelea na matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali pamoja na kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali.

Bodi ya Mfuko wa Barabara

322. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bodi ya Mfuko wa Barabara imepanga kukusanya jumla ya **Shilingi 917,548,000,000.00** zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 642,284,000,000.00** zitapelekwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu 98 -Ujenzi) na **Shilingi 275,264,000,000.00** zitapelekwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56).

323. *Mheshimiwa Spika*, Bodi imepanga kukamilisha taratibu za ukaguzi wa magari na ukusanyaji wa fedha za ukaguzi kama chanzo mojawapo cha fedha za Mfuko. Aidha, Bodi itakamilisha na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji tozo kwa magari yanayozidisha uzito yaani **ePayment system for Overloading Fees**. Aidha, Bodi itashirikiana na TANROADS kukamilisha uweki ya mfumo

wa pamoja wa kielektroniki na kamera za CCTV kwenye vituo vyta mizani ya kupimia uzito wa magari ili kuwezesha taarifa za vifomo vya magari na faini kufika ofisi za Bodii kuititia mfumo wake wa taarifa (RFB Management Information System). Vilevile, Bodii itafanya tathmini ya mtandao wa barabara (road inventory and condition survey) ili kubaini thamani, urefu na hali ya barabara kwa ujumla. Takwimu hizi zitasaidia kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara nchini. Bodii pia itaendelea na ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote nchini.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

324. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Bodii imepanga kusajili wahandisi **1,500**, mafundi sanifu **150** na kampuni za ushauri wa kihandisi **20**. Bodii pia imepanga kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu **1,303**. Idadi hii inahusisha wahandisi wahitimu **903** wanaoendelea na mafunzo na **400** wapya wanaofadhiliwa na Serikali na sekta binafsi. Aidha, Bodii itaendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi pamoja na kutembelea na kukagua miradi yote ya ujenzi wa barabara Tanzania Bara, ikiwa ni pamoja na barabara za Halmashauri. Bodii pia itaendelea kusimamia mafunzo ya kuijendeleza kitaaluma kwa wahandisi watalaam na washauri wote, kwa ajili ya kuwaendeleza wahandisi kwa ujumla pamoja na kuwashawishi wahandisi watalaam ili waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani na hivyo kusogeza huduma hii muhimu karibu na watumiaji.

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

325. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bodii ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi imepanga kusajili watalaam **223** katika fani za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na fani

zinazoshabihiana nazo. Aidha, Bodi imepanga kusajili kampuni **29** za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi.

Bodi vilevile imepanga kuendelea na mpango wa kuwajengea uwezo wahitim **110** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo kupitia mafunzo kwa vitendo. Aidha, Bodi imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **2,000** katika mikoa yote pamoja na kusajili miradi ya majengo **800**.

326. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bodi imepanga kuendesha mashindano ya kubuni nyumba ya gharama nafuu ambayo itatolewa kwa wananchi wa kipato cha chini. Vilevile, Bodi itaendesha mashindano ya insha kwa wanafunzi wa sekondari kama njia ya kuwahamasisha kusoma masomo ya sayansi, na hatimaye kusomea taaluma za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

327. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bodi imepanga kusajili jumla ya makandarasi wapya **950**. Bodi pia itakagua jumla ya miradi ya ujenzi **1,900** nchi nzima. Aidha, Bodi imepanga kuendesha kozi tano za mafunzo kwa makandarasi katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma.

Bodi pia itaendeleza mfuko maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia makandarasi wadogo na wa kati (Contractors Assistance Fund) pamoja na kuendelea na jitihada za kuhamasisha makandarasi wazalendo kujunga ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia.

Baraza la Taifa la Ujenzi

328. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Baraza litaendelea kushirikiana na Wizara ili kukamilisha mapitio ya Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003 pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wa sera hiyo; kuendelea kufanya mapitio ya Sheria Na. 20 ya mwaka 1979 iliyoanzisha Baraza

la Taifa la Ujenzi na kufanyiwa marekebisho mwaka 2008; kuratibu mfumo wa majoribio wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi ili kukuza uwazi na uwajibikaji (Construction Sector Transparency Initiative - CoST) katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi. Baraza pia litaendelea kuratibu na kutoa mafunzo katika sekta, ushauri na utatuzi wa migogoro; kuboresha ukusanyaji, uwekaji na utoaji wa takwimu na taarifa za sekta ya ujenzi kwa kuboresha kituo cha rasilimali ya habari na kukipatia nyaraka muhimu pamoja na kutathmini, kuhuishwa na kuchapisha nyaraka zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi na kuchapisha matokeo ya tafiti zikiwemo bei za vifaa vya ujenzi na ukokotoaji wa bei kwa kipimo cha mraba.

329. *Mheshimiwa Spika*, Baraza pia litaendelea na jitihada za kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund - CIDF*) kwa kushirikiana na Taasisi inayoshughulika na Sekta binafsi (*Tanzania Private Sector Foundation - TPSF*) na wadau wengine wa maendeleo. Aidha, Baraza litaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi yenye lengo la kukuza vipato vya wananchi katika maeneo husika pamoja na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kitega uchumi katika maeneo ya Regent Estate, Mbezi Beach jijini Dar es Salaam na kiwanja kilichopo Dodoma.

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

330. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kituo kitasambaza taarifa zinazohusu teknolojia mbalimbali katika Sekta ya Usafirishaji pamoja na kuendelea kutoa huduma ya maktaba ya Kituo. Aidha, Kituo kimepanga kuendesha mafunzo kwa wadau yanayolenga kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya usafirishaji, kuendelea kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na usafirishaji. Kituo kitaendelea kushirikiana na Chuo Kikuu

cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Morgan cha Marekani na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto za msongamano wa magari katika miji na majiji nchini kwa kuanzia Jiji la Dar es Salaam.

SEKTA YA UCHUKUZI

Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

331. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Uchukuzi ni **Shilingi 91,142,025,000**. Aidha, Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi 2,477,931,183,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.6**. Maeleo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

332. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Sekta ya Uchukuzi imepanga kutekeleza miradi ifuatayo ya reli ya Kati:

i. Kuendelea na ujenzi wa reli ya Kati kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Dodoma kwa kiwango cha *standard gauge* ambapo Shilingi milioni 900,000 zimetengwa;

ii. Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa njia ya reli katika Mtwara – Mbambabaya na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa *standard gauge* pamoja na kumwajiri Mshauri Mwelekezi (Transaction advisor) atakayekuwa na jukumu la kuunadi mradi ili kupata fedha za ujenzi wa reli hiyo. Shilingi milioni 2,000 zimetengwa;

iii. Shilingi milioni 1,000 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli kwa *standard gauge* katika Arusha – Musoma, pamoja na matawi yake kwenda Engaruka na Minjingu;

- iv. Kukarabati njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka, kuboresha njia za reli zilizopo bandari ya Dar es Salaam pamoja na kukarabati madaraja na makaravati yaliyopo katil ya Dar es Salaam na Isaka. Kazi hizi zinagharamiwa na Benki ya Dunia ambapo Shilingi milioni 200,000 zimetengwa;
- v. Kununua mtambo wa kupima ubora wa njia ya reli, Shilingi milioni 4,045 zimetengwa
- vi. Kuboresha mfumo wa mawasiliano (Dar - Dodoma, Tabora-Kigoma/Tabora- Mwanza na Kaliua - Mpanda, Shilingi milioni 4,760 zimetengwa;
- vii. Kufanya usanifu na ujenzi wa madaraja 38 yaliyo katika hali mbaya, Shilingi millioni 6,521 zimetengwa;
- viii. Kuboresha kituo cha kuhudumia makasha cha llala; kuboresha kituo cha Isaka pamoja na kununua *Reach stackers* (2), *Tractor* (1) na *forklift* (1). Kazi hizi zinagharamiwa na Benki ya Dunia ambapo Shilingi milioni 11,459 zimetengwa; na
- ix. Kukamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli Jijini Dar es Salaam, zikiwemo zile za kwenda maeneo ya Pugu kuititia uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Mbagala/Chamazi, Luguruni/ Kibaha na Bunju/Bagamoyo, Shilingi milioni 2,000 zimetengwa.

333. *Mheshimiwa Spika*, ili kuboresha huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu, katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga:

- (i) Shilingi milioni 3,040 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa meli moja mpya ya kubeba abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika;
- (ii) Shilingi milioni 6,300 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Meli moja mpya ya kubeba abiria na mizigo katika Ziwa Victoria;

- (iii) Shilingi milioni 6,000 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa meli ya MV.Victoria;
- (iv) Shilingi milioni 2,520 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa meli ya MV.Butiama;
- (v) Shilingi milioni 3,773 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa meli ya MV Liemba;
- (vi) Shilingi milioni 1,571 kwa ajili ya kuanza ukarabati wa meli ya MV Umoja; na
- (vii) Shilingi milioni 1,292 kwa ajili ya kuanza ukarabati wa meli ya MV Serengeti.

334. *Mheshimiwa Spika*, ili kukabiliana na changamoto zinazotokana na uwezo mdogo wa bandari kuhudumia meli kubwa, uchakavu wa miundombini katika bandari za Mwambao na Maziwa Makuu na kukosekana kwa Mifumo sahihi ya mawasiliano (TEHAMA), mwaka 2017/2018, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) itatenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Shilingi milioni 187,123 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam kwa kuimarisha na kuongeza kina cha gati Na. 1-7; kujenga gati jipya la Ro-Ro; kufanya utafiti wa kuhamisha gati la mafuta lillipo kurasini (KOJ); kujenga gati jipya la kisasa la kushushia mafuta aina zote; kujenga gati la Nyamisati na kituo cha mafuta na gesi; kuongeza maeneo ya kuhudumia shehena, ukarabati wa ‘flow meters’; ukarabati wa minara ya kuongozea meli (pamoja na control tower), kujenga bandari Kavu eneo la Ruvu (Vigwaza), kuboresha bandari Kavu ya Isaka, kuweka sakafu (paving) eneo la NASACO na kuboresha mifumo ya kazi ya TPA kutoka katika mifumo ya kawaida na kuingia katika mifumo ya kielektroniki (automation);

ii. Katika bandari ya Tanga, Shilingi milioni 12,604 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa maegesho ya meli na sehemu ya kupakulia shehena; kukarabati

miundombinu ya barabara ya kuingilia bandarini; kuimarisha ulinzi katika maghala na mnara wa kuongozea meli; kujenga uzio eneo la *flow meters*; kukarabati mnara wa kuongozea meli; na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Mwambani;

iii. Kuhusu bandari ya Mtwara, Shilingi milioni 87,044 zimetengwa kwa ajili ya kujenga gati la mita 300 la kuhudumia Shehena mchanganyiko (Multi-Purpose Terminal); uboreshaji wa mfumo wa usalama; kuboresha maegesho ya meli; kujenga gati la mafuta Shangani na kukarabati eneo la gati namba 3 ili kuongeza eneo la kufanya kazi na kuhifadhi mizigo. Aidha fedha hizo pia zitatumika kujenga gati katika bandari ya Lindi na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga magati ya Kilwa na Rushungi;

iv. Shilingi milioni 6,295 zimetengwa kwa ajili kuboresha miundombinu ya Bandari za ziwa Victoria. Kazi hizi ni pamoja na uboreshaji wa mfumo wa usalama; ujenzi wa ofisi na jengo la abiria bandari ya Bukoba na Kyamkwikwi; ukarabati wa miundombinu iliyopo Mwanza South; kujenga bandari kubwa na ndogo za Nyamirembe, Chato na Magarine. Aidha, mradi huu utajumuisha ujenzi wa 'Dhow Wharves' ya Mwigobero; uongezaji kina katika Bandari ya Nansio na Mwanza *South*; kuboresha sehemu ya kushukia abiria Mwanza *North* na Ukarabati wa 'Link Span' ya bandari ya Mwanza *South*;

v. Shilingi milioni 18,500 zimetengwa ili kuboresha miundombinu ya bandari za Ziwa Tanganyika. Miradi itakayotekelawa ni pamoja na uboreshaji wa mfumo wa usalama na maegesho ya meli (gati) na kuhudumia abiria pamoja na mizigo katika vijiji vya Lagosa, Sibwesa, Kabwe na Ujiji. Aidha, mradi utajumuisha upembuzi yakinifu wa bandari ya Karema; kujenga ofisi ya Bandari; kuboresha miundombinu ya bandari ya Kasanga pamoja na barabara ya kuelekea katika bandari ya Kipili;

vi. Miradi ya kuboresha miundombinu ya bandari za Ziwa Nyasa imetengewa Shilingi milioni 15,290. Kazi

zitakazotekelawa ni pamoja na uboreshaji wa mfumo wa usalama; kufanya Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa gati za Mbamba Bay, Manda na Matema; Ujenzi wa gati la Ndumbi na ujenzi wa sakafu (pavement) katika bandari ya Kiwira na kuboresha sehemu ya kushukia abiria; na

vii. Ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kuhudumia meli na mizigo katika bandari zote nchini umetengewa Shilingi milioni 160,425.

335. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kampuni ya Ndege (ATCL) imetengewa shilingi milioni 500,000 kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege 3 ambapo ndege mbili (2) ni za aina ya CS 300 zenye uwezo wa kubeba abiria 127 kila moja na ndege kubwa moja (1) ya masafa marefu aina ya Boeing 787-8 Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 262. Aidha, fedha hizo pia zitatumika kwa ajili ya gharama za bima, mafunzo (marubani, wahandisi na wahudumu), gharama za kuanzia (start up cost) pamoja na malipo ya awali ya ndege nyingine ya aina ya Boeing 787 (Dreamliner).

336. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuboresha huduma zinazotolewa za Wakala wa Ndege za Serikali. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga Shilingi milioni 10,000 kwa ajili ya kufanya matengenezo ndege 4 za serikali ili kuhakikisha kuwa huduma ya usafiri wa anga inatolewa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni ya uhakika, salama na inayokidhi viwango.

337. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imetenga fedha ili itatekeleza miradi mbalimbali ya kuboresha shughuli za udhibiti wa usafiri wa anga. Miradi hiyo ni pamoja na:

i. Kuboresha miundombinu pamoja na huduma za usafiri wa anga nchini;

- ii. Kuendelea kutoa huduma za uongozaji ndege kwenye eneo la Bahari ya Hindi hadi umbali wa nyuzi 44 mashariki;
- iii. Kuendelea na juhudzi za kuendeleza ujenzi wa chuo kipywa huko Fukayose - Bagamoyo ili kuhakikisha chuo kinadahili wanafunzi wengi ambao watahitimu katika nyanja ya usafiri wa anga;
- iv. Kufunga mtambo wa ILS –Zanzibar; na
- v. Kununua na kufunga Rada nne (4) za kuongozea ndege za kiraia.

338. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Chuo cha Bahari (DMI) kimetengewa Shilingi milioni 2,500 kwa ajili ukarabati na upanuzi wa karakana ya mafunzo ya uhandisi; ununuzi na ufungaji wa mashine mbalimbali pamoja na ukarabati wa madarasa na majengo ya Chuo. Aidha, Chuo kitaandaa Mpango Kabambe (Master Plan) wa matumizi ya eneo la Chuo lenye ukubwa wa ekari 500 lilipo Mkuranga na kujenga bwawa la kuogelea kwa ajili ya mafunzo.

339. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Sekta ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetengewa Shilingi milioni 5,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:

- (i) Shilingi milioni 1,600 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya zimamoto kwa viwanja vya ndege vya Mpanda, Shinyanga, Iringa;
- (ii) Ununuzi wa vifaa vya mawasiliano katika viwanja vyenye ratiba maalum vya Dodoma, Mwanza, Mtwara, Kigoma, Songwe, Bukoba, Tanga, Tabora na Musoma, Shilingi milioni 160 zimetengwa;
- (iii) Shilingi milioni 2,400 zimetengwa kwa ajili ya Ununuzi wa mitambo ya ukaguzi wa abiria na mizigo (X-ray

machines) kwa viwanja vya ndege vya Mwanza, Iringa, Songea, Kigoma, Dodoma na Tanga;

(iv) Uandaaji wa matumizi ya ardhi katika viwanja vya ndege vya Mwanza, Songwe, Arusha na Msalato, Shilingi milioni 200 zimetengwa;

(v) Kurudia upembuzi yakinifu wa viwanja vya ndege vya Arusha, Mafia na Mwanza, Shilingi milioni 340 zimetengwa; na

(vi) Kufanya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kiwanja kipya katika Mkoa wa Manyara, Shilingi milioni 300 zimetengwa.

340. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kuboresha huduma zinazotolewa na Kampuni ya Reli (TRL). Kazi zitakazotekeliza ni pamoja na:-

i. Kujenga upya vichwa 7 vya sogeza (shunting engines) ambapo Shilingi milioni 13,900 zimetengwa;

ii. Shilingi milioni 9,400 zimetengwa ili kukarabati mabehewa 200 ya mizigo;

iii. Shilingi milioni 1,842 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa viberenge (Motor Trolleys) 3;

iv. Ukarabati wa mabehewa 17 ya abiria umetengewa Shilingi milioni 3,101; na

v. Kufanya matengenezo ya kawaida ya njia ya reli (normal track maintenance), Shilingi milioni 2,557 zimetengwa.

341. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Serikali kuititia SUMATRA imetenga Shilingi bilioni 65.74 katika bajeti yake kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuongeza uwezo wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

- ii. Kuimarisha ushindani na kuhakikisha huduma za usafiri wa nchi kavu na majini zinakuwa endelevu;
- iii. Kuimarisha usalama, ulinzi na ubora wa huduma za usafiri wa nchi kavu na majini;
- iv. Kuhakikisha mazingira endelevu sambamba na maendeleo ya huduma ya usafiri kwa jamii; na
- v. Kuboresha sheria, kanuni na mahusiano ya kitaasisi katika sekta za usafiri wa nchi kavu na majini.

342. *Mheshimiwa Spika*, ili kuendelea kuboresha miundombinu ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), jumla ya Shilingi milioni 26,000 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, kwa ajili ya ukarabati wa vichwa vya treni (traction motors) na ununuzi mitambo kwa ajili ya karakana ya kuzalisha kokoto Kongolo.

343. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Mamlaka ya Hali ya Hewa imetengewa Shilingi milioni 6,200 kwa ajili ya ununuzi wa Rada na vifaa vya hali ya hewa; kugharamia miundombinu; kuboresha miundombinu ya Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma na vituo vya hali ya hewa.

SEKTA YA MAWASILIANO

344. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Mawasiliano imepanga kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:

TEHAMÀ

i. Utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa mradi wa ujenzi wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano na kufikisha huduma zake hadi makao makuu ya Wilaya zote nchini na ujenzi wa vituo viwili (2) vya kutunzia data (Data Centre) - Dodoma na Zanzibar, pamoja na kuwezesha uwekazaji wa viwanda nchini;

NAKALA YA MITANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ii. Ujenziwa Muundombinuwamawasiliano ya mitandao "Public Key Infrastructure - (PKI)";

iii. Kuratibu matumizi ya huduma za TEHAMA nchini (National IT systems and services/applications);

iv. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa usalama wa mitandao (National Cyber security strategy); na

v. Kusimamia uanzishwaji wa mkakati wa mtandao wa TEHAMA wenyewe kasi zaidi (National Broadband Strategy).

MAWASILIANO

i. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016; Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 na Mpango Mkakati wake wa utekelezaji;

ii. Kukamilisha mpango mkakati wa utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA nchini na kusimamia utekelezaji wake; na

iii. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi katika miji mikuu ya mikoa Morogoro, Lindi, Mbeya, Dodoma, Kagera, Mwanza, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Unguja Kusini na Geita ikiwa ni pamoja na kuhimiza matumizi ya mfumo husika.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

345. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itatekeleza masuala yafuatayo:

i. Kuendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu sheria, haki na wajibu wa watumiaji, kuhusu matumizi ya mfumo mpya wa anwani za makazi na

Postkodi, uhakiki wa usajili wa laini za simu za kiganjani, wajibu wa watumiaji katika masuala ya tahadhari dhidi ya uhalifu kupitia mtandao;

ii. Kuendelea kutekeleza usimamizi wa usalama wa mitandao ya mawasiliano kupitia TZ-CERT;

iii. Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kumbukumbu za simu za kiganjani kwa kushirikiana na watoa huduma wa simu za kiganjani (CEIR);

iv. Kuendelea kuratibu uendelezaji wa viwango vytaalam ili viendane na viwango vyta kikanda na kimataifa katika vifaa mbalimbali vyta mawasiliano;

v. Kuendelea kutekeleza mfumo wa Mobile Number Portability (MNP) kwa kuhamasisha watumiaji wa simu waweze kuhamza kwa hiyari kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine ili kuboresha ushindani na kuongeza ubora wa huduma;

vi. Kuendelea kutekeleza mifumo ya utendaji kazi (Quality Management System) ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa Mawasiliano ya simu, Posta na Utangazaji;

vii. Kuratibu uuzaaji wa masafa kwa kutumia mnada kama njia mpya ya kuongeza mapato ya Serikali;

viii. Kufuatilia ujenzi wa mifumo na uratibu wa huduma za mawasiliano kwa kutumia mtambo wa TTMS na kuhakikisha serikali inapata mapato stahiki kutokana na huduma za mawasiliano;

ix. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA) ya mwaka 2010 kupitia kanuni zake; na

x. Kuendelea kujenga uwezo wa kukabiliana na uhalifu wa matumizi mabaya ya mtandao kwa Taasisi za Ulinzi na Usalama.

Shirika la Posta Tanzania (TPC)

346. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 Shirika la Posta Tanzania litatekeleza masuala yafuatayo:

(i) Kuimarisha usambazaji wa barua, nyaraka, vipeto na vifurushi kwa kupitia mfumo wa Misimbo ya Posta na anwani za makazi;

(ii) Shirika litaimarisha huduma ya "Posta Mlangoni" inayolenga kuwafikishia wateja barua, nyaraka, vipeto na vifurushi kupitia miundombinu ya Postkodi na anwani za makazi. Shirika pia litaongeza vifaa vyaa utendaji kazi kama vile magari, pikipiki na ramani za kuonesha mitaa na namba za nyumba za makazi na Ofisi;

(iii) Litaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa kuongeza ofisi 10 zilizounganishwa katika mtandao wa kielektroniki wa *Postglobal Netsmart* hadi kufikia ofisi 150. Kuunganishwa kwa ofisi hizi kutaziwezesha kutoa huduma za kufuatilia (Track and Trace) nyaraka, vifurushi na vipeto vinavyotumwa kupitia mtandao wa Posta;

(iv) Shirika pia litaimarisha huduma za Duka Mtandao zilizoanzishwa kupitia tovuti: <http://www.stamps.tz.post>;

(v) Litaendelea kufungua vituo na kuimarisha huduma ya Posta "Jamii Centre" pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa "Payment Switch" ya kuimarisha shughuli za fedha na uwakala. Hii itasaidia pia Shirika kufikisha huduma za kifedha sehemu za vijiji; na

(vi) Shirika limefungua kituo cha huduma ya 'Jamii Centre' Dar es Salaam, huduma hii itaendelea kupanuliwa katika miji ya Dodoma, Morogoro, Mwanza, Arusha na Zanzibar ambayo inakusudia kuweka huduma za kijamii chini ya dari moja.

Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)

347. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18 Kampuni ya Simu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kupanua Mtandao wa kisasa wa simu za kiganjani wa 2G/3G, 4G LTE nchi nzima ifikapo mwaka 2017/18, pamoja na kujenga, kusimamia na kuendesha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kituo mahiri cha kutunzia kumbukumbu (National Internet Data Centre);

(ii) Kuongeza Tija na Ufanisi wa Kampuni kwa kuboresha Mapato hadi Shilingi bilioni 266.9 mwaka wa fedha 2017/18;

(iii) Kuongeza idadi ya wateja hai (Active Customers) wa huduma mbalimbali za simu (voice na data) kutoka 208,259 mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 1,036,228 kwa mwaka wa fedha 2017/18;

(iv) Kuendelea na uboreshaji wa makusanyo ya Mapato na Madeni ya Kampuni yanayotokana na huduma za simu zinazototolewa kila mwezi kwa wateja wake, ikiwemo Serikali kuu na taasisi zake; na

(v) TTCLitaendeleanajukumulakuhakikisha kuwa mawasiliano ya kuaminika katika nyanja zote kuisadia Serikali kwenye ajenda yake ya maendeleo ya kiuchumi.

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

348. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) utatekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijiji iliyoanzishwa ili kuhakikisha kuwa huduma zinawafikia wananchi;

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- (ii) Kufikisha matangazo ya runinga ya kidigitali katika vijiji 200;
- (iii) Mfuko unatarajia kutoa vifaa vya TEHAMA na kuunganisha mtandao wa intaneti katika shule 40;
- (iv) Kutekeleza mradi wa kuanzisha vituo 12 vya TEHAMA nchini kwa kutumia ofisi za Posta; kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 350; na
- (v) Kuendeleza ushirikiano na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili katika uunganishwaji wa mtandao wa mawasiliano katika hospitali za Serikali ili kuleta ushirikiano wa kitabibu kwa njia ya mtandao na kuondoa tatizo sugu la uhaba wa madaktari bingwa.

Tume ya TEHAMA (ICTC)

349. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Tume ya TEHAMA itatekeleza mambo yafuatayo:

- (i) Kusajili wataalam wa TEHAMA na kutekeleza programu ya kuendeleza wataalam (*Continued Professional Development*); kutekeleza programu ya mafunzo viwandani kwa wahitimwa vyuo (*ICT Graduates Industry Apprenticeship (IGIA) Program*); kusanifu na kutekeleza mpango wa dijitali Tanzania (*Digital Tanzania Program*);
- (ii) Kutekeleza mradi wa uundaji wa vifaa vya TEHAMA kwa kutumia vifaa vilivytumika (*e-waste management and ICT Hardware Assembly*);
- (iii) Kutekeleza mpango wa ubunifu wa TEHAMA nchini (*ICT innovation enhancement program*);

(iv) Kuajiri na kuendeleza watumishi wa Tume na kukusanya rasilimali;

(v) Kuwezesha utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa miaka mitano 2017/2018-2022/2023; na

(vi) Kufanya utafiti katika maeneo ya TEHAMA yanayolenga kuwezesha upatikanaji wa huduma za intaneti katika maeneo maalum ya umma kwa teknolojia rahisi, kubaini na kuboresha miundombinu muhimu ya TEHAMA (*Critical ICT Infrastructure*) na kuwezesha uanzishaji wa kituo mahiri cha TEHAMA (*ICT Park*).

TAASISI ZA MAFUNZO Chuo cha Ujenzi Morogoro

350. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Chuo cha Ujenzi Morogoro kimepanga kufundisha jumla ya wanafunzi **1,050** wa fani za barabara na ukaguzi wa madaraja, majengo, magari, mfumo wa umeme na elektroniki, mafunzo ya madereva wa magari ya Umma (*Public professional drivers*), madereva wa magari ya abiria (PSV), fani za ufundi mbalimbali, (*Basic Artisans*) madereva wa awali, madereva wa magari ya abiria, utengenezaji wa mitambo (*Plant Mechanics*) na uendeshaji wa mitambo (*Plant operation*). Aidha, Chuo kitaendelea na mipango ya kutoa mafunzo kwa makandarasi wanaotekeleza shughuli za ukarabati wa Barabara, Majengo na Umeme, hasa kwa wale makandarasi wa kazi maalum (*Specialized Contractors*) daraja la I – III na wale waliosajiliwa na bodi ya makandarasi wa madaraja ya chini.

Chuo pia kimepanga kuendelea na kazi ya ukarabati wa mabweni manne, kukamilisha ujenzi wa karakana mbili za ufundi, kununua vifaa vyta maabara vyta barabara na majengo (*apparatus for materials laboratory*), kukarabati jengo la utawala, kukarabati miundombinu ya maji safi na taka pamoja na kuweka lami nyepesi (Single surface dressing) kutoka lango kuu hadi ofisi ya utawala.

**Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Appropriate Technology Training Institute – ATI)
- Mbeya**

351. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Chuo cha mafunzo ya Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvu kazi kimepanga kuendesha mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe; mafunzo ya uwekaji tabaka la lami (surface dressing) kwa Wahandisi (10), Mafundi Sanifu (30) na wasimamizi wa barabara (30); kufanya matengenezo ya barabara kwa ajili ya utoaji mafunzo hapa nchini kwa kupitia barabara zilizo chini ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na Halmashauri kwa ajili ya kuendelea kuelimisha wananchi juu ya matumizi stahiki ya teknolojia ya nguvu kazi; kuboresha mitaala ya Chuo ya utoaji wa mafunzo ya teknolojia stahiki ya nguvukazi pamoja na kuanzisha mafunzo mapya (Tailor made courses).

Chuo pia kitaendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake kushiriki katika kazi za barabara hapa nchini pamoja na kutoa mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa vitendo. Aidha, Chuo kitaendelea na utoaji wa mafunzo na kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kwa umma, kwa njia ya makongamano na kuendelea kutoa ushauri wa matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvu kazi kwa wadau mbalimbali.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

352. *Mheshimiwa Spika*, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeendelea kukabiliwa na changamoto za uhaba na uchakavu wa miundombinu. Ili kukabiliana na changamoto hizo, katika mwaka 2017/2018, Shilingi milioni 10,300 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Shilingi milioni 5,800 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Rasilimali Mafunzo na ukarabati wa majengo ya chuo na ujenzi wa Kituo cha ukaguzi wa magari;

ii. Shilingi milioni 4,000 ni kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia; na

iii. Shilingi milioni 200 kwa ajili ya matengenezo ya ndege ya mafunzo; na Shilingi milioni 300 kwa ajili ya kununulia gari la kufundishia.

353. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kimetengewa shilingi milioni 2,500 kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Kuimarisha karakana kwa ajili ya mafunzo ya wahandisi wa meli, Shilingi milioni 800; na

ii. Kununua vifaa vya kufundishia kozi za usalama katika sekta ya mafuta na gesi, Shilingi milioni 1,700.

MASUALA MTAMBUKA

Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Barabara

354. *Mheshimiwa Spika*, ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imepanga kuendesha mafunzo kwa makandarasi wanawake kuhusu namna ya kutumia teknolojia ya nguvukazi katika ukarabati na matengenezo ya barabara pamoja na namna ya kuandaa zabuni; kuchapisha na kugawa kwa wadau nakala 450 za Mwongozo wa Uimarishaji Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wadau kuhusu matumizi ya mwongozo huo kuitia warsha pamoja na kufuatilia makandarasi wanawake waliokwishapokea mafunzo ya awali ya ukandarasi ili kuona maendeleo ya kazi zao za ukandarasi na kusaidia kutatua changamoto wanazokumbana nazo. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wasichana wa shule za sekondari wasome

masomo ya sayansi ili kuongeza idadi ya wanawake katika fani ya uhandisi kwa kutembelea shule za wasichana katika mikoa itakayopangwa.

Rasilimali Watu

355. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara itaendelea kuwaendeleza kitaaluma watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kulingana na mpango wa mafunzo ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

356. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu kupambana na gonywa hatari la UKIMWI, katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu mbinu za kujikinge na maambukizi ya ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na upimaji kwa hilari. Wizara pia itaendelea kuhamasisha watumishi ili washiriki katika mashindano mbalimbali ya michezo kwa lengo la kuboresha afya zao pamoja na kujenga mahusiano.

F. SHUKURANI

357. *Mheshimiwa Spika*, ninaendelea kuwashukuru sana viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mheshimiwa Mhandisi Edwin A. Ngonyani (Mb.), Naibu Waziri; Mhandisi Joseph M. Nyamhanga, Katibu Mkuu (Ujenzi), Mhandisi Dkt. Leonard M. Chamuriho, Katibu Mkuu (Uchukuzi), Mhandisi Dkt. Maria L. Sasabo, Katibu Mkuu (Mawasiliano), Mhandisi Angelina Madete, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano), Wakuu wa Idara/Vitengo; Wenyeviti wa Bodizilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika utekelezaji wa majukumu yao.

358. *Mheshimiwa Spika*, nachukua fursa hii kuwashukuru washirika mbalimbali wa maendeleo ambao wametoa michango yao kwa namna moja au nyingine katika

kuendeleza sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hapa nchini. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Uingereza (DFID), Uhlanzi (ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki, OPEC Fund, BADEA, HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, CRDB, TIB, Asasi Zisizokuwa za Kiserikali pamoja na sekta binafsi.

359. *Mheshimiwa Spika*, mwisho, napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba yangu hii inapatikana katika tovuti za Sekta ya Ujenzi (www.mow.go.tz), Sekta ya Uchukuzi (www.uchukuzi.go.tz) na Sekta ya Mawasiliano (www.mst.go.tz).

G. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

360. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,516,883,061,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,929,705,714,000.00** nikwaajili ya Sekta ya Ujenzi, **Shilingi 2,569,073,208,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi na **Shilingi 18,104,139,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)

361. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi 1,929,705,714,000.00** za Sekta ya Ujenzi zinajumuisha **Shilingi 34,123,282,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 32,068,153,018.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 2,055,128,982.00** ni za Matumizi Mengineyo. Bajeti ya

Maendeleo ni Shilingi **1,895,582,432,000.00** ambazo zinajumuisha **Shilingi 1,350,000,000,000.00** fedha za ndani na Shilingi **545,582,432,000.00** fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 642,284,000,000.00** fedha za Mfuko wa Barabara.

SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)

362. Mheshimiwa Spika, jumla ya Shilingi **2,569,073,208,000.00** za Sekta ya Uchukuzi zinajumuisha **Shilingi 91,142,025,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **52,896,450,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na Shilingi **38,245,575,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. **Shilingi 2,477,931,183,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,227,646,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 250,285,183,000.00** ni fedha za nje.

SEKTA YA MAWASILIANO (FUNGU 68)

363. Mheshimiwa Spika, jumla ya Shilingi **18,104,139,000** za Sekta ya Mawasiliano zinajumuisha **Shilingi 4,104,139,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **2,267,001,000** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 1,837,138,000** ni za Matumizi Mengineyo. **Shilingi 14,000,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, zikiwa ni fedha za ndani.

364. Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekeliza katika mwaka wa fedha 2017/2018 (**Kiambatisho Na. 1 - 7**) ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

365. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. (*Makofii*)

MHE. PROF. NORMAN A. S. KING - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na taarifa hii, naomba niungane na wenzangu waliota pole kwa misiba ambayo Bunge lako Tukufu limeweza kuipata. Mungu azilaze mahali pema peponi roho za marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Awali ya yote, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* kwa sababu ya muda na ukubwa wa Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtiririko wa taarifa hii umezingatia maeneo makubwa matatu yafuatayo:-

Sehemu ya kwanza utangulizi; sehemu ya pili mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ikijumuisha, makusanyo ya mapato, upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2016/2017, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati, mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, makisio ya makadirio ya makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018, makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, mambo mengine muhimu yaliyojitokeza

wakati wa kuchambua na kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2017/2018; na sehemu ya tatu, maoni na ushauri wa Kamati na hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2), Kamati ilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata 2017/2018. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati imechambua mafungu matatu yaani Fungu 62 - Sekta ya Uchukuzi; Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi; na Fungu 68 - Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2016/2017, upatikanaji wa fedha. Sehemu hii inabainisha utolewaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Jedwali Na.1 hapo chini linaonyesha upatikanaji fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi kufikia Machi, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo si wa kuridhisha kwani kumeendelea kuwepo changamoto ya kutokutolewa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo hasa fedha za ndani. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, hadi kufikia Machi, 2017, Sekta ya Ujenzi ilipata asilimia 47, Uchukuzi asilimia 27.12 na Mawasiliano asilimia 3.8 tu ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo. Hii imekuwa ni changamoto kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia mwezi Machi baadhi ya miradi iliwa haijapata fedha yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,

inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 4,516,885,061,000. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonyeshwa kwenye jedwali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, bajeti iliyotengwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, imeongezeka kwa takribani Sh. 326,651,339,882 ukilinganisha na Mwaka wa Fedha uliopita yaani huu tunaomaliza 2016/2017. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa fedha zilizotengwa kwa baadhi ya miradi hususan upanuzi wa Bandari ya Mtwara, Bandari ya Tanga, Bandari ya Ziwa Victoria, Bandari ya Ziwa Tanganyika, Bandari ya Ziwa Nyasa na *TAZARA* ambayo mwaka uliopita haikupewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine yaliyojitekeza wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2017/2018 yanapatikana kwa kina katika sehemu ya 3.3 ya taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati ambao umetolewa katika vikao pamoja na ziara mbalimbali zilizofanywa na Kamati. Ushauri huu wa Kamati umezingatia umuhimu wa kuharakisha maendeleo katika nchi yetu. Ikumbukwe kuwa miundombinu ndiyo itakayowezesha tija na utendaji bora wa sekta zingine za kiuchumi au kijamii. Ni matarajio ya Kamati kuwa bajeti ya mwaka huu wa fedha, fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mwaka huu wa fedha kwa ajili ya sekta hizi zitatolewa kwa wakati ili kuharakisha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi. Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Uchukuzi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka lakini bado kiwango kilichotengwa hakipatikani kwa wakati hivyo kushindwa kukidhi malengo ya sekta hii kwa ukamilifu. Kama ilivyoelezwa awali, kiasi cha fedha za ndani ni asilimia 27.12 kilichotolewa hadi Februari, 2017 ni ndogo sana ukilinganisha na miradi

mikubwa iliyopo kwenye Sekta ya Uchukuzi kama vile, ukarabati na ununuzi wa vichwa vyatreni na mabehewa, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya treni na uboreshaji na upanuzi wa bandari. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kiasi cha fedha kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kinatolewa kwa ukamilifu na kwa wakati ili kuweza kuwa na ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa miradi hatimaye kufikia malengo tuliojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa reli ya Kati, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusaini mkataba na Kampuni ya YAPI MERKEZI ya Uturuki na MOTA-ENG/ ya Ureno kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ambapo jiwe la msingi la ujenzi wa kipande hicho cha reli umefanyika mwezi Aprili, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali wakati inaendelea na kipande hicho cha Dar es Salaam - Morogoro kuangalia uwezekano wa kujenga na kuimaliza reli hii ya kati na matawi yake yote ambayo ni kutoka Dar es Salaam - Tabora- Uvinza- Kigoma, Kaliua-Mpanda-Karema, Uvinza - Msongati, Tabora- Isaka - Shinyanga hadi Mwanza. Katika kujenga reli hii ni vizuri kipaumbele kiwe kwenye reli yenye matarajio ya mzigo mkubwa ili kuitengenezea mazingira stahiki Serikali kurudisha fedha zitakazokuwa zimetumika. Kukamilika kwa reli ya kati ni wazi kutainufaisha zaidi ya mikoa 15. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaishauri Serikali kuanza kufanya utafiti wa kupanua matawi (*spurs*) ya reli ya kati kutoka Bandari kavu ya Isaka (Shinyanga) hadi Rusumo Mkoani Kagera, hivyo kuwezesha mradi wa kuchimba madini ya *nickel*/huko Kabanga kutekelezeka. Hali kadhalika, ujenzi huu uende sambamba na kudhibiti maeneo korofi ya Kilosa na Gulwe na kuimarisha karakana za treni nchini ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi na kwa namna endelevu. Vilevile, Serikali iharakishe kukamilisha mchakato wa kuyaunganisha mashirika ya RAHCO na TRL, MSCL na TPA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TAZARA*. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake na Mwaka wa Fedha 2017/2018, kutenga kiasi cha shilingi billioni 26 kwa ajili ya ukarabati wa vichwa vyta treni pamoja na ununuzi wa mitambo kwa ajili ya karakana ya kuzalisha kokoto katika kituo cha Kongolo. Kamati inashauri Serikali pia ijenge kipande cha reli chenye urefu wa kilometra 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka katika eneo hilo la Magamba ni mkubwa hivyo unaweza kuipatia *TAZARA* mapato ya kutosha kuijendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kulipa sehemu kubwa ya madeni ya *TAZARA* ambapo kiasi cha shilingi billioni 16.8 zimelipwa kati ya shilingi billioni 22.9 zilizokuwa zinadaia. Bado Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kulipa deni lote linalodaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri *TAZARA* kubuni mbinu za kuijendesha kibashara ikiwemo kuangalia upya bei zake kwani wafanyabiashara wengi wamehamia kwenye usafiri wa barabara kwa kuwa ni nafuu kuliko treni. Kwa mfano, gharama za kusafirisha mbao kutoka Mbeya kwa gari ni Sh. 2,000,000 wakati kukodi behewa kwa mbao hizo hizo ni Sh. 3,600,000 bila ya kujumuisha gharama za kupeleka mzigo kupakia na baadaye kushusha na kupeleka sehemu ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe inaimarisha Menejimenti ya Kiwanda cha Kokoto cha Kongoro ili kiweze kujitegemea na *TAZARA* inunue kokoto hizo badala ya mfumo wa sasa ambapo *TAZARA* inatumia kokoto hizo bila kununua. Kwa sasa zaidi ya asilimia 60 ya kokoto zinazozalishwa hapo hutumiwa na *TAZARA* na kiasi kidogo kinauzwa kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bandari, Bandari ya Dar es Salaam ndiyo bandari kubwa kuliko zote Tanzania inayohudumia 90% ya shehena za aina mbalimbali karibu nchi nane ikiwemo Tanzania, Zambia, *DRC*, Burundi, Rwanda,

Uganda, Zimbabwe na Malawi. Kamati imekuwa ikitoa ushauri mara kwa mara ili kuhakikisha bandari hii na bandari nyingine zinafanya kazi katika mazingira yanayovutia wengi na kuliingizia Taifa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ushauri wa Kamati kuanzia (a - g) umetolewa mara kwa mara, naomba uchukuliwe kama ulivyo maana umeshatolewa mara ya tatu sasa. Kwa hiyo naomba niendelee na (h). Mfumo wa *TANCIS* wa *TRA* kutokurushu kugawanya *Bill of Lading* ili kutoa mizigo ambayo haina tatizo panapokuwa na tatizo la mizigo mmoja badala ya mizigo wote kuzuiwa na kusababisha gharama za tozo za hifadhi kwa mteja ambazo sio za lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa tozo kutokana na *Government Chemical Agencies* kutoza dola moja ya Marekani kwa tani hadi kufikia dola 100 kwa ya *Bill of Lading* kwa bidhaa ambazo wanazikagua kama vile mbolea na hivyo kuongeza gharama kutoka wastani wa dola 500 hadi kufikia dola 20,000 au zaidi kutokana na ukubwa wa mizigo. Idara ya Serikali na Mabenki kutokufanya kazi saa 24. Kamati inaishauri Serikali kutengeneza utaratibu wa kuhakikisha kuwa benki zinazohudumia bandari ya Dar es Salaam kufanya kazi saa 24, hii ni pamoja na wadau wote wanaohusika na bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iharakishe kuboresha mazingira ya Bandari ya Dar es Salaam kwa kuongeza kina katika gati namba 1 – 7 na upanuzi wa lango la kuingilia meli na kujenga gati namba 13 na 14. Kamati inapendekeza kuwa adhabu kali itolewe kwa mawakala yaani *freight and forwarders* wanaobainika kuongeza gharama kwenye hati za malipo ikiwemo kufutiwa leseni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kuwa na eneo la maegesho Kurasini Shimo la Udongo ambalo litatumika kuegesha magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini sasa ufanyike kwa haraka ili eneo hilo lipatikane kwani mojawapo ya kero za wafanyabishara wanaotumia

Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwa na maegesho jambo ambalo husababisha usumbufu na gharama zisizotabirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*), ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza tija na ufanisi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau asilimia 50 ya maduhuli yaani *retention* yatokanayo na viwanja vya ndege ili kusaidia kuongeza kasi ya shughuli za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini. Serikali ihakikishe kwamba kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha, fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya Mamlaka hii zitolewe ili kuendeleza viwanja vya ndege nchini hususan viwanja vya ndege vya Mwanza, Songwe, Mtwara, Songea, Iringa, Shinyanga, Sumbawanga na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, Kamati inaendelea kutoa masikitiko yake kwa kuwa mapendekezo yake ya umuhimu wa uwanja wa *KIA* kuendeshwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*) haujatekelezwa. Kamati inasisitiza kuharakishwa kwa mchakato wa kubadilisha uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro kutoka *KADCO* kwenda Mamlaka ya Viwanja vya Ndege yaani *TAA* ili kuweza kuongeza mapato, ufanisi na tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali ihakikishe inapata hati miliki za viwanja vyote vya ndege kwani Kamati imebaini kwamba ni viwanja vichache tu ambavyo vina hati. Vilevile, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania iwezeshwe kisheria kuwa Mamlaka kamili badala ya Wakala wa Serikali kama ilivyo sasa. Hii itawezesha taasisi kupitia Bodi yake kufanya maamuzi yanayohusu kazi na mambo mbalimbali kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vikosi vya zimamoto katika viwanja vya ndege, Kamati inashauri vikosi hivi viwe vikosi maalum vitakavyowajibika moja kwa moja kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kwani ilivyo sasa uwajibikaji wa vikosi hivi upo chini ya Wizara ya Mambo ya

Ndani ya Nchi wakati majukumu yao ya kila siku yapo chini ya Mamlaka ya Viwanja nya Ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania - *ATCL*, Kamati inashauri mafunzo ya menejimenti ya biashara ya ndege kwenda nchi zilizofanikiwa kama vile China na nchi nyingine yafanyike kwa viongozi wa Bodi na viongozi wakuu wa kampuni hii ili kuweza kujifunza jinsi ya uendeshaji wa biashara ya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inaishauri Serikali kuwa na mikakati ya kitaifa ya kuhakikisha kuwa *ATCL* inakuwa na uwezo wa kushindana na kutengeneza faida. Kwa sasa hakuna mtenganisho wa usimamizi wa sera na usimamizi wa biashara ya *ATCL*. Inaonekana kama *ATCL* ni Idara tu ndani ya Wizara badala ya kuwa Kampuni ya Biashara ya Taifa yenye mamlaka na mikakati yake kamili ya kuendesha biashara ya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *ATCL* iangaliwe kama shirika la kibiashara sio idara ya kiserikali kwa kuhakikisha inafanya biashara na siyo *routine functions* za idara za Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuwa na muundo wa *ATCL* unaokisi kazi rasmi za shirika la ndege ambayo ni biashara ya ndege. Muundo huo uipe Bodi madaraka kamili ya uendeshaji wa shirika na bodi pamoja na Mtendaji Mkuu yaani *CEO* wapimwe kwa matokeo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATCL* ijitangaze kwenye vyombo rasmi nya Kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijpange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo nya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja na kuwa na bei nafuu ili kuhakikisha kuwa abiria wengi zaidi wanatumia ndege hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Hali ya Hewa, Kamati inaipongeza Serikali kwani mwaka huu fedha yaani 2017/2018 imetenga shilingi bilioni 6.2 kwa ajili ya kuboresha utabiri wa hali ya hewa nchini, ununuzi wa rada

saba (7), ununuzi wa vifaa na kuimarisha miundombinu ya utabiri wa hali ya hewa. Kamati inashauri Serikali kuendelea kipatia Mamlaka hii muhimu fedha ili iendeleelee kujiiimarisha zaidi. Aidha, Serikali itoe ruzuku kwa ajili ya kusomesha wataalam wa hali ya hewa waliopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi. Katika Sekta ya Ujenzi, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itekeleze sera yake ya kuunganisha mikoa na mikoa kwa lami (*trunk roads*) kama vile Mikoa ya Mbeya -Makete- Njombe, Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora na Kigoma-Kagera. Aidha, miradi ya barabara hizi iendelee kupewa kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembizi yakinifu.

(ii) Serikali ijenge kwa kiwango cha lami barabara zote zinazounganisha nchi yetu na nchi nyingine hasa Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inajenga barabara pamoja na mambo mengine ni muhimu kuzingatia vigezo vya kiuchumi, kijamii pamoja na ahadi za Marais walostaaafu na Rais aliyeko madarakani. Mfano wa barabara zinazotakiwa kupewa kipaumbele ni pamoja na:-

Barabara ya Kitulo - Matamba- Chimala inayoelekea Hifadhi ya Taifa ya Kitulo; barabara ya Mlangali - Lupila - Ikonda, Muleba – Kanyambogo – Rubya – Nshamba – Muhtwe, barabara ya Runazi – Karambi – Kasindaga, Runazi – Burigi, barabara ya Njombe – Makete – Isyonji, barabara ya Mpanda – Kigoma, barabara ya Sumbawanga – Mpanda, barabara ya Masasi – Nachingwea – Ruangwa, barabara ya Mtwara – Newala –Masasi, barabara ya Liwale - Nachingwea, barabara ya Morogoro - Mziha-Handeni, barabara ya Njombe – Ludewa, barabara Mpanda – Mlele - Nyonga-Sinkenga - Tabora- Uvinza, barabara ya Malagarasi, barabara ya Kibo – Mwese, Manyoni - Kishapu, barabara ya Ngudu, barabara ya Ikwiriri – Masengi, barabara ya Kisarawe – Mlandizi, barabara ya Makofia – Mlandizi – Nzenga, barabara

ya Kilema – Mandaka – Babati, barabara ya Nongwi na barabara ya Lupembe, Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali na kuunga mkono juhudzi zake za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kuitia miradi mbalimbali kwa mfano mradi wa *DART* na ujenzi mbalimbali wa *flyovers*. Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo sheria za barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kuitia runinga, magazeti, redio na simu za mkononi. Pia vyombo vinavyohusika na usimamizi wa Sheria ya Barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu amejenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa ama kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee kukamilisha zoezi zuri liliolianzishwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli wakati alipokuwa Waziri wa Ujenzi kwa kuonesha mipaka ya barabara na hivyo, kupusha uvamizi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mzani unaopima magari huku yakiwa kwenye mwendo yaani *weigh in motion* katika eneo la Vigwaza - Kibaha na Mikese - Morogoro. Serikali iendelee kufunga mizani ya kisasa kama hii hasa katika vituo ambavyo vina msongamano mkubwa. Serikali iimarishe uwezo wa Wakala wa Majengo Tanzania yaani Tanzania *Building Agency* ili iweze kuzalisha fedha na kuchangia pato la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mawasiliano. Ufuatao ni ushauri wa Kamati kuhusu Sekta hii. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuharakisha kutafuta ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya makampuni ya simu kwa kutumia mtambo wa *TTMS* ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kuitia simu za mkononi. Ni vyema sasa *TCRA* kuhakikisha mazungumzo na mkandarasi yanakamilika ili kuweza kufunga mfumo wa *Revenue Assurance Management system* - yaani *RAMS* ambao utaweza kufahamu makusanyo halisi ya mauzo kwa kampuni kwa kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, kupertia *TCRA*, ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na changamoto zake, kama vile, uhalifu wa mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostahili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, *TCRA* iendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutekeleza Sheria ya *Cyber Crime*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iiwezeshe na kuipa fedha *TTCL* kwa ajili ya kupanua miundombinu yake kwa kuwa soko la ushindani kwenye Sekta ya Mawasiliano ni kubwa sana. Aidha, kwa kuwa *Airtel* imekuwa ikitangaza haipati faida kila mwaka, ni vyema sasa Serikali ikanunua asilimia 60 ya hisa zinazomilikiwa na *Airtel* ili kuweza kutumia miundombinu yake na kuongeza wigo wa maeneo yanayofikiwa na *TTCL* kwa haraka. Kamati inatambua kuwa uwekezaji wa *TTCL* kufikia kiwango cha kuenea nchi nzima unaweza kuhitaji fedha nyingi zaidi kuliko kununua hisa asilimia 60 zinazomilikiwa na *Airtel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali na Mashirika zilipe madeni ya *TTCL* yanayofikia takribani shilingi bilioni 9.8. Serikali kuhakikisha Wizara, Taasisi na Mashirika yake yanatumia Kituo cha Kanzi Data ya Taifa yaani *Internet Data Center* kilichojengwa kwa ajili ya kutunza na kuhifadhi kumbukumbu. Kamati inaona kuwa hakuna sababu ya Taasisi na Mashirika ya Serikali kupoteza fedha kwa kujenga vituo huku kituo hiki kipo kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, ni muhimu sana kuongeza uthibiti na usalama wa *data* kwa kuharakisha ujenzi wa vituo vingine vya kanzi data yaani *back up* haufanyiki.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kamati inaamini ushauri wake utazingatiwa ili kumsaidia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake kutekeleza mipango ya maendeleo na kuwapa Watanzania maendeleo.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa spika, kipekee, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Mwandisi Profesa Makame Mbarawa Mnyaa, Mbunge na Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Edwin A. Ngonyani, pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara hii Mhandisi Joseph Nyamuanga ambaye ni upande wa Ujenzi; Mhandisi Daktari Leonard Chamuriho (Uchukuzi); Mhandisi Daktari Maria Sasabo (Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Angelina Madete upande wa mawasiliano. Pia, Kamati inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hii ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua wajumbe kwa kuwataja majina kama walivyoordheshwa kwenye orodha na sitawasoma kwa ajili ya muda.

Mheshimwa Naibu Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah pamoja na Sekreterieti ya Kamati ikiongozwa na Ndugu Msigwe D. Bisile, Ndugu Hosiana John, Richard Masuke na Ndugu Catherine Kitutu pamoja na wafanyakazi wote Bunge kwa kuihudumia Kamati na kukamilisha taarifa hii. Mwisho namshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kutuwezesha kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mwenyekiti wa Kamati.

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA
UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA
FEDHA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO
KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa Taarifa hii umezingatia maeneo makubwa matatu (3) yafuatayo:-

1) SEHEMU YA KWANZA
Utangulizi

2) SEHEMU YA PILI

a) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ikijumuisha:-
i) Makusanyo ya Mapato 2016/17;
ii) **Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2016/2017;**
iii) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2016/2017;
iv) **Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

b) **Mpango wa Makadirio** Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018
i) Makisio ya Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

ii) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

iii) Mambo mengine muhimu yaliyojitekeza wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Wizara hii kwa Mwaka 2017/2010.

3) SEHEMU YA TATU

- i) Maoni na Ushauri wa Kamati; na
- ii) Hitimisho.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2), Kamati ilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na vikao vya kuchambua taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha (2016/2017) na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata (2017/2018). Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati imechambua mafungu yafuatayo:-

- a) Fungu 62- Sekta ya Uchukuzi;
- b) Fungu 98- Sekta ya Ujenzi; na
- c) Fungu 68- Sekta ya Mawasiliano.

SEHEMU YA PILI

2.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

2.1 *Makusanyo ya Mapato kuanzia Julai, 2016 hadi Februari, 2017*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, mafungu mawili (Fungu 62- Sekta ya Uchukuzi na Fungu 68- Sekta ya Mawasiliano) hayakuwa na Makadirio ya Makusanyo. Kwa upande wa Fungu 98- Sekta ya Ujenzi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi milioni 58,004,000.00** ambapo hadi kufika mwezi Februari, 2017 jumla ya **Shilingi milioni 28,290,000.00** zilikusanywa sawa na **asilimia 49** ya kiwango kilichokadiriwa kukusanywa kwa Sekta hii.

2.2 *Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2016/2017*

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii inabainisha utolewaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Jedwali Na. 1, Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi Kufikia Machi, 2017

SEKTA	Fedha Zilizoidhinishwa 2016/17			Fedha zilizotolewa hadi Machi, 2017		
	Mishahara na Matumizi Menginayo	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo	Mishahara na Matumizi Menginayo	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo
Uchukuzi	91,519,632,000	2,322,603,400,000	173,210,730,000	58,177,277,090.31	629,816,995,812.07 (27.12%)	131,677,689,289.22 (76.02%)
Ujenzi	35,941,266,000	1,831,365,922,000	344,838,635,000	23,061,572,448.19	853,422,431,000 (47%)	212,793,110000 (61.7)
Mawasiliano	3,073,949,000	5,000,000,000	87,730,110,000	2,262,734,561	190,309,000 (3.8%)	37,105,223,723 (42%)

Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano 2016/17

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo si wa kuridhisha kwani kumeendelea kuwepo changamoto ya kutokutolewa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo hasa fedha za ndani. Kwa mfano, katika mwaka 2016/2017 hadi kufikia mwezi Machi, 2017 Sekta ya Ujenzi imepata **asilimia 47**, Uchukuzi **asilimia 27.12** na Mawasiliano **asilimia 3.8** tu ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo. Hii imekuwa ni changamoto kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2017 baadhi ya miradi haikuwa imepata fedha yoyote. Miradi hiyo ni ujenzi wa Viwanja vya ndege vya Kigoma, Mpanda, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga na Shinyanga, uboreshaji wa bandari ya Dar es Salaam, bandari za Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Tanga na Mtwara.

2.3 Matokeo ya Utaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii inabainisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 98 (1), kwa lengo la kujiridhisha na utekelezaji wake. Kwa ujumla, Kamati imebaini changamoto kubwa iliyopo katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni kutokopatikana kwa fedha za miradi kwa wakati.

Jedwali Na.2, Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa na Fedha zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2017

N a	Fungu	Jina la Miradi	Fedha Miradi zilizoidhinishwa 2016/17		Fedha za Miradi zilizotolewa hadi Machi, 2017	
			Ndani	Nje	Ndani	Nje
1	98-Ujenzi	4138- Barabara ya Tegeta Kibaoni-Wazo Hill-Goba-Mbezi Mwisho Ardhi-Makongo-Goba	13,230,858,486.85	-	6,768,363,462.00	-
		4161- Ujenzi wa flyovers Dsm na barabara unganishi	20,428,000,000	6,284,545,000	1,547,938,000	7,459,520,000
		4123-Barabara ya Dumila-Klosa, Morogoro	2,838,000,000	-	-	-
2	62-Uchukuzi	4289- Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) Dar es Salaam	26,000,000,000	32,000,000,000	-	-
		4219- Treni ya kusafirisha Abiria Dar es Salaam (Dsm City Commuter Train)	7,500,000,000	-	-	-
3	68- Mawasiliano	4283- Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano	2,000,000,000	-	95,154,500	-

Chanzo; Taarifa ya WizChanzo: Taarifa Utekelezaji ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano 2016/17

2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2016/17, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kuhusu Bandari, Reli, Barabara na Mawasilino. Napenda

kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya masuala yaliyoshauriwa yapo yaliyozingatiwa kikamilifu na yapo yanayoendelea kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya ushauri wa Kamati ulioanza kuzingatiwa ni pamoja na ule wa kubaini changamoto za ushindani kati ya bandari ya Dar es Salaam na bandari zingine hususan Bandari ya Mombasa kwa mzigoto wa Rwanda na Uganda; Kamati imejulishwa kuwa Serikali imefanya yafutayo:-

i) Ujenzi wa reli ya kisasa ya *Standard Gauge* umeanza;

ii) Kuanzisha "block trains" ambapo mizigo ya nchi moja itasafirishwa peke yake bila kuchanganya na nchi nyingine ili kupunguza ucheleweshaji na upotevu wa mizigo;

iii) Jitihada za kuanza kutumika kwa Bandari Kavu ya Isaka ili kuwapunguzia wateja wa Rwanda na Uganda umbali wa kuchukuwa mizigo; na

iv) Kujenga bandari kavu katika maeneo ya kimkakati ya Ruvu, Mwanza na Arusha ili wateja wa Uganda na Rwanda wasikazimike kusafiri hadi Dar es Salaam au Tanga kuchukuwa mizigo yao.

Vilevile, kuhusu TAZARA; Kamati imejulishwa kuwa Serikaliimeendelea kulipa madeni ya Wafanyakazi wa TAZARA ambapo jumla ya **shilingi billioni 16.8** zimelipwa kati **shilingi billioni 22.9** zilizokuwa zinadaiwa. Hii ikiwa ni pamoja na kuanza kupeleka makato ya wafanyakazi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya ujenzi, baadhi ya ushauri wa Kamati ulioripotiwa kuanza kutekelezwa ni pamoja na kuendelea kuongeza mizani zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo (*weigh in motion*) ambapo mizani ya aina hiyo imekamilika kujengwa katika eneo la Mikese, na hivyo kupunguza msongamano mkubwa wa magari uliokuwa kero katika eneo hilo.

Aidha, ushaurii kuhusu namna kupunguza athari za matuta ya barabarani, Serikali imesambaza mwongozo kwa mameneja wa Mikoa wa TANROADS ili wajenge matuta kwa kizingatia viwango vilivyoainishwa katika mwongozo wa usanifu wa barabara wa mwaka 2011 (*Road Geometric Design Manual*) ya Mwaka 2011. Vilevile, tafiti mbalimbali zinaendelea ili kupata vigezo na viwango vya usanifu wa barabara bora zaidi ambapo usanifu na ujenzi kwa kutumia “super pave” umeanza kutumika ili kudhibiti barabara kuharibika mapema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Mawasiliano, baadhi ya masuala yaliyotolewa ushauri na Kamati na kuanza kutekelezwa ni pamoja na suala la Mamlaka ya Mapato Tanzania- TRA kutokuanza kutumia taarifa za takwimu za “Mobile Money” baada ya usimikwaji wa “Mobile Money Monitoring Solution”.

Kamati imejulishwa kuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imewapatia mafunzo maafisa watatu (mmoja wa TRA na wawili wa BOT) juu ya kuziona na kuchukuwa takwimu za miamala ya simu kwenye mfumo wa Mobile Money kwenye TTMS. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake kuhusu baadhi ya Makampuni ya Simu kukiuka Sheria ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 kwa kuhamishia nje ya nchi sehemu ya huduma ya uendeshaji wa mitambo ya mawasiliano (*Network Observation Centre*) hususan India na kufanya kazi kutoka huko. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA ilifanya uchunguzi na kubaini ukweli ambapo kutokana na udanganyifu huo Makampuni hayo ya Simu yalitozwa faini ya **shilingi millioni 100** kwa kila Kampuni.

3.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

3.1 *Makisio Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/18*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara ya Ujenz, Uchukuzi na Mawasiliano hususan Sekya ya

Ujenzi inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi milioni 62,004,000.00** kutoka Idara zenyeye vyanzo vya kama vile Idara ya Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Kiufundi, Kitengo cha Menejimenti ya Huduma za Ununuzi na Ugavi.

3.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi triliioni 4.5 (4,516,885,061,000)**. Mchanganuo wa fedha zinazoombwu unapatikana katika jedwali lifuatalo:-

SEKTA	MATUMIZI YA KAWAIDA	MIRADI YA MAENDELEO	JUMLA
Ujenzi	34,125,282,000	1,895,582,432,000	1,929,707,714,000
Uchukuzi	91,142,025,000	2,477,931,183,000	2,569,073,208,000
Mawasiliano	4,104,139,000	14,000,000,000	18,104,139,000
JUMLA KUU	<i>Chanzo Taarifa ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018</i>	<i>131,278,677,782</i>	<i>4,424,781,298,000</i>
			<i>4,516,885,061,000</i>

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, bajeti iliyotengwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka huu wa Fedha 2017/18 imeongezeka kwa takribani **shilingi 326,651,339,882** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha uliopita 2016/17. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa fedha zilizotengwa kwa baadhi ya hususan upanuzi wa bandari ya Mtwara, bandari ya Tanga, Bandari ya Ziwa Victoria, Bandari ya Ziwa Tanganyika, Bandari ya Ziwa Nyasa na TAZARA ambayo mwaka uliopita haikutengewa fedha.

3.3 Mambo Mengine yaliyojitekeza wakati wa Kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2017/2018

3.3.1 Sekta ya Uchukuzi

a) Uimarishwaji wa Mtandao wa Reli Nchini

Mheshimiwa Spika, katika mipango ya Sekta ya Uchukuzi ya Mwaka 2017/2018, mionganoni mwa malengo yaliyowekwa kuhusu kuimarisha miundombinu ya reli nchini ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati ya *Standard Gauge*. Serikali kwa kutambua umuhimu wake imetenga **shilingi bilioni 900(900,000,000,000.00)**.

Vilevile, Kamati imejulishwa kuwa zimetengwa **shilingi bilioni 5(5,000,000,000.00)** kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa njia za reli kwa Kiwango cha *Standard Gauge* kati ya Mtwara-Mbambabay, matawi ya Mchuchuma na Liganga, Tanga-Arusha-Musoma, pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu ikijumuisha njia mpya ya reli katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, **shilingi bilioni 26(26,000,000,000.00)** zimetengwa kwa ajili ya uboreshaji wa TAZARA na **shilingi bilioni 30.8 (30,800,000,000.00)** kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vichwa na mabehewa ya treni ya TRL.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusaini mkataba na Kampuni ya Uturuki pamoja na Ureno wa kujenga reli kutoka Dar es salaam mpaka Morogoro (Km. 205). Ujenzi wa reli hiyo yenye kasi ya 160 km kwa saa itasaidia kurahisisha usafiri hasa wa abiria kutoka Morogoro hadi Dar es Salaam. Hata hivyo, ili reli hii iweze kufanya kazi ipasavyo na kuwa na tija ni matarajio ya Kamati kuwa kasi ya ujenzi itaongezeka ili kukamilisha haraka Reli ya Kati na Matawi yake yote na kurahisisha usafirishaji wa abiria na mali ghafi hatimae kuchochaea ukuaji wa viwanda na hata kuongeza Pato la Taifa.

b) Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

i) Bandari ya Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, bandari hii ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu na inahudumia nchi jirani ambazo hazina bandari kama vile Rwanda, Burundi, Jamhuri ya kidemokrasia ya watu wa Kongo, Uganda, Zambia na Malawi. Hata hivyo, bado bandari hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za miundombinu inayounganisha bandari kama vile reli na kutokuwapo kwa maegesho kwa ajili ya magari yanayokwenda kupakia mizigo bandarini. Kwa ujumla, changamoto hizi zinasababisha nchi kupoteza wateja wengi waliokuwa wakitumia bandari ya Dar es Salaam na kwa sasa kuhamia katika bandari zingine shindani za Mombasa- nchini Kenya, Beira-nchini Msumbiji, nchini Durban- Afrika Kusini na Walvis Bay-huko Namibia.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto hizo, ni vyema Serikali kuhakikisha inakamilisha miradi ifuatayo:-

- (a) Mradi wa ujenzi na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam kwa kuimarisha na kuongeza kina cha gati Na.1-7;
- (b) Kujenga gati jipya la Ro-Ro;
- (c) Ujenzi wa jengo la kituo kimoja cha huduma kwa wateja (*One Stop Centre*);
- (d) Kuhamisha gati la mafuta la Kurasini (KOJ) na kujenga gati jipya la kisasa la kushushia mafuta ya aina zote;
- (e) Kuongeza maeneo ya kuhudumia shehena;
- (f) Karabati wa *flow meters*; na
- (g) Ukarabati wa minara ya kuongozea meli.

Mheshimiwa Spika, wakati ukarabati na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam unaendelea ni vyema Serikali

ikaanza pia ukarabati wa bandari nyingine muhimu kama vile bandari ya Tanga, bandari ya Mtwara , bandari ya Ziwa Tanganyika, bandari ya Ziwa Nyasa.

**c) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania
(Tanzania Airport Authority-TAA)**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kwani pamoja na kutekeleza majukumu yake mengine, katika kipindi cha 2016/2017/17 imesajili ndege 14 kwa mara ya kwanza nchini na kupewa vyeti vya ubora. Aidha, ndege zingine sabini na tisa (79) zilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora. Vilevile viwanja vikubwa kama vile Julius Nyerere, Aman Abedi Karume na Kilimanjaro vilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora baada ya kukidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, Licha ya kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- TAA imeondolewa jukumu la ujenzi wa viwanja vya ndege na kubaki na jukumu la kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege pamoja na kuboresha miundombinu, nyenzo na huduma zitolewazo kwenye kwenye viwanja vya ndege nchini. Changamoto kubwa ya imeendelea kuwa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendeleza viwanja vya ndege na kuboresha miundombinu na uboreshaji wa hivyo nchini.

Changamoto nyingine ni kuwapo kwa askari wa zimamoto katika viwanja vya ndege ambao wanawajibika kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilhali majukumu yao yapo chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania. Hali hii inaleta mkanganyiko katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Kamati imebaini nchi zingine kama vile Uganda, Kenya na Ghana katika kuepusha mkanganiko kama huu, Mamlaka inayoshughulika na viwanja vya ndege ndio inayokuwa na jukumu la kuajiri pamoja na kutoa mafunzo kwa askari wa zimamoto katika maeneo ya viwanja vya ndege. Hali kadhalika, katika Kiwanja cha Kimataifa cha Kilimanjaro askari wa zimamoto wameajiriwa moja kwa moja na chombo kinachosimamia kiwanja hicho ili kuleta ufanisi katika usimamizi wa utendaji kazi zake.

d) **Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga **shilingi bilioni 500** katika mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya ununuzi wa ndege mpya ambapo hadi mwezi Februari, 2017 **shilingi bilioni 234.9** zilikuwa zimetolewa. Vilevile yameshafanyika malipo ya awali ya asilimia 30 ya ununuzi wa ndege zingine nne (4) ambapo moja inatarajiwa kuwasili nchini Juni, 2017 na ndege nyingine mbili (2) zitawasili nchini Juni, 2018. Aidha, ndege kubwa aina ya Boeing 787 yenye uwezo wa kubeba abiria 262 itawasili Julai, 2018.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, ATCL inakabiliwa na changamoto zifuatazo; -

a) Uhaba wa rasilimali fedha;

b) Upungufu wa wataalam hasa marubani na waandisi ambaao wengi wao wamefikisha umri wa kustaafu;

c) Kuchelewa kurejea katika Chama cha Mashirika ya Ndege Duniani (IATA);

d) Kushindwa kuanza baadhi ya safari kwa wakati kwenye baadhi ya mikoa kama vile Katavi kutokana na mapungufu katika viwanja hivyo ikiwemo ukosefu wa magari ya kuzima moto.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa changamoto hizi zinapaswa kutafutiwa ufumbuzi kama inavyoelekezwa katika mapendekezo ya taarifa hii.

3.3.2 Sekta ya Ujenzi

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ujenzi kuititia Wakala wa Barabara ina jukumu la kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo kwenye mtandao wa barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa jumla ya kilomita 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilometa 22,214 ni barabara za mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara zetu ziweze kuitikta kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa

uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mpango na Mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

a) Miradi ya ujenzi wa Barabara

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri zinazoendelea kutekelezwa za ujenzi wa barabara nchini, changamoto kubwa imekuwa ni rasilimali fedha ambapo kuchelewa kwake mara nyingine kumesababisha gharama za miradi kuongezeka. Kwa Mfano, katika ujenzi wa barabara ya Dumila -Rudewa-Kilosa-Mikumi (km 142) ambapo kipande cha Dumila- Rudewa (km 45) kimejengwa kwa kiwango cha lami na ujenzi wa barabara hii umekuwa na gharama kubwa. Gharama ya ujenzi wa barabara hii ilikuwa **shilingi billion 41.9** lakini baada ya kutokukamiliwa kwa wakati, ongezeko la riba ilikuwa ni **shilingi billion 22.4**. Ongezeko hili ni kubwa zaidi ya nusu ya gharama za mwanzo za ujenzi kwani fedha hizi zilizoongezeka zingeweza kujenga nusu nyingine ya barabara kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini changamoto nyingine ya Wakala wa Barabara nchini ya kujenga barabara kwa vipande vidogo vidogo jambo linalosababisha miradi kutokumalizika na kuleta tija iliyyotarajiwa. Kwa mfano, katika barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es salaam, hususan barabara ya Tegeta kibaoni- Wazo hili-Goba-Mbezi yenye urefu wa kilomita 20, tenda imetangazwa kwa kilomita 5 tu. Aidha, barabara ya Ardhi - Makongo-Goba yenye urefu wa kilomita 9 lakini zinaanza kujengwa kilomita 4 tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujenga barabara kuu ili kufungua fursa za maendeleo na kuhakikisha miji yote mikuu na mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo mwishoni mwa 2017/18 bado kuna Mikoa mingine ambayo haijaunganishwa kwa barabara ya lami hususan mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Mbeya – Makete- Njombe, Lindi- Morogoro,Lindi-Ruvuma n.k. Aidha,

baadhi ya barabara za Mikoa ziko katika hali isiyoridhisha na nyingine hazipitiki wakati wa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

b) Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ufundu na Umeme Tanzania (*The Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency-TEMESA*) ni Wakala muhimu sana kwani unatoa huduma ya matengezezo ya magari, mitambo, pipipiki, mifumo ya umeme, majokofu na viyoyozi. Vilevile Wakala huu unasimamia ukodishaji wa magari na mitambo ya kusaga kokoto pamoja na kutoa ushauri katika nyanja mbalimbali za kihandisi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Wakala huu unakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za uchakavu wa miundombinu na vifaa vyta karakana, vitendea kazi vilivyopitwa na wakati na uendeshaji wa vivuko ambavyo haviwezi kujidesha vyenyewe.

Changamoto nyingine kubwa imekuwa ni Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali kutokulipa gharama za huduma na hivyo kusababisha Wakala kuwa linadai deni kubwa ambapo hadi kufikia Machi, 2017 jumla **shilingi bilioni 10,339,454,416.84** zilikuwa zinadaiwa. Deni hili limekuwa likiathiri utendaji kazi wa Wakala hasa kukosekana kwa vipuri, vilainishi na mafuta ya kuendeshea mitambo na gharama nyingine za uendeshaji. Kamati inaona ni wakati sasa vyombo vyta Serikali kuanza kulipia huduma zake ili kunusuru utendaji wa Mashirika yake yenyewe.

c) Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa viwanja vya ndege ni muhimu sana hasa ukuzingatia wakati huu ambapo tunajivunia kuwa na ndege zetu wenyewe. Hata hivyo, miradi hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya kutokutolewa fedha kwa wakati. Mfano, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 viwanja ambavyo hadi kufikia Februari, 2017

vilikuwa havijapata fedha yoyote kwa ajili ya ujenzi ni pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, Mpanda, Songwe, Mtwara, Sumbawanga na Shinyanga.

Kutokutolewa fedha za miradi hii kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ujenzi kwani kumekuwa na ongezeko la gharama kutokana na riba, mabadiliko ya bei za vifaa vya ujenzi na mabadiliko viwango vya kubadilisha fedha.

2.3.3 Sekta ya Mawasiliano

a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA ilianzishwa kwa Sheria Na. 12 ya Mwaka 2003 kwa ajili ya Kusimamia na Kuthibiti Mawasiliano Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu, naomba nitoe shukrani kwako na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuridhia Kamati hii kupatiwa mafunzo ambayo yamewezesha Kamati kuzielewa na kujionea shughuli za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA. Wakati wa mafunzo hayo, Kamati ilielezwa kuwa jitihada mbalimbali zimeendelea kufanya ambapo hadi sasa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania wameweza kuona idadi ya dakika zinazopigwa kwa simu za ndani kwa kila mwezi. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo bado hawajaweza kujua mapato yatokanayo na simu za ndani kwa kila mwezi. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inashirikiana na wadau wengine amba ni Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA, Benki Kuu ya Tanzania -BOT pamoja na vyombo vya Usalama kufanya majadiliano na mzabuni wa mtambo ili kuweza kupata ufumbuzi wa kupata takwimu za gharama za simu za ndani kwani mfumo uliopo sasa wa kukadiria mapato unakosesha Serikali fedha nydingi.

Mheshimiwa Spika, ikiwa kwa sasa tunaweza kupata takwimu sahihi za simu za Kimataifa zinazoingia nchini na kuweza kukusanya mapato pamoja na kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao (*mobile money*

transaction); kwa nini ishindikane kupata takwimu sahihi za simu za ndani ya nchi? Kuendelea kutegemea taarifa za mapato kutoka kwenye makampuni ya simu kuna uwezekano mkubwa kwa nchi kutokopata taarifa sahihi.

Mheshimiwa Spika, usajili walaini za simu umekuwa ni wa lazima baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA) ya 2010. Usajili huu unatakiwa kufanywa kwa kutumia vitambulisho vinavyotolewa na Serikali kama vile kitambulisho cha Taifa, kitambulisho cha kupigia kura, Hati ya kusafiria pamoja na leseni ya udereva ambavyo taarifa zake ziko kwenye mtandao wa Serikali. Kuchelewa kukamilika usajili wa vitambulisho vya Taifa pamoja na kuwa na anwani za makazi kumesababisha baadhi makampuni kukiuka masharti ya usajili wa laini na kutumia vitambulisho vingine.

b) Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta

Mheshimiwa Spika, kupitia Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 Serikali, imedhamiria kuanzisha mfumo wa anwani za makazi na misimbo ya posta. Sera hii kwa upana wake imejikita katika kuchangia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 yenye madhumuni ya kuwaondoa Watanzania kutoka kwenye umaskini na kuinua ubora wa maisha yao. Lengo ni kurahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa kama vile huduma za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi na usalama, huduma za dharura kama zima moto, magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi.

Kamati ilielezwa kuwa mfumo huu uko tayari nchi nzima, kinachosubiriwa ni Serikali za Miji na Mitaa kutekeleza katika maeneo husika. Mamlaka imeweka postikodi yaani namba za nyumba na majina ya mitaa maeneo ya mfano katika jiji la Dar es Salaam, Arusha na Dodoma. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa kutokuwa na mipango miji, ujenzi holela na hata ugumu wa kupatikana majina ya mitaa kutokana na mabishano juu ya majina katika ngazi za Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, bado upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu umeendelea kuwa kuwa ni changamoto. Mfano katika Mwaka wa Fedha uliopita mradi huu ulimetengewa kiasi cha **shilingi billion 3**, hadi kufikia Februari, 2017 kiasi cha fedha zilizopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ni **shilingi milioni 95,154,500** ambazo ni sawa na **asilimia 3** tu ya kiasi chote kilichotengwa.

Aidha Katika mwaka huu wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga **shilingi bilioni 3.8** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Ni matarajio ya Kamati kwamba fedha hizo sasa zitatorewa kwa wakati ili kutekeleza miradi hiyo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

c) Shirika la posta Tanzania

Mheshimiwa spika, Shirika hili linahitaji mtaji ili liweze kuijendesha kibiashara na kukabiliana na ushindani wa changamoto za Sekta hiyo. Kamati imejulishwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha imeendelea kulipa deni la shilingi bilioni 5.1 ambapo hadi mwezi Februari, 2017 zilikuwa zimelipwa shilingi **bilioni 2.7**.

Mheshimiwa spika, Shirika la Posta limekuwa likisuasua kutokana na kuwekwa kwenye horodha ya Mashirika yanayokusudiwa kurekebishwa jambo linalosababisha kushindwa kupata kibali cha kukopa fedha kwa taasisi za fedha kwa ajili ya kuongeza mtaji na kuendeleza rasilimali za Shirika. Kamati inaamini kwamba Bodi mpya pamoja na Mtendaji Mkuu mpya ailiyeteuliwa hivi karibuni watafanya marekebisho ili kuweza kulinusuru Shirika hili kwa kulifanya liweze kuzalisha na kupeleka kuanza kupeleka gawio Serikalini.

d) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF)

Mheshimiwa spika, Mfuko huu ulianzishwa na Serikali kwa Sheria Na. 11 ya Mwaka 2006 kwa lengo la kupeleka

mawasiliano kwenye sehemu zisizokuwa na mvuto kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijiji. Pamoja na juhudzi za Serikali kutoa ruzuku kwa kampuni za simu ili ziweze kufikia maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Kamati imebaini kuwa Makampuni makubwa ya simu bado hayajahimizwa vya kutosha kupanua huduma zao katika maeneo hayo.

e) **Kampuni ya Simu Tanzania – TTCL**

Mheshimiwa Spika, Kamati imeelezwa kuwa Serikali imenunua hisa asilimia 35 zilizokuwa zinamiliikiwa na *Bhati Airtel* na hivyo kumilliki hisa kwa asilimia 100 za Kampuni ya Simu Tanzania. Sheria ya Fedha Na. 2 ya mwaka 2016 inayataka Makampuni yote ya simu kuuza hisa asilimia 25 kwa watanzania kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam. Hata hivyo, kutokana na Kampuni hii kuijendesha kwa hasara wanunuzi wa hisa wanakosa uhakika wa usalama wa uwekezaji wanaokusudia kufanya kwa kampuni hii.

Mheshimiwa Spika, ili Kampuni hii iweze kuijendesha inahitaji kiasi cha takribani dola za Kimarekani **shilingi million 400** ili kuweza kuimarisha miundombinu ya kufikia katika mikoa yote. Kamati inaamini zipo njia nyingi ambazo Serikali inaweza kufanya kuinusuru Kampuni hii. Moja ya njia hizo ni kununua hisa asilimia 60 zinazamiliikiwa na Airtel Tanzania na kuwa na hisa zote asilimia 100. Hii itawezesha Shirika la Simu Tanzania kusambaza miundombinu yake kwa sehemu kubwa. Ni hatari kwa nchi kutokuwa na Kampuni yake ya mawasiliano yenye mtandao mpana wa kuweza kusikika nchi nzima.

Mheshimiwa spika, namna nyingine ya kuinusuru Kampuni hii ni kuhakikisha wadaiwa wake ambao kwa kiasi kikubwa ni Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali yanalipa madeni yao yote. Baadhi ya Mashirika/Taasisi za Serikali ambao wanadaiwa na Kampuni ya Simu Tanzania ni Jeshi

Ia Polisi Tanzania, Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA), TAMISEMI, Idara ya Uhamiaji, Shirika la Reli Tanzania, Shirika la Ndege Tanzania, Jeshi la wananchi Tanzania na taasisi zingine ambapo zinadaiwa takribा kiasi cha **shilingi bilioni 9, 804,401,878.88**. Kamati inaanmini kabisa Mashirika na Taasisi hizo zina bajeti kwa ajili ya kulipia huduma za mawasiliano, hivyo ni vema kulipa ili kuleta tija katika utendaji kazi wa Kampuni hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha kituo cha kisasa cha Kanzi Data ya Taifa kwa njia ya mtandao (*Internet Data Center*) ambacho kilianza kufanya kazi tangu Agost, 2016. Hiki ni kituo chenye kinauwezo mkubwa wa kuweza kutunza kumbukumbu kwa Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma, na hata Mashirika Binafsi na hata Watu Binafsi. Kamati imebaini kutokuwepo kwa hamasa kwa Serikali na Taasisi/Mashirika yake kwani mpaka sasa ni taasisi 13 tu ndizo zinazotumia kituo hiki. Hofu ya Kamati ni ikiwa Taasisi na Mashirika ya Umma yatajikita kujenga vituo vingine kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake wakati kituo hiki kipo na kinauwezo mkubwa wa kutunza kumbukumbu hizo. Taasisi kama vile Bunge inaweza kutunza taarifa rasi za Bunge (*Hansard*) na vilevile Mahakama inaweza kutumia kituo hiki kwa kutunza na mashauri yaliyokwisha tolewa uamuvi kwa mahakama (*Judgement*).

SEHEMU YA TATU

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati ambao umetolewa katika vikao pamoja na ziara mbalimbali zilizofanywa na Kamati. Ushauri huu wa Kamati imezingatia umuhimu wa kuharakisha maendeleo katika nchi yetu. Ikumbukwe kuwa miundombinu ndiyo itawezesha tija na utendaji bora wa sekta zingine za Kiuchumi au Kijamii. Ni matarajio ya Kamati kuwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017, fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya Sekta hizi zitatolewa kwa wakati ili kuharakisha maendeleo.

4.1 *Sekta ya Uchukuzi*

1) **Mheshimiwa Spika**, bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Uchukuzi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka lakini bado kiwango kinachotengwa hakipatikani kwa wakati hivyo kushindwa kukidhi malengo ya Sekta hii kwa ukamilifu. Kwa mfano, kiasi cha fedha za ndani cha asilimia 27.12 kilichotolewa hadi mwezi Februari, 2017 ni kidogo sana ukilinganisha na miradi mikubwa iliyopo kwenye Sekta ya Uchukuzi kama vile, ukarabati na ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya reli na uboreshaji na upanuzi wa bandari. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kiasi cha fedha kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kinatolewa kwa ukamilifu na kwa wakati ili kuweza kuwa na ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa miradi hatimaye, kufikia malengo tulyojilwekea;

2) Kuhusu ujenzi wa reli ya Kati, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusaini Mkataba na Kampuni ya YAPI MERKEZI ya Uturuki na MOTA-ENGI ya Ureno kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ambapo jiwe la msingi la ujenzi wa kipande hicho cha reli umefanyika mwezi April, 2017. Kamati inashauri Serikali wakati inaendelea na kipande hicho cha Dar es Salaam-Morogoro kuangalia uwezekano wa kujenga na kuimaliza reli hii ya kati na matawi yake yote ambayo ni kutoka:-

- i) Dar es Salaam – Tabora- Uvinza- Kigoma;
- ii) Kaliua-Mpanda-Karema;
- iii) Uvinza – Msongati;
- iv) Tabora- Isaka- Shinyanga- Mwanza; na

Katika kujenga reli hii ni vizuri kipaumbele kiwe kwenye reli yenye matarajio ya mzigo mkubwa ili kuitengenezea mazingira stahiki Serikali kurudisha fedha zitakazokuwa zimetumika. Kukamilika kwa reli hii kutainufaisha takribani

Mikoa 15 ya Tanzania kwa kusafirisha mizigo na abiria. Vilevile, kukamilika kwa reli hii kutasaidia bandari zetu kuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kushindana na Bandari zingine za nchi jirani;

3) Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuanza kufanya utafiti wa kupanua matawi (*spurs*) ya reli ya katika kutoka Bandari kavu ya Isaka (Shinyanga) hadi Rusumo Mkoani Kagera, hivyo kuwezesha mradi wa kuchimba madini ya nikeli huko Kabanga kutekelezeka. Hali kadhalika, ujenzi huu uende sambamba na kudhibiti maeneo korofi ya Kilosa na Gulwe, na kuimarisha karakana za treni nchini ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi na kwa namna endelevu;

4) Vilevile, Serikali iharakishe kukamilisha mchakato wa kuyaunganisha mashirika ya RAHCO na TRL, MSCL na TPA;

5) Kuhusu TAZARA, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake na mwaka huu wa fedha (2017/18) kutenga kiasi cha shilingi bilioni 26 kwa ajili ya ukarabati wa vichwa vya treni (traction motors) pamoja na ununuzi wa mitambo kwa ajili ya karakana ya kuzalisha kokoto katika kituo cha Kongolo. Kamati inashauri Serikali pia ijenge kipande cha reli chenye urefu wa kilometra 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mizigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kuipatia TAZARA mapato ya kutosha kuijendesha;

6) Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kulipa sehemu kubwa ya madeni ya TAZARA ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 16.8** zimelipwa kati ya shilingi **bilioni 22.9** zilizokuwa zinadaiwa. Bado Kamati inaendelea kusitiza Serikali kulipa deni lote linalodaiwa;

7) Kamati inashauri TAZARA kubuni mbinu za kuijendesha kibiashara ikiwemo kuangalia upya bei zake kwani wafanyabiashara wengi wamehamia kwenye usafiri wa barabara kwa kuwa ni nafuu zaidi ukilinganishwa na usafiri

wa treni. Kwa mfano, gharama za kusafirisha mbao kutoka Mbeya kwa gari ni shilingi 2,000,000 mzigo unafika mpaka Dar es Saalm ukilinganishwa na behewa moja linalokodiwa kwa kiasi cha shilling 3,600,000 bila ya kujumuisha gharama za kupeleka mzigo kupakia na baadaye kushusha na kupeleka sehemu ya biashara;

8) Serikali ihakikishe inaimarisha menejimenti ya kiwanda cha kokoto cha Kongoro ili kiweze kujitegemea na TAZARA inunue kokoto hizo badala ya mfumo wa sasa ambapo TAZARA inatumia kokoto bila kununua. Kwa sasa zaidi ya asilimia 60 ya kokoto zinazozalishwa hapo hutumiwa na TAZARA na kiasi kidogo kinauzwa kwa watu binafsi.

9) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu bandari, Bandari ya Dar es Salaam ndiyo bandari kubwa kuliko zote Tanzania inayohudumia asilimia tisini (90%) ya shehena za aina mbalimbali za nchi karibu nane yaani Tanzania, Zambia, DRC, Burundi, Rwanda, Uganda, Zimbabwe na Malawi. Kamati imekuwa ikitoa ushauri mara kwa mara ili kuhakikisha bandari hii na bandari nyingine zinafanya kazi katika mazingira yanayovutia wateja wengi kuzitumia na kuliingizia Taifa Mapato.

Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kwa Serikali kutafuta ufumbuzi wa masuala yafuatayo:-

a) Hofu ya wateja kutokana na kuanzishwa kwa Sheria ya kodi ya ongezeko la thamani (*Value Added Tax-VAT*) kwa huduma zitolewazo na mawakala kwenye mizigo inayosafirishwa kwenda nchi jirani (*VAT on transit goods*) ambayo ni kinyume na Sheria za Kimataifa. Kuwepo wa Sheria hii unawafanya wateja kutotumia bandari za Tanzania kwa sababu ya garama;

b) Mgongano wa tozo za hifadhi za mizigo ''*Customs Warehouse Rent*'' inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA na ''*Storage Charges*'' zinazotozwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA. Malipo haya yanafanana isipokuwa yametofautiana majina tu, hivyo

wafanyabiashara kuona kuwa wanalipa mara mbili igharama ya hifadhi za mizigo;

c) Tozo za barabara (*Road Tolls*) ambapo hutozwa **Dola za Kimarekani 16** kwa Kilomita ukilinganisha na **Dola za Kimarekani 8** kwa Kilomita zinazotozwa katika nchi zenye bandari shindani;

d) Tozo ya **Dola za Kimarekani 23** kwa tani kwa mizigo wa shaba ambapo bandari nyingine shindani kama Durban hutoza Dola za **Kimarekani 17.86**;

e) Kwa mujibu wa makubaliano ya mwanzo, kuna tozo kubwa kwa mizigo yote inayotoka ama kwenda Zambia tofauti na tozo za nchi nyingine kama Rwanda na Burundi. Kwa mfano, kasha la *urefu wa futi 40* linatozwa **Dola za Kimarekani 530** kwa mizigo wa Zambia badala ya **Dola za Kimarekani 320** ambazo hutozwa kwa kasha hilo hilo linalokwenda Rwanda au Burundi;

f) Himaya ya Forodha kwa Pamoja (*Single Customs Territory*) kwa mizigo wa Congo umeleta utata na kupunguza motisha kwa wafanyabiashara wa nchi hiyo kwa kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Hii inatokana na kuwa mfumo wa ukusanyaji kodi ndani ya DRC unatoa mwanya kwa baadhi ya wafanyabiashara katika nchi hiyo kutolipa kodi kwa asilimia mia moja (100%) tofauti na mizigo inayopatikana kwenye mfumo wa "*Single Customs Territory*" ambayo hutozwa kodi kwa asilimia mia moja (100%) jambo linalosababisha baadhi ya wafanyabiashara wa Congo kuona gharama kubwa kuitisha mizigo yao Tanzania;

g) Muda mfupi (*Short grace period of Transit Bulk liquid*) kwa mizigo wa mafuta wa nchi za jirani (Siku 30) bila kujali mazingira ya usafirisha wa barabara katika nchi yetu tofauti na nchi nyingine shindani ambazo ni siku 60 hadi 90 na utaratibu duni;

h) Mfumo wa TANCIS wa TRA kutokurushu kugawanya "*Bill of Lading*" ili kuruhusu kutoa mizigo ambayo

haina tatizo panapokuwa na tatizo la mzigo mmoja badala ya mzigo wote kuzuiwa na kusababisha gharama za tozo za hifadhi kwa mteja ambazo sio za lazima;

i) Kuongezeka kwa Tozo kutokana na "Government Chemical Agencies" kutoza USD 1.00 Kwa Tani badala ya USD100 Kwa "Bill of lading" kwa bidhaa ambazo wanazikagua kama vile mbolea na hivyo kuongeza kutoka wastani wa USD 500 hadi USD 20,000 au zaidi kutokana na ukubwa wa mzigo;

j) Idara za Serikali (OGD's) na Mabenki kutokufanya kazi masaa 24 /7. Kamati inaishauri Serikali kutengeneza utaratibu wa kuhakikisha benki zinazohudumia bandari ya Dar es salaam kufanya kazi masaa 24, hii ni pamoja na wadau wote wanaohusika na bandari;

k) Serikali iharakishe kuboresha mazingira bandari ya Dar es Salaam kwa kuongeza kina katika gati namba 1-7, upanuzi wa lango la kuingilia meli na kujenga gati namba 13 & 14;

l) Serikali kuharakisha TICS kuuza hisa **asilimia arobaini (40%)** kwa wafanyakazi na wananchi wa kawaida kupitia soko la hisa la Dar es Salaam. Pia Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuboresha mkataba huo;

m) Adhabu kali zitolewe kwa mawakala (*freight& forwarders*) wanaobainika kuongeza gharama kwenye hati za malipo ikiwemo kufutiwa leseni; na

n) Mchakato wa kuwa na eneo Kurasini-Shimo la Udongo ambalo litatumika kuegesha magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini sasa ufanyike kwa haraka ili eneo hilo lipatikane kwani mojawapo ya kero za wafanyakishara wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwa na maegesho jambo ambalo husababisha usumbufu na gharama zisizotabirika;

10) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA, ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza tija na ufanisi; Kamati inashauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau **asilimia 50** ya maduhuli (*retention*) yatokanayo na viwanja vya ndege ili kusaidia kuongeza kasi ya shughuli za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini;

11) Serikali kuhakikisha kabla ya mwaka wa fedha (2016/2017) kuisha, fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya Mamlaka hii zinatolewa ili kuendeleza viwanja vya ndege nchini hususan Kiwanja cha ndege cha Mwanza, Songwe, Mtwara, Songea, Iringa, Shinyanga, Sumbawanga na Kigoma;

12) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kupewa fedha zote zinazotakiwa kwa ajili ya ulipaji fidia kwa viwanja vya ndege vya Julius Nyerere International Airport-JNIA, Mwanza, Bukoba, Omukajunguti, Msalato, Kigoma, Shinyanga, Songwe, Sumbawanga, n.k;

13) Serikali kuharakisha kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa Jengo la Tatu (*Terminal III*) la abiria katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili mradi huu uweze kukamilika katika muda uliopangwa yaani Disemba 2017. Kamati inashauri wakati ujenzi wa jengo la tatu unaendelea, ni vyema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi;

14) Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro; Kamati inaendelea kutoa masikitiko yake kwa kuwa mapendekezo yake juu ya umuhimu wa uwanja wa KIA kuendeshwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA haujatekelezwa. Kamati inasisitiza kuharakishwa kwa mchakato wa kubadilisha uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro kutoka KADCO kwenda Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA na kuweza kuongeza mapato, ufanisi na tija;

15) Aidha, Serikali kuhakikisha inapata Hati Miliki za Mali zake zote kwani Kamati ilibaini viwanja vingi nya ndege nchini havina Hati Miliki isipokuwa Viwanja nya Arusha, Moshi, Dar es Salaam, Musoma na Tanga. Kuwa na Hati Miliki na kuweka mipaka kwa mfano, uzio au nguzo kutaepusha migogoro na wananchi wanaoishi kando kando ya viwanja nya ndege na kuzuia uvamizi;

16) Vilevile, Mamlaka ya Viwanja nya Ndege Tanzania iwezeshwe Kisheria kuwa Mamlaka Kamili badala ya Wakala wa Serikali kama ilivyo sasa. Hii itawezesha taasisi kuititia Bodi yake kufanya maamuzi yanayohusu kazi na mambo mbalimbali kwa wakati;

17) Kuhusu vikosi nya zimamoto katika viwanja nya ndege, Kamati inashauri vikosi hivi viwe vikosi maalum vitakavyowajibika moja kwa moja kwa Mamlaka ya Viwanja nya Ndege Tanzania kwani ilivyo sasa uwajibikaji wa vikosi hivi upo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakati majukumu yao ya kila siku yapo chini ya Mamlaka ya Viwanja nya Ndege;

18) **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL, Kamati inashauri mafunzo ya Menejimenti ya biashara ya ndege kwenda nchi zilizofanikiwa kama vile China n anchi zingine yafanyike kwa viongozi wa bodi na viongozi wakuu wa Kampuni hii ili kuweza kujifunza jinsi ya uendeshaji wa biashara ya ndege;

19) Kamati pia inaishauri Serikali kuwa na mikakati ya kitaifa ya kuhakikisha kuwa ATCL inakuwa na uwezo wa kushindana na kutengeneza faida. Kwa sasa hakuna mtenganisho wa usimamizi wa Sera na usimamizi wa biashara ya ATCL Inaoekana kama ATCL ni idara tu ndani ya Wizara badala ya kuwa Kampuni ya biashara ya Taifa yenye mamlaka na mikakati yake kamili ya kuendesha biashara ya ndege;

20) Aidha, ATCL iangaliwe kama shirika la kibashara na sio idara ya kiserikali kwa kuhakikisha inafanya

biashara na siyo “*routine functions*” za idara za Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuwa na muundo wa ATCL unaoakisi kazi rasmi za shirika na ndege ambayo ni biashara ya ndege. Muundo huo uipe Bodi madaraka kamili ya uendeshaji wa shirika; na bodi pamoja na Mtendaji Mkuu (CEO) wapimwe kwa matokeo; na

21) ATCL ijitangaze kwenye vyombo rasmi nya Kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa *iijipange* kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo nya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja na kuwa na bei nafuu ili kuhakikisha abiria wengi wanatumia ndege hizi.

22) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mamlaka ya Hali ye Hewa, Kamati inaipongeza Serikali kwani mwaka huu fedha (2017/18) imetenga **shilingi bilioni 6.2** kwa ajili ya kuboresha utabiri wa hali ya hewa nchini, ununuzi wa rada saba (7), ununuzi wa vifaa na kuimarisha miundombinu ya utabiri wa hali ya hewa. Kamati inashauri Serikali kuendelea kuipatia Mamlaka hii muhimu fedha ili iendeletelee kujimarisha zaidi. Aidha, Serikali itoe ruzuku kwa ajili ya kusomesha wataalam wa hali ya hewa (*meteorogist*) ili kukabiliana na uhaba wa wataalam wa hali ya hewa wenye shahada ya kwanza ambayo ndicho kigezo ama matakwa ya Shirika la Hali ya Hewa Nchini.

4.2 *Sekta ya Ujenzi*

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Ujenzi, Kamati inashauri yafuatayo;-

1) Serikali kutekeleza Sera yake ya kuunganisha Mikoa kwa barabara za lami (*Trunk Roads*) kama vile Mikoa ya Mbeya -Makete- Njombe; Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora na Kigoma-Kagera. Aidha, miradi ya barabara hizi ambayo inaendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembizi yakinifu.

Vilevile, Serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara zote zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine (*Boarder Roads*) hususani Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara;

2) TANROADS ipewe fedha za kutosha ili kujenga barabara za lami zenyeniyi viwango, hivyo, kuepusha hasara kubwa inayotokana na ukarabati wa mara kwa mara wa barabara zinazojengwa kwa changarawe ambayo huondoshwa na mvua muda mfupi baada ya kuwekwa hasa Wilaya zenyeniyi mvua nyingi;

3) Wakati Serikali inajenga barabara pamoja na mambo mengine ni muhimu kuzingatia vigezo vya kiuchumi, kijamii pamoja na ahadi za Marais waliostaafu na Rais aliye madarakani. Mfano wa baadhi ya barabara za kupewa kipaumbele ni pamoja na barabara ya Kitulo- Matamba-Chimala inayoelekea hifadhi ya Taifa ya Kitulo; barabara ya Mlangali-Lupila-Ikonda, Muleba-Kanyambogo-Ruby-Nshamba- Muhutwe; barabara ya Runazi- Karambi-Kasindaga; Runazi – Burigi; barabara ya Njombe- Makete-Isyonji; barabara ya Mpanda- Kigoma; barabara ya Sumbawanga-Mpanda; barabara ya Masasi-Nachingwea- Ruangwa; barabara ya Mtwara-Newala-Masasi; barabara ya Liwale-Nachingwea, barabara ya Morogoro-Mziha- Handeni; barabara ya Njombe -Ludewa; barabara Mpanda- Mlele-Nyonga-Sinkenga- Tabora- Uvinza; barabara ya Malagarasi, barabara ya Kibo- Mwese; Manyoni- Kishapu, barabara ya Ngudu; barabara ya Ikwiriri- Masengi; barabara ya Kisarawe- Mlandizi; barabara ya Makofia- Mlandizi- Mzenga; barabara ya Kilema-Mandaka; barabara ya Dodoma- Kondo- Babati na barabara ya Nongwi, barabara ya Lupembe, Morogoro;

4) Kamati inaipongeza Serikali na kuunga mkono juhudzi zake za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam kuititia miradi mbalimbali kwa mfano mradi wa DART chini ya TAMISEMI, ujenzi wa *fly overs*; barabara ya Dar es Salaam- Chalinze expresswayna ukarabati, upanuzi na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara

zinazounganisha maeneo ya Dar es Salaam (*Feeder Roads*). Kamati inashauri barabara ya Ardhi-Makongo iendelezwe kutoka Makongo CCM - Shule ya Msingi Londa hadi daraja la Kawe ili kufungua njia ya kwenda makaburi mapya Makongo; Aidha, Wakala wa Barabara Tanzania, unapojenga barabara kuhakikisha kuna fedha za kutosha ili kuweza kupunguza riba zinazotozwa na wakandarasi pale ujenzi unapokuwa umeshindikana kuisha kwa wakati uliopangwa;

5) Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vyaa habari kama Runinga, magazeti, redio na Simu za Mkononi. Pia vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee kukamilisha zoezi la zuri lilolianzishwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli wakati alipokuwa Waziri wa Ujenzi kwa kuonesha mipaka ya barabara, na hivyo, kuепusha uvamizi wa maeneo ya barabara;

6) Serikali kuharakisha kuleta Sheria bungeni ya Vyuma Chakavu ili kuweza kusaidia kupambana na watu wachache waliokosa uzalendo ambao wanaiba vyuma zenye alama za barabarani na kuviuza kama vyuma chakavu. Vilevile, kuchukuwa hatua kali za kulipa faini kwa magari ambayo yanagonga vibao vyaa alama barabarani;

7) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mzani unaopima magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weigh in Motion*) katika eneo la Vigwaza- Kibaha na Mikese Morogoro. Serikali iendelee kufunga mizani ya kisasa kama hii hasa katika vituo ambavyo vinamsongamano mkubwa wa magari kwenye mizani ili kuokoa muda;

8) Serikali kuimarisha uwezo wa Wakala wa Majengo Tanzania-TBA ili iweze kuzalisha fedha na kuchangia Pato la Serikali. Ni vyema Wakala huu pamoja na kujenga

nyumba za gharama nafuu, kuhakikisha zinakuwa katika hali ya ubora na viwango vinavyostaili; na

9) Kamati inaendelea kusisitiza kuunganishwa kwa Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo cha Matumizi Staiki ya Nguvu Kazi Mbeya (*Appropriate Technology Training Institute-ATTI*) na kuvisajili ili mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivi yaweze kutambulika.

4.3 Sekta ya Mawasiliano

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni ushauri wa Kamati kuhusu Sekta ya Mawasiliano;

1) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuharakisha kutafuta ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya Makampuni ya Simu kwa kutumia mtambo wa TTMS ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kuititia simu za mkononi. Ni vyema sasa TCRA kuharakisha mazungumzo na mkandarasi ili kuweza kufunga mfumo wa (*Revenue Assurance Management system-RAMS*) ambao utaweza kufahamu makusanyo halisi ya mauzo kwa kila kampuni kwa mwezi;

2) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuharakisha kutafuta ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya Makampuni ya Simu kwani Serikali mpaka sasa haijui kila kampuni kwa mwezi inakusanya kiasi gani cha fedha;

3) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kuititia njia ya mtandao na kuimarisha usalama wa watu na mali zao;

4) Serikali, kuititia TCRA, ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na changamoto zake, kama vile, uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa

picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kushirkiana na Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya *Cyber Crime* na kuwabana wahalifu;

5) Kamati inatambua kazi nzuri ya Serikali ya kusambaza Mawasiliano katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara kupitia Mfuko wa Mawasilino kwa Wote-UCSAF. Hata hivyo, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijiji. Kamati inashauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA kuweka masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni ya Simu pamoja na masharti mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii (*Corporate Social Responsibility*);

6) Kuhusu usajili wa namba za simu, Kamati inasitiza kasi ya zoezi hilikuongezwa ili kuweza kuwa na taarifa za kila mmiliki au mtumiaji wa simu kwa ajili ya usalama na kutekeleza Sheria ya Mawasiliano na Posta. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya kutoa vitambulishao vya Taifa ili kila Mtanzania aweze kutambuliwa na kuepuka udanganyifu unaofanywa kwenye mitandao;

7) Kuhusu mradi wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta, ili mradi huu uweze kutekelezeka kwa haraka na ufanisi, Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa;

8) Serikali kuwekeza kwa kuipa fedha TTCL kwa ajili ya kupanua miudombinu yake kwa kuwa soko la ushindani kwenye Sekta ya Mawasiliano ni kubwa sana. Aidha, kwa kuwa Airtel imekuwa ikitangaza kuwa haipati faida kila mwaka. Ni vyema sasa Serikali ikanunua asilimia 60 ya hisa zinazomilikiwa na Airtel ili kuweza kutumia miundombinu yake na kuongeza wigo wa maeneo

yatakayofikiwa na TTCL kwa haraka. Kamati inatambua kuwa uwekezaji wa TTCL kufikia kiwango cha kuenea nchi nzima unaweza kuhitaji fedha nyingi zaidi kuliko kuinunua hisa asilimia 60 za Airtel.

9) Vilevile, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali na Mashirika/Taasisi zake ziilipe madeni ya TTCL yanayofikia takribani **shilingi bilioni 9.8**, kwani katika bajeti ya taasisi hizo kuna fedha ambazo huwa zinatengwa kwa ajili ya kulipia gharama za mawasiliano sasa iweje washindwe kulipia mpaka deni kuwa kubwa kiasi hiki?;

10) Serikali kuhakikisha Wizara, Taasisi na Mashirika yake yanatumia Kituo cha Kanzi Data ya Taifa (*Internet Data Center*) kilichoengwa kwa ajili ya kutunza na kuhifadhi kumbukumbu. Kamati inaona kuwa hakuna sababu ya Taasisi / Mashirika hayo kupoteza fedha kwa kujenga vituo vyao huku kituo hiki kipo kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, ni muhimu sana kuongeza uthibiti na usalama wa data kwa kuharakisha ujenzi wa vituo vingine visaidizi vyta kanzi data (*back up*).

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kamati inaamini ushauri wake utazingatiwa ili kumsadia Rais na Serikali yake kutekeleza mipango ya maendeleo na kuwapa watanzania maendeleo.

Mheshimiwa spika, Napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Eng. Prof. Makame Mbarawa Mnyaa, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, (Mb), pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara hii Eng. Joseph Nyamuanga (Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Eng. Angelina Madete (Mawasiliano). Pia, Kamati inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua wajumbe kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

- | | |
|--|---------------|
| 1.Mhe .Prof Norman Adamson Sigalla King, Mb | - Mwenyekiti |
| 2.Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb | - M/wenyekiti |
| 3.Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb | Mjumbe |
| 4.Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb | " |
| 5.Mhe. Mizar Bakari Haji, Mb | " |
| 6.Mhe. James Francis Mbatia, Mb | " |
| 7.Mhe. Mansoor Shanif Hirani, Mb | " |
| 8.Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | " |
| 9.Mhe. Saul Henry Amon, Mb | " |
| 10.Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb | " |
| 11.Mhe. Quambalo Willy Oulwi, Mb | " |
| 12.Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb | " |
| 13.Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb | " |
| 14.Mhe. Dkt.Chuachua Mohamad Rashid, Mb | " |
| 15.Mhe. Mery Deo Muro, Mb | " |
| 16.Mhe. Ritta Enespher Kambati, Mb | " |
| 17.Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb | " |
| 18.Mhe. Khadija Salum Ally Al-Qassym, Mb | " |
| 19.Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb | " |
| 20.Mhe. Dua William Nkurua, Mb | " |
| 21.Mhe. Mussa Rashid Ntimizi, Mb | " |
| 22.Mhe. Lathifah Hassan Chande, Mb | " |
| 23.Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb | " |
| 24.Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb | " |
| 25.Mhe. Emmanuel Mwakasaka, Mb | " |
| 26.Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb | " |
| 27.Mhe. Charles Kitwanga, Mb | " |
| 28.Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mb | " |

Mheshimwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge. Dkt Thomas D. Kashililah pamoja na

Sekreterieti ya Kamati ikiongozwa na Ndg. Msigwe D. Bisile, Ndg. Hosiana John, Ndg. Richard Masuke na Ndg. Catherine Kitutu pamoja nawafanyakazi wote Bunge kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii. Mwisho namshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/18 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Prof. Norman Adamson Sigalla King, (Mb)
Mwenyekiti
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu

27/04/2017

NAIBU SPIKA: Sasa tutamsikia Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MHE. JAMES F. MBATIA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kusoma hotuba ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Mpango wa Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yake ina sehemu saba, sehemu ya kwanza ni utangulizi na kabla ya kuanza hotuba yangu nimpe pole Mheshimiwa James Francis Mbatia kwa kuugua kidogo kutokana na matatizo yake ya mguu

Iakini namshukuru Mwenyezi Mungu amerudi pamoja na Naibu Wake Waziri Mheshimiwa Qambalo ambao wote wana matatizo ya kiafya kidogo. Kwa hiyo, nimeomba kuwasilisha kwa niaba yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba ya Mheshimiwa Mbatia iingie kama ilivyo na mimi nitakuwa nasoma kwa kuruka kwa sababu ni hotuba ndefu sana. Kwa hiyo, nitajaribu kupitia baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Mwaka 2016/2017, utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya sekta zilizo chini ya Wizara. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hususan katika Idara ya Ujenzi iliidhinishiwa shilingi triliioni 2.167 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi triliioni 1.831 ni fedha za ndani ambazo zinajumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali yaani *Consolidated Fund* shilingi triliioni 1.248 na fedha za Mfuko wa Barabara shilingi bilioni 582. Aidha, shilingi bilioni 344 ni fedha za kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotolewa hadi Machi, 2017 ni shilingi triliioni 1.066 na kati ya fedha hizo shilingi bilioni 853 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 212 ni fedha za nje. Ukiangalia takwimu hizo ni kwamba fedha za ndani zilizotolewa kwa kulinganishwa na zile zilizopitishwa na Bunge ni 46.6 na fedha za nje zilizotolewa kwa kulinganisha na zilitokuwa zimeahidiwa ni 61.7%. Maana yake ni kwamba wahisani kwa ahadi zao wametekeleza zaidi kuliko upande wetu wakati miundombinu ni mali yetu. Naomba hii iingie maana kwenye kitabu ilikosewa kidogo hawakuweka hizo takwimu za *percentage*.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo kwa idara ya mawasiliano zilitengwa shilingi bilioni tano kama fedha za ndani na fedha za maendeleo kutoka nje zilitengwa shilingi bilioni 87.7. Kiasi kilichotolewa kutekeleza miradi ya

maendeleo kutoka kwenye fedha za ndani ni shilingi milioni 190 sawa na 3.8% huku fedha za nje zikitolewa shilingi bilioni 37.105 sawa na 40.2%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashindwa kuelewa ni kwa nini Serikali inatoa fedha za maendeleo kutoka kwenye chanzo cha fedha zetu za ndani kwa 3.8% tu, huku tukiwaaminisha Watanzania kwamba tunatekeleza miradi ya maendeleo kwa fedha zetu za ndani. Je, tumedhamiria kuwadanganya Watanzania au tunajidanganya sisi wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali haiko tofauti pia kwenye Idara ya Uchukuzi ambayo iliidhinishiwa shilingi trilioni 2.495 na kati ya fedha hizo shilingi trilioni 2.322 ni fedha za ndani na shilingi milioni 173 ni fedha za nje. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Februari, 2017 kiasi cha fedha zillizokuwa zimetolewa ni shilingi bilioni 761.5 sawa na 30.51% ya fedha zote za maendeleo. Fedha hizo zilizotolewa, kwa maana ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 816.995 ambazo ni sawa na 27.12%, huku fedha za nje zilitolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 131.677 ambazo ni sawa na 76.02%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata ufanuzi kuhusu fedha zilizotolewa na Serikali, yaani fedha za ndani, kwa nini kiasi kinachotolewa na Serikali ni kidogo kulinganisha na fedha za nje, kama tulivyoonesha hapo juu. Je, kuna tatizo gani ndani ya Serikali kwenye jambo hilo na Serikali ina utaratibu upi wa kuondoa tatizo hilo? Ikiwa tunataka kweli kutekeleza miradi ya maendeleo, kwa nini tusitoe fedha za ndani kwa asilimia kubwa kuliko fedha tunazotegemea kutoka nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Wizara kukosa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kama ilivyokuwa imekusudiwa ni dhahiri kwa mwaka huu wa fedha kumejitokeza matatizo ya kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali iliyoko chini ya Wizara hii, kulimbikiza madeni ya wakandarasi wanaojenga barabara mbalimbali hapa nchini

pamoja na miradi mingine ya kimaendeleo, ni kielelezo kwamba baadhi ya miradi ilishindwa kufanyika kutokana na ukosefu wa fedha. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu ya masuala yafuatayo:-

(i) Nini kilipelekea Hazina kushindwa kutoa fedha kwa wakati kama zilivyokuwa zimepitishwa na Bunge na wakati huo huo Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato kwa maana *TRA* wakitoa taarifa ya kuongezeka kwa mapato ambapo hadi Machi 2017, *TRA* inakusanya shilingi trillioni 10.87.

(ii) Ni hasara gani imepatikana kwa Serikali kutokana na kucheleweshwa kwa fedha hizo za miradi ya maendeleo.

(iii) Kwa kuwa fedha nyingi zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 zimekwenda kulipa madeni ya wakandarasi, je, tunapaswa kulipa riba au tozo za ucheleweshaji malipo kiasi gani baada ya Serikali kushindwa kutekeleza mkataba wa malipo kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muktadha huo, ikiwa Serikali inakusanya mapato hadi kuvuka lengo lake la ukusanyaji na ikiwa Taifa liliwekeea Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao uliidhinishwa na Bunge lako Tukufu na ikiwa Serikali pamoja na kukusanya mapato kupita lengo la ukusanyaji waliojiwekea lakini bado fedha kwa Miradi ya Maendeleo hazipelekwi hata nusu, kwa mujibu wa takwimu za Wizara hadi mwezi Februari 2017, tunapaswa kuna tatizo sehemu gani, hata kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi haipendi kukiri kuhusu hali hii mbaya, lakini Bunge hili tunao wajibu kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba, kuisimamia Serikali. Aidha viashiria vya kupeleka fedha kidogo kwenye miradi ya maendeleo wakati Serikali inakusanya fedha zaidi ya malengo iliyojiwekea ni ishara kwamba kuna tatizo la msingi ambapo Serikali haitaki kuliweka wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka 2017/2018. Sekta ya Ujenzi - Fungu 98, imetengewa jumla ya shilingi trillioni 2.17 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni ya kimkakati na isiyo ya kimkakati. Kati ya fedha hizo shilingi trillioni 1.831 ni

fedha za ndani na zilizobaki ni kutoka nje. Aidha, Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, imetengewa jumla ya shilingi triliioni 1.932 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi triliioni 1.350 ni fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi bilioni 582 ni fedha za nje na shilingi bilioni 682.284 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha ni pungufu kwa shilingi bilioni 243.354 ukilinganisha na makadirio ya mpango wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, vipaumbele vyaa miradi vitakavyotekelawa ni miradi inayoendelea kutekelezwa, miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo na miradi iliyopo kwenye Mpango wa Pili wa Taifa wa Miaka Mitano kwa maana ya 2016/2017 mpaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwaka jana na mpango ambao kwa mujibu wa Wizara hii, hauendani na miradi iliyowasilishwa kwenye bajeti ya Wizara hii. Aidha, baadhi ya miradi ambayo iko kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambayo ilipaswa kutekelezwa, miradi mingine haipo na miradi mingine imetengewa kiasi kidogo cha fedha kinyume na mpango uliopitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021), mpango wa kujenga mradi wa barabara ya Dar es Salaam- Chalinze - Morogoro (*express way*), kilometra 200 kwa mwaka huu wa Fedha 2017/2018 unapaswa kutengewa shilingi bilioni 231.16 lakini kwenye randama mradi huo unaonekana ukitengewa kiasi cha bilioni 12.771.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano huo hapo juu maana yake ni kwamba miradi itakayotekelawa ni ile inayoendelea sasa ambayo kimsingi mingine ilikwama

kutokana na Serikali kutopeleka fedha kwenye miradi hiyo. Miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo na miradi hii iliyoko kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ambayo nimeionesha hapo juu haijapangiwa fedha kama mpango wetu unavyotuelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwa makini na kutekeleza vipaumbele kama ambavyo vimepangwa. Kwa kutoteketeza Mpango wa Taifa maana yake ni kwamba Bunge lako Tukufu lilitumia rasilimali fedha na muda kama kivuli tu, huku Serikali ikifahamu kuwa mpango huu hautekelezeki. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona ipo haja ya kudurusu mpango huo kama unatekelezeza pia kuna haja ya kuwepo kwa sheria mahsusii ya kusimamia mpango huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, kwa kuwa Serikali katika makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018 inatarajia kukusanya jumla ya mapato ya Sh. 62,002,000.00 kutoka Idara ya Tawala na Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Ufundii na Idara ya Menejimenti ya Ununuzi na ugavi na kwa kuwa, kiasi cha fedha kinachotazamiwa kukusanya ni kikubwa kuliko makadirio ya mwaka 2016/2017 ambapo walikuwa wamepanga kukusanya Sh.58,000,000 na hivyo kufanya makadirio ya makusanyo kwa mwaka huu wa fedha kuongezeka kwa Sh. 3,998,000. Kwa kuwa vyanzo vya mapato vilivyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni vilevile vilivyoainishwa kutumika kwa mwaka wa fedha 2017/2018, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu:-

(i) Sababu zilizopelekea Wizara hii kushindwa kukusanya mapato yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zaidi ya nusu ya matarajio ya makusanyo waliyojipangia kukusanya kutoka vyanzo hivyo vilivyoorodheshwa sasa.

(ii) Serikali iliambie Bunge lako Tukufu mikakati thabitii ipi na endelevu ambayo Wizara hii inakuja nayo ili kuhakikisha makadirio ya makusanyo yanaongezeka badala ya utaratibu

wa sasa wa kuongeza idadi ya fedha tu, kwa mikakati ile ile na vyanzo vya mapato vilevile bila ubunifu wowote unaoongezeka. Ikizingatiwa kwamba vyanzo vya mapato vya Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Ufundu na Idara ya Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi vyote kwa pamoja vilishindwa kukusanya hata nusu ya makadirio kwa mwaka 2016/2017.

(iii) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa ufanuzi wa sababu ya utaratibu wa kuongeza takwimu kwenye bajeti, huku ikijua kabisa kwamba hakuna uhalisia wowote baina ya namba kubwa za takwimu, zinazoongezwa na au kutajwa na uhalisia wa makusanyo ya mapato. Je, kufanywa hivyo kuna maana nyininge zaidi ya kuwahadaa Watanzania na wananchi kwa ujumla?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataku kupewa ufanuzi, kushindwa kutekelezwa kwa miradi hiyo ya maendeleo kama ambavyo Serikali iliwaahidi Watanzania kuitia bajeti ya 2016/2017 ni dalili tosha kwamba mabadiliko ambayo Watanzania walihidiwa kuitia bajeti hiyo, yalikuwa matumaini hewa na hivyojamii ya Kitanzania sasa inazidi kushuhudia matatizo yanayotokana na miundombinu mibovu yakishindwa kukamilika kutoptaka na bajeti ya Serikali kushindwa kutekelezeka hata kwa kiwango cha asilimia 50%. Ucheleweshaji wa kumalizika miradi ya ujenzi pamoja na ongezeko la gharama za miradi ambazo kwa kiasi kikubwa hutokana na uwepo wa maslahi binafsi ya wachache katika nchi yetu vimezidi kuwa changamoto katika Awamu hii ya Tano ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akiwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka wa 2016/2017, Msemaji Mkuu alisema mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa barabara za lami zilizojengwa tangu tupate uhuru mwaka 1961 kwa kiwango cha lami ni wastani wa asilimia 16 tu ya barabara zote nchini zenyе urefu wa zaidi ya kilometra 35,000. Kwa kasi hiyo ya ujenzi ingeligharimu Taifa zaidi ya miaka 62 ijayo ili kukamilisha ujenzi wa kilometra 29,432 ambazo ni sawa

na asilimia 84 ya barabara zote zilizosalia kujengwa kwa kiwango cha lami nchini bila kujumuisha barabara mpya zinazosanifiwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia ilinukuu sehemu ya hotuba ya aliyekuwa Waziri wa Ujenzi ambaye kwa sasa ndiye Rais wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliyowasilisha katika Bunge la Kumi na kukiri kuwa Serikali ya CCM katika Awamu ya Nne ilishindwa kutekeleza ilani zao kikamilifu za uchaguzi za mwaka 2005 - 2015, kwa kujenga barabara nchini kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometra 5,568 sawa na asilimia 31 kwa lengo walilojiwekea la kujenga barabara zenye urefu wa kilometra 17,762.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni illata Serikali hili ya Awamu ya Tano kutoa maelezo ya kina mbele ya Bunge hili kuhusu mipango ya uhakika na endelevu ya kukamilisha ujenzi wa barabara hizo kwa viwango vinavyokubalika kimataifa na kwa kuzingatia vipaumbele kwa misingi ya kitaalam, badala ya ahadi nyingi zisizotekelzeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuitaka Serikali kufanya hivyo na pamoja na ukweli kwamba aliyekuwa Waziri wa Ujenzi katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne, ndiye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini bado utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi umezidi kudorora na hali hii inaudhishirishia umma wa Watanzania walio wengi kwamba hakuna utofauti wowote wa kimipango na mikakati thabitii ya kutatua tatizo la barabara hapa nchini kwa kuwa bajeti ya miradi ya maendeleo inatekelezwa chini ya 50%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi, kupandishwa hadhi, kukasimishwa barabara za Wilaya kuwa barabara za Mikoa. Halmashauri nyingi nchini kama si zote zimekuwa zikipeleka Wizarani maombi ya kupandisha/ kukasimu barabara hizo kuwa barabara za mikoa kwa

Wakala wa Barabara (*TANROADS*) baada ya barabara hizo kukidhi vigezo na baada ya maombi hayo kupitia vikao halali ngazi za wilaya na mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya barabara yanahitaji fedha nyingi na kwa vile Serikali Kuu haipeleki fedha za kutosha kwa halmashauri, uwezo wa kushughulikia unakuwa ni mdogo mno. Aidha, muda mrefu umepita tangu barabarani zipandishwe hadhi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali Kuu kupitia *TANROADS*ione haja ya kuzipandisha barabara mara kwa mara ili kutoa unafuu wa matengenezo kwa halmashauri lakini pia kuzijenga kwa ubora kama ambavyo zinakuwa zimepandishwa hadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya makandarasi na wahandisi washauri wa miradi ya barabara. Hadi kufikia Februari 2017, wakandarasi na wahandisi washauri walikuwa wanaidai Serikali takribani shilingi bilioni 788 ikililinganishwa na deni liliokuwepo 30 Juni, 2016 la takribani shilingi bilioni 930.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu siyo utaratibu mzuri kwa Serikali kuendelea kuwakopa wakandarasi ilhali wameshamaliza au kukamilisha wajibu wao wa kimkataba na kwa wale ambao hawajakamilisha ujenzi wa miradi yao huongeza kasi ya utekelezaji kutokana na namna ambavyo Serikali imekuwa ikitoa fedha kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana nyingine, kutowalipa wakandarasi kwa muda unaotakiwa na kadri ya mikataba imekuwa na athari kubwa, ikiwemo miradi kutokamiliika kwa muda na pia kuongezeka kwa gherama zinazotokana na riba. Ikiwa Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikijigamba sana kwamba inakusanya fedha nyingi sana, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulipa madeni yote ya wakandarasi na wahandisi washauri. Kuna msemo unaosema, "ujanja ni kulipa na siyo kukopa". (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala wa sheria katika miradi inayojengwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu dhamira ya Serikali kuhusu miradi mbalimbali inayojengwa hapa nchini. Pamoja na dhamira hii kuna tatizo la kutofuatwa kwa sheria za nchi zinazohusu utoaji wa tenda na manunuzi ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za mwanzoni mwa utawala wa Awamu ya Tano, Serikali ilisitisha shughuli za Sherehe za Uhuru na kuamriwa pesa ambazo zingetumika kwenye sherehe hiyo zielekezwe kwenye upanuzi wa barabara ya Mwenge. Tunafahamu pia umuhimu na dhamira ya kujenga mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa nyumba za kota eneo la Magomeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema hiyo, lakini si busara kukiuka sheria na kanuni tulizojiwekea ili kuendesha sekta hii ya ujenzi. Swali tunalojiuliza na ambalo Watanzania wengi wanataka kupata ufanuzi ni, je, Serikali ilitangaza lini tenda za miradi yote mitatu iliyotajwa hapo juu. Kama ndio tenda hizo zilitangazwa kwa kipindi gani na nani aliyeshinda tenda hizo? Ikiwa hakuna utaratibu wa kutangaza tenda hizo ni kwa nini Serikali yenye jukumu la kulinda na kuitetea Katiba ya nchi pamoja na sheria zake inakuwa ya kwanza kutofuata sheria hizo huku ikiwataka wananchi watii sheria bila shuruti? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 13 Machi, 1995 Baba wa Taifa Mwalimu Julius K.Nyerere aliongea na Watanzania kupitia hotuba yake kwa Klabu ya Waandishi wa Habari wa Tanzania. Katika hotuba hiyo Hayati Mwalimu Nyerere alieleza kuwepo kwa nyufa katika Taifa letu na mionganini mwa nyufa hizo ilikuwa ni pamoja na ufa wa pili aliouita "kupuuza na kutokujali Katiba, pamoja na ufa wa tatu aliouita kuendesha mambo bila kujali sheria". (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Mkuu wa Nchi kutoa kibali cha ujenzi kwa baadhi ya wakandarasi bila kufuata taratibu za kutoa tenda kinaacha maswali mengi ya kujiuliza. Hata kama Mheshimiwa Rais alikuwa na nia

njema, lakini sasa wananchi lazima wajiuilize kuhusu Serikali yao, kuna maslahi gani na wakandarasi waliopewa majukumu ya kukamilisha ujenzi wa miradi hiyo? Je, umuhimu wa kuwa na sheria pamoja na taratibu za kusimamia tenda za Serikali umesitishwa au hautumiki tena? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*). Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini ndiye mmiliki wa viwanja vya ndege hapa nchini. Kati ya viwanja vyote ni viwanja viwili tu vya Kilimanjaro na Dar es Salaam ndivyo vyenye uwezo wa kujiendesha. Viwanja vilivyobaki havina uwezo wa kujiendesha kutokana na mapato duni yanayozalishwa kutokana na viwanja hivyo. Hivyo, gharama za uendeshaji hutegemea mapato yanayopatikana kutoka katika viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii ni dhahiri kabisa kwamba sekta ya usafiri wa anga nchini inakabiliwa na changamoto kubwa ambazo ni pamoja na miundombinu hafifu, matatizo ya menejimenti, kushindwa kutolewa kwa fedha za kukamilisha miradi ya viwanja vya ndege kama ambavyo imeidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Sehemu ya pili inahusu ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere, sehemu ya tatu ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ambayo ndiyo nitaisoma, inahusu Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*). Tanzania imebahatika kuwa na ukanda mrefu wa bahari na pia kuwa nchi inayoweza kuhudumia mataifa ambayo kijigrafia hayajapakana na bahari na hivyo kuwa kitovu cha biashara katika ukanda huu kama ilivyo Dubai, Singapore na Hongkong kwani imepakana na nchi sita zisizokuwa na bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na bahati hii ya kijigrafia, bado bandari zetu, reli zetu zimeshindwa kutoa ushindani wa kibashara kwa bandari zingine za ukanda huu. Bandari ya Dar es Salaam ambayo hapa kwetu ndiyo kubwa

kuliko zote, imeendelea kuwa ya mwisho ikilinganishwa na bandari za ukanda huu kama vile Durban, Beira na Mombasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingi katika bandari yetu ambazo zimeongelewa mara nyingi ni pamoja na zifuatazo: Lango dogo la kuweza kupokea meli kubwa; kina kifupi cha maji; kodi ya *VAT on auxillary goods*; ushuru wa himaya ya forodha ya pamoja; urasimu uliokithiri na kadhalika. Hivyo vyote vimechangia kupoteza wateja, shehena ya mizigo na pia mapato ya Serikali kuendelea kushuka kila kukicha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano inahusu ujenzi wa gati nafikiri wataisoma na kuijibu, lakini nitasoma tu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu juu ya suala hilo. Mchakato wa ujenzi wa gati 13 na 14 umefikia wapi mpaka sasa? Baada ya kusitishwa kwa mchakato na mkataba wa awali ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali dhidi ya waliohusika na mchakato ambaao ulikiuka sheria za nchi? Ni lini ujenzi wa gati hizi utakamilika ili kuweza kuendana na mpango mkuu wa bandari hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita usafirishaji majini, nafikiri mtaisoma na kuzingatia kuhusu vivuko (a), (b) na (c).

Sehemu ya saba, ujenzi wa reli ya katì na matawi yake. Ujenzi wa reli hii umegawanyika katika vipande vinne vya Dar es Salaam – Morogoro (km 202), Morogoro – Makutopora (km 336), Makutopora – Tabora (km 294), Tabora – Isaka (km 133) na Isaka – Mwanza (km 254). Aidha, mkataba tulio nao na kampuni ya kutoka nchini Uturuki ni wa kujenga kipande cha Dar es Salaam – Morogoro. Bado ujenzi wa vipande vingine vya reli haviko katika mpango wowote na kwa kuwa ujenzi wa reli hii pia ni ushindani wa mizigo iliyoko nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Rwanda na kwa kuwa tunafahamu pia kwamba nchi washindani wanajenga reli kama hii kutoka Mombasa - Uganda- Rwanda ambako ujenzi wake umefikia mbali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina wasiwasi mkubwa, nikirejea kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya kwamba ili mradi uwe *economically viable* ni lazima tuweze kupata mizigo kutoka nchi za Burundi pamoja na DRC Kongo. Hivyo ujenzi wa vipande vifupi na kuacha eneo kubwa ambalo litawenza kuleta faida kubwa kiuchumi kama ushauri wa Waziri wa Fedha ulivyokuwa, inaonekana ni hasara kubwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umesainiwa mkataba wa shilingi trilioni 2.8 wa ujenzi wa reli ya Dar es Salaam - Morogoro zote zikiwa ni fedha za ndani kama Mheshimiwa Rais alivyosema Iakini vilevile Rais huyohuyo anasema Waturuki ndiyo watakaojenga kwa fedha za mkopo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kufahamu ukweli ni upi juu ya fedha zitakaojenga reli hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali Watanzania tuliaminishwa kuwa reli hii mpya itajengwa na Wachina kwa kutumia mkopo toka *Exim Bank* ya Uchina. Tanzania ilituma timu ya viongozi Uchina akiwemo Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Waziri wa Ujenzi na timu hiyo iliporudi tuliambiwa China imekubali kutusaidia na hatimaye kipande hiki cha Dar-es Salaam - Morogoro kitajengwa, ilipotangazwa makampuni mengi ya Kichina yalichukua vitabu lakini hawakuvirudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa reli inajengwa na Kampuni ya Kituruki kwa mkopo wa mkataba wa miezi 30 mpaka kukamilisha. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni nini kimetokea kwa mkopo uliokwishakubalika kutoka China? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba hotuba yote iingie na yale marekebisho niliyoyafanya, naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Silinde.

**MAONI YA MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA RASMI YA
UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA JAMES FRANCIS MBATIA
(MB) KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA
MWAKA 2016/2017 NA MPANGO WA MAPATO NA MATUMIZI
YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA
MWAKA WA FEDHA WA 2017/2018 KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

A: UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili niweze kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KRUB), kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, wizara ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano kwa mujibu wa tangazo la serikali namba 144 la terehe 22/04/2016 wizara hii imepewa majukumu makubwa ya kusimamia mambo yafuatayo: uandaaji wa sera za usanifu na ujenzi, usafiri na usafirishaji, teknolojia ya mawasiliano, (ICT) Posta na simu na kusimamia utekelezaji wake, kusimamia ujenzi wa barabara, madaraja, vivuko na maswala ya kiufundi, kusimamia kazi za umma na majengo ya umma, kusimamia shughuli za uhandisi na usanifu, usafirishaji wa reli na bandari; usafiri na usafirishwaji wa anga na viwanja vya ndege; utoaji wa leseni za usafirishaji, usalama katika usafirishaji na hali ya hewa; kuongeza tija katika utendaji kazi pamoja na kuendeleza rasilimali watu na kusimamia Idara na taasisi zilizo chini ya wizara.

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI
CHA MWAKA 2016/2017.**

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA
ZILIZO CHINI YA WIZARA:**

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na

Mawasiliano – Idara ya Ujenzi iliidhinishiwa shilingi 2, 176,204,557,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **1,831,365,922,000.00** ni fedha za ndani ambazo zilijumuisha fedha za mfuko mkuu wa serikali yaani consolidated fund shilingi 1,248,721,422,000 na fedha za mfuko wa barabatira shilingi 582,644,500,000.00. Aidha, shilingi **344,838,635,000.00** zilikuwa fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotolewa hadi machi, 2017 ni shilingi milioni 1,066,215.547 na katii ya fedha hizo shilingi milioni **853,422.431** ni fedha za ndani na shilingi milioni **212,793.11** ni fedha za nje. Maana yake mheshimiwa spika ni kwamba fedha zilizotolewa kwa wingi ni fedha za nje kuliko fedha za ndani na kwa maana hiyo kama Taifa hatuna dhamira inayoonekana kwa vitendo isipokuwa maneno matupu ambayo hayalisaidii taifa hili.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo kwa idara ya mawasiliano zilitengwa shilingi 5,000,000,000.00 fedha za ndani na fedha za maendeleo kutoka nje 87,730,110,000.00. Kiasi kilichotolewa kutekeleza miradi ya maendeleo kutoka kwenye **fedha za ndani ni shilingi 190,309,000 sawa na 3.8%** huku fedha za nje zikitolewa shilingi 37,105,223,723.00 sawa na 40.2%.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inashindwa kuelewa ni kwa nini serikali inatoa fedha za maendeleo kutoka kwenye chanzo cha fedha zetu za ndani kwa 3.8%, huku tunawaaminisha watanzania kwamba tunatekeleza miradi ya maendeleo kwa fedha zetu za ndani, je tunadhamiria kuwadanganya watanzania au tunajidanganya sisi wenyewe?

Mheshimiwa Spika, hali haiko tofauti pia kwenye idara ya uchukuzi ambayo iliidhinishiwa shilingi **2,495,814,130,000.00** na katii ya fedha hizo shilingi 2,322,603,400,00.00 ni fedha za ndani na shilingi 173,210,730,000 ni fedha za nje. Aidha hadi kufikia tarehe 31 Februari, 2017 kiasi cha fedha zilizokua zimetolewa ni shilingi 761,494,685,101.99 sawa na 30.51% ya fedha zote za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zilizotolewa, kwa fedha za **ndani** za miradi ya maendeleo ni shilingi 816,995,812.07 ambazo ni sawa na **27.12%**, huku fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 131,677,689,289.92 ambazo ni sawa na 76.02% zilitolewa.

Mheshimiwa Spika, kambi rasmi ya upinzani bungeni inataka kupata ufanuzi kuhusu fedha zinazotolewa na serikali, **yaani fedha za ndani**, kwanini kiasi kinachotolewa na serikali ni kidogo kulinganisha na fedha za nje zilizotolewa, kama tulivyoonesha hapo juu, je kuna tatizo gani ndani ya serikali kwenye jambo hilo na serikali ina utaratibu upi kuondoa tatizo hilo? Na ikiwa tunataka kweli kutekeleza miradi ya maendeleo kwa nini tusitoe fedha za ndani kwa asilimia kubwa kuliko fedha tunazotegemea kutoka nje?

Mheshimiwa Spika, kutokana na Wizara kukosa fedha za kutekeleza miradi ya mandeleo kama ilivyokuwa imekusudiwa ni dhahiri kwa mwaka huu wa fedha kumejitokeza matatizo ya kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali iliyoko chini ya wizara hii, kulimbikiza madeni ya wakandarasi wanaojenga barabara mbalimbali hapa nchini pamoja na miradi mingine ya kimaendeleo, ni kielelezo kwamba baadhi ya miradi ilishindwa kufanyika kutokana na ukosefu wa fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inataka kupata majibu ya masuala yafuatayo:

i. Ni nini kilipelekea hazina kushindwa kutoa fedha kwa wakati kama zilivyokuwa zimepitishwa na Bunge na wakati huo huo serikali kupitia mamlaka ya mapato nchini (TRA) wakitoa taarifa ya kuongezeka kwa mapato. Ambapo hadi Machi 2017 TRA ilikusanya TSHS triliuni 10.87?

ii. Ni hasara gani imepatikana kwa serikali kutokana na ucheleweshwaji wa fedha hizo za maendeleo

iii. Kwa kuwa fedha nyingi zilizotengwa kwenye bajeti ya 2017/2018 zinakwenda kulipa madeni ya wakandarasi, je tutapaswa kuwalipa riba au tozo la ucheleweshaji malipo kiasi gani baada ya serikali kushindwa kutekeleza mkataba wa malipo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, toleo la 2005, Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano **chenye madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri serikali** ya Jamhuri ya Muungano na **vyombo vyake vyote** katika **utekelezaji wa majukumu** yake kikatiba.

Mheshimiwa spika, katika muktadha huo, ikiwa serikali inakusanya mapato hadi kuvuka lengo lake la ukusanyaji na ikiwa Taifa lilijiwekea Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ambao uliidihiishwa na Bunge lako tukufu, na ikiwa Serikali pamoja na kukusanya mapato kupita lengo la ukusanyaji waliojiwekea lakini bado, fedha kwa miradi ya maendeleo hazipelekwi hata nusu, kwa mujibu wa takwimu za Wizara hadi mwezi February 2017.

Mheshimiwa spika tunapaswa kujiuliza wapi kuna tatizo, hata kama Serikali ya Chama Cha Mapinduzi haipendi kukiri kuhusu hali hii mbaya lakini bunge hili tunao wajibu kwa mujibu wa ibara ya 63 ya katiba, kuisimamia serikali. Aidha viashiria vya kupeleka fedha kidogo kwenye miradi ya maendeleo wakati Serikali inakusanya fedha zaidi ya malengo ilijojiwekea ni ishara kwamba kuna tatizo la msingi sehemu ambayo serikali haitaki kuliweka wazi.

C. BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/ 2018

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ujenzi fungu 98 imetengewa jumla ya shilingi **2,176,204,557,000/-** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni ya kimkakati na isyo ya kimkakati. Na kati ya fedha hizo shilingi **1,831,365,922,000/-** ni fedha za ndani na zilizobaki ni kutoka nje. Aidha sekta ya ujenzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imetengewa jumla ya shilingi 1,932,850,115,000.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo , shilingi 1,350,000,000.00 ni fedha za ndani kutoka mfuko mkuu wa serikali na shilingi 582,850,115,000.00 ni fedha za nje na shilingi 682,284,000,000.00 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya mfuko wa barabara.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha ni pungufu kwa shilingi 243,354,442,000.00 ukilinganisha na makadirio ya mpango wa bajeti ya wizara ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano kwa mwaka 2016/2017. Aidha vipaumbele vya miradi vitakavyotekelvezwa ni miradi inayoendelea kutekelezwa, miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo na miradi iliyopo kwenye Mpango wa Pili wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017-2020/21.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka Mitano, uliowasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwaka jana na mpango ambaao kwa mujibu wa Wizara hii, hauendani na miradi iliyowasilishwa kwenye bajeti ya wizara hii. Aidha baadhi ya miradi ambayo iko kwa mujibu wa mpango wa maendeleo ya miaka mitano, ambayo ilipaswa kutekelezwa, miradi mingine haipo na miradi mingine imetengewa kiasi kidogo kinyume na mpango uliopitishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano(2016/17-2020/21), mradi wa Dar es salaam- Chalinze- Morogoro Express way, (200-km)kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 unapaswa kutengewa (Tshs. Billion) 231.16 lakini kwenye randama mradi huo unaonekana ukitengewa kiasi cha Million 12,771.00. Mradi wa Ujenzi wa fly over eneo la TAZARA, mradi ambaao kwa mujibu wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano, mradi huu ulipaswa kutengewa 53.27 billion lakini mradi huu umetengewa shilingi Millioni 25,564.000. Ujenzi wa mradi wa njia ya mchepuko (construction of interchange at Ubungo) mpango wa miaka mitano unataka mradi huu kutengewa 74.23 (Tshs Billion) lakini kwenye randama kiasi kilichotengwa ni 20,326.000 (shilingi milioni)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano hapo juu, maana yake ni kwamba miradi itakayotekelvezwa ni ile inayoendelea sasa, ambayo kimsingi mingine ilikwama kutokana na serikali kutopeleka fedha kwenye miradi hiyo, Miradi inayofadhiliwa na washirika wa Maendeleo na miradi hii iliyoko kwenye

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano , ambayo nimeionesha hapo juu kwamba haijapangisha fedha kama mpango wetu unavyotuelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kuwa makini na kutekeleza vipaumbele kama ambavyo vimepangwa. Kwa kutotekeleza mpango wa Taifa , maana yake ni kwamba Bunge lako tukufu lilitumia rasilimali fedha na muda kama kivuli tu, huku serikali ikifahamu kuwa mpango huo hautekelezeki, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona ipo haja ya kudurusu mpango huo kama unatekelezeka pia kuna haja ya kuwepo kwa sheria mahususi ya kusimamia mpango.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Bajeti iliyopita ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilipanga kukusanya jumla ya shilingi **58,004,000.00** kuititia idara zenye vyanzo vyatia mapato ambazo ni idara ya utawala, idara ya huduma za ufundu na idara ya menejimenti ya ununuzi na ugavi.

NA KWA KUWA Serikali kuititia taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya wizara ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano imekiri kwamba hadi kufikia mwezi februari, 2017 Serikali imefanikiwa kukusanya shilingi 28,290,000.00 sawa na 48.77% ya malengo ya mwaka wa fedha 2016/2017,

NA KWA KUWA Serikali katika makadirio ya mpango na bajeti ya wizara ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018 inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi **62,002,000.00** kutoka idara ya tawala na rasilimali watu, idara ya huduma za ufundu na idara ya na idara ya menejimenti ya ununuzi na ugavi.

NA KWA KUWA, kiasi cha fedha kinachotazamiwa kukusanywa kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018, cha shilingi 62,002,000.00 ni kikubwa kuliko makadirio ya mwaka 2016/2017 ambapo shilingi 58,004,000.00 zilitarajiwaa kukusanywa na hivyo kufanya makadirio ya makusanyo kwa mwaka huu wa fedha kuongezeka kwa shilingi 3,998,000.00

NA KWA KUWA vyanzo vya mapato vilivyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni vile vile vilivyoainishwa kutumika mwaka wa fedha 2017/2018

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inaitaka serikali kulieleza bunge hili tukufu;

i. Mosi, sababu zilizopelekea wizara hii kushindwa kukusanya mapato yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zaidi ya nusu ya matarajio ya makusanyo waliyojipangia kukusanya kutoka vyanzo hivyo hivyo vinavyoorodheshwa sasa.

ii. Pili, Serikali iliambie bunge lako tukufu mikakati thabit na endelevu ambayo wizara hii imakuja nayo ili kuhakikisha makadirio ya makusanyo yanaongezeka badala ya utaratibu wa sasa wa kuongeza idadi ya fedha tu, kwa mikakati ile ile, na vyanzo vya mapato bila ubunifu wowote unaongezeka, ikizingatiwa kwamba vyanzo vya mapato vya idara ya utawala na rasilimali watu, idara ya huduma za ufundi na idara ya menejimenti ya ununuzi na ugavi vyote kwa pamoja vilishindwa kukusanya hata nusu ya makadirio kwa mwaka 2016/2017.

iii. Tatoo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa ufanuzi wa sababu ya utaratibu wa kuongeza takwimu kwenye bajeti, huku ikijua kabisa kwamba hakuna uhalisia wowote baina ya namba kubwa za takwimu zinazoongezwa na au kutajwa na uhalisia wa makusanyo ya mapato, je kufanya hivyo kuna maana nyingine zaidi ya kuwa hadaa watanzaniana wananchi kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, kushindwa kutekelezwa kwa miradi hiyo ya maendeleo kama ambavyo serikali iliwaahidi watanzania, kupitia bajeti yake ya 2016/2017 ni dalili tosha kwamba mabadiliko ambayo watanzania walihidiwa kupitia bajeti hiyo, yalikuwa matumaini hewa na hivyo jamii ya Kitanzania sasa inazidi kushuhudia matatizo yanayotokana na miundombini mibovu yakishindwa kukamilika kutokana na bajeti ya serikali kushindwa

kutekelezeka hata kwa kiwango cha asilimia 50%. Ucheleweshaji wa kumalizika miradi ya ujenzi pamoja na ongezeko la gharama za miradi ambazo kwa kiasi kikubwa hutokana na uwepo wa masilahi binafsi ya wachache katika nchi yetu vimezidi kuwa changamoto katika awamu hii ya tano ya serikali hii.

Mheshimiwa Spika, wakati akiwasilisha maoni ya kambi Rasmi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, alisema mbele ya bunge lako tukufu kuwa barabara za lami zilizojengwa tangu tupate uhuru mwaka 1961 kwa kiwango cha lami ni wastani wa asilimia 16 tu ya barabara zote nchini zenyе urefu wa zaidi ya kilometra 35,000. Kwa kasi hiyo ya ujenzi ingeligharimu Taifa zaidi ya miaka 62 ijayo ili kukamilisha ujenzi wa kilometra 29,432 ambaо ni sawa na asilimia 84 ya barabara zote zilizosalia kujengwa kwa kiwango cha lami nchini bila kujumulisha barabara mpya zinazosanifiwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya upinzani Bungeni pia ilinukuu sehemu ya hotuba ya aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi ambaye kwa sasa ni Rais wa serikali ya awamu ya tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliyowasilisha katika bunge la 10, na kukiri kuwa Serikali ya CCM katika awamu ya nne ilishindwa kutekeleza ilani zao kikamilifu za uchaguzi za mwaka 2005 mpaka mwaka 2015, kwa kujenga barabara nchini kwa kiwango cha lami zenyе urefu wa kilometra 5,568 sawa na asilimia 31 kwa lengo walilojiwekea la kujenga barabara zenyе urefu wa kilometra 17,762.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya hotuba hiyo, ambayo pia ili nukuliwa na Kambi Rasmi ya uUpinzani Bungeni ilisema;

"Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha serikali ya awamu ya nne, serikali imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Katika kipindi hicho, barabara zenyе urefu wa jumla ya kilometra 17,762 zimekuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo barabara zenyе urefu wa jumla ya kilometra 5,568 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

Aidha, barabara zenyе urefu wa jumla ya kilometra 3,873 zimeendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Katika kipindi hicho, barabara zenyе urefu wa jumla ya kilometra 4,965 zimefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na serikali inatafuta fedha za kuzijenga kwa kiwango cha lami. Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zenyе jumla ya kilometra 3,356 unaendelea"

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitaka Serikali hii ya awamu ya tano, kutoa maelezo ya kina mbele ya bunge hili kuhusu mipango ya uhakika na endelevu ya kukamilisha ujenzi wa barabara hizo kwa viwango vinavyokubalika kimataifa na kwa kuzingatia vipaumbele kwa misingi ya kitaalamu, badala ya ahadi nyingi zisizotekelzeza.

Mheshimiwa spika, Pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuitaka serikali kufanya hivyo, na pamoja na ukweli kwamba aliyejewa waziri wa ujenzi katika kipindi cha serikali ya awamu ya nne, ndiye Raisi wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania lakini bado utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika wizara ya ujenzi, mawasiliano na uchukuzi umezidi kudorora na hali hii inaudhihirishia umma wa watanzania walio wengi kwamba hakuna utofauti wowote wa kimipango na mikakati thabiti ya kutatua tatizo la barabara hapa nchini kwa kuwa bajeti ya miradi ya maendeleo inatekelezwa chini ya 50%

D. SEKTA YA UJENZI

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Wizara hii imeendelea kushindwa kutekeleza kikamilifu ahadi zake ilizozitoa mara kwa mara za kujenga barabara kwa viwango bora pamoja na vivuko, badala yake jamii ya kitanzania imeendelea kukumbana na changamoto za usafiri, mijini na vijijini. Katika jiji la Dar es Salaam na majiji mengine yanayokua kwa kasi kama vile Mbeya, Mwanza, Arusha na muda si mrefu Dodoma msongamano wa magari barabarani hasa vipindi

vya asubuhi na jioni limeendelea kuwa kero kwa wananchi wengi, hivyo kuchangia nguvu kazi kutokutoa tija inayokusudiwa...

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya vijiji ni hususan vipindi nya mvua, barabara nyngi nchini huwa hazipitki na TANROADS na Halmashauri za Wilaya kushindwa kutoa huduma za matengenezo. Hali hii imekithiri katika mikoa yenye mvua nyngi kama vile; Njombe, Iringa, Mbeya, Morogoro.

Mheshimiwa Spika, maandiko yanasema kuwa Tanzania inaelekeea kuwa nchi ya uchumi wa viwanda ambao kwa sehemu kubwa itategemea mazao ya wakulima kufika sokoni kwa muda unaohitajika. Jambo hili litaendelea kuwa nadharia kama serikali hawatakuwa na mipango makini yenye vipaumbele vinavyotekelzeza.

Mheshimiwa Spika, maneno upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, matangazo ya tenda yamekuwa ni kichaka cha kujifichia kwa serikali hii ya CCM. Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani na hatua hii ya kihandisi, lakini mara nyngi hatua hizi zimetumia fedha nyngi na matunda yake hayaonekani. Hivyo tunaitaka Serikali kuweka muda maalum wa kumaliza hizo ngonjera ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ili miradi ijulikane ni lini miradi inaanza na kumalizika.

Mheshimiwa Spika, Nchi hii tunayo sera inayotoa kipaumbele kwa kujenga kwa kiwango cha lami barabara zinazounganisha mikoa yetu. Pamoja na uwepo wa sera hii ni muda sasa bado mikoa mingi haijaunganishwa kama vile Arusha- Mara, Arusha-Simiyu, Manyara -Simiyu, Manyara-Tanga, Morogoro -Ruvuma, Morogoro -Lindi, Mbeya-Njombe n.k

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza watanzani ni lini barabara hizo zitajengwa kwa kiwango cha lami kama sera inavyosema.

1. KUPANDISHWA HADHI/ KUKASIMISHWA BARABARA ZA WILAYA KUWA BARABARA ZA MKOA/ TANROADS

Mheshimiwa Spika, Halimashauri nyingi nchini kama si zote zimekuwa zikipeleka wizarani maombi ya kupandisha/ kukasimu barabara hizo kuwa barabara za mkoa, kwa wakala wa barabara (TANROADS) baada ya barabara hizo kukidhi vigezo na baada ya maombi hayo kuitia vikao halali ngazi za wilaya na mikoa

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara yanahitaji fedha nyingi na kwa vile serikali kuu haipeleki fedha za kutosha kwa halimashauri, uwezo wa kuzishughulikia unakuwa ni mdogo mno. Aidha ni muda mrefu umepita tangia barabarani zipandishwe hadhi. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuu kuitia TANROADS ione haja ya kuzipandisha barabara mara kwa mara ili kutoa unaafuu wa matengenezo kwa halimashauri lakini pia kuzijenga kwa ubora zaidi.

II. MADENI YA MAKANDARASI NA WAHANDISI WASHAURI WA MIRADI YA BARABARA.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari 2017, makandarasi na wahandisi washauri walikuwa wanaidai serikali takribani shilling billioni 788 ikilinganishwa na deni liliokuwepo 30/06/2016 la takribuni shilingi bilioni 930.

Mheshimiwa Spika, huu siyo utaratibu mzuri kwa serikali kuendelea kuwakopa makandarasi ili hali wameshamaliza au kukamilisha wajibu wao wa kimkataba na kwa wale ambao hawajakamilisha ujenzi wa miradi yao huongeza kasi ya utekelezaji kutokana na namna ambavyo serikali imekuwa ikitoa fedha kwao. Kwa maana nyingine mheshimiwa spika, kutowalipa wakandarasi kwa muda unaotakiwa na kadri ya mikataba imekuwa na athari kubwa ikiwemo miradi kutokamilika kwa muda na pia kuongezeka kwa gharama zinazotokana na riba. Ikiwa serikali ya awamu ya tano imekuwa ikijigamba sana kwamba inakusanya fedha nyingi

na majigambo hayo ni ya kweli, Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inaitaka serikali kulipa madeni yote ya makandarasi na wahandisi washauri. Kuna msemo unaosema "ujanja ni kulipa na siyo kukopa"

III. UTAWALA WA SHERIA NA MIRADI INAYOJENGWA:

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu dhamira ya serikali kuhusu miradi mbalimbali inayoendelea kujengwa hapa nchini; pamoja na dhamira hii kuna tatizo la kutofuatwa kwa sheria za nchi zinazohusu utoaji wa tenda na manunuzi ya umma. Katika siku za mwanzo wa utawala wa awamu ya Tano, Serikali ilisitisha shughuli za sherehe za uhuru na kuamriwa pesa ambazo zingetumika kwenye sherehe hiyo zielekezwe kwenye upanuzi wa barabara ya MWENGE, Tunafahamu pia umuhimu na dhamira ya kujenga mabweni ya chuo kikuu cha Dar es salaam pamoja na ujenzi wa nyumba za kota eneo la Magomeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema lakini si busara kukiuka sheria na kanuni tulizojiwekea ili kuendesha sekta hii ya ujenzi. Swali tunalojiuliza na ambalo watananzania wengi wanataka kupata ufanuzi ni je, serikali ilitangaza lini tenda za miradi yote mitatu iliyotajwa hapo juu, kama ndiyo tenda hizo zilitangazwa kwa kipindi gani na nani aliyeshinda tenda hizo? Ikiwa hakuna utaratibu wa kutangaza tenda hizo ni kwanini serikali yenye jukumu la kuitetea katiba ya nchi pamoja na sheria zake inakuwa ya kwanza kutofuata sheria hizo huku ikiwataka wananchi watii sheria bila shuruti?

Mheshimiwa Spika, tarehe 13, machi 1995 Baba wa Taifa Mwalimu Julius K.Nyerere aliongea na watananzania kuititia hotupa yake kwa klubu ya waandishi wa habari wa Tanzania. Katika hotuba hiyo Hayati Mwalimu Nyerere alilieleza taifa kuwepo kwa nyufa katika taifa letu, na miongoni mwa nyufa hizo ilikuwa ni pamoja na ufa wa pili aliouita "kupuuza na kutokujali katiba, pamoja na ufa wa tatu aliouita kuendesha mambo bila kujali sheria

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mkuu wa nchi kutoa kibali cha ujenzi kwa baadhi ya wakandarasi bila kufuata taratibu za kutoa tenda kinaacha maswali mengi ya kujuliza hata kama mheshimiwa Rais alikuwa na nia njema, lakini sasa wananchi lazima wajiuilize kuhusu serikali yao, kuna maslahi gani na wakandarasi waliopewa majukumu ya kukamilisha ujenzi wa miradi hiyo? Je umuhimu wa kuwa na sheria pamoja na taratibu za kusimamia tenda za serikali umesitishwa au hautumiki tena?

E. SEKTA YA UCHUKUZI

I. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE (TAA)

Mheshimiwa spika mamlaka ya viwanja vya ndege nchini (TAA) ndiye mmiliki wa viwanja vya ndege hapa nchini, katika viwanja vyote hivyo, ni viwanja 2 tu, ambavyo ni viwanja vya Kilimanjaro, na Dar es salaam ndivyo vyenye uwezo wa kuijendesha. Viwanja vilivyobaki havina uwezo wa kuijendesha kutokana na mapato duni yanayozalishwa kutokana na viwanja hivyo, hivyo gharama za uendeshaji hutegemea mapato yanayopatikana kutoka katika viwanja vitatu tu.

Mheshimiwa spika, kwa hali hii ni dhahiri kabisa kwamba sekta ya usafiri wa Anga nchini inakabiliwa na changamoto kubwa ambazo ni pamoja na miundombinu hafifu, matatizo ya menememjimenti, kushindwa kutolewa kwa fedha za kukamilisha miradi ya viwanja vya ndege kama ambavyo imeidhinishwa na Bunge hili tukufu.

II. UWANJA WA NDEGE WA MWALIMU JULIUS NYERERE (TERMINAL THREE)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo la tatu la abiria (terminal III) katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilitengewa bilioni 26, Aidha fedha hizi hadi kufikia mwezi December 2016 zilikuwa hazijatolewa.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutoa ufanunuzi, ni kwanini fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi kama hii muhimu zinakuwa hazitolewi?

III. UJENZI WA UWANJA WA NDEGE WA SONGWE:

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa ndege wa Songwe ni kiungo muhimu, katika sekta ya uchukuzi hasa ukizingatia maeneo yanayohudumiwa na uwanja huo. Kwa takribani miaka miwili mfululizo ujenzi wa uwanja huu umekuwa ukisua sua bila serikali kutoa sababu za msingi, wakati kuna viwanja vimeanza kujengwa hivi karibuni hapa nchini na maendeleo yake yanaonekana kila kukicha. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 mradi huu ultengewa kiasi cha shillingi bilioni 5. Mwaka wa fedha uliofuada 2016/2017 mradi huu pia ultengewa fedha shillingi bilioni 7 lakini pia kufikia mwezi December 2016 hakuna fedha iliyotolewa kwa ajili ya mradi huu.

Ikiwa mradi huu unahitaji kiasi cha shillingi bilioni 16.154 ili kukamilisha ujenzi wake, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni, kuwa serikali wakati inafanya majumuisho hapa watoe kauli kwa wananchi wanao tarajia huduma bora kutokana na uwanja wa ndege wa Songwe, kuhusu sababu za msingi za kutopewa kipaumbele wakati huo huo miradi mingine ikipewa kipaumbele kutekelezwa.

IV. MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA)

BANDARI YA DAR ES SALAAM

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebahatika kuwa na ukanda mrefu wa bahari na pia kuwa nchi inayoweza kuhudumia mataifa ambayo Kijigrafia hajizapakanana na Bahari na hivyo kuwa kitovu cha biashara katika ukanda huu kama ilivyo Dubai, Singapore na Hongkong kwani imepakana na nchi sita zisizokuwa na Bandari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bahati hii ya kijiografia, bado bandari zetu, Reli zetu zimeshindwa kutoa ushindani wa kibashara kwa bandari zingine za ukanda huu. Bandari ya Dar es Salaam ambayo hapa kwetu ndiyo kubwa kuliko zote, imeendelea kuwa ya mwisho ikilinganishwa na bandari za ukanda huu kama vile Durban, Beira na Mombasa.

Mheshimiwa Spika, Changamoto nyingi katika bandari yetu ambazo zimeongeleta mara ni nyingi ni pamoja na zifuatazo; langoo dogo kuweza kupokea meli kubwa, kinakifupi cha maji, Kodi ya VAT on auxillary goods, ushuru wa himaya moja ya forodha (SCT), urasimu uliokithiri n.k hivyo vyote vimechangia kupoteza wateja, shehena ya mizigo na pia mapato ya Serikali kuendelea kushuka kila kukicha.

V. UJENZI WA GHATI NAMBA 13 & 14 BANDARI YA DAR ES SALAAM

Mheshimiwa spika, Hotuba ya msemaji mkuu wa kambi rasmi ya upinzani bungeni kwa wizara hii, katika mwaka wa fedha 2013/2014, kipengele cha 3.3.1 kuhusu ujenzi wa ghati 13 & 14 bandari ya Dar es salaam ilisema na ninaombaa kunukuu kwa lengo la kuikumbusha serikali.

"Mheshimiwa spika, kutokana na kandarasi iliyotolewa na mamlaka ya usimamizi wa Bandari kwa kampuni ya China Communication Construction Ltd iliyoleta mtafaruku mkubwa hapa nchini wa kujenga ghati namba 13&14 katika bandari ya Dar es salaam, mpango ambao ultokana na mpango mkuu wa bandari (Port Master Plan 2009-2028) mradi ambao ulikisiwa kutumia kiasi cha Dola za kimarekani milion 323 sawa na bilioni 517 fedha za kitanzania" kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi kuhusu uteuzi wa mshauri muelekezi na mkandarasi katika mradi huu iliyotolewa tarehe 9 Novemba 2012 na PPRA kamati ya uchunguzi kuhusu uteuzi wa mshauri muelekezi na mkandarasi wa ujenzi wa Ghati namba 13 & 14 katika Bandari ya Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa katika Bunge la 10 mkutano wa saba wa Bunge hilo kulikuwa na majadiliano ya kina kuhusiana na ujenzi wa ghati hizi, na Bunge liliagiza kuwa mradi huu utekelezwe kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya China kama ilivyopendekezwa na Mamlaka ya Bandari.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitaka kupata majibu juu ya masuala yafuatayo:

a. Mchakato wa ujenzi wa Ghati 13 & 14 umefikia wapi mpaka sasa?

b. Baada ya kusitishwa kwa mchakato na mkataba wa awali ni hatua gani zimechukuliwa na serikali dhidi ya waliohusika na mchakato ambao ulikiuka sheria za nchi.

c. Ni lini ujenzi wa Ghati hizi utakamilika ili kuweza kuendana na mpango mkuu wa bandari nchini?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kufanya hivyo, serikali haikuona nia thabiti ya kutekeleza mradi huo. Aidha miaka miatatu baadaye kamati ya bunge lako tukufu nayo inaona kuna tija kwa serikali kujenga gati namba 13 & 14 kama mkakati wa kullongezea taifa mapato. Kambi rasmi ya upinzani bungeni inasisitiza ushauri huo kama ilivyoshauri katika bajeti ya mwaka 2013/2014, ushauri ambao sasa kamati ya bunge ya miundombinu pia imeendelea kushauri katika vikao vyao na TPA.

VI. USAFIRISHAJI MAJINI:

a. KIVUKO CHA MV DAR ES SALAAM

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni katika mwaka wa fedha 2016/2017 alihoji kuhusu kivuko hiki, baada ya ripoti ya mkaguzi na mthibiti wa hesabu za serikali kubainisha kwamba kivuko hicho

hakikuwa na “delivery certificate” pamoja na madhaifu mengine ya kivuko hicho kutotimiza matakwa ya kimkataba.

Aidha Serikali ilikiri mbele ya Bunge lako Tukufu na kwa mujibu wa Hansard, serikali ililiambia Bunge hili kwamba Kivuko kile hakikupokelewa kwa sababu hakikuwa na vigezo vyta kimkataba na kwamba badala yake, kampuni iliyoizua Tanzania kivuko kile ilikuwa inakifanya matengenezo ili kiweze kukidhi vigezo vyta kimkataba likiwemo tatizo la speed ambalo ilikuwa kinyume na matakwa ya kimkataba.

Mheshimiwa Spika, wakati ambapo watanzania wanasubiri taarifa ya kama ukarabati wa kivuko kile umekamilika na kama kivuko kile sasa rasmi kimekadhiwa kwa serikali, Serikali kupitia Mheshimiwa Rais mapema mwaka huu aliutangazia umma wa Tanzania kwamba kivuko hicho sasa ni mali ya jeshi la wananchi wa Tanzania. Taarifa hiyo aliiota katika hotuba fupi baada ya sherehe fupi za kuapishwa kwa *wateule wake katika jeshi, polisi na mashauriano ya kigeni*, Mheshimiwa Rais Magufuli alinukuliwa akisema ile meli/kivuko cha “Mv Dar es Salaam” ambacho watu wamelikuwa wakiisemasema, sasa nimeamua kukigawa kwa JWTZ kikosi cha Wanamaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni haioni tatizo la maamuzi hayo ya Mheshimiwa Rais ikiwa lengo la kugawa Kivuko hicho ni kurahisisha ulinzi na patrol katika eneo la bahari ya Hindi ili kuweza kudhibiti magendo na uingizaji wa bidhaa haramu pamoja na wahamiaji haramu wanaotumia pwani na fukwe za bahari ya Hindi kuingia ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na nia hiyo thabiti tunayokubaliana nayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kufahamu mambo yafuatayo:

i. Ni lini marekebisho ya kivuko hicho yalikamilika, na ni lini kivuko hicho kilikabidhiwa kwa serikali Rasmi kwa maana ya kupokea Derivery certificate?

ii. Kwa vile bajeti ya kununuliwa kwa kivuko ililenga kuondoa tatizo la usafiri kutoka Dar es salaam hadi Bagamoyo mkoani Pwani, na sasa kivuko hicho kimebadilishwa matumizi na kukabidhiwa kwa Jeshi letu, Je, serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kununua kivuko kingine ambacho kitafanya kazi ambayo ilikusudiwa kufanywa na kivuko cha MV-DAR ES SALAAM?

iii. Kutokana na malengo ambayo umma wa watanzania tuliambiwa kwamba kivuko kinakwenda kufanya, je kivuko kile ambacho kilisanifiwa na kutengenezwa kwa ajili ya kusafirisha abiria, kinakithi vigezo kwa matumizi ya kijeshi kama iliyotangazwa?

b. USAFIRI KATIKA ZIWA VICTORIA

Mheshimiwa Spika, usafiri katika ziwa Victoria kwa wananchi wa mikoa na wilaya zinazolizunguka ziwa hili imekuwa ni changamoto kwa kiasi kikubwa. Katika ziwa hili meli mbili za serikali zilizokuwa zinatoa huduma ya usafiri kwenda kisiwa cha Ukerewe (Mv Butiama na Mv Clarius) zote ni mbovu kwa kipindi kirefu sasa na hivyo wananchi kutegemea usafiri wa meli binafsi ya Mv Nyahunge ambaao haukidhi mahitaji na kusababisha adha kubwa ya usafiri.

Katika bajeti ya 2016/2017 serikali ilitenga jumla ya shilingi Tsh 3.5 billion kwa ajili ya meli ya Mv Butiama lakini hadi sasa hivi matengenezo bado hayajaanza. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka serikali kutoa kauli ya lini fedha hizo ambazo ziliidhinishwa na bunge lako tukufu zitatolewa ili wananchi wa ukerewe waondokane na kero ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, Meli ya Mv Clarius ni meli iliyochoka na kuchakaa sana kwani imekuwepo tangia enzi ya mkoloni, jukumu la kutengeneza meli hii wameachiwa Marine Service Company Ltd (MSCL) ambaao nao wamechoka sana maana hata kulipana mishahara yao ni shida hadi kulipwa na Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inajuliza kampuni hii inapataje uwezo wa kutengeneza meli? Aidha ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuitaka

serikali kuja na suluhisho la usafiri wa uhakika kisiwani Ukerewe. Hasa ukizingatia kuwa mzabuni aliyeshindwa hatua ya awali ya ununuzi wa meli moja ameshindwa kukidhi matakwa ya zabuni baada ya kuleta taarifa za ufundi.

VII. UJENZI WA RELI YA KATI NA MATAWI YAKE

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa reli hii umegawanyika katika vipande vinne vya Dar es salaam – Morogoro (km 202), morogoro – Makutopola (km 336), makutopala – Tabora (km 294), Tabora – Isaka (km 133) na Isaka – Mwanza (km 254). Aidha mkataba tulio nao na kampuni ya kutoka nchini UTURUKI ni wa kujenga kipande cha Dar es salaam – Morogoro. Bado ujenzi wa vipande vingine vya reli haviko katika mpango wowote na kwa kuwa ujenzi wa reli hii pia ni ushindani wa mizigo iliyoko nchini Jamhuri ya Kidemkrasia ya Kongo, (DRC) Burundi na Rwanda na kwa kuwa tunafahamu pia kwamba nchi washindani wanajenga reli kama hii kutoka Mombasa- Uganda- Rwanda ambako ujenzi wake uko katika hatua za mbele zaidi.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina wasiwasi mkubwa, nikirejea kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba illi mradi huu uwe “**economically viable**” ni lazima tuweze kupata mizigo kutoka nchini DRC na Burundi. Hivyo ujenzi wa vipande vifupi vifupi na kuacha eneo ambalo litawenza kuleta faida kiuchumi kama ushauri wa Waziri wa fedha ulivyokuwa, inaonekana ni hasara kubwa kwa taifa.

Mheshimiwa Spika, Umesainiwa mkataba wa Tsh triliioni 2.5 ujenzi wa reli ya Dar es salaam – Morogoro zote zikiwa ni fedha za ndani kama Mhe Rais alivyosema, lakini pale pale anasema Waturuki ndio watajenga kwa fedha za mkopo, Kambi Rasmi inataka kufahamu ukweli ni upi katika hilo?

Mheshimiwa Spika, awali Watanzania tuliaminishwa kuwa Reli hii mpya itajengwa na Wachina kwa kutumia mkopo toka EXIM Bank ya Uchina. Tanzania ilituma timu ya viongozi Uchina akiwemo Rais Mstaifu wa Awamu ya NNE,

Waziri wa Ujenzi na timu hiyo iliporudi tuliambiwa China imekubali kutusaidia na hatajenga kipande hiki cha Dar-Moro, ilipotangazwa makampuni mengi ya Kichina yalichukua vitabu lakini hawakuvirudisha.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Reli inajengwa na Kampuni ya Kituruki kwa mkopo na mkataba wa miezi 30 kukamilisha. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali iwaeleze watanzania ni nini kimetokea kwa mkopo uliokwisha kubalika toka Uchina?

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizochapishwa na gazeti la kila siku la The Citizen katika ukurasa wa mbele zileleza kuwa benki ya Exim kutoka china ilikubali kutoa mkopo wenye riba nafuu wa Tsh trilion 17.5 au dola za Kimarekani bilioni 7.6 kwa ajili ya kuanza rasmi na kukamilisha ujenzi huo wa reli ya kati huku serikali ya Tanzania ikitangaza kutoa Tsh trilion 1, kwa ajili ya hatua za awali za mradi huo. Aidha baadhi ya watanzania pia wanafahamu kuwa Tanzania iliomba mkopo wa fedha kutoka India kiasi cha Tsh Trillion 17.5 ili kufanikisha ujenzi wa reli ya kati.

Mheshimiwa Spika, habari ya Benki ya Exim ya China kukubali kutoa mkopo wenye masharti nafuu wa dola za Marekani Bilioni 7.6 sawa na Zaidi ya shilingi trilion 17.6 za kitanzania kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa mradi mkubwa wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa, na taarifa za utajji saini makubaliano ya awali ya ujenzi wa reli ya kati (standard gauge) ziliripotiwa pia na serikali kupitia kitengo cha mawasiliano Serikalini,Wizara ya Ujenzi , Uchukuzi na Mawasiliano na shirika la Utangazaji la Uingereza BBC, tarehe 20 julai , 2016 . Aidha kwa mujibu wa taarifa hiyo, mradi wa ujenzi wa reli ya kati utahusisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha kisasa kutoka Dar es salaam – Tabora- Isaka- Mwanza. Tabora – Mpanda – Kalemela. Tabora – Uvinza- Kigoma na Isaka- Keza -Msongati.

Mheshimiwa spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka serikali kutoa kauli sahihi kuhusu mkanganyiko huu, je, Ni kweli reli ya kati inajengwa kwa fedha za ndani kama

ambavyo inasemekana? Ikiwa ni ndiyo je mkopo kutoka benki ya Exim China unahusu ujenzi wa reli ipi na nini kilichotokea makampuni ya China ambayo yalikuwa awali yanatajiwa kujenga mradi huu kutojenga na ghafla kampuni ya kutoka nchini UTURUKI ikapewa tenda hiyo? Ni vyema watanzania ambao wanawajibika kulipa mikopo hii kuitia kodi zao, wakaondolewa sintofahamu iliyopo mionganoni mwao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wakati akizindua ujenzi wa reli ya kati alinukuliwa akiwaambia watanzania kuwa dereva mzuri wa lori ni yule ambaye hasikilizi kelele za abiria wake na yeye kama Dereva hatasikiliza kelele hizo. Kelele hizo yamkini ni maoni yanayotolewa dhidi ya miradi mbalimbali inayoendelea hapa nchi; Aidha kauli hiyo pia inakiuka ibara ya 63 ya katiba ya nchi, kwa kuwa kuishauri serikali siyo kupiga kelele kama inavyodaiwa. Pamoja na hayo hajjalishi kama kelele hizo zina nia njema au hazina nia njema, anachosema dereva huyu ni kwamba hayuko tayari kusikiliza ushauri wowote, uwe mzuri au mbaya anachoamini ni kwamba yeye anafahamu kila kitu na hapaswi kushauriwa. Aidha pamoja na kasumba hii ya serikali hii ya awamu ya tano, ya kutopenda kupokea ushauri hata ukiwa na tija kiasi gani kwa taifa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kurudia ushauri ufuatao kwa manufaa ya taifa letu la Tanzania kuhusu ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa;

i. Taifa linahitaji reli inayojengwa, kujengwa kwa mtazamo mpya wa kisasa na wa upeo wa miaka mingi ijayo. Tunahitaji reli ambayo itaendana na mazingira tuliyonayo ya ukubwa wa nchi na fursa tuliyonayo ya nchi zilizotuzunguka zinazotegemea bandari zetu. Aidha hoja za mwendo kasi na uwezo wa kubeba uzito mkubwa ni vitu vya kuzingatia katika ujenzi huo.

ii. tunashauri na tunaendelea kushauri reli ijengwe kwa mtazamo wa mbali wa zaidi ya miaka 50 ijayo, tuanze na reli moja sambamba na hii iliyopo, lakini mpango uwe kuwa na zaidi ya reli moja hapo baadaye ili kuwezesha

usafirishaji katikati ya Tanzania na nchi jirani kuwa wa muda mfupi zaidi, ili kuzivuta nchi jirani kuona reli yetu ndiyo ya pekee ya kuwafkishia mizigo yao kwa muda mfupi na kwa usalama zaidi, ikiwepo sababu za kiutendaji.

iii. Ujenzi wa ‘Standard Gauge’ uende sambamba na kuimarisha mawasiliano katika kuendesha shughuli za reli ili kuongeza ufanisi.

iv. Ili kufupisha muda wa ujenzi, kuwepo na wakandarasi ambao watapewa vipande vidogo vya takribani kilomita 200 ambavyo vitajengwa kwa wakati mmoja ili kuwezesha reli hii ikamilike kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa majibu niwapi , fungu lipi imetengwa bajeti ya kujenga reli ya umbali wa km 1,220 kutoka Tabara-kigoma, Isaka – Mwanza, Uvinza- Msongati na kaliua-Mpanda-Karema, reli ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano awamu ya Pili inapaswa kuwa imetengewa shilingi Billion 102.89.

a. KUSHINDWA KUJENGWA KWA RELI NYINGINE

Mheshimiwa spika, Ujenzi wa reli ya kutoka Mtwara-Mbambabay na matawi ya kwenda Liganga na Mchuchuma yenye umbali wa 1,000 km kwa kiwango cha standard gauge (bil 340.50), ujenzi wa reli ya Tanga –Arusha-Musoma na matawi kwenda Minjingu na Engaruka (shilingi bilioni 110.43), ununuzi wa mabehewa ya mizigo 2,234 (shilingi bilioni 0.19) pamoja na ununuzi wa vichwa vya treni 63 (shilingi bilioni 0.26) ni mionganoni mwa vipaumbele vya taifa hili ambavyo tulikubaliana katika mpango wa miaka mitano lakini ujenzi huu pamoja na ununuzi huu wa mabehewa hazionekani katika bajeti ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa spika, Miradi ya maendeleo kwenye sekta ya Uchukuzi inaonesha kwamba serikali imetenga shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kukamilisha upembusi yakinifu na usanifu wa awali wa njia za reli kwa standard gauge kat

ya mtwara –Mbambabayi na matawi ya mchuchuma na Liganga; Tanga- Arusha –Musoma pamoja na matawi yake kwenda Engaruka na Minjingu na njia mpya za reli katika jiji la Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Taifa linakuwa na mpango wa Maendeleo kama dira inayoliongoza Taifa, na kwa kuwa kuna shida ya kukosekana kwa kushabihiana kati ya Mpango wa Taifa wa miaka mitano na Bajeti ya Serikali kwa Wizara hii ni ishara tosha kwamba, serikali hii inaendeshwa bila kuzingatia vipaumbele vya taifa, kwa maana nyingine Bunge lako tukufu mheshimiwa spika linatumika kujadili na kuidhinisha mipango ambayo haiwezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa niaba ya watanzania inataka kufahamu, ikiwa mpango wa taifa wa miaka mitano uliowasilishwa mbele ya bunge lako tukufu na kujadiliwa bungeni uliandaliwa na Serikali hii ya chama cha mapinduzi, na vipaumbele vya kutekelezwa viliidhinishwa na Serikali hiyo hiyo na kwa kuwa pia bajeti za serikali inaandaliwa na serikali hiyo hiyo lakini vitu hivi viwili vinakuwa tofauti. Hii ni ishara kwamba serikali hii haina mipango wala mikakati mbadala ya kushughulikia matatizo ya watanzania na matokeo yake mpango huu utashindwa kutekelezwa kama ambavyo mipango iliyotangulia ilishindwa.

Mheshimiwa Spika, maendeleo hayawezikupatikana bila ya kuwa na nidhamu ya kutekeleza mipango tuliojiwekea wenyewe na nidhamu inayoongeleta ni kuwa na bajeti ya utekelezaji wake.

VIII. RELI YA TANZANIA NA ZAMBIA (TAZARA)

Mheshimiwa Spika, Reli ya Tazara ilijoengwa miaka ya 1970 ikitokea Dar es Salaam hadi New Kapirimposhi Zambia, uwezo wake wa kusafirisha mizigo na abiria umeshuka sana kutokana na sababu mbalimbali. Aidha Reli hiyo yenye uwezo wa kubeba tani milioni tano za shehena

kwa mwaka, hivi sasa inaweza kubeba tani 100,000 tu kwa mwaka, sababu kubwa ni uchakavu wa miundombinu kama vile njia ya reli, injini na mabehewa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo yanayoikabili TAZARA ili iweze kujiendesha kibashara lakini inaonekana serikali pamoja na menejiment ya TAZARA kwa pamoja wako "busy" wakifanya siasa badala ya kufikilia namna bora ya kulifanya shirika hili kujiendesha kwa faida.

Mheshimiwa Spika changamoto zinazoendelea kulikwamisha shirika la reli la TAZARA zinatokana na ufdhaili, umiliki wake pamoja na sheria inayoismamia. Mionganii mwa changamoto hizo ni pamoja na;

i. uchakavu wa miundombinu, kama injini na mabehewa ambayo yamepitwa na wakati kwa kipindi kirefu sasa na TAZARA kushindwa kujiendesha kwa faida kwa kipindi kirefu,

ii. TAZARA kushindwa kulipa mishahara kwa wafanyakazi wake na kutegemea serikali kuwalipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara na huku likiendelea kufanya biashara kwa hasara.

iii. Changamoto zinazotokana na mapungufu ya sheria namba 23, ya mwaka 1975 kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria namba 4 ya mwaka 1995.

iv. Wanahisa kutegeana na kutoa kipaumbele kwa reli zinazomilikiwa na kwa 100% na nchi husika kwa mfano TRL, RAHCO na NRZ.

v. Deni kubwa linalofikia Trilioni moja.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli uliodhahiri kwamba TAZARA haitaweza kujiendesha kwa faida kama mabadiliko makubwa ya kiutawala hayatafanyika. Pamoja na mapendekezo ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni 2016/17 iliyatoa katika hotuba yake, inaonekana kama

mawazo hayo hayakupewa kipaumbele kwa kiwango cha kutosha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa majibu ya mambo yafuatayo:

Kwanza, Ni lini serikali itaweka mikakati thabiti ya kuiwezesha TAZARA kujientesha kwa faida kuliko ilivyo sasa?

Pili, serikali itaendelea kulipa mishahara ya wafanyakazi wa TAZARA hadi lini na ni mkakati gani ambao serikali ilifanya na au inafanya ili kumaliza matatizo ya menejimenti ambayo yamekuwa yakijitokeza, ikizingatiwa kwamba viongozi waliopo wanadaiwa kutozingatia utawala bora, uwazi na uwajibikaji?

Tatu, Kwa kuwa matataizo yaliyo mengi inaonekana kuwa ni matokeo ya madhaifu ya kisheria yaliyoko kwenye sheria namba 23 ya mwaka 1975, kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria namba 4 ya mwaka 1995, je Serikali inampango gani wa kuleta bungeni marekebisho ya sheria hiyo ili kuondoa changamoto hiyo inayokwamisha TAZARA kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM imekuwepo madarakani kwa kipindi chote cha uhai wa reli hii kamwe haitakwepa lawama na dhambi kubwa ya reli hii kutoweka.

Mheshimiwa Spika, yaliyotokea na yanayoendelea kutokea TAZARA yatoe funzo na iwe darasa kwa nchi yetu katika kuendeleza na kusimamia reli zetu. Hivi sasa nchi inajenga reli ya kati kwa kiwango cha standarg gauge kwa takribani kiasi cha shilingi Trillioni 17 wakati TAZARA ilijengwa kwa kipindi hicho dola milioni mia mbili hamsini.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka seriakali kuweka mpango mahususi wa kuifanyia marekebisho reli hiyo na hivyo tunaona kwamba mapendekezo ya kambi yakifanyiwa kazi TAZARA inaweza kusimama imara na ikajiendesha kwa faida.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa maendeleo ya reli amba tulishauri uundwe na ukaundwa siku za hivi karibuni umetumika bayana kuwa utatumika kwa miradi ya miundombinu ya reli nchini na tunauhakika kwamba kama matumizi ndio yale yaliyopelekea uanzishwaji wake basi matawi mengine ya Reli yatajengwa kwa kiwango cha standard gauge bila ya uhitaji wa kukopa fedha kwa masharti ya kibiashara kama ambavyo inafanyika hivi sasa.

F. SEKTA YA MAWASILIANO

a. ANUANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Anuani za makazi na Postikodi ulizinduliwa Sept 2016, hapa Dodoma unatekelezwa kwa kasi ndogo sana na ni wananchi wachache wanaoufahamu mpango huu.

Mpango huu unaumuhimu mkubwa katika kuwezesha ufikishaji wa huduma mbalimbali kwa haraka kwa jamii. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa watanzania ili wapate uelewa mpana kuhusu mpango huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya utekelezaji wa mradi wa majoribio katika baadhi ya maeneo katika mikoa ya Dodoma, Arusha, na Dar es Salaam, sasa mpango uliopo ni Serikali za mitaa kuendeleza katika maeneo yao. Kambi Rasmi ya Upinzani inao wasiwasi mkubwa kama kweli Halmashauri zitafaulu kutokana na kuwa na fedha kidogo wanazokusanya kuweza kukidhi mpango huu. Kwa sababu hiyo tunaitaka Serikali (TAMISEMI) itenge bajeti maalum ya kuendeleza mpango huu muhimu katika kufikisha huduma kwa haraka, kinyume na hapo hata uwekezaji uliokwisha fanyika utakuwa ni kazi bure.

b. SHERIA YA MAKOSA YA MTANDAO NAMBA 14 YA MWAKA 2015

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, akitoa maoni ya kambi

mwaka wa fedha 2016/2017 allieleza bunge lako tukufu jinsi ambavyo Bunge la Jamhuri ya Muungano lilipitisha sheria namba 14 ya mwaka 2015 tarehe 1.4.2015. Pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kупinga kупитishwa kwa sheria hiyo kutokana na kuwepo kwa vifungu ambavyo vilikuwa vinaminya uhuru wa utoaji na upokeaji wa taarifa kwa njia ya mtandao na baadhi ya wabunge wake wakiwasilisha majedwali ya marekebisho kwa ajili ya kufuta au kurekebisha vifungu kandamizi, lakini sheria hiyo ilipitishwa na bunge lako tukufu kutokana na wingi wa wabunge wa CCM kwa kuwa walipinga marekebisco hayo.

Mheshimiwa Spika, zipo kila dalili zinazoonesha kuwa Sheria hiyo kandamizi ilitungwa kwa mashinikizo ya Chama tawala kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015 kutokana na kasi ya vijana ambao wengi ndio watumiaji wa mitandao ya kijamii nchini ambao wengi walikuwa wakiunga mkono upinzani. Mara baada ya kumalizika uchaguzi mkuu, ushahidi unaonesha kuwa Sheria hii mbaya ilitungwa kwa makusudi ya kuwabana watanzania ambao wapo tayari kukosoa utendaji mbovu wa awamu ya tano na kuleta utawala wa kiimla na kidikteta katika taifa hili changa ambalo mpaka sasa halijafanikiwa kuwa taifa la uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, Taifa limeathirika kwa namna moja au nyininge kwa kitendo cha MCC kuiondoa Tanzania kama mnufaika wa misaada yake kutokana na tamko la uamuvi wa Bodi ya Wakurugenzi ya MCC iliyotolewa tarehe 28 Machi 2016 kuwa mojawapo ya sababu za Tanzania kuondolewa katika MCC ni uwepo wa Sheria ya Makosa ya Mitanado ambayo imetumika kama mojawapo ya njia za kuminya uhuru wa mawazo, ikiwemo kukamatwa kwa baadhi ya watu kwa makosa yanayohusiana na mitandao kipindi cha uchaguzi. Zaidi, tamko hilo lilieleza kuwa mazingaombwe na marudio ya uchaguzi wa Zanzibar tarehe 20 Machi 2016 na Sheria kandamizi ya Makosa ya Mitandao vinakinzana na azma ya uwepo wa demokrasia na uchaguzi huru na wa haki. Hivyo MCC ikatangaza kuvunja utekelezaji wa mpango wa pili wa maendeleo wa MCC kwa kushirikiana na Tanzania. Mojawapo wa sekta zilizokua zikipokea fedha za MCC ni

sekta ya ujenzi wa miundombinu. Baadhi ya miradi iliyokuwa inafadhiliwa na MCC kwa Sekta ya Ujenzi nchini Tanzania ni pamoja na; Mradi wa Barabara, kilometra 67 kutoka Songea-Namtumbo, Mtwara corridor, Tanga – Horohoro, Tunduma na Mafia Island airport.

Mheshimiwa spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua hatua ya miradi hiyo iliyokuwa ikifadhiriliwa na MCC, pamoja na ukweli mchungu uliojificha kwamba huenda mionganoni mwa sababu za kwanini serikali imeshindwa kutekeleza miradi yake ya maendeleo hata kwa nusu ya bajeti ni matatizo kama haya ya kusitishwa kwa miradi ya ufadhere.

G. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuhitimisha kwa kusema kuwa Kushindwa kutekelezwa kwa bajeti kwa kiwango kinachoridhisha ni matokeo ya matendo ya serikali na kushindwa kutekeleza miradi ambayo imepangwa kutekelezwa na Serikali yenye. Huu ni udhaifu mkubwa, kama mpangaji wa mipango ni wewe na wewe ndiye unashindwa kutoa fedha za utekelezaji, je ni nani anatakiwa kutekeleza mipango hiyo? Hoja kuwa ni masuala yasiyokuwa kwenye mipango kupewa nafasi kubwa kuliko mipango iliyopangwa na kuitishwa na Bunge. Kwa maneno mengine hii ni dharau kwa Mhimili huu unaoisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, mpango wa miaka mitano 2016/17 – 2020/21 “**Nurturing Industrialization for Economic Transformation and Human Development**” ni mpango uliopitishwa na Bunge hili na kwa vyovoyote vile ndio dira ya mipango mingine yote inayoletwa ili kupata idhini ya Bunge letu. Hivyo basi kutokuzingatia mipango ambayo tayari ilikwishapata Baraka za Bunge na kuleta mambo mengine inatufanya tutafakari kwamba, mpango huo ulikuwa ni wa njonzi za mchana na baada ya Serikali kuona kwamba hautekelezeki inaanza kuukimbia kwa kuleta mipango mingine. Kambi Rasmi ya Upinzani inaelewa kwamba mpango bila fedha za utekelezaji ni bure na ni hadaa tupu.

Kwa maana hiyo, tunaomba tufahamishwe je, Bunge ndilo liliopigwa changa la macho kwa kuitisha mpango hewa? Au Serikali ndio inashindwa kuwa makini katika utoaji fedha katika kutekeleza miradi ya maendeleo? Huo uchumi wa viwanda tutaufikiaje kwa kutokuzingatia yale tuliyokubaliana?

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

.....
WILLY Q.QAMBALO (MB)

k.n.y Waziri Kivuli wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,

27 April 2017

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji lakini kabla ya hapo niweke kumbukumbu sawasawa kwenye *Hansard*. Maeleo kuhusu Ndugu yetu Alphonce Simbu, Mheshimiwa Waziri aliandika hapa na nadhani ni vizuri yakiingia kwenye *Hansard* kama inavyotakiwa. Mheshimiwa Waziri Dokta Harrison Mwakyembe ametoa maeleo kwamba wiki iliyopita, Ndugu yetu Alphonce Simbu alishiriki kwenye Mashindano ya 37 ya London Marathon yaliyovutia karibu washiriki 40,000 na alishika nafasi ya tano. (*Makofii*)

Vilevile Ndugu yetu Alphonce Simbu mapema mwaka huu alishinda na kupata medali ya dhahabu kwenye mashindano ya Mumbai Marathon. Pia, Alphonce Simbu Agosti 2016 alishinda nafasi ya tano kwenye mashindano ya Marathon ya Olympics Rio de Janeiro Brazil. Kwa hiyo, rekodi iweke taarifa hizi sawasawa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe na Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niwe mchangiaji katika Wizara hii muhimu. Kwanza naomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, Mawaziri wote wa Serikali pamoja na Makatibu Wakuu wote kwa utendaji wao mzuri uliotukuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwaambie wenzangu wanaosema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haikutimiza ilani zake; nawaambia Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetimiza ilani yake kwa kiasi kikubwa ndiyo sababu wakachaguliwa Wabunge wengi wa Chama cha Mapinduzi kutoka katika majimbo mbalimbali, lakini pia wakachaguliwa Madiwani wengi wa Chama cha Mapinduzi kutoka katika kata mbalimbali, lakini pia Halmashauri nyngi zimeongozwa na Madiwani, Wenyevitii wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya mambo mazuri sana. Napenda nimpe pongezi za kipekee Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa anayoifanya katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam toka kuchaguliwa kwake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu alipochaguliwa tu, alifanya upanuzi wa haraka wa barabara ile ya Morocco kwenda Mwenge. Pia alifanya ufunguzi wa Daraja la Kigamboni, daraja muhimu sana; alizindua ujenzi wa *flyover* ya TAZARA, mradi ambao unagharimu shilingi bilioni 99; alifungua mradi wa mabasi yaendayo kasi ambayo yamekuwa msaada mkubwa sana kwa wananchi wa Dar es Salaam ambao walikuwa na tatizo kubwa la msongamano wa magari. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Sema, sema, sema! (*Makofii*)

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Rais alifanya mapokezi ya ndege mbili za

Bombadier katika Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam; alizindua mradi wa *interchange* ya Ubungo, mradi ambao unagharamia pesa kiasi cha shilingi billioni 177; alizindua ufunguzi wa mradi wa ujenzi wa Mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; amefungua ujenzi wa reli ya *standard gauge* kule Pugu, Dar es Salaam, mradi ambao utatumia pesa takribani *USD* billioni 1.2; hilo siyo suala dogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais pia alizindua ujenzi wa nyumba za wakazi wa Magomeni; ametoa pesa katika mradi wa Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam ili ukamilike kwa haraka, hiyo siyo kazi ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nawaomba wananchi wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam, nami ndio Mbunge wenu kutoka Chama cha Mapinduzi, millionileta Bungeni njie niwawakilishe, nawaambieni Serikali hii imeamua kwa dhati kabisa kuhakikisha Mkoa wa Dar es Salaam sasa unakuwa mkoa wa utalii, miundombinu yote inaboreka, ndege tumepata; lakini kubwa mimi nilipoingia katika Bunge hili kipindi kilichopita, nilizungumzia juu ya Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika,...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kissangi, naomba ukae.

Mheshimiwa Waitara, taarifa kwa kifupi.

TAARIFA

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji ambaye anazungumza sasa, mwalimu mwenzangu,

kwamba Dar es Salaam inaongozwa na UKAWA na sisi ndio Wabunge wa kuchaguliwa katika mji ule; yeze ni Mbunge mwenzetu. Kwa hiyo, aseme siyo CCM peke yao, na sisi tupo na tumesimama imara kweli kweli. Ahsante. (*Makofii*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Martha Mlata naomba ukae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam naomba usubiri kidogo. Mheshimiwa Waitara nadhani unafahamu kwamba Mheshimiwa Mariam Kisangi ni Mbunge wa Viti Maalum. Kwa hiyo, ni Mbunge wa Mkoa mzima. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mariam Kisangi naomba uendelee.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunitolea ufanuzi, maana anaelewa Mwalimu mwenzangu, anajifanya haelewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi, Serikali ya Tanzania inaongozwa na Mheshimiwa Rais wa Chama cha Mapunduzi na itaendelea kuwa Serikali ambayo inatekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi na yeze Mheshimiwa Waitara anatakiwa atekelze llani ya Chama cha Mapinduzi, atake asitake afanye hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niendelee. Tunataka kujengewa nyumba za wakazi wa Magomeni na tumesikia kilio cha wananchi wale, jinsi walivyokuwa wanalia kwa kunyanyaswa kuondolewa katika maeneo yao. Wananchi wale leo Mheshimiwa Rais ameona kilio chao; ameamua kwa dhati ya moyo wake kuhakikisha anawapatia makazi bora wananchi wale wa Magomeni. Siyo jambo dogo, ni jambo ambalo sisi kama Wabunge wa Dar es Salaam, tena nampongeza sana Mbunge wangu wa

Kinondoni kwamba ye ye alishiriki pamoja na kwamba yuko Upinzani, alishirikiana na Mheshimiwa Rais akaenda pale kwenye uzinduzi wa nyumba zile, hiyo ndiyo siasa. Wanasiasa tufike sehemu, pale yanapofanyika mazuri tuunge mkono, siyo kila kitu tunapinda tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa hilo tena nasema zile nyumba azijenge kwa haraka, wananchi wale wakae. Sambamba na hao, wananchi wa llala Mchikichini nao wanazisubiri kwa hamu nyumba hizo wajengewe na wananchi wa Temeke mwisho nao wanazisubiri. Nimwambie Mheshimiwa Rais na Wizara na Mawaziri, kazeni buti, fanyeni kazi, tekelezeni llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara hii sasa, nitajikita katika maeneo yafuatayo; kwanza nitachangia katika barabara, bandari, uwanja wa ndege, reli na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa barabara, naomba kabisa Serikali pamoja na kumsikia Mheshimiwa Waziri kwamba kuna mpango wa ujenzi wa *flyover* ya Charambe, naiomba Serikali mpango huo utekelezeze kwa sababu idadi ya watu Mbagala imekuwa kubwa. Kuna msongamano mkubwa kutoka kwenye *round about* ya Mbagala Rangitatu kuelekea Charambe, Chamazi na Mbande. Mpango huo ukitekelezwa, basi Mbagala yetu sasa nayo itaendelea kuwa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara inayotoka kwenye Daraja la Kigamboni kuelekea Kibada na Kigamboni, hiyo sasa ifanyiwe kazi kwa haraka kwa sababu wakati huu wa mvua barabara hiyo ilikuwa tatizo. Pamoja na daraja zuri tulilojengewa na Serikali, lakini pale upande mwingine kumalizia kile kipande, naiomba Serikali kwa kupitia NSSF wawaamrishe wafanye kwa haraka sana ujenzi ule ukamilike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie ujenzi wa barabara ya Nzasa – Kilungule kuvuka kwenda Buza. Barabara hiyo itaungana na ile barabara ya *Jet-Davis Corner* inayotoka *Jet* inakwenda *Davis Corner*. Barabara hiyo ni msaada mkubwa kwa wananchi. Barabara hiyo inawasaidia watu ambapo kunapokuwa na msongamano mkubwa Mbagala Rangitatu, wanaotoka kwenda *Airport* wanapita Nzasa wanashuka Bondeni wanaunganisha Buza wanaenda wanakutana na ile barabara mpaka *Jet*, mtu anakwenda uwania wa ndege kwa haraka sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, mara nyingi barabara hii imekuwa ikiingizwa kwenye mipango, inatoka; mara inaenda kwenye mpango mwingine. Naiomba sasa Serikali, kupitia Mheshimiwa Waziri wangu akaisimamie, barabara hii ni msaada mkubwa kwa wakazi wa Mbagala. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Serikali iangalie uwezekano wa kujenga barabara kutoka Mbande kwenda Mipecu - Mkuranga. Wananchi wanapata shida sana hususan akina mama wajawazito, magari hayapiti hata yenye *four wheel*, lakini wanabebwa kwenye pikipiki kuja Mbande kupata huduma ya afya ya mama na mtoto. Naomba barabara hiyo ijengwe. Ikjengwa barabara hiyo, itakuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi wanaotoka Mipecu kuja kupata huduma za afya, hasa akina mama kwenye hospitali au *dispensaryya* Mbande, Temeke. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie upande wa bandari. Pamoja na kazí kubwa inayofanywa na bandari na hasa ile ambayo inaendelea kufanywa ya kuungeza kina cha bandari kutoka geti namba moja mpaka namba saba, lakini naomba sasa bandari itueleze ajira ndogo ndogo zinazotolewa na bandari kwa vijana, nataka mpango wa ajira ndogo ndogo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza sana Serikali, Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wote wa Wizara ya Uchukuzi. Fanyeni kazi kwa bidii. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kisangi, nipe mkono, hongera sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande ajiandae.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika hii Wizara. Kwanza kabisa napenda niungane na wananchi wangu wa Jimbo la Kavuu ambao wamepata athari kubwa sana kutokana na mvua ambazo zinakaribia kuisha, athari ambazo zimesababisha watu karibu saba hivi kupoteza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda niishukuru Serikali kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu ambao baada ya kusikia tatizo hilo, wameweza kufika mahali pale na kuweza kufanya tathmini na kutoa huduma ya kwanza kwa wale walioathirika, takribani nyumba 200 hawana makazi mpaka sasa. Nawaomba wananchi wangu wa Jimbo la Kavuu, Mwenyezi Mungu atupe wepesi wa kuvumilia na tatizo hili ninalishughulikia na niko pamoja na ninyi katika matatizo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niishukuru sasa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ambayo imeanza kutekeleza ilani yake. Unajua waswahili wanasesma, mti wenye matunda hauishi kupigwa mawe. Ukiona mti haupigwi mawe, ujue una kasoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa wetu ni mti wenye matunda na sasa tunatekeleza na haya ndiyo

tunayotekeleza. Amesaini mikataba mingi ambayo Mheshimiwa amekwishaongea, sitaki kurudia, lakini ni ukweli na uwazi ambao unaonekana kwa juhudii ya Serikali ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, namna ambavyo inafanya kazi kwa bidii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja sasa katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Napenda niishukuru Serikali kuitia Wizara hii, nimekuwa na kilio cha muda mrefu sana kuhusu daraja langu la Kavuu ambalo ni kiungo cha barabara ya kutoka Majimoto mpaka Inyonga. Daraja hili ninavyosema, katika ufunguzi wa Mbio za Mwenge zilizofanyika Mkoa wa Katavi lilipitika. Aaah, nilitaka kusema CCM oyee!

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema napongeza sana. Kelele zangu na juhudii zangu zimezaa matunda daraja lile linapitika. Namuomba Mheshimiwa Waziri, sasa zile kilometra kumi zinazounganisha Majimoto kuitia daraja hilo kwenda Inyonga, sasa ziishe na daraja lile wananchi waweze kulitumia kwa ukamilifu kwa sababu, limetumia pesa nydingi ambazo ni kodi za wananchi. Kuliacha hivi hivi kwa kutokuwa na barabara tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wa Jimbo la Kavuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa maana kwamba Hospitali ya Wilaya iko Inyonga, wananchi wanalazimika kwenda Hospitali ya Mpanda ambako ni mbali. Sasa ni vema tukamaliza ile barabara tuwasaidie akina mama, watoto na wananchi kwa ujumla ambao wanaenda kupata matibabu mbali.

Pili, litatusaidia pia kuwasaidia wananchi wale kuweza kufanya biashara zao kati ya Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa barabara yangu ya Starike - Mpanda

imekamilika; lakini naomba barabara ya kutoka Kizi – Kibaoni yenye kilometra 76.6 imalizike. Barabara ile kuptitia upande wa pili wa Mlima wa Lyamba Lya Mfipa, imekuwa ni tatiozo na kisababishi kikubwa cha ajali kwa sababu, hakijamalizika pale. Kwa hiyo, magari mengi yanakuwa yanatumbukia kule chini kiasi ambacho siyo rahisi kuokoa na imekuwa ikisababisha vifo vya watu wengi. Naomba barabara ile ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba barabara inaishia pale Kibaoni, barabara hii ya kutoka kibaoni ambayo imekuwa ikiulizwa humu na maswali mengi ambayo yamekuwa na majibu yasiyotosheleza, barabara ya kutoka Kibaoni kupita Muze mpaka Kilyamatundu ambayo inaenda kupita Daraja la Momba, naomba Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako utakapohitimisha, tunahitaji majibu ya uhakika. Hatuhitaji kurudia maswali, tunataka leo tupate majibu ya uhakika, ni lini barabara hii itafanyiwa usanifu na ni lini itaanza kuwekewa lami? Kwa sababu, ni miaka kumi imepita tukiiongelea hii barabara ya kutoka Kibaoni mpaka Kilyamatundu kupitia Muze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nije kwenye aya ya 50 inayoongelea barabara ya Mpanda – Tabora – Ipole mpaka Sikunge. Barabara hii nashukuru imetengewa pesa na angalau tuna kilometra 30 kutoka Tabora Mjini mpaka Sikunge, sawa. Mahali pabaya ni kutoka Sikunge kupita Koga mpaka Mpanda. Sielewi kigugumizi kiko wapi hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara Mheshimiwa Rais alipokuwa Waziri wa Ujenzi alinihakikishia na alinishirikisha maongezi na Mwakilishi Mkazi wa *ADB* pamoja na *World Bank* na wakakubali na pesa zilikuwa zimeshatoka. Ukitosha kwenye hii aya, wanakwambia pesa zilikuwa zimetoka, sasa ina maana zimeenda kufanya kazi zipi? Ama zinaendelea kufanya kazi ipi? Ni vema tukajua *status* ya hii barabara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara tumekuwa tukiipgia kelele kila siku. Kwa kweli, Serikali yangu naipenda,

inafanya kazi vizuri na ni sikuvi. Naomba barabara hii sasa tuipe kipaumbele ili wananchi wa kule nao waweze kuondoa mazao kule. Mazao yako kule na mvua zimenesha, mazao yameharibika, hawana pa kuyapeleka kwa sababu ya barabara mbovu. Tunaondokaje na umaskini na sisi tunataka twende kwenye kima cha kati? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, Profesa, nafikiri unanielewa ninapoongelea hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pungezi za dhati kwa Serikali kuonesha nia ya kujenga reli ya kati. Napenda ni sema, reli ya kati haiishii Mwanza, ina matawi yake aliyojenga Mjerumani ambayo inakwenda mpaka Mpanda mpaka Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Mheshimiwa Nsanzugwanko, aliongea vizuri sana kuilewesha jamii ya Tanzania pamoja na Serikali kwa ujumla reli ya kati maana yake ni nini?

Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunaenda kwa vipande, naomba basi vile vipande vinyoyobakia vingine visiishie Mwanza. Raha ya reli ya kati ifike Mpanda. Nashukuru kwamba mnatoka Mpanda mnaenda mpaka Karema, Karema mnajenga bandari pale mpaka Kalemii, tunashukuru sana. Sasa itoke pia Tabora - Urambo mpaka Kigoma. Hapo tutakuwa tumeweza kuwaunganisha wananchi wa huku kwetu pamoja na Ukanda wa Kongo, Burundi, Rwanda na Zambia kwa ajili ya biashara. Tunaweza tukainua uchumi kwa haraka sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la viwanja vya ndege. Nimeona katika kiwanja cha ndege cha Mpanda ambapo pesa imetengwa kwa ajili ya kumlipa mkandarasi. Sasa tukishamlipa yule mkandarasi sijaona mwendelezo kwamba nini kitafanyika pale. Ule uwanja umejengwa, hautumiki. Ni kiungo kikubwa kwa kukuza uchumi kupitia maliasili zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *Katavi National Park* pale, kila siku nasema jamani, ile mbuga ina wanyama

wakubwa hakuna mfano. Kuna twiga mrefu hakuna mfano, kuna twiga chotara ambaye hutampata Tanzania kokote. Naomba kile kiwanja; kitatuunganisha sisi na mbuga za Kigoma, tunaunganishwa na mbuga zinazotoka huko Kaskazini, watu watapenda kutembea sehemu mbalimbali za Tanzania. Tusingubiri mpaka sijui *Clouds* nini wale, wafanye utalii ndiyo na sisi tuamke, hapana. Naomba kabisa kwa dhati kile kiwanja mkiendeleze. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa kule kutokana na ubovu wa barabara, msifikiri hawana uwezo wa kupanda ndege, uwezo huo tunao. Sisi tunalisha karibu nusu ya Tanzania, tushindwe kupanda ndege!

Kwa hiyo, tunaomba kabisa kile kiwanja sasa kifiki mahali tuone ndege zinatua, zinaondoka na watalii wanashuka pale, ili tuone ni kwa namna gani ambavyo tunaweza kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kwa mara nyingine, pamoja na kwamba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. DKT. PUDENCIA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nitaleta maombi binafsi kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusu barabara zangu za Katavi. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nichangie Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na naomba nianze kwa kutoa pongezi kubwa kwa kazi kubwa ainayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara zaidi ya kilometra 17,000 huwezi kutenganisha na Mheshimiwa Magufuli. Ujenzi wa viwanja vya ndege nchini unaoendelea, huwezi kuacha kumtaja Mheshimiwa Rais Magufuli; umeme vijiji ambapo tunamalizia vijiji hivi, huwezi kumuacha Mheshimiwa Rais Magufuli; mabasi yaendayo kwa kasi Dar es Salaam ni kwa sababu ya Rais Magufuli, ujenzi *flyover* leo Dar es Salaam, kwa kweli ni Mheshimiwa Rais Magufuli; Daraja la Mkapa, Daraja la Kikwete, Daraja la Kigamboni, Daraja la Kilombero huwezi kuyatenganisha na Mheshimiwa Rais Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli ya kati ya kisasa (*standard gauge*) ambayo mara ya mwisho reli hii imejengwa mwaka 1906 leo Mheshimiwa Rais Magufuli anaandika historia ya kujenga reli Tanzania. Kuimarisha Shirika la Ndege la ATC ni kazi ya Mheshimiwa Rais Magufuli, kudhibiti matumizi ya Serikali ni Mheshimiwa Rais Magufuli, ukusanyaji wa mapato ni Mheshimiwa Rais Magufuli. Leo tunaona elimu bure, ni Mheshimiwa Rais Magufuli, mabweni ya *University of Dar es Salaam* ni Mheshimiwa Rais Magufuli. Upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na Mtwara ni Mheshimiwa Rais Magufuli, kuanza kujenga upya uchumi wa viwanda ameanza Mheshimiwa Rais Magufulina na kudhibiti maliasili ni Mheshimiwa Rais Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo hakika kwa kazi kubwa inayofanyika ya miumbombini, safari ya kuondoa umaskini wa Watanzania Mheshimiwa Rais Magufuli ameianza. Pia naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, ninayo hakika atayekuja kuandika historia ya Tanzania nina hakika jina la Mheshimiwa Rais Magufuli litaandikwa kwa wino wa dhahabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie baadhi ya maeneo; barabara ya Mwandiga - Chankere kwenda Kagunga, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri ameipandisha lakini fedha iliyowekwa ni kidogo sana kwa sababu barabara hii ni ndefu na inapita kwenye milima mikubwa sana. Pia suala la barabara ya

Mwandiga, fidia Mwandiga - Manyovu nakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mbarawa, usimchonganishe Mheshimiwa Rais Magufuli na watu wa Kigoma Kaskazini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Magufuli alikuja kwenye kampeni, aliahidi kwamba lazima atawafidia ambaao hawajafidiwa kwenye barabara hiyo ya Mwandiga - Manyovu na barabara ya Mwandiga - Kidahwe. Nakuomba sana utekeleze ahadi hii. Pia barabara ya kutoka Simbo kwenda llagala kilometra kumi za lami naomba zianze kujengwa, Mheshimiwa Rais Magufuli alihaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kwa nini nasema hivi? Mheshimiwa Rais Magufuli akiahidi anatekeleza. Naombeni ninyi watu wa Serikali, Wizara msimchonganishe Rais, kwa sababu aliahidi naombeni mtekeleze hizi ahadi zake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bandari ya Kagunga, nawapongeza sana watu wa bandari kujenga gati ya Kagunga. Nawaomba sana watu bandari, ili bandari ya Kagunga iwe na maana kibiashara ni lazima na soko la Kagunga mlichukue muweze kulifanyia kazi. Halafu baadaye Halmashauri ya Kigoma tutaungana na bandari, tutafanya *revenue sharing*, mkishamaliza kutoa fedha zanu, *then* mtaturudishia jengo lile, lakini nina hakika bandari ile itakuwa na maana kama tutakuwa na soko la Kagunga. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, pale kwenye Soko la Kagunga tupafanye kuwa *free trades zone area* ili watu wote wapeleke bidhaa pale. Nina hakika Warundi na Wakongo watakuja pale kwenye soko lile na tutapata fedha nydingi sana kama nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nilitaka niliseme vizuri sana, ni suala la barabara vijijini na *TANROADS*. Nimesikia Serikali inataka kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini. Nashauri na naomba sana tayari tunayo *TANROADS*, inafanya vizuri sana, hivi badala ya kuanzisha Wakala mwingine ambaao ni matumizi, ni fedha, ni mzigo, badala

yake kwenye *TANROADS* pale fuwafanye waende mpaka Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote hapa ndani mmekuwa mnaomba barabara zipandishwe, sasa kama tunaomba barabara zipandishwe, basi tuamue.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge, tuamue niombe Serikali kwamba sasa *custodian* wa barabara nchini iwe *TANROADS* peke yake ili fedha zote za mafuta tunazokusanya, badala kumpelekea *TANROADS* asilimia 67, tumpelekee asilimia 100 kwamba suala la barabara Tanzania tunashughulika na *TANROADS* peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashuri yapo mambo mengi ya kufanya, tuwanyang'anye hili la barabara. Nina hakika Wakala huu tukiupanua tukawapa fedha zote mtu mmoja, kwanza tutakuwa tume-save fedha za *administration* kwa sababu itabaki ni ile ile; kama ni Mkuu wa Taasisi atabaki ni yule yule, Wakurugenzi watabaki ni wale wale. Tukianza taasisi nyengine, hizi ni gharama. Na mimi ninaamini *spirit* ya Serikali hii ni kupunguza matumizi. Nani anataka kuleta habari ya kuanzisha mawakala wengi, wakati tunaweza kuamua ma-engineerwote tunawapeleka na *one umbrella*, wao ndio wafanye kazi ya kuhakikisha nchi yetu barabara zinajengwa na mtu mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa naibu Spika, mwisho ni suala la barabara ya kutoka Kibondo kuja Kasulu kwenda Manyovu. Nawaomba sana, nimeona kwenye kitabu mmeandika kwamba ipo *under NEPAD*. Habari ya *NEPAD* tumeisikiliza huu ni mwaka wa saba. Nadhani imefika wakati sasa, na kwa kweli jamani, tullobaki hatujapata barabara ni sisi watu wa Kigoma. Naombeni sana mjitahidi tumalizie barabara hiso za watu wa Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nataka kuwakumbusha tu watu wa Serikali, inawezekana Mheshimiwa Waziri Mbarawa labda hili hulijui vizuri sana. Reli

ya kati Tanzania; *definition* ya reli ya kati toka wakati wa Mjerumani ni Kigoma - Dar es Salaam. Toka 1906 ni Kigoma - Dar es Salaam. Halafu kuna matawi ya Tabora - Mwanza kuna matawi ya kutoka Kaliua kwenda Mpanda, haya ndio matawi. Naombeni tusi-*diverge from the original*/reli ya kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kwa nini nasema Kigoma? Ni kwa sababu moja tu; kwa sababu Kigoma tunayo bahati; Kigoma tuna Burundi na Kongo ambako huko kuna mzigo wa biashara. *Investment* hii inayofanyika ni kubwa sana, lazima tuanze kuifikiria kibia shara. Tutumie jiografia yetu kutengeneza pesa. Mungu ametuunga *geographically* tuko *well located*, tuitumie nafasi hii kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sana nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa kazi kubwa sana wanayofanya. Nawapongeza watu wa bandari, wanafanya kazi kubwa sana. Tumeongea habari ya gati 13 na 14 nikiwa Bunge hili karibu miaka kumi. Sasa naona kuna mwanga, gati 13 na 14 linaenda kutekelezwa; gati namba moja mpaka saba inatekelezwa, kupanua mlango na kuchimba *dragging* ya Dar es Salaam inatekelezwa. Naombeni miradi hii iende kwa kasi ili nasi tuweze ku-*compete* katika biashara ya huko mbele tunakokwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande. (*Makofii*)

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote napenda kwanza kuanza kwa kuchangia sekta ya ujenzi hususan barabara. Katika Mkoa wetu wa Lindi tunashukuru barabara imejengwa ambayo tunaunganishwa kutoka Mkoa wa Lindi hadi Mkoa wa Mtwara na kuelekea Ruvuma. Sasa utata unakuwepo katika barabara za kuelekea kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala la kusikitisha sana kwa sababu inafika wakati unaenda kwenye Wilaya ya Liwale na Nachingwea lakini inakuwa kama ile ni barabara ya kuelekea kijijini. Naiomba Serikali iangalie katika kujenga barabara zinazoelekeea katika hizo Wilaya ili nazo ziweze kuwa katika kiwango cha lami kuliko kila siku kuendelea kuiboresha katika kiwango cha vumbi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii pia inaleta adha kubwa kwa watumiaji wa hizi barabara hususan Wana-Lindi pale wanapohitaji kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine. Imepelekeea hadi akina mama wanapoteza maisha yao pale ambapo wanahitaji kuhamishwa kutoka Hospitali ya Wilaya na kupelekwa kwenye Hospitali Mkoa ya Lindi, kutokana adha hii ya barabara kuwa mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu umefanyika kutoka barabara ya Nanganga kuelekea Ruangwa. Sasa sjui ni kwa kuwa kuna Waziri Mkuu ambaye ana *interest* pale, kwa sababu inawezekanaje kuwe na mpango wa kujenga barabara ya kutoka Nanganga kwenda Ruangwa na iachwe hii inayolekeea Nachingwea na Liwale?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuliangalia hilo ili kuwatoa wananchi wa eneo hilo kwenye adha ya tatizo la usafiri, especially kipindi hiki cha masikika, usafiri inakuwa ni shida. Kwa gari dogo unatumia siku mbili kutoka Nangurukuru hadi kufika Liwale kwa kuititia barabara ya Njinjo ambayo ina urefu wa kilometra 230. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hata wafanyabiashara wanaishia kuharibikiwa na magari njiani na kutoweza kuendelea kutokana na ubovu huu wa barabara na kupelekua hadi kufika siku saba, ambayo ni wiki nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali iweze kuangalia hili na pia ikiwezekana Waziri husika aweze kutupa jibu; lini atahakikisha kwamba barabara hizi za kutoka

Nanganga - Nachingwea hadi Liwale na kutoka Nangurukuru hadi kufika Liwale zitajengwa katika kiwango cha lami? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia katika sekta ya uchukuzi juu ya matumizi ya bandari yetu katika kukuza mapato ya Taifa letu. Hadi sasa hivi shehena zinazopita katika bandari zetu zinaendelea kushuka na zimeshuka kutoka asilimia 5.2 mwaka 2014/2015 hadi kufika asilimia 0.1. Hii ni ishara mbaya sana kwa mapato ya nchi yetu. Maana yake ni kwamba mapato ya bandari yanaendelea kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2017 takwimu za *TRA* zinaonyesha kwamba mapato yaliyotokana na forodha, ikiwemo bandari ni shilingi triliioni 4.3. Sasa kama kusingekuwa na upungufu wa shehena katika Bandari, maana yake haya mapato yangeongezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia bajeti nzima ya mwaka 2016/2017 ni shilingi triliioni 29.54, lakini tumeendelea kushuhudia mapato ya bandari yanavyozidi kushuka kwa kasi. Sasa je, tutaweza vipi kuboresha vyanzo vyetu vya mapato kwa usimamizi mbovu kama huu? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumebarikiwa kijiografia kuwepo katika Ukanda wa Maziwa Makuu, lakini hii lawama Serikali haiwezi kuikwepa kutokana na kuwa na sera mbovu juu ya uratibu wa shughuli za bandari. Hili ni janga kwa Taifa letu.

Napenda kuishauri Serikali iweze kuboresha sera zake juu ya uratibu wa bandari ili tuweze kutumia vizuri baraka hizi tulizopewa na Mwenyezi Mungu ya kuwa *strategically positioned* na hatimaye kuweza kuongeza mapato yatokanayo na bandari. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia juu ya hii sekta ya uchukuzi kuhusiana na Shirika la Ndege Tanzania (*ATCL*). Naungana mkono na juhudhi zilizotumika

katika kufufua Shirika hili la Ndege la *ATCL*, lakini siungi mkono njia zinazotumiwa na Serikali katika kusimamia Shirika hili la Ndege. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu kitendo cha Serikali kununua ndege kwa gharama ya shilingi bilioni 500 na kuzikodisha hizi ndege kwa Shirika la *ATCL* naona ni kitu ambacho ni kibaya kwetu sisi kama Taifa ambalo kwa sasa hivi uchumi wetu upo dhaifu na bajeti ikiwa *ime-under perform*. Kwa nini tumeshindwa kuendelea na mfumo wa *Public Private Partnership (PPP)* ambapo wenzetu wa Kenya tukiangalia *Kenya Airways* asilimia 29.7 *shares* zinamilikiwa na Serikali ya Kenya huku asilimia 26.8 zinamilikiwa na Shirika la Ndege la *KLM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wamejingiza katika soko mitaji, soko la hisa Dar es Salaam, Uganda na Nairobi ambapo umma nao umeweza kumiliki hizo *shares* nyingine zillizobaki. Kwa nini ishindikane kwetu sis? Tuna mambo mengi ambayo tunahitaji ku-*prioritize* na siyo kununua ndege. Kwa sababu tungeweza kuendelea huu mfumo wa *PPP*, japo tulifanya vibaya, hii siyo kwamba tuachane kabisa na huu mfumo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili suala la Serikali kununua ndege kwa gharama hizo za shilingi bilioni 500 kwangu mimi naona siyo sahihi kwa sababu tuna mambo mengi. Vijijini maji hamna, dawa hamna katika sekta ya afya, elimu pia haijaboreshwa kwa kiwango kile inavyotakiwa, lakini tunahangaika kununua hizi ndege. Napenda kupata majibu juu ya kwa nini Serikali imeshindwa kuendelea na huu mfumo wa *PPP?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuishauri Serikali iweze kusisitiza *ATCL* iweze kukabidhi mahesabu yake kwa sababu hadi Februari Waziri Mkuu aliagiza *CAG* iweze kupatiwa mahesabu ya madeni na mali juu ya *management* nzima ya *ATCL* tangu waweze kupatiwa hizi ndege mwaka 2016. Nashauri kwamba wakabidhi mahesabu haya ya tangu 2009 ambayo tangu mwaka 2009 walishindwa kuyakabidhi kwa *CAG*. Kwa sababu kuna *poor management* ya *ATCL* inayopelekea kuongezeka kwa madeni na kutokuweza kujua

exactly mali zetu za ATCL ziko kiasi gani mpaka dakika hii. Kwa hiyo, kikubwa napenda pia kushauri Serikali iweze kufanya hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo. Ahsante, nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wabunge, dakika zilizobaki hazitaweza kutosha kwa mchangiaji yeoyote. Nitayasoma majina ya wachangiaji tutakaoanza nao mchana. Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Suleiman Saddiq, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Hongoli Joram na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji kutoka CHADEMA watakuwa Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mheshimiwa Mary Deo Muro na Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela.

Wachangiaji kutoka CUF watakuwa ni Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale. Kwa hiyo, hawa ndio watakaochangia mchana na pengine kama muda utatosha wengine wataongezeka. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

(Saa 6.57 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Dau na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub ajiandae.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi nyingine tena mchana huu ili tuweze kuitendea haki hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naanza kwa kuunga mkono hoja hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Wizara hii ndiyo ambayo kwetu sisi Wakristo, kuna maneno fulani yamo kwenye vitabu vitukufu, yanasema: "Tazama nakwenda kufanya nchi mpya na mbingu mpya, ya kale yamepita na tazama yamekuwa mapya." Nchi hii tunaiona inavyobadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona Tanzania mpya inakwenda kuzaliwa. Unaweza ukaona kuanzia Mwalimu Nyerere mpaka Rais Kikwete, makao makuu ya nchi hii yalikuwa Dar es Salaam; kuanzia kwa Rais Magufuli, makao makuu ni Dodoma sasa. Kuanzia mkoloni, Nyerere mpaka Rais Kikwete tulikuwa na *meter gauge*, kuanzia Mheshimiwa Magufuli na kuendelea tunakwenda kuwa na *standard gauge*. Hiyo ndiyo Tanzania mpya tunayoitaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Rais wetu alipokuwa Mgombea, aliimbia Tanzania na Dunia nzima, watu wakataka kwenda mahakamani akasema, *M for change*, wakasema ameibia sera fulani, lakini alikuwa anasema *Magufuli for Change* na *M4C* hiyo kweli tunaiona. Hongera Rais wetu. Tunaweza tukasema hakika ya kwamba huyu anaweza akawa ni mionganini mwa Manabii wa kizazi kipyaa.

MBUNGE FULANI: Amen.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Anaitabiria Tanzania mambo mazuri na kila mmoja anaona. Kwa maana hiyo niseme, Wizara ya Miundombinu kwa maana ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ndiyo inakwenda kuifanya Tanzania

hii iwe mpya ili hata Mataifa mengine watakapokuja hapa, watauona uso wa Tanzania ukiwa umepambwa na *flyovers*, ukiwa na madaraja ambayo yako kwenye viwango, ukiwa na treni ambazo zinakwenda kwa haraka. Kwa maana hiyo, hata uwekezaji katika Taifa hili utakuwa ni wa uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta nyininge muhimu za viwanda, uzalishaji, kilimo, zinategemea sana ni namna gani tunavyokuwa na mawasiliano ya haraka. Hata Mwekezaji akija hapa, atapenda sana kuona ni namna gani itakavyoweza kuwa anasafirisha bidhaa zake kama *at-import* au *ata-export*, muda gani anautumia hapo? Ndipo tutaona kwamba watu hawa wanaweza wakaja kutusaidia na tukaenda kwenye Tanzania ya viwanda tunayoitaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme neno moja ambalo napenda Watanzania waliskie, kwamba kuna baadhi ya Watanzania wanafanya michango yao katika Taifa hili, wakati mwigine wasitambuliwe. Nichukue hata dakika chache kumsifu bwana mmoja anaitwa *Engineer Patrick Mfugale*. Amekuwa ni chachu katika *TANROADS* na hata sasa kwa wale wasiojua, ndiye anayeongoza timu inayojenga *standard gauge* ya Tanzania. Kwa maana hiyo, mtu huyu ni hazina ya nchi hii na hongera sana kwake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala zima la miundombinu ya barabara hasa Jimboni kwangu. Namuomba Mheshimiwa Waziri, barabara yetu ya Mtengorumasa – Iparamasa - Mbogwe mpaka Masumbwe inayotuunganisha Watanzania na watu wa Uganda na Mikoa jirani ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora mpaka Dar es Salaam, ijengwe kwa kiwango cha lami. Watanzania wa maeneo haya na wenyewe wangependa kufaidi keki ya nchi hii kwa kupata sehemu ya keki hiyo kuititia barabara ya lami kwenye barabara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara ya kutoka Kahama mpaka Geita, nashukuru ipo kwenye bajeti ya

mwaka huu, naomba utekelezaji wake ufanyike haraka iwezekanavyo. Pia, niende haraka sasa, niseme tu kwamba Bandari ya Dar es Salaam ndiyo lango kuu ambalo nchi nydingi zinategemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa uongozi wake, ahakikishe yale magati namba moja mpaka saba, uchimbaji wake ufanyike kwa haraka; na gati namba 13 na 14 ambayo yalikuwa yakipigiwa kelele kila wakati katika Bunge hili, ujenzi wake ukamilike. Bandari za Tanga, Bagamoyo na Mtwara, nazo zipewe umuhimu wa pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa *standard gauge* hatua ya kwanza umeanza, naomba na mchakato wa hatua zile nyininge zilizosalia ukamilike ili kwamba ile ndoto ambayo tumekuwa tukiiwaza kwa muda mrefu, Tanzania inayokwenda kuwa na barabara nzuri na treni inayokwenda kwa kasi inayotumia umeme, iweze kufikiwa kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii inayo majaliwa ya kuwa na madini mengi; tuna Mchuchuma, Liganga, tuna *nickel* kule Kabanga na *graphite* kule Lindi. Maeneo haya yote uchimbaji wake utategemea sana miundombinu ya barabara na Reli zitakazojengwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwatie moyo tu viongozi wa Wizara hii, wapige kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ununuzi wa ndege mpya, nalo ni maono mapya ya Mheshimiwa Rais wetu, nayo yanafanyiwa kazi. Tumuombee Mungu ndoto yake hii iweze kutimia katika kipindi cha uongozi wake. Ndiyo Tanzania mpya hiyo itakayokuwa na Shirika la Ndege la Kimataifa na ndiyo tunayoitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Jaku Hashimu Ayoub na Mheshimiwa Mary Deo Muro, ajandae.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakukushuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kumpa pongezi kubwa sana mto a hoja, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa na timu yake yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekeze pia pongeze zangu kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa hatua zake thabiti na za dhati katika kuhakikisha kwamba analifufua Shirika letu la Simu la *TTCL*, imewekwa pale *management* ya vijana, *management* nzuri kabisa. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, muasaidie sana hawa katika kuwaongeza mtaji ili waweze *ku-compete* vizuri katika soko hill ambalo lina ushindani mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nianze kujielekeza katika katika kuchangia hotuba hii. Katika hiki kitabu, ukurasa wa 49 na 50 unazungumzia ujenzi na ukarabati wa vivuko mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea Mafia, sisi kule hatuna namna yoyote, lazima tupate boti au meli ya aina yoyote ili kututoa kwenye kisiwa kikubwa na kutuleta huku sehemu ya bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mwaka 2016 wakati nachangia hotuba hii, nilimuomba Mheshimiwa Waziri, naye anakumbuka kwamba sisi watu wa Mafia tuna matatizo sana ya usafiri wa kuingia na kutoka Mafia. Akatuahidi kwamba ile iliyokuwa *MV Dar es Salaam*, ambayo ilikuwa imeegeshwa pale, haina shughuli yoyote, tulipoimba akatukubalia, lakini akasema ina matatizo kidogo ya kimkataba na ya kiutaalam; wakishayamaliza watatuletea Mafia iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumesikia tangazo, mwenye mamlaka ameichukua ile meli, amewapelekea

watu wa Jeshi, hatuna tatizo na hilo. Tatizo letu ni kwamba je, Mheshimiwa Waziri baada ya kutuondolea ile *MV Dar es Salaam*, katika hotuba yako, nimeisoma na kuirudia hapa kwenye maeneo ya vivuko hivi na *ferry mbalimbali*, hakuna mkakati wowote wa kuondoa tatizo la usafiri baina ya Nyamisati na Kilindoni katika kisiwa cha Mafia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwa sababu naye anatokea kisiwani vilevile, baadhi ya maeneo mengine yamepangiwa kwa *alternative route*, wengine wanaona kama vile kuzunguka; mnawajengea vivuko wafupishe safari zao, lakini sisi hatuna namna, lazima tupande boti. Sasa hatusemi kwamba maeneo mengine wasipelekewe vivuko, lakini haya maeneo ambayo yana *alternative route* japokuwa ya kuzunguka, yasubiri kwanza mtupe kipaumbele sisi ambao hatuna namna yoyote, lazima tuvuke maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa majibu ya kusema kwamba jaribuni kuwashawishi *private sector* waje wasaidie, tumefanya sana na Mheshimiwa Waziri ni shahidi, tumeongea na Bakhresa, tumeongea na Zacharia, bado wanasisita kuleta usafiri baina ya Kilindoni na Nyamisati. Sasa hili moja kwa moja ni jukumu la Serikali sasa, mtuletee huduma hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenye kiti chako hapo, uniandike jina langu kabisa, nitazuia shilingi mpaka nipate majibu, ni lini Serikali itakuja na mkakati thabiti kabisa kuhakikisha kwamba inapatikana meli au boti ya kisasa ili kuondoa tatizo la usafiri baina ya Nyamisati na Kilindoni Mafia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, gati la Nyamisati. Nianze kwa kumpungeza Mheshimiwa Waziri, walituahidi mwaka 2016 hapa wametenga shilingi bilioni 2.5 na kweli zimekuja tumeona mkakati unaanza pale, wataalamu wapo, utafiti wa udongo umeshaanza na ujenzi na tenda imetangazwa wiki iliyopita na ujenzi utaanza hivi karibuni. Tunaipungeza sana Serikali na tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa gati lile utachukua mwaka mmoja kukamilika. Katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, wananchi bado wanapata matatizo. Bandari ya Nyamisati haina sehemu ya abiria, kuna banda tu bovu bovu pale, hakuna vyoo, hakuna maji, hakuna hata ngazi ambayo inaweza ikarahirisha abiria kupanda kwenye boti na kushuka. Tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri kuptitia Mamlaka ya Bandari, naamini wapo, watusaidie pale. Na mimi binafsi nimefanya juhud, nimeandika barua kwa Katibu Mkuu wa Ujenzi na nimemskia asubuhi hapa akitambulishwa, Ndugu Nyamuhanga kwamba tunaiomba ile ngazi iliyoleta pale inatumika kwa ajili ya *MV Dar es Salaam* ambayo haifanyi kazi kwa sasa, mtuletee Nyamisati kwa kipindi hiki cha muda wa mwaka mmoja wakati ujenzi unaendelea, isaidie. Sijabibiwa ile barua, wala sina taarifa zozote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, ninaamini Serikali ni sikivu na Mheshimiwa Waziri sasa nalileta kwako rasi, tunaomba sana mtupatite ile ngazi angalau kwa muda huo wa mwaka mmoja tuweze kuondoa tatizo la kupanda na kushuka katika gati la Nyamisati.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kilindoni mpaka Rasi Mkumbi, Kilometra 55 ilikuwa ni ahadi ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete alipokuja kuomba kura Mafia mwaka 2005 na 2010 tena na kwenye llani ya Uchaguzi, 2015 - 2020 imo, kwamba barabara ile itafanyiwa upembizi yakinifu. Nimekiangalia hiki kitabu kuna mahali nimeona kuna shilingi bilioni 1.5. Tafsiri yake sijaipata, lakini naomba utakapokuja kuleta majumuisho hapa, uniambie labda hiyo ndiyo kwa ajili ya usanifu na uchambuzi wa kina kuhusu barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, hususan Mheshimiwa Naibu Waziri yeeye alikuja Mafia na tukamwambia kwamba Mafia ni kisiwa, kuna tatizo la udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kuikarabati ile barabara, wataalamu wanasema udongo uliobaki utafaa

kwa miaka miwili tu, baada ya hapo utakuwa umekwisha na mkitaka kujenga barabara ya lami itabidi udongo muutoe Dar es Salaam gharama itakuwa ni kubwa sana.

Kwa hiyo, naomba sana mtuharakishie ujenzi ule wa barabara ya lami Kilindoni mpaka Rasi Mkumbi kilometra 55 tu ili tusije tukakumbwa na tatizo la ukosefu wa udongo ambaao unakwisha kutokana na matengenezo ya kila mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu alifanya ziara Mafia Septemba, 2016, tukamwambia kilio chetu, *ATCL* ije Mafia, usafiri ni taabu, ni gharama kubwa sana usafiri wa ndege Mafia. *Round* moja tu ya kwenda *one way* ni shilingi 160,000; kwenda na kurudi inakwenda shilingi 300,000 mpaka shilingi 320,000. Tumeona *ATCL* wameanza *route* ya kwenda Mtwara, tunaomba sana ile ya kwenda Mtwara ipitie Mafia – Mtwara; ikitoka Mtwara – Mafia – Dar es Salaam; itatusaidia sana kutuondolea tatizo hili la gharama kubwa ya usafiri wa ndege. Tukifika sisi Magharibi pale, jua likizama Mafia, huna namna ya kutoka. Akipatikana mgonjwa huna namna ya kutoka kwa sababu ndege zinazokuja pale ni ndogo na usiku uwanja ule hauna taa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nukta hiyo labda nizungumzie tena huu Uwanja wa Ndege. Tunaishukuru Serikali iliutanua, lakini bado kuna hilo tatizo la taa. Uwanja hauna taa na ikifika usiku, akitokea mgonjwa amepata dharura, basi mjue huyo mgonjwa *chance* za kupoteza maisha ni kubwa zaidi kwa sababu hakuna namna ya kutoka ndani ya Mafia ila ni kuititia bahari na ukiingia kwenye boti ni safari ya saa tano mpaka sita.

Kwa hiyo, tunaomba sana na Mheshimiwa Naibu Waziri ulikuja Mafia, tukakwambia hili jambo, ukasema utorialilia kipaumbele. Nimejaribu kuangalia kwenye kitabu hiki, sijaona uwekaji wa taa na utanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mafia. Naomba sana wakati unakuja kuhitimisha hoja yako utuelezee mikakati ya kuhakikisha kwamba Uwanja wa

Ndege wa Mafia unawekwa taa na unaongezwa ukubwa ili kuongeza fursa za kitalii pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki mbili zilizopita nililetwa swali hapa...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Deo Muro na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ajiandae.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Bila kupoteza muda wala kurembaremba sana, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na baadhi ya watendaji wake, maana wengine siwajui) kwa umakini wao na utendaji wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumsifia Mheshimiwa Waziri, ikiwa ye ye ana pumzi zake, na mimi nina pumzi zangu. Watu wengi baada ya mtu kuondoka ndiyo humsifu mtu kwamba alikuwa mzuri; lakini namsifu nikiwa niko hai na ye ye yuko hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ni mionganoni mwa Mawaziri wa Dkt. John Pombe Magufuli aliyeokuwa bora katika utendaji wake, bila kuficha! Mheshimiwa Waziri ni msikivu, utendaji wako tumekuwa tukiiona ambao hautaki *torch*. Ni Waziri unayeshindana kidogo na Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchomba, kwa muda mfupi amechukua Wizara mbili kuongoza na huo ni kutokana na umakini wako Mheshimimiwa Waziri. Waziri ambaye hana Jimbo, akitokea ikulu mara nyingi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na elimu yake, utendaji wake, umakini wake na busara zake, ndio maana Marais wengi huvutiwa na wewe kutokana na umakini wako. Mheshimiwa kuna usemo usemao; mgema akisifiwa, tembo hutia maji, unatokea Zanzibar. Hata Mheshimiwa Kishimba anatamani kuwa Mzanzibari Mbunge wa Kahama, lakini Mungu hajamjalia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaigusa Bandari ya Dar es Salaam na nitakuwa sijamtendea haki Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe kwa kazi aliyoifanya pale. Mabenki yale baada ya kuchangia kipindi cha mwaka uliopita, akafungua benki na tumeziona. Mheshimiwa *Dr. Mwakyembe keep it up! (Makofi)*

MBUNGE FULANI: Naye bora, au siyo? (*Makofi*)

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hapa, kidogo Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa umakini kabisa; na *ball pen* iwe karibu kuandika; yatamgusa *Engineer Kakoko* wa bandari ile na *Port Manager* ambaye ana-act, Fredy John Liundi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo katika bandari ya Dar es Salaam bado kuna matatizo, kauli siyo nzuri na sisi Waislamu tunasema maneno mazuri ni sadaka au methali inayosema, kauli nzuri humtoa nyoka pangoni. Sasa Mheshimiwa Waziri anza kuandika mwanzo. *Customer care* kwanza haipo katika bandari ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *customer care* katika bandari ile haipo. Mheshimiwa Kakoko siyo kila anayepepesuka ni mlevi. Kazi zote hizi Mheshimiwa Kakoko huwezi kuzifanya peke yako. Kama yupo juu, basi nafikiri utakuwa unasikia huko. Madaraka haya lazima mgawane na wenzio, utakuja kuumia, sisi bado tunakuhitaji. Huu ni ushauri wangu, bado tunakuhitaji. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, ndungu yangu, *trendya* mizigo ya miaka kumi au saba

ya nyuma, mizigo ilioingia na iliyotoka na sasa hivi, kaiangalie. Tuelezane ukweli, mizigo ilioingia na kutoka imeshuka. Ni ushauri wangu. Kaangalie *trend* ile ya miaka saba au sita ya nyuma au mitano iliyotoka hivi sasa, utaona ukweli ulipo. Hali siyo nzuri kusema ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni *declare interest*, mimi ni mfanyakishara, siwezi kudharau dafu kwa embe la msimu. Hii siasa kesho Mungu akijaalia haipo, lakini dafu siku zote unaweza kulipata. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *VAT on transit* hivi vitu wananchi wanalamikia sana. Ajira mnavyotangaza, hivi juzi mmetangaza ajira, sijui kama mmeztangaza, lakini kuna watu mmewaaajiri. Tuwe wawazi, tuwe wakweli katika bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, *DG* baadhi ya wafanyakazi wanamwogopa sasa hivi. Kama wanapita njia hii wafanyakazi wanamwogopa, wanapita njia nyingine. Liandike, ulifuatilie kama nasema ni ya kweli ama siyo ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wengine wanaomba muda wao wa kustaaifu kabla haujafika, wanaogopa bandarini kutokana na matukio yanayotokea. Suala za wizi limekuwa wizi tu. Ndiyo yale niliyosema, siyo kila anayepepesuka ni mlevi. Muda wa kustaaifu wafanyakazi haujafika, watu wanataka kustaaifu kuondoka, wameshachoka. Tena wale wazoefu; tutakuja kutafua rasilimali hiyo wakati huo hatuna. Huu ni ushauri wangu, Mheshimiwa Waziri fuatilia niliyokwambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije *DMI* (Chuo cha Baharia). Kuna eneo pale limekaa miaka nane au kumi, kibanda kimeshaanguka. Unafanya biashara; mimi mwenyewe binafsi nilishapeleka barua pale, lakini hakuna majibu, hakuna kilichofanya. Nafikiri wenyewe wapo hapo. Imekuwa kama nyoka wa mdimu Mheshimiwa Waziri. Nyoka wa mdimu hukaa kwenye mdimu, ye ye hana kazi nazo na ukienda kuchuma, anakurukia, faida iko wapi? Siyo kitu kizuri!

Kodi zingesaidia! Wengine wamekodishwa maeneo yale, wengine hawajakodishwa, wako kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika Bandari ya Letakii, hapa pana dhambi na maonevu makubwa. Wafanyabiashara wa Zanzibar na Zanzibar tegemeo lake kubwa ni biashara. Leo viazi, *cabbage*, pilipili ina-**megati** nane inapekuliwa. Vipo hapa hapa, *local food* hiyo, hatutendi haki. Kama unataka, nitakutajia; kuna geti namba tatu Mheshimiwa Waziri. Malindi pana geti pale pale, mita 50 haijafika, pana mizani, halafu unakuta mizani yenyewe. Usumbu, mnasema mnapunguza foleni, huku mnazidisha foleni. Umefunga mlango wa mbele wa nyumba wa nyuma umefungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanalipa ada za bandari pale kwa muda mrefu, lakini *charge* zimekuwa nydingi. Bandari zimekuwa na mapote; ikija mvua tope, likija juu, vumbi; wafanyakazi wana mazingira magumu katika kazi ile. Nampongeza sana *Acting Port Manager*, John Liundi, kazi anayofanya pale nitakuwa sijamtendea haki na nitakuwa mtovu wa adabu wa mwisho kama sikumshukuru kwa mazingira ya kazi anayofanya pale. Hongera *Port Manager* unayekaimu kwa muda. Pengine Mungu atakujalia muda siyo mrefu utatoa fupa hilli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna yule mlinzi pale anayeshughulikia ulinzi wa bandari. Kwa muda mrefu ulinzi umeimarika bandari ya Dar es Salaam. Tuwape haki zao. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Jamaa wa pale anaitwa Twange, amefanya kazi nzuri ya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla muda haujamalizika, nije kwenye ndege, *Bombardier* sasa.

Mheshimiwa Waziri chukulia mfano Pemba kule Makombeni kuna mabonde ya mpunga, umelima, umeshaotesha mpunga wako, kuna ndege wanaitwa tongwa wale, ukishauacha unakuja kuuvuna. Hawa wana malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, umenunua baiskeli, leo unashindwa kununua *pump* tu kujaza upepo baiskeli! Hebu waingizeni pesa tusije tukawalaumu, baadaye tukawa tunasema Tanzania wanafanya vibaya. Wanahitaji mtaji hawa. Kama hamuwezi, wakopesheni *five billion*. Leo tunafanya vitu vizuri, baadaye tutakuja ku-fail.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu msikivu sana yule *CO* hata jina lake siliui mimi. Ni rasilimali kubwa sana yule. Maneno yake tu ukisikia akizungumza utafikiri asumini zinatoka mdomoni, harufu yake. Ndiyo yale walisema, maneno mazuri ni sadaka. Ongeza mtaji wa Mtanzania. Hawawezi kufanya kazi wale bila kuwa na mtaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka hapo utaratibu wa *Bombardier* jamani, kuja usiku sisi kama walinzi tumechoka. Jaribuni kupanga utaratibu, Bunge linaanza Jumanne. Pangeni Jumatatu angalau saa 10.00 tuondoke kule. Badilisheni utaratibu huu. Halafu bei zake zikoje? Leo unanunua bei nyingine, kesho bei nyingine, kiti ndiyo kile kile. Hebu jaribuni kufanya utaratibu (*format*) mwengine. Bunge hapa linaanza Jumanne, Jumatatu angalau ndege ingeondoka saa 10.00 pale.

MBUNGE FULANI: Aah, ah!

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Hayo ni maoni yangu, nanyi kama hamtaki mtachangia. Kila mmoja ana uhuru wake wa kusema. (*Kicheko/Makofi*)

MBUNGE FULANI: Sawa sawa. (*Makofi*)

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Nije kwa *SUMATRA*.

Mheshimiwa *Branch Manager*, sheria hii inaumiza watu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MBUNGE FULANI: Unga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa...

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, bado dakika moja, nimeweka *stop watch*. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha. Ahsante sana Mheshimiwa Jaku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mary Deo Muro, atafuatiwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu ajiandae.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia mada iliyopo mezani. Kwanza namshukuru Mungu kwa kuwa na afya njema. Napenda kuchangia kwa ujumla na sehemu nyingine kutoa ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchangia juu ya ucheleweshaji wa pesa kutoka Serikalini kwenda kwenye Wizara na madhara yanayopatikana kwa ucheleweshaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunatembelea miradi, tumekuta kwamba kutokana na ucheleweshaji wa fedha hizo, madhara yaliyojiteza ni gharama za ujenzi kuongezeka mara mbili. Mfano, barabara ilijoengwa kutoka Dumila kuelekea Ludewa, badala ya kujengwa kwa shilingi bilioni 42 imejengwa kwa shilingi bilioni 42 *plus variation* ya shilingi billioni 22. Unaangalia, unasikitika na kukuta kwamba hali hii itasababisha ujenzi wa kilometa chache mahali ambapo ingeweza kujengwa kilometa nyingi kutokana na hizo *variations*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukumbuke kwamba kunapotokea *variations* kubwa kama hizo, kuna *negotiation*, ndipo *loophole* zile za ufisadi zinapoingia. Kwa hiyo, naishauri Serikali kama ina nia ya dhati ya kuhakikisha kilometa nyingi

zinajengwa kama walivyojipangia, wapeleke fedha kwa wakati ili kutokuruhusu hizo *variations* ambazo zina mianya ya ufisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye viwanja vya ndege. Kwenye viwanja wa ndege tumetembelea; nimekuta kwamba vingi viko chini ya viwango, kiasi kwamba pamoja na ununuaji wa ndege zilizonunuliwa, lakini viwanja vya ndege bado vingi ni vibovu. viwanja vya Shinyanga, viwanja vya Moshi. Moshi, kiwanja ambacho kina mlima wa Kilimanjaro ambapo ungeweza kuleta mapato makubwa, unavitegemea viwanja vitatu ambavyo vinazalisha. Sasa ukiwa na viwanja ambao vinazalisha na viwanja *vinavyo-consume*, ujue bado hujafanya kazi ya faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, kama ina nia ya dhati ya kutengeneza pato kwa Taifa, ihakikishe kabisa viwanja hivi *vinavyo-consume* faida inayotoka kwenye viwanja vile *vinavyozalisha*, inavitengeneza na viweze kufanya kazi na viweze kuleta faida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchangia sehemu ya bandari. Bandari yetu ya Tanzania tofauti yake na bandari nyingine za wenzetu ni kwamba bandari ya Tanzania kwa mfano, kwenye ushushaji wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za wenzetu mafuta yanashushwa kwenye matenki ya Taifa na *flow meter* inakuwepo tanki la Taifa, ndilo linalogawanya mafuta yale kwenye matenki ya watu binafsi. Sisi kama Tanzania unakuta kwamba matenki ni ya watu binafsi. Kwa hiyo, sisi tunahangaika na *flow meter* kugawanya kwenye matenki ambayo siyo ya kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba manteki ya Taifa yanakuwepo ili tunapopata mafuta tuweze kugawa kwenye mantaki ya wafanyabiashara ili Taifa liweze kupata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie miundombinu na mwanamke. Napenda hii lugha kwa sababu nafahamu kabisa mwanamke wa Tanzania ndiye anayezaa watu wote tulioko hapa; ametuzaa mwanamke, lakini hakuna hata mtu mmoja hajui kama huyu mwanamke alizalia wapi, alisafiri kwa usafiri gani mpaka akafika sehemu aliyojifungulia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiliangalia hilo kwa jicho la uchungu, tutafikiria barabara za vijiji ziboreshe, mgao ule inaogawa Serikali ihakikishe kwamba inagawa mgao ambao utasababisha barabara za vijiji kujengwa kwa viwango ambavyo mama mjamzito akiwa anaenda kujifungua, hataweza kufia njiani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano hai kabisa, nina ndugu yangu ambaye alibebwa kwa toroli, akawa anatembezwu kupelekwa hospitali. Zile kukuru kakara zote, akapata *rupture* njiani na akafia njiani. Yote hiyo ni kwa sababu tu barabara zile zilikuwa ni mbovu na hakuna njia nyininge, ilikuwa ni kumbeba aidha kwa mzega ama kwa toroli. Sasa tufikirie kama Serikali, huyu mwanamke ambaye ndiye anayezalisha mashambani huko, akitaka kupeleka mazao sokoni anashindwa apitishe wapi ili akafikishe sokoni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke huyo ndiye ambaye anazaa; anapohitaji kujifungua, hajui apite njia gani mpaka afike hospitali, ukuzingatia kwamba Tanzania sasa hivi bado hatujafika sehemu kila kijiji kuwa na hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iliangularie hilo na ichukue umuhimu kuhakikisha kwamba mafungu yale yanawafikia na uwezekano wa kupata barabara ambazo zinapitika ili kurahisisha hawa wanawake waweze kujifungua vizuri na uzazi salama uweze kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia eneo la *DARTS*. Nimeangalia Dar es Salaam mradi wa *DARTS*, ni mpango mzuri kabisa. Pia kuna treni ile (*commuter*), naomba

basi, kwa sababu tulitembelea na nikaona jinsi gani kama ile *commuter* itapata vichwa ambavyo siyo *long safari*, inaweza kuleta faida kubwa kabisa, tena faida ya wazi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya *calculations* tukakuta kwamba kwa kupata *short safari*, vichwa na mabehewa yake tunaweza tukatengeneza faida na Wizara hii ikaweza kuleta faida kubwa kuliko inavyotegemea. Kwa sababu sasa hivi treni ile ya pale Dar es Salaam inayoenda Pugu inatumia vichwa vyta *long safari*, kwa hiyo, mafuta yanayotumika ni mengi. Kwa hiyo, inashindwa kuleta faida tarajiwa. Natamani kuona ile treni inapata vichwa na mabehewa ya *short safari* ili iweze kutengeneza faida iliyotarajiwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie upande wa *TCRA*; napenda kupongeza *TCRA* kwa kazi nzuri wanayofanya ambayo ina faida kubwa, lakini pia naomba Serikali iangalie *TCRA* kwa macho ya huruma kwa sababu maduhuli inayokusanya inapeleka Serikalini hela nydingi, lakini mrejesho wake unakuwa ni wa shida sana kwa ajili ya urasimu wa kurejesha zile hela ili *TCRA* waweze kufanikisha utendaji wao. Hivyo naishauri Serikali kwamba kwa kuwa *TRCA* wanafanya kazi nzuri, basi ni vizuri wanapoomba pesa ili waweze kuleta utendaji mzuri, waweze kurejeshewa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kuchangia kuhusu *Data Center* Taifa ambayo iko chini ya Wizara hii. Naishauri Serikali kuhakikisha kwamba taasisi zote za Serikali zinatumia *Data Center* ile iweze kufanya kazi iliyotarajiwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo, nashukuru sana. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mary Deo Muro. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Serengeti, lakini pia nichukue nafasi hii kuwapa pole kwa tatizo kubwa la njaa walilonalo. Nafahamu wana hali mbaya kweli kweli, lakini niwaambie tu Serikali imekubali kufanya tathimini ya mahindi yaliyopo Shinyanga kwenye ghala la Serikali na watapata mgao wa mahindi kwa ajili ya kupunguza mfumuko wa bei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, sasa nijielekeze moja kwa moja kwenye Wizara husika. Naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako mnisikilize kweli kweli hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 mmekuja ndani ya Wilaya ya Serengeti kuhusu barabara ya Makutano - Mgumu - Mto wa Mbu. Ni barabara ambayo imeanza kujengwa tangu mwaka 2013 mwezi wa tatu. Kipande cha kilometra 50 kuanzia Makutano mpaka Sanzate, mwaka 2016 nimeongea hapa sana; sasa hivi ninavyoongea hapa wamepewa *almost* shilingi bilioni 26 kama sikosei, lakini mpaka leo miaka zaidi ya minne bado hata kilomita moja haijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuja Jimbo la Serengeti kutembelea ile barabara, bahati nzuri tulikuwa naye, tulikaa tukaongea na alitoa tamko kwenye vyombo vya habari kwamba ikifika mwezi wa nne, kama hata kilometra moja haijakamilika, hawa wakandarasi tunawatumbua. Mheshimiwa Waziri, huu ni mwezi wa ngapi? Hata kilometra moja bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Waziri anapokuja ku-*wind up* aniambie lile tamko alilolitoa kwenye vyombo vya habari na huu ni mwezi wa nne umeisha, hata kilometra moja bado haijakamilika, umechukua hatua gani kulingana na maneno aliyojasema ambayo kimsingi wananchi wa Mkoa wa Mara, Musoma, Bunda na Serengeti walimsikia akitoa tamko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri, barabara hii ilitakiwa itengenezwe kwa kiwango cha lami kuanzia Makutano mpaka mpaka wa Hifadhi ya Serengeti *National Park* pale Tabora B; naona mmekomea pale Mugumu Mjini. Kilometra 18 hazieleweki. Naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kusema, atuambie hizi kilometra 18 kutoka Mugumu mpaka mpakani mwa Hifadhi ya Serengeti kwa maana ya geti la Tabora B, wataitangaza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye barabara hii mwaka 2016 imetengewa shilingi bilioni 20; upande wa Arusha shilingi bilioni nane na upande wa Mara shilingi bilioni 12. Sasa mwaka huu mpaka ninavyoongea kipande ambacho kimetangazwa cha kuanzia Mugumu kwenda Nata na Isenye bado mkandarasi hajapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda sasa kupitisha bajeti ya Mheshimiwa Waziri na Mkandarasi hajapatikana, nitaomba aseme chochote kuhusu upatikanaji wa mkandarasi wa kujenga hii barabara. Na mimi namwomba Mheshimiwa Waziri, bahati nzuri yeye sio mwanasiasa, amekuja pale nimemwona, hana mambo ya ubaguzi ubaguzi kama wengine, nampongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie ili barabara hii ikamilike. Kimsingi, tunawapenda wakandarasi wa ndani, lakini kama hawawezi kufanya kazi kwa mujibu wa mkataba, kwa nini tuendelee kuwa-entertain?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri ukumbuke Mheshimiwa Waziri, hii barabara ilianza kuwekwa kwenye llani ya CCM tangu enzi za Nyerere. Nyerere akaondoka akaja Mwinyi, akaja Mkapa; na wakati wa Mkapa kumbuka pia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli ndiye aliyekuwa Waziri wa Ujenzi. Akaondoka, amekuja Kikwete; Mheshimiwa Dkt. Magufuli huyo huyo ndiye alikuwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie tu kwamba wananchi wa Serengeti na wananchi wa Mkoa wa Mara, walimpa kura Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa sababu walijua

akiwa Rais, hizi barabara zitakamilika upesi. Sasa tunaenda 2020 sijui mtasemaje kama zitakuwa hazijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, barabara ya Tarime - Mugumu inafanyiwa *feasibility study*. Wananchi wa Jimbo la Serengeti wanataka wajue ni lini barabara hii itaanza kulimwa? Kwa hiyo, utakapokuja naomba useme kuhusu barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niseme, tuna barabara ya Musoma inaitwa Nyankanga - Rung'abure ambayo kimsingi mkoa kwa maana ya *TANROADS*wameanza kujenga kilometra mbili, wameanza kidogo kidogo. Kwa hiyo, naomba kwa niaba ya wananchi wa Serengeti na wananchi wa Mkoa wa Mara, barabara hii iingizwe kwenye barabara za kufanyiwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka niseme, ni vizuri mfahamu kwamba Hifadhi ya Serengeti ambayo ndiyo hifadhi inayoongoza Afrika kwa kuingiza watalii wengi na watalii wengi wanaoingia Hifadhi ya Serengeti wanatokea Kenya, ni vizuri mfahamu umuhimu wa barabara hii kwamba ni kiungo kikubwa cha kiuchumi katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri mfahamu kwamba *Serengeti National Park* ambayo ina tembo na simba wengi, wanaathiri watu wa Serengeti, ni vizuri mkafahamu ni mbuga ambayo duniani inatambulika, lakini unapoenda Serengeti unatwanga vumbi kuanzia Bunda mpaka Mugumu; kuanzia Tarime mpaka Mugumu na kuanzia Musoma mpaka Mugumu, sidhani kama mnamtendea haki hata Baba wa Taifa ambaye jana tulikuwa tunamuenzi kwa sababu ya makubaliano ya Muungano walioufanya na Rais wa Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, katika Jimbo la Serengeti, bado hali ya mawasiliano kwa maana ya minara ni shida kweli kweli. Mwaka 2016 nilisema hapa kwamba ukienda kwenye

maeneo ya mbuga yetu ya Serengeti ambako kimsingi tuna *population* kubwa mle ya watalii na nini, mawasiliano ni shida kwa maeneo ya Robo, Birira, Seronera na maeneo mengine ya mbuga yanahitaji mawasiliano ya uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Wilaya ya Serengeti, kuna maeneo ambayo tunahitaji minara. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye hili la minara, naomba uniambie, ni lini maeneo hayo yatapata minara ya simu, ama *Vodacom* ama *Halotel*? Kwa hiyo, ni jambo la msingi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo, nachukue nafasi hii kukuomba hayo mambo ya msingi ambayo wananchi wangu wa Serengeti wamenituma, wanataka kusikiliza kutoka kwako Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk ajiandae. (*Makof*)

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hoja hii ambayo ni ya muhimu sana kwa mwananchi wa kawaida na hata mwananchi yoyote wa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, napenda kumshukuru sana Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli na hususan Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa. Kazi ambayo Wizara hii imeifanya katika kipindi kifupi ni kazi ambayo inatakiwa isifiwe na ni kazi ambayo kila mtu ameiona. Katika kipindi kifupi Serikali hii ya Awamu ya Tano imeweza kutufanya mambo mengi, imeweza kuleta ndege hapa. Kuna ndege sita; mbili zimeshafika. Zaidi ya kuleta ndege hizi kuna nchi nyingine ndogo tu kama Mkoa hapa nchini, zina ndege

kubwa na sisi nchi hii tumeshindwa kuleta ndege na Mheshimiwa Rais ameweza kuifufua ATCL. Kwa hiyo, tumpongeze sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ameweza kuleta *flyover*. *Flyover* zimeanza kujengwa, zitapunguza msongamano mkubwa sana hapa nchini hasa ukichukulia maanani pia kwamba watu wote wanahamia hapa Dodoma sasa hivi, kwa hiyo, msongamano kule Mjini Dar es Salaam utapungua kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha msingi zaidi ni kuweza kuleta treni ya *standard gauge* ambayo kwa kweli ni treni ya kisasa. Kule nchi za nje wenyewe wanaiita *bullet train*. Sasa umuhimu wa treni hii kwa kweli utakuja kuonekana hasa wale ambao wataingia Bungeni mwaka 2020; wataacha magari yao yote Dar es Salaam na kuingia kwenye hizi treni. Kwa hiyo, mambo haya pamoja na mambo mengine ya vivuko ambavyo vimewahi kufanyika na mambo mbalimbali ambayo yamewahi kufanyika kwa kweli napenda kumpongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Mbarawa ametembea nchi nzima hii kwa ajili ya kukagua miradi, ametembea kote, amekuja Tanga karibu zaidi ya mara tatu, ingawaje bado Muheza hajafika, namsubiri. Lakini nangependa kumshukuru sana, yeye na wataalam wake kazi ambayo wameifanya kwa kweli ni kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudzi zote hizo, lakini pia safari hii Wizara hii imeweza kuangalia Mkoa wa Tanga; tunajua tumepata zabuni ya kutengeneza bomba la mafuta kutoka Hoima kule Uganda mpaka kwenye Bandari ya Tanga, lakini kwenye kitabu hiki nashukuru sana Wizara imeanza kuboresha Bandari ya Tanga na tumefanikiwa kupata karibu shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kutengeneza bandari hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha msingi ni kwamba Mheshimiwa Waziri amesahau kuangalia reli ya Tanga. Reli

ya Tanga ndiyo chimbuko, tena reli ya Tanga imeanza kabla hata ya hii reli ya kat, lakini sijui kwa nini hakuigusia, hata kuiangalia. Namuomba aangalie kwa kadri atakavyoweza tukitilia maanani kwamba tuna bomba la mafuta, tuna kazi kubwa, Tanga inataka kufufuka, kwa hiyo, tunaomba aangalie atafanya namna gani ili na reli ya Tanga iweze kuwa kwenye kupata *standard gauge*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, pia kuna na barabara ambazo zimesaidia sana, zinataka kutoa vitu kutoka Mkoa wa Tanga ili viende kwenye Mikoa mingine. Mheshimiwa Waziri ametusaidia sana kwenye barabara ya Bagamoyo - Saadani - Pangani ambapo barabara hii kwa kweli ndiyo tumepata hela ambazo ni kianzio tu, lakini tunashukuru sana. Tunaamini kwamba baada ya barabara hii kutengenezwa basi Tanga inaweza kufunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo, ukitalia maanani pia tuna barabara ya Handeni - Kibarashi pamoja na Kibaya ambayo inakuja kutokea Singida. Barabara hii imewekewa hela ndogo, lakini tunaamini kwamba huu ni mwanzo tu, atawea kuifikiria kuweza kuongezea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi zaidi ambalo limenifurahisha kwenye bajeti hii ni kuweza kuweka hela za kutengeneza barabara ya kutoka Amani mpaka Muheza kilometra 36. Barabara hii safari hii imewekewa hela karibu shilingi billioni tatu. Najua ni mwanzo tu, najua kutokaza na jinsi nilivyokuwa namghasi Mheshimiwa Waziri atatuongezea hela, lakini hii ni chachu! Barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi katika Wilaya ya Muheza na ninaamini kabisa kwamba wana Muheza hasa watu wa Amani kama wanansikia watafarajika sana kuona kwamba barabara hii safari hii imewekewa hela. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami namwambia Meneja wa *TANROADS*, Engineer Ndumbaro ambaye yupo kule, anafanya kazi nzuri sana na mara baada ya hizi fedha kufika, basi barabara hii, kama watu wa Amani wanansikia, itaanzia Amani kuteremka mpaka Muheza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tuliahidiwa kilometa tatu na Mheshimiwa Rais alipokuja, alipata vumbi sana pale Muheza na akaahidi na tunazitegemea hizo kilomita tatu basi zitapunguza vumbi ambalo lipo pale Mjini Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko barabara nyingine ambayo inatoka kwenye *junction* ya Pangani, Boza. Barabara hii ni muhimu sana kwa watu wa Muheza. Sasa hivi inashughulikiwa na *TANROADS* na tuliomba sana iingizwe kwenye mpango huu wa sasa hivi kwa sababu barabara hii inatoka *Boza junction* na inapita Muheza, inakwenda moja kwa moja mpaka inapita Misozwe, inakwenda mpaka Maramba. Sasa barabara hii tuliomba hata tupewe hela ziingie hata kidogo kwa ajili ya kufanyia upembuzi yakinifu tayari kwa kuwekewa lami. Tungeshukuru sana kama utasikia kilio hiki kwa sababu nilliwahi kuiongelea barabara hii kwenye bajeti iliyopita na ninaamini kwamba hata safari hii utaweza kuangalia unaweza kuifanyia vipi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambazo tuliomba zipandishwe hadhi na ziweze kushughulikiwa na *TANROADS* na barabara hizo tumeshazipitisha kwenye *RCC*. Barabara hizo zipo tano; kuna barabara ya Kilulu ambayo inakwenda mpaka Mtindiro inapita kwa Fungo. Tunaomba sana ipandishwe hadhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya Kibaoni - Misarai - Zirai inatoboa mpaka inakwenda Korogwe. Barabara hii ningefurahi sana kwa sababu inatoboa kwenye Jimbo la Profesa wangu Maji Marefu. Tumekuwa tunaipigia makelele sana; tungefurahi sana kama ingeweza kupandishwa hadhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara ya Potwe - Shambakapori na Amtiko inapitia Masuguru mpaka Kerenge. Sasa tutashukuru sana kama ungeweza kutuangalizia barua hizo ambazo tumeshapitisha kwenye *RCC* na tungeshukuru sana kama ungeweza kutusaidia hizi barabara zishugHulikiwe na *TANROADS*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano. Tarafa ya Amani ina matatizo sana ya mawasiliano, nilizungumzia bajeti liliyopita na nilishakuja Wizarani na nikatoa kilio hichi kwamba uchumi wa Muheza unategemea sana Amani, lakini sasa watu wenyewe kule hawana mawasiliano ya simu. Tulikuwa tunaomba kampuni moja ya simu ituwekee minara kule. Maeneo ya Misarai, Mbombole, Zirai, Kwemdimu, Tongwe na Kiwanda kote kule kuna matatizo sana ya mawasiliano ya simu. Kwa hiyo, ningeshukuru sana kama ungewaamuru hata kampuni moja tu iweze kutuwekea, ingewasaidia sana watu wa Amani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miradi, Wizara hii ina miradi mingi sana, lakini ningeshukuru sana kama miradi hii ingeanza kushirikiana na *PPP*. Watu binafsi ni watu muhimu sana. Nchi zote duniani sasa hivi zinashirikiana na watu binafsi na bila watu binafsi tutachukua miaka mingi sana kukamilisha hii miradi. Mmewahi kuona acha hii miradi mikubwa ya madaraja au barabara, lakini barabara zote sasa hivi, hata nchi zilizoendelea zinatumia *road toll*. Sasa huu mpango ambaao unatumia sasa hivi wa kukata hela kidogo za mafuta hauna *effect*. Mimi ningeshukuru sana kama mnganezisha *road toll* ili watu binafsi wajenge hizi barabara na mwingie makubaliano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini kama Mheshimiwa Waziri ukisimamia vizuri huu urasimu ambaao upo hapo *treasury* wa kuweza kutoa hizi zabuni kwa watu binafsi, ungeusimamia naamini kabisa kwamba sasa hivi tungekwenda kama *rocket* kwenye hii nchi. Kwa hiyo, uchukue hayo mawazo na uangalie kwamba utaweza kuyatekeleza kwa namna gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaamini kabisa kwamba mambo yote ambayo Mheshimiwa Waziri ameyafanya, safari hii ameionna Tanga vizuri, lakini tunaomba aangalie kabisa suala la reli yetu ya Tanga na pia tunaomba aangalie kwenye kiwanja chetu cha ndege kwa sababu kitakuwa *busy* sana sasa hivi, tunategemea kupata Waziri wa Viwanda hapa, ndugu yangu

ametuletea kiwanda kikubwa sana kule, sasa kutakuwa na mambo mengi sana Tanga, bandari inafanya kazi vizuri na imeshaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, tunaomba uangalie kiwanja chetu na chenyewe kiweze kusaidiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ninazidi kuipongeza Wizara hii kwa kazi ambayo imefanya. Wizara hii imekuwa ni kioo cha Wizara nyingine nyingi hapa. Kazi ambazo zimefanyika, zinaonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kushukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk na Mheshimiwa Vedasto Ngombale ajandae.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara hii. Kwanza kabisa nianze kutoa pongezi zangu kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Naibu Waziri *Engineer Ngonyani*, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa taasisi zote katika Wizara hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, na mimi kwa kweli kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu nianze kupongeza kazi nzuri ambazo zimefanywa na Serikali ya Awamu hii ya Tano kama vile ujenzi wa Daraja la Kigamboni, ujenzi wa mabweni *UDSM*, uzinduzi wa ujenzi wa reli ya katì, uzinduzi wa miradi ya *flyovers*, *TAZARA* na Ubungo, Serikali kumiliki asilimia 100 *TTCL*, mradi wa ujenzi wa upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam na ununuzi wa ndege ya *ATCL* na kubwa kuliko zote, Serikali kuanza kulipa wakandarasi na washauri shilingi bilioni 788 kutoka katika deni la shilingi bilioni 930.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali hili zoezi liwe endelevu ili miradi yetu ikamilike kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuzungumzia kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege. Naipongeza Serikali kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege kote nchini, ni pamoja na jengo lile la abiria *Terminal III* Kiwanja cha Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa tulipotembelea tulikuta kuna changamoto ya pesa kutopelekwa kwa wakati, sasa naiomba Serikali ipeleke pesa kwa wakati ili jengo liweze kukamilika na liendane na ununuzi wa ndege zetu. (*Makofii*)

Niendelee kupongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja chetu cha Nduli. Hiki kiwanja kwa kweli tumekuwa tukikidai kwa muda mrefu, sasa tunaishukuru Serikali angalau imeweza kutenga pesa na sisi kiwanja chetu cha Nduli sasa kitajengwa na najua hata *Bombardiers* sasa itatua pale. Nitoe tu ushauri, kwamba pamoja na kuwa huu mradi tayari wananchi wa pale wameshaukubali sasa waweke alama katika yale maeneo ambayo upanuzi utafanyika ili yale maeneo yasiweze kuendelezwa, kwa sababu yakiendelezwa wakati wa kulipa fidia itakuwa tatizo kubwa sana.

Vilevile niiombe Serikali sasa, kuna viwanja vingi sana havina hati miliki kikiwemo hiki cha Iringa. Kwa hiyo, sasa itengeneze hati ili wananchi wasiendelee kuvamia katika hivi viwanja vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na ujenzi wa barabara nchini. Niipongeze sana Serikali kwa kuendelea na ujenzi wa miradi ya barabara kwa kiwango cha lami.

Naomba niunge mkono ushauri, Mheshimiwa Serukamba alipokuwa akichangia amesema kwamba angalau zile barabara za Wilaya *TANROADS* iendelee kuzihudumia, kwa sababu tunaona hata sisi wenyewe tulipokuwa tunachangia watu wengi sana wanalamikia barabara zilizopo katika vijiji kwamba miradi haiendi kwa wakati na vilevile tumeona kwamba hakuna wataalam wengi kwenye Halmashauri zetu. Kwa hiyo, kama barabara

hizi zitamiliikiwa na *TANROADS* tuna imani kabisa zitakwenda vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pia labda uwepo upembuzi yakinifu katika miradi ya barabara zetu, kwamba zile za kiuchumi ziweze kupewa kipaumbele, kwa sababu tumekuwa na barabara nyingi za kiuchumi katika halmashauri zetu ambazo zinakuwa hazijengwi kwa kiwango cha lami kiasi kwamba sasa wakati wa mvua malori yanakwama. Kwa mfano pale Iringa tuna miti, kama Mgololo kule unaona wakati wa mvua malori yanakwama na kuna ajali nyingi sana zinatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini vile vile ubovu huu wa barabara hasa vijiji ni unasababisha hata vifo vya akina mama na watoto. Kwa sababu ya miundombinu ambayo ipo katika barabara zetu zilizopo vijiji ni wakati wa mvua akina mama wengi hawafikiwi. Kwa hiyo, mimi niombe hizi barabara zipewe kipaumbele ili kupunguza pia vifo vya akina mama na watoto katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie pia barabara zilizopo katika Mkoa wetu wa Iringa. Tunashukuru sana Serikali katika bajeti hii imeweza kutenga pesa kuanza ujenzi wa barabara inayokwenda katika mbuga ya Ruaha. Muda mrefu sana tumekuwa tukizungumzia barabara hii kwa sababu utalii utaongezeka katika mkoa wetu na mikoa iliyopo katika Nyanda za Juu Kusini. Kwa hiyo, mimi nishukuru kwamba japo kuwa wametenga pesa, Iakini sasa ujenzi ufanyike kwa sababu kutenga pesa ni kitu kingine na kuanza ujenzi ni kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo barabara za kiuchumi kama barabara ya Mafinga – Mgololo, Kinyanambo – Isalavanu – Saadani – Rujewa, kuna Kiponzelo – Wasa, kuna barabara ile ya Kilolo mpaka Iringa Mjini. Tunaomba Serikali yetu izipe kupaumbele kwa sababu uchumi wa mkoa wetu unazitegemea sana hizi barabara ambazo ziko katika wilaya hizo nilizozitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie watu wenyewe ulemavu. Sisi wote hapa ndani ni walemauvu watarajiwa. Nilipoongea na watu wenyewe ulemavu katika Mkoa wangu wa Iringa yapo mambo ambayo wanalamikia hasa miundombinu katika magari. Inaonekana kwamba watu wengi wenyewe ulemavu bado Serikali hajawaangalia. Watu wanakuwa na baiskeli lakini hawawezi kupandisha kwenye gari kwa sababu hakuna miundombinu inayoruhusu mtu mwenye ulemavu kuweka baiskeli yake kwenye gari lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile majengo yetu bado si rafiki sana na watu wenyewe ulemavu kiasi kwamba yanasa babisha hawa watu wenyewe ulemavu kukosa hata huduma nyingine. Utakuta mama mwenye ulemavu ni mjamzito anashindwa kupandisha ngazi kwenda kumuona daktari. Kwa hiyo, mimi ningeomba sheria iwepo ili watu wenyewe ulemavu pia wazingatiwe wakati wanajenga haya majengo yote yakiwepo hata majengo ya shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile *TCRA* labda iangalie, pia hata katika televisheni zetu bado hawajaweka watu kutafsiriwa zile lugha za watu wenyewe ulemavu. Kwa hiyo mambo yote hayo yazingatiwe. Hakuna pia michoro kwenye barabara kuonesha watu wenyewe ulemavu wanapopita, kwa hiyo mimi naomba haya mambo yazingatiwe kwa sababu sisi wote ni walemauvu watarajiwa, huwezi kujua wewe lini utakuwa mlemauvu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuzungumzia kuhusu Shirika la Posta Tanzania. Kwa sababu Serikali imeanza kuyafufua mashirika nchini, ni kwa nini sasa Serikali isitoe mtaji wa kutosha ili hili shirika liweze kujiendesha. Shirika hili lilikuwa na deni kama la shilingi bilioni 5.1 ambapo Serikali imelipa shilingi bilioni 2.5 tu kwa shirika.

Sasa mimi ningeomba sasa hivi hili shirika lizingatiwe kwa sababu lilikuwa lina mali nyingi sana hapo zamani. Kwa hiyo mimi naomba wapatiwe pesa zao zilizobaki ili na lenyewe liweze kujiendesha ili wafanyakazi wale pia waweze kufanya kazi kwa kujiamini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nizungumzie mradi wa *postal code* na *symbol* za posta. Huu mradi kwa kweli umekuwa mara nyingi sana; kwanza ni muhimu sana kwa sasa hivi kwa sababu kwanza makazi yatatambulika, na isitoshe hatakukusanya kodi tutakusanya kwa urahisi kama nyumba zitakuwa zinatambulika kutokana na hizi *symbol* za posta, lakini mara nyingi sana imekuwa ikitengewa pesa kidogo sana kila mwaka, mimi naomba safari hii...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale. Mheshimiwa Cecil Mwambe ajiandae.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia leo kuwa na afya njema na kuweza kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi. Vilevile pia nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tanga kwa kazi walijonipa ya kuja kuwawakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano. Tatu naanza kwa kuunga mkono Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi sitapongeza sana, lakini niseme tu sisi watu wa Pwani tuna kawaida tunajua kwamba baba ndio mlezi wa familia na anapotimiza majukumu yake ametimiza majukumu hakuna haja ya kumsifu, ndiyo kazi yake hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza moja kwa moja kuchangia sekta ya barabara. Kwa muda mrefu tumetoa kilio watu wa Tanga kwa barabara ya Tanga – Pangani – Bagamoyo. Barabara hii ni ya kihistoria, barabara hii imepita katika majimbo matatu, kuanzia Tanga Mjini, Pangani hadi Bagamoyo na pia Muheza na ina Wabunge watatu au

wanne, lakini kwa muda mrefu imekuwa haikufanyiwa matengenezo lakini safari hii tunaambiwa imetengewa shilingi bilioni nne ambayo ni sawasawa na asilimia 15 ya mradi mzima wa barabara.

Mimi kwanza niiombe Serikali ikamilishe asilimia 100 kabisa ili barabara ile iweze kutumika kwa wakati wote. Kwa sababu tukumbuke barabara ya Pangani imepita ahadi za Marais wanne waliopita, Rais Nyerere, Rais Mwinyi, Rais Mkapa na Rais Kikwete, wote walihidi kujenga katika kiwango cha lami lakini ilishindikana. Tunaomba safari hii barabara ile ijengwe kwa kiwango cha lami na tusije tukaambiwa fedha bado hazijapatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachoiombea barabara ya Pangani kujengwa, kuna Mbuga ya Saadani ambayo ni mbuga pekee duniani ukifika *time* za jioni kama hizi utakuta wanyama wote wamekusanyika *beach* kama vile binadamu. Kwa hiyo, hiyo nayo ni hali tunayoitaka barabara ya Pangani ijengwe itakuwa ni chanzo cha uchumi lakini pia itaboresha uthalii wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linguine ninalotaka kuzungumzia ni suala zima la reli. Kuhusu reli ya kiwango cha *standard gauge* niliwahi kusema mwaka jana kwenye bajeti kama hivi kwamba waswahili wanasema mwiba uingiapo ndipo utokeapo. Reli ya Tanzania au Tanganyika wakati huo ilianza kujengwa Tanga kuanzia mwaka 1905 ikaanzia Tanga ikaenda mpaka Moshi ikafika mpaka Arusha baadaye ikagawanya wa ikapita Dar es Salaam ikaingia Morogoro hadi kufika Kanda ya Ziwa, lakini leo tunaona wenzenetu katika *standard gauge* mnatutenga watu wa Tanga. Tunataka tuwaambie watu wa Kanda ya Ziwa sisi Tanga ndio walimu wenu, kwa hiyo, nataka reli ya *standard gauge*, Serikali pamoja na kwamba wanataka kuianzisha Dar es Salaam, lakini Tanga msije mkaisahau kwa sababu Moshi, Tanga yote hiyo ndiyo reli ya kwanza ilianza kujengwa.

Kwa hiyo, tunapenda keki hii ya Taifa igawanywe kwa usawa ambaao hautaleta manung' uniko. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa majini, nashukuru kwamba kampuni ya Bakhresa imetuletea meli kubwa inayofanya usafiri kati ya Pemba na Tanga na sasa ajali zitakuwa zimepungua. Kama mtakumbuka Januari, 09 iliokea ajali kubwa kabisa ya boti ikaua zaidi ya watu 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfanyakishara binafsi amejitolea kuleta meli, lakini bado kuna siku na siku; tunataka Serikali nayo ituwekee meli pale ili hata kama mfanyakishara anaweza kuamua wakati wowote akiona hapati faida akaamua kuondoa meli yake, lakini ya Serikali itakuwa inahudumia wananchi wake. Kwa hiyo, mimi nakutaka Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri mhakikishe Serikali nayo ilete meli katika bandari ya Tanga itakayotoka Tanga kwenda Pemba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote Tanga zimekuwa zikitokea ajali za mara kwa mara. Nimekusikia Mheshimiwa Mbarawa asubuhi ukisema kuna kikosi kazi cha uokoaji, lakini kikosi kazi kile hakina zana za kufanya kazi, na hata pale wanapokuwa na zana za kufanya kazi hawana mafuta. Iliwahi kutokea ajali moja, mimi na Mheshimiwa Khatib, wakati huo mimi ni Diwani, tukakubali kutoa hata mafuta ili wakaokolewe ndugu zetu ambao boti ilikuwa inawaka moto, lakini ikawa pia tunaambiwa mpaka Meneja wa Bandari atoe *go ahead* ndipo chombo kianze kutoka, kwa hiyo, hili ni tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kikosi cha uokoaji kama kipo kweli Mheshimiwa Waziri akiimarishe kiwe na helikopta, kiwe na boti, kisisaidie tu kuokoa maisha ya watu wanaopata ajali baharini, lakini hata zinapotokea ajali za magari. Leo imetokea ajali Daraja la Wami au barabarani watu wengine wanapoteza maisha kwa sababu hakuna usafiri wa haraka unaoweza kuwafikisha katika hospitali zetu.

Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri katika bajeti yako uongeze fungu ambalo litasaidia kupata hata helikopta za uokoaji zisaidie kuwahisha majeruhi katika hospitali zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu usafiri wa anga. Usafiri wa anga Tanga imekuwa kuna kizungumkuti kidogo, uwanja ni uleule wa tangu mkoloni. Tunahitaji Tanga kutokana na uwekezaji mkubwa unaokuja tupate kiwanja cha ndege cha kimataifa (*Tanga International Airport*) kwa sababu pana uwekezaji wa bomba la mafuta, Tanga kuna utalii, vile vile Tanga pia kuna *Tongoni Ruins, Amboni Caves* na mambo mengine pamoja na *Amani Research Institute*, zote hizo zinatakiwa tuweke uwanja wa ndege wa kisasa ili tuweze kupata mafanikio ya uchumi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine katika hicho kikosi pia pawe na *divers*. Tumeona wakati wa ajali ya *MV Bukoba* watu walishindwa kuokolewa kwa sababu hatuna *divers*, tumeagiza *divers* kutoka Mombasa - Kenya, hii ukiangalia inatutia udhaifu kidogo nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhsu suala la Daraja la Wami. Nimekuwa nikisema Daraja la Wami ni *link* yaani kiunganishi kati ya Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na hata nje ya nchi kama Kenya kupitia Nairobi mpaka Ethiopia huko. Lakini daraja lile ni la tangu mkoloni, daraja lile lina *single way* hayawezni kupita magari mawili kwa wakati mmoja, hivi Serikali inashindwa kujenga Daraja jipya la Wami? Nimeona kwenye taarifa ya bajeti yako umetenga fedha, lakini nasema iwe ni kweli. Daraja la Wami limekuwa likipoteza maisha ya watu na mali zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, naomba Daraja la Wami lijengwe daraja kubwa na jipya la kisasa kama lilivyokuwa la Kigamboni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Bandari ya Tanga. Bandari ya Tanga imekuwa ikikimbiwa na wafanyabiashara kwa sababu kuna tofauti kubwa na usumbufu mwingi unaotoka katika Bandari ya Tanga na uliwhi kutoa taarifa kwamba Bandari ya Tanga imekuwa inafanya kazi kwa hasara, inafanya kazi kwa hasara kwa sababu wafanyabiashara wanaikimbia. Mfanyabiashara yuko radhi apitishe mzigo wake Bandari ya Mombasa, Kenya azunguke Holili, Kilimanjaro ndipo aje Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu cha kodi ni kimoja katika mipaka yetu yote ya Tanzania kwa nini watu wanaakimbia Bandari ya Tanga? Ni kwa sababu pana usumbufu na vilevile pana dosari za hapa na pale. Si hivyo tu hata *borderya* Horohoro kuna matatizo, wafanyabiashara pia wanakimbia na sasa hivi Serikali imeanzisha utaratibu kwamba kuna watumishi wa *TRA* ambao wapo Mombasa, Kenya wanafuatilia makontena huko huko, ukija Horohoro tena ushushe mzigoto tena, ni usumbufu kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nimshauri Mheshimiwa Waziri, aboreshe Bandari ya Tanga pasiwepo na usumbufu, mizigo itoke kwa muda mfupi ili wafanyabiashara waweze kuitumia vizuri Bandari ya Tanga, lakini pia tuongeze mapato ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala zima la ununuji wa ndege. Tunashukuru kuwa *Bombardier* zimepatikana, zifike Tanga, lakini ndege zile...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Bakari huku Bara wazazi huwa wanapenda waambiwe ahsante, umemwona Mheshimiwa Selasini hapo, wanae hawaombi kabla hawajasema ahsante.

Pia Mheshimiwa Profesa Mbarawa naona hiyo kazi tumepewa mimi na wewe, sina uhakika kama tutaifanyaje hiyo kazi.

Mheshimiwa Vedasto Ngombale, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mheshimiwa Hasna Mwilima ajandae.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili basi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza nichukue nafasi hii kutoa pole kwa majirani zangu wa Rufiji kwa mafuriko maana kuanzia jana Mto Rufiji umefurika, kwa hiyo, nitoe pole sana, hata yale maghorofa yetu yote yameanguka chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mawasiliano. Katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini kuna kata ambazo bado hazijapata mawasiliano ya simu; kuna Kata za Kibata, Kandawale na Kijumbi hazijapata mawasiliano ya simu, lakini pia kuna vijiji vya Namakolo na Chapita katika kata ya Namayuni havijapata mawasiliano ya simu. Katika kata ya Kipatimu kuna kijiji cha Nkarango na kijiji cha Nandete havijapata mawasiliano ya simu. Niishauri Serikali ijitahidi maeneo hayo niliyoyataja yaweze kupata mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara; nianze na barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale ambayo ina kilometra 230. Barabara hii ina umuhimu katika mambo makuu matatu; kwanza ni barabara ambayo imepitia katika majimbo matatu, Jimbo la Kilwa Kusini, Jimbo la Kilwa Kaskazini na Jimbo la Liwale, lakini la pili ni barabara ambayo imepita katika Hifadhi yetu ile ya Selous. Kwa hiyo, barabara hii kama ingekuwa imetengenezwa ingetusaidia sana katika utalii. Pia la tatu Waheshimiwa Wabunge tusijisahau, nyakati zile za uchaguzi Wabunge wengi huelekea maeneo ya Liwale, maeneo ya Ngende kwa sababu ya mambo yetu yale, mimi nafikiri ninyi mnayafahamu, lakini cha kushangaza ni kwamba barabara hii inasahaulika. Kwa hiyo, niiombe Serikali, barabara hii ni muhimu sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine nashangaa ni vigezo gani vinatumika kuamua sasa ni barabara ipi ijengwe kwa kiwango cha lami? Kutoka Nangurukuru mpaka Liwale ni mbali sana, Wilaya ya Liwale

iko pembezoni kabisa na katika llani ya Chama cha Mapinduzi ilieleza kwamba ingefanya upembuzi yakinifu lakini nimeangalia katika hotuba hakuna chochote kilichopangwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nikuombe basi uwafikirie wale watani wangu Wangindo na sisi Wamatumbi ili basi na sisi tufaidi matunda haya ya uhuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kwankocho – Kivinje. Barabara hii ni ya urefu wa kilometra tano na ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Barabara hii inaunganisha barabara inayokwenda Kilwa Masoko na Hospitali ya Wilaya ya Kinyonga pamoja na Mji wa kitalii wa Kilwa Kivinje. Barabara hii imeahidiwa lakini mpaka sasa hakuna chochote kilichofanyika. Niombi Serikali iijenge barabara hii kwa kiwango cha lami ili basi tupate urahisi wa kwenda katika hospitali ile ya Wilaya ya Kilwa Kivinje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Njianne – Kipatimu. Barabara hii inahudumiwa na wenzetu wa TANROADS lakini inapita katika miinuko ya milima na kuna milima ambayo kama itatengenezwa katika kiwango cha changarawe basi tutaendelea kupata matatizo tu. Niishauri Serikali milima ile kwa mfano Milima ya Ndundu pale Namayuni, Ngoge, Kinywanyu pamoja na na Mlima wa Karapinda pale darajani basi ingewekwa katika kiwango cha lami ili kuhakikisha kwamba barabara ile inapitika kwa wakati wote. (*Makof*)

Lakini isitoshe, nikumbushe pia, Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete katika sherehe za kumbukumbu ya Vita ya Majimaji mwaka 2010 kule Nandete aliahidi kujenga barabara kutoka Nandete mpaka Nyamwage, ahadi ile imeota mbawa sijui kama utekelezaji wake unakwenda vipi. Niikumbushe Wizara, Mheshimiwa Rais aliahidi na ningependa kuona utekelezaji wake unafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo yanayotoka kwamba Mkoa na Mkoa utaunganishwa kwa barabara ya lami, lakini sisi Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Morogoro

hatujaunganishwa kwa barabara. Niishauri Serikali ione uwezekano sasa wa kujenga barabara kutoka Mkoa wa Lindi kwenda Mkoa wa Morogoro, na hii pengine inatengeneza uwezekano mwingine wa kwenda katika Mikoa ya Kusini, isiwe lazima ukitokea Dodoma uende Dar es Salaam, ufile Rufiji, uende Kilwa kwenda Kusini basi ukifika Morogoro uingie Liwale - Nachingwea uende Kusini. Naomba ombi hili lishughulikiwe kwa sababu na sisi watu wa Lindi tuna haki ya kuunganishwa na wenzetu wa Morogoro ili basi kuleta ustawi wa watu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie sasa suala zima la ukarabati wa uwanja wa ndege wa Kilwa Masoko. Kwenye bajeti ya mwaka jana tulichangia bajeti lakini hakuna chochote kilichofanyika. Niishauri Serikali iufanyie ukarabati uwanja wa ndege wa Kilwa Masoko kwa sababu ni muhimu sana kwa shughuli za utalii, kama ambavyo mnafahamu Mji wa Kilwa ni mji wa kitalii, ni mji wa kale, watalii wengi wanakuja lakini hatuna uwanja wa uhakika wa ndege, kwa hiyo Serikali ishughulikie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la upanuzi wa Bandari ya Kilwa Masoko. Kilwa Masoko tuna bandari ya asili, lakini mpaka sasa ile bandari hajifanyiwa chochote. Niishauri Serikali ione uwezekano wa kupanua bandari ya Kilwa Masoko ili basi meli kubwa ziweze kutia nanga pale na sisi watu wa mikoa ya Kusini au watu wa Kilwa mazao yetu basi yauziwe pale pale Kilwa, maana Meli kubwa zikija hatutakuwa na sababu ya kupeleka mazao Dar es Salaam. Tunalima korosho, tunalima ufuta, bandari ya Kilwa ikifanya kazi basi mazao yale tunaweza tukayauzia Kilwa na hivyo kupandisha bei ya mazao ya wakulima

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa masikitiko makubwa nzungumzie suala zima la *stand* ya mabasi kwa Mikoa ya Kusini. Mikoa ya Kusini kwa jiografia yake, barabara inayosafirisha abiria kutoka Dar es Salaam kwenda Mikoa ya Kusini inatokea maeneo ya Mbagala Rangi tatu, lakini mpaka sasa hatuna *stand* inayoleweka ya mabasi kutoka Mikoa ya Kusini. Tunapata shida kubwa maana *stand* zinazotumika

pale Mbagala Rangi tatu ni stendi za watu binafsi, na kwa sasa kuna ubaguzi mkubwa unafanyika kwa magari yanayotokea Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelazimishwa kwa magari yanayotokea Kilwa tuka-park uchochoroni huko ambako zina-park daladala hali ya kwamba Kilwa ni mkoa wa Lindi na kuna mabasi mengine ya Mkoa wa Lindi yana-park katika *stand* ambayo iko barabarani sasa tunashindwa kuelewa ni kwa nini watu wa Kilwa tutengwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nichukue nafasi hii pia kuishauri Serikali ijenge *stand* kwa ajili ya mabasi ya mikoa ya Kusini; kwa sababu kwa jiografia ya Jini la Dar es Salaam haiwezekani mtu anayetoka Mtwara, Kilwa au Lindi kwenda Ubungo, haiwezekani. Kwa hiyo Serikali ifikirie kujenga hiyo stendi ili kuondoa adha hii kwa wananchi wa mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru, ahsante.
(Makofî)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Cecil Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Wizara ambayo iko mbele yetu sasa hivi. Kabla sijaenda mbali sana nilitaka niongee mambo mawili kimsingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa ni kuishauri Wizara ya Miundombinu kwamba waangalie ni namna gani wanaweza wakawashauri wahusika wa bandari, kwa sababu ninafahamu Kisheria, watu wa bandarini wanaruhusiwa kuuza mali mbalimbali zilizoko bandarini ambazo wahusika wameshindwa kulipia ushuru ikiwemo pamoja na magari na vitu vingine. Bahati mbaya kabisa kuna wananchi Watanznaia zaidi ya 2,000 ambao wamenunua magari kwa njia za mnada bandarini lakini bado wanalazimishwa kulipa *port charges* pamoja na *other*

charges za bandari. Sasa Watanzania wanatamani kutaka kufahamu kwamba kimsingi unaponunua chombo chochote kama gari bandarini kupitia kwenye mnada unalazimika kulipia tena na *other charges*? Kwa nini wanaruhusu kufanya mnada kama bado mtu haambiwi hali halisi au gharama halisi za ununuzi wa vyombo vile ambavyo wananchi wameshindwa kuvilipia bandarini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili nililotaka nichangie ni kuhusiana na suala la barabara. Sisi wakazi wa Mtwara kwa kipindi kirefu kama wengi mnavyofahamu katika hata Mabunge yaliyopita walitokea wazee wetu ambao walikuwa Wabunge wa Mtwara, walikuwa wanatamani upande wa Mtwara uunganishwe na upande wa Mozambique kwa sababu ya shida kubwa ya barabara ambazo tulikuwa tunazipata. Miaka ya karibuni Serikali imeamua kujenga barabara na ndiyo sasa hivi tunaweza kufika Mtwara kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado tuna tatizo moja kubwa sana. Tunapoongelea suala la uchumi wa Mtwara tunaongelea kuhusu *ring roads* za barabara zetu ambazo zinaunganisha mkoa wa Mtwara pamoja na Lindi. Ukienda kwenye Kitabu cha Mheshimiwa Waziri, taarifa aliyotoa hapa ukurasa wa 165, utakuta hapa anaongea kuhusu barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay. Sina uhakika kama yamefanyika makosa kwenye *ku-record* lakini pesa inayooonekana imetengwa hapa wanaongea habari za shilingi 64,514,000.144. Sasa labda kama ni bilioni basi mje kutuambia; lakini hata kama mtasema ni bilioni, hizo barabara tunazoziongelea kwa kutumia hiyo bilioni 64, tunaanza kuongea kuanzia barabara ya Masasi - Songea kuelekea Mbamba Bay. Lakini pia barabara hii inajumuisha pamoja na kulipa gharama mbalimbali za wakandarasi waliofanya kazi kwenye barabara ya Masasi kuelekea Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kilometra 70 za Mangaka – Nakapanya ziko ndani ya hii shilingi bilioni 64 kama si milioni. Kuna kilometra nyingine 66 ziko ndani ya hii

shilingi bilioni 64, kuna kilometra nyingine 65 Mangaka – Mtambaswala ziko ndani ya hizo hizo pesa; kuna kilometra zingine 59 Tunduru na Matemanga zinaongea kuhusu hizo shilingi bilioni 64. Kuna kilometra 60 za Kilimasera – Matemanga. Mwisho kabisa wanasema, barabara za Masasi – Newala (Mtwara), sehemu ya Mtwara – Navira kilometra 50 na kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay kilometra 66, Masasi – Nachingwea – Nanganga kilometra 91.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko kabisa ninataka kusema bado tunarudi na lile lile wazo letu la zamani kwamba kama Serikali haina mapenzi mema na watu wa Kusini mtupe hii taarifa tuamue kujitenga wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ngombale ametoka kuchangia hapa karibuni, mmesikia kuhusu matatizo makubwa ya barabara inayoanzia Nangurukuru kuelekea Liwale. Watu hawa hawa wa Liwale wanatumia masaa sita kutokea Nachingwea mjini kuelekea Liwale kipindi hiki ambacho hakuna mvua, lakini wakati wa mvua wanakwenda kwa masaa tisa mpaka 12 umbali wa kilometra 95 Nachingwea – Liwale. Sijui katika hii mika zaidi ya 50 ya uhuru mnataka kutuambia nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule ndani unakuja kukuta bado kuna shida. Sasa hivi Serikali imeamua kuhamisha makao makuu ya nchi kuja kuyaweka Dodoma. Sisi wakazi wa Mikoa ya Kusini; Mtwara, Lindi pamoja na Ruvuma ili tuweze kufika Dodoma tunalazimika kupita tena Dar es Salaam. Tulikuwa tunakwenda Dar es Salaam kwa sababu ndiko ambako yalikuwa yanajulikana kama makao ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake alichokitoa hapa leo, sijaona kama Serikali ina mpango wowote wa kutaka kuunganisha mikoa ya Kusini kuititia Masasi, Nachingwea, Liwale hadi Morogoro kwa sababu ndio njia fupi sana ya kutuwezesha sisi kuweza kufika Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Waziri ni mtu anayetokea Jimbo la Namtumbo ambalo ni karibu tu na haya maeneo niliyoyataja, lakini ye ye akiwa bado Wizarani hajaona kama kuna namna au kuna haja kweli ya ndugu zake wa Namtumbo kuhakikisha anawapitisha njia fupi ya kufika Dodoma pamoja na Wabunge wote na watu wote wanaotakiwa kufika Dodoma kwa wakati. (*Makof*)

Kwa hiyo, niiombe Serikali ifikirie sasa ione namna ya kuunganisha Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Ruvuma kutokea Masasi, Nachingwea kuititia Liwale mpaka kufika Mahenge – Morogoro na kutoka Mahenge kuja Ifakara na maeneo mengine ni njia fupi sana ya kuweza kutufikisha Dodoma badala ya kung'ang'ana na ile njia ya zamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pilii nakuja suala la reli. Mheshimiwa Naibu Spika kwa taarifa yako labda kama umesoma vizuri historia ya Tanzania, na nataka niwakumbushe pia na Waheshimiwa Mawaziri, mwaka 1949 ilizinduliwa reli ya kwanza ya Kusini, ilikuwa inatokea Mtwara inapita Mkwaya, Mnazi mmoja na vijiji vingi, Lukuledi kuelekea Nachingwea. Siku moja Mheshimiwa Nape hapa aliuliza na Serikali miaka miwili, mitatu iliyopita ilisema wana mpango wa kufufua reli ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hapa kuna *crisis*, kuna watu wengi ambaao walikuwa wanatamani kuwekeza kwenye reli ya katika ambayo sasa inakwenda kwenye *standard gauge*. Sasa niwaombe, watu wale ambaao wameshindwa kuwekeza kwenye reli ya katika tuwaombe waje kuwekeza kwenye reli hii ya Kusini ambayo inakwenda Mchuchuma, Liganga itapita Tunduru, itakwenda Songea itaweza sasa kuboresha na kuongeza mapato ya Taifa kwa ajili ya bandari ya Mtwara ambayo ni bandari inayozalisha gesi. (*Makof*)

Kwa hiyo tuwaombe Serikali jambo hili mlifikirie kwa ajili ya kuongeza uchumi lakini pia kurahisisha usafiri. Barabara zetu hizi ambazo tumezilalia kwa muda mrefu toka wakati wa uhuru mpaka miaka mitatu iliyopita zinakwenda

kuharibika kwa kupitisha magari yenyé uzito mkubwa tofauti na stahiki zake. Magari yanayobeba makaa kutoka Mchuchuma na maeneo mengine, magari yanayobeba makaa ya mawe ambayo yanatakiwa yalete Bandarini Mtwara. Kwa hiyo, tuiombe Serikali kwa namna ya kipekee watueleze; kama itashindikana basi tutaishia kutoa shilingi; wana mpango gani na reli ya Kusini, hilo tunataka tulifahamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni suala la ndege. Si maeneo mengi sana yanayotumia ndege katika maeneo yetu lakini wachache wanatamani kutumia ndege. Tumeona sasa Serikali hata kama walifanya nje ya bajeti ya kawaida kabisa lakini wameamua kuzileta ndege. Sasa hivi kwenda Mtwara, *one way ticket* ni shilingi 631,000 kutoka *Precision Air*. Ukiwahi kukata mapema utapata hiyo *ticket* kwa shillingi 410,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yanatokea maeneo mengi, tumeona Serikali sasa inataka kuleta ndege maeneo yale na wanatangaza kwamba itakuwa ni yenyé gharama nafuu; lakini tuwaombe ndege ile isiishie Mtwara Mjini. Watu wa Masasi wanatamani kutumia ndege, watu wa Ndanda wanatamani kutumia ndege ambazo ni kilometra 200, pamoja na watu wa Nachingwea. Maeneo yote haya yana viwanja vya ndege tena vikubwa vya siku nydingi.

Kiwanja cha Nachingwea kilikuwa kinatumika wakati wa vita za ukombozi Kusini mwa Afrika kila mtu anatambua, kiwanja cha Nachingwea pale kuna kambi kubwa ya jeshi ambao wanahitaji ndege kutua pale. Viwanja hivi sasa viboreshwe viweze ku-*accommodate* kwa ajili ya kutua ndege za Serikali ambazo tunaamini pamoja na kuwa *commercial* lakini nia yake hasa ni kutoa huduma kwa ajili ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuwaombe, kama hamna mpango, kwa sababu sijaona kwenye vitabu vyenu, wa kuboresha viwanja vya ndege vya Masasi na Nachingwea, watu wale wanaozunguka viwanja vile vya

ndege ni bora tukawaeleza ili waweze kuendelea na shughuli zao za kawaida za uchumi, kufuga pale Mbuzi na vitu vingine kwasababu nyumba zao zilichorwa "X" na lile eneo sasa hivi limekuwa vichaka, linafaa kabisa kuwa malisho ya mifugo. Kama mnapatia nafasi Mheshimiwa Waziri nikuombe twende pamoja ukalione hili, kimsingi niunge mkono hoja...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha.

MHE. CECIL D. MWAMBE: ...hoja ya upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hasna Mwilima, atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Suleiman Saddiq ajindae

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kusini naomba nichangie Wizara hii nyeti yenye masuala ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niipongeze Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa pamoja na Naibu wake, lakini pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara hii, kwa kweli kwa Jimbo langu mimi la Kigoma Kusini Wizara hii imetutendea mema mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kuzungumzia barabara ya Simbo – Kalya. Barabara hii ya Simbo – Kalya kwa muda mrefu sasa inatengenezwa kwa kiwango cha changarawe. Sasa tulikuwa tuna ombi, kwanini Wizara isifike sasa mahali ikaona namna gani inaweza ili ikafanya kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami ili kuondoa usumbufu wa kufanya *maintenance* ya mara kwa mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba pia nizungumzie kipande cha barabara kutoka Uvinza kwenda Malagarasi kilometra 51.1. Barabara hii ina muda mrefu sana, hawamalizii kile kiwango cha lami kinachokwenda kuunga mpaka Malagarasi. Nimeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri anazungumzia kwamba tunatarajia pesa za wafadhili kama mfuko wa Abudhabi na mifuko mingine. Sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri aone namna ya kutusaidia wananchi wa Uvinza kumalizia hizi kilometra 51.1, na ikizingatiwa kamba barabara hii ni barabara kubwa inayopita *Ma-semi trailer* yanayobeba mizigo ya kwenda Congo na kwenda Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie vile vile kipande cha kilometra 40 kinachotoka Chagu hadi Kazilambwa. Kipande hiki ni korofi sana wakati wa mvua, na tumekuwa tunaomba hapa, hata bajeti iliyopita nillimuomba sana Mheshimiwa Waziri aone ni jinsi gani wanaweza wakatafuta namna ya kumalizia hizi kilometra 40. Kwa hiyo ninaomba sana Mheshimiwa Waziri utusaidie wana Uvinza namna ya kutumalizia kipande hiki cha Chagu – Kazilambwa Wilaya ya Kaliua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie vile vile barabara ya kutoka Uvinza kwenda Mpanda ambayo tuna kilometra kama 60 zinazokwenda Mishamo. Sisi tunacho kijiji kinaitwa kijiji cha Ubanda. Wananchi wa kijiji cha Ubanda wanatoka kata ya Kalya hawawezi kusafiri kwa njia yoyote zaidi ya kutumia hii barabara ya Mpanda. Kwa hiyo, tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri aone namna ya kuangalia hizi barabara za vijjini, hali ya huko vijjini si nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba atumalizie hicho kipande cha kilometra 60, na ikiwezekana basi waweze kuanza ujenzi wa hizi kilometra 35 kama alivyotenga kwenye kitabu chake, kwenye taarifa yake hii ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie masuala ya uchukuzi. Jimbo langu nina vijiji kama 33 viko Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Nimeona kwenye kitabu cha

Mheshimiwa Waziri amezungumzia ujenzi wa gati tatu; gati ya Sibwesa, gati ya Lagosa na gati ya Kalya; na amesema kwamba gati ya Sibwesa na gati ya Lagosa ujenzi umekemilika kwa asilimia 50. Mheshimiwa Waziri mimi nikuombe sana, nimeshaomba sana hapa, nimeomba kwenye bajeti iliopita lakini nimeomba pia katika maswali ya nyongeza. Wananchi wa Ukanda huu wa Ziwa Tanganyika wanapata tabu mno. Usafiri wanaotumia ni meli ya Liemba, hatuna gati hata moja inayofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna gati ambayo ilitakiwa ijengwe, hiyo ya Kalya, Sibwesa, gati ya Mgambo, gati ya Lagosa na gati ya Kirando, hakuna iliokamilika hata moja tangu uhuru, miaka 56. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, nilikuwa napitia kwenye kitabu chako nimeona baadhi ya maeneo wana magati matatu, wana magati manne; nini tatizo kwenye Jimbo la Kigoma Kusini kutupa hata gati tatu zikamilike ili meli ya Liemba iweze kupata maeneo ya kuegesha na abiria wapate kutoka kwenye usumbufu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie Daraja la Ilagala. Tumekuwa tunapata shida sana na Daraja la Ilagala na Mheshimiwa Waziri umetuahidi kwamba Wizara yako inafanya mkakati wa kutujengea daraja la muda mfupi ili wananchi pamoa na magari waweze kuvuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mimi ni mkazi wa Kigamboni. Sambamba na daraja langu la Ilagala naomba pia nizungumzie Daraja la Nyerere – Kigamboni. Tuna kilometa 3.8 kutoka Tungi kwenda Kibada; hivi karibuni tumekwama pale siku tatu tunashindwa kufika kwenye daraja kwa sababu ya mvua nydingi zinazonyesha pale Kigamboni. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri, maadamu umezungumzia kwamba kuna pesa zimetengwa za kujenga hizi kilometa 3.8 kutoka Tungi kwenda Kibada tunaomba basi uweze kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitoe pongezi kwa Serikali kwa ujenzi wa meli mpya ambayo inatarajia kuanza hivi karibuni, ambayo itakuwa inabeba abiria pamoa

na mizigo kwenye Ziwa Tanganyika; natoa pongezi sana, lakini pia natoa pongezi kwa ukarabati wa meli ya Liemba ambapo wote tunajua hii meli ya Liemba kihistoria ni meli ya Wajerumani na nimeona kwamba Mheshimiwa Waziri anasema wanataraji kusaini mkataba hivi karibuni ili *maintenance* hiyo iweze kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba pia nitoe pongezi kwa Serikali kwa ununuzi wa ndege mbili. Wananchi wa Kigoma tulikuwa tunapata taabu sana na usafiri, lakini tangu Mheshimiwa Rais, amenunua hizo ndege mbili kwa kweli wananchi wa Kigoma tunamshukuru sana tena sana kwa kuturahisishia usafiri wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo naomba pia nzungumzie ujenzi au upanuzi wa uwanja wa ndege wa Kigoma. Mheshimiwa Waziri unakumbuka mwaka jana kulikuwa na mvutano wa wananchi wa Kibirizi na wananchi wa maeneo ya jirani ya uwanja wa ndege. Sasa tulikuwa tunaomba basi upanuzi uanze mara moja ili kuondoa ile kizungumkuti, kulikoni Serikali imelipa fidia wananchi lakini hakuna lolote linaloendelea la kupanua uwanja wa ndege wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nzungumzie reli. Kwa sababu ujenzi wa reli hii ya *standard gauge* inapita pia kwenye Jimbo langu kwa maana Uvinza kwenda Msongati, Mpanda mpaka Karema. Hizo kilometa 150 ambazo mpo katika hatua ya kufanya upembuzi yakinifu, Mheshimiwa Waziri mimi nipongeze sana kwa jitihada hizo. Lakini pia nipongeze jitihada za reli yetu ya katil ambayo inatoka Kaliua - Mpanda - Tabora - Kigoma kilometa 411; nipongeze pia kwani hiyo pia ni jitihada nzuri kwa sisi wananchi tunaotumia reli ya katil.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nzungumzie pia ujenzi wa.....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hasna Mwilima muda wako umemalizika.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA:...Wizara hii, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Ezekiel Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Saddiq, Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, mimi na sisi sote tulipo hapa ili tuweze kuwawakilisha wananchi wetu kama ambavyo Katiba inataka tufanye.

Pili, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuitikia maombi ya Watanzania. Mwaka 2014/2015 Watanzania tulikuwa tunaomba katika imani zetu mbalimbali. Tuliomba kwamba tupate Rais mwenye maamuzi, tuliomba kwamba tupate Rais mwenye vitendo, tuliomba kwamba tupate Rais mwadilifu na tuliomba kwamba tupate Rais ambaye kweli atakuwa ni mtetezi wa wanyonge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimeshiriki katika maombi kwa nyakati tofauti na ushahidi kina mama Jenista Mhagama, tumeshiriki nao tukimuomba Mwenyezi Mungu kwamba atupatie Rais ambaye atakuwa ni mtetezi wa wanyonge. Kinachotokea nchini kwetu dhahiri inaonyesha kwamba Rais John Pombe Magufuli wa Awamu ya Tano ni mwitikio wa maombi ya Watanzania. Ni Rais aliyetoka kwa Mungu na mimi ninaamini mtu ye yeyote akijaribu kumbeza atakuwa anabeza maamuzi ya Mungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa kujiamini na kwa uwazi kabisa na kwa dhati ya moyo wangu, kwa sababu yapo mambo mengi ambayo yamekuwa ni hadithi ya miaka mingi leo tunayaona yakitokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka miaka yote tulikuwa tukizungumzia kwa mfano sekta ya utalii ambayo mimi nimewahi kuhudumu, kwamba ili uweze kukuza uchumi wa nchi ni lazima uangalie miundombinu na hasa usafiri wa anga. Na ili kukuza utalii tukasema tunahitaji sana Shirika la Ndege la Tanzania liweze kufufuliwa. Kufufua kwa Shirika la Ndege la Tanzania kunamaanisha kwanza, tunatangaza nchi yetu, lakini pili, tunaongeza idadi ya wageni wanaotembelea nchi yetu, na jambo la tatu na muhimu zaidi, ili kunufaika na idadi ya wageni unaowapata ni lazima uangalie wageni hao wanatumia fedha zao kwenye maeneo yapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafiti zilizofanyika, asilimia zaidi ya 65 ya fedha anazotumia mtalii anayetoka nje anatumia kwenye usafiri hasa usafiri wa anga, usafiri wa nje na usafiri wa ndani na asilimia karibia 25 anaitumia kwa ajili ya *accommodation*. Kwa hiyo, ili Taifa liweze kunufaika na idadi kubwa ya watalii inaopata ni lazima tuboreshe na tufufue Shirika letu la Ndege. Kimekuwa kilio cha Watanzania, leo *ATCL* imefufuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashangaa kumsikia Mtanzania ambaye anajua maana ya kukuza uchumi, akibeba maamuzi hayo. Tumezungumzia sana kuhusu mawasiliano hasa ya reli, mimi wananchi wangu pale Isaka ilifika mahali wakawa wamekata tamaa, hotuba zote nilizokuwa ninawaeleza walikuwa wanaona kama ninawadanganya. Leo wameshuhudia uwekaji wa jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa reli ya katika *standard gauge*. Ni mambo ya kihistoria ambayo yalikuwa hayajawahi kutokeea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuitikia maombi yetu Watanzania kutuletea Rais ambaye alihitajika sana kwa wakati huu tulionao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme jambo lingine moja, hata nidhamu Serikalini sasa ipo na hata hapa Bungeni niliwahi kufika wakati fulani kule nyuma kipindi cha Bunge

kama hiki, watu ambao walikuwa hawana nia njema na nchi hii walikuwa wanajaa kwenye mahotelii, wanakutana na Wabunge kuweka mashinikizo ili Serikali iweze kufanya mambo ambayo wanayataka. Ilifika mahali Serikali ikawa inaundwa kutoka nje ya matakwa ya Serikali yenyewe. Linawekwa shinikizo mtu fulani afanyiwe hivi kwa sababu tu wameathirika na maamuzi yaliyofanywa na viongozi wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo uhuni huo haupo, Serikali ipo *stable* na Mawaziri wanafanya kazi kwa kujiamini. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa na msimamo na kutumia vyombo viliviyowekwa Kikatiba katika kumpa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa. Kwenye hotuba yake ya mwaka uliopita nilisema kwamba kwa kiasi kikubwa hakunifurahisha, lakini alinieleza kwamba Mheshimiwa Mbunge barabara yako ya kwenda Kahama kwenda Geita hatujaiwekea fedha wakati huu kwa sababu tuna madeni ya wakandarasi wa miradi inayoendelea. Ninakuhakikishia awamu ijayo ambayo ni bajeti hii barabara hiyo itakuwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimemsikiliza. Ukiangalia aya ya 257 ya hotuba yake bila kupepesa macho amesema barabara ya Kahama kwenda Geita itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Naompongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa maamuzi hayo, ni Waziri muungwana alichokisema ametenda, ninajua wapo wengine kwa namna moja ama nyingine wanaweza matarajio hayajafikiwa kwa wakati huu. Lakini niwaombe mbona mimi mwaka uliopita niliambiwa nitulie nikatulia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaombe sote kwa pamoja bajeti hii ni nzuri sana na niwaome katika upigaji kura wote tuunge mkono bajeti hii kwa sababu matarajio ya wananchi na maombi ya kwetu yamekuwemo. Naomba

kwa kumalizia, kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameonyesha usikivu, nimpungeze sana pia Katibu Mkuu *Engeneer* Nyamuhanga kwa sababu haya yamefanyika kwa ushauri ambao akimpa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuweka maombi ya nyongeza ambayo ninaamini kwa ushahidi huu tulionao sasa yatakelezwa. Kuna barabara ambayo ilikwisha kuwekwa kwenye llani kwa ajili ya kuanza kujenga ujenzi wa kiwango cha lami, barabara ya kutoka Kahama - Bulige - Mwakitolyo - Salawe hadi Mwanza. Kwenye kitabu hiki inaonyesha kuwa itafanyiwa *up grading* pamoja na *rehabilitation* ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sasa angalau kwenye bajeti ijayo, kama tulivyofanya mwaka huu, najua kwamba angalau *feasibility study* haitaweza kufanyika mwaka huu basi mwaka ujao iweze kufanyika *feasibility study*. Lakini pia kuna barabara nyingine inayotoka Kahama inaunganisha na Karume makao makuu ya Nyang'hwale kwenda hadi Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kwa upande wa Sengerema na Geita, wamekwisha kuanza kuifanya maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami. Kipande cha kutoka Kharumwa makao makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale kuja hadi Kahama hakiko kwenye mpango wowote wa Serikali kwa ajili ya kuweka kiwango cha lami. Nimuombe Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla angalau hii barabara na yenye we ili ikamilike kama ambavyo *ipo designed* iwe kwa kiwango cha lami kutoka *junction* ya Nyambula kupita Busangi kupita Nyang'holongo kwenda mpaka Kharumwa hadi Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema; Mheshimiwa Waziri alipomaliza hotuba yake mimi nilisimama. Pamoja kwamba mimi ni Mbunge wa kawaida lakini niliunga mkono hotuba tu kabla ya kufika kwenye hoja yenye we. Naomba nikuhakikishie nakuunga mkono Mheshimiwa Waziri, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100 na ninaomba

nikuhakikishie nitafanya kampeni ili bajeti hii ipite kwa sababu maombi yangu na maombi ya Waheshimiwa Wabunge tulio wengi umeyazingatia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi naomba niseme naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Suleiman Saddiq atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Christine Ishengoma ajiandae.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi pia niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, kwa kuwa nina mambo mengi ya kusema, naomba nitamke kabisa kwamba naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia bajeti hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza sana sana Mheshimiwa Rais wetu. Mheshimiwa Rais amethubutu na ameweza kufanya mambo makubwa na mazito katika sekta ya barabara, anga, reli na bandari. Mheshimiwa Rais amefanya mambo mengi sana kwenye sekta hiyo na ameendelea kufanya mambo mengi katika maeneo mbalimbali na katika Jimbo langu la Mvomero kulikuwa na barabara ya lami ambayo ilikuwa imesimama kwa miaka mitano.

Mheshimia Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipokuja mwaka 2015 kuomba kura kama mgombea, alitamka iwapo atachaguliwa kuwa Rais, barabara ile itawekwa lami. Na kweli ujenzi umeanza mwaka 2016 lami ile imeshakamilika kwa kilometra 40 bado kilometra nane zimebaki, tuna mategemeo mwezi wa nane wa tisa itakuwa imekamilika. Kwa mazuri yote haya anayofanya Mheshimiwa Rais ndani ya nchi yetu na ndani ya Wilaya ya Mvomero, Mheshimiwa

Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimpigie *salute* Mheshimiwa Rais. Nampigia *salute* ya heshima, nampigia *salute* ya upendo, Mwenyezi Mungu ampe imani zaidi, ampe afya njema aendelee kuliongoza Taifa letu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer Mfugale*, *Engineer* wa *TANROADS* Mkoa Morogoro Mama yetu *Engineer Mtenga*, kwa kazi kubwa wanayofanya katika kusimamia masuala yote ya barabara katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na reli. Serikali yetu sasa hivi ina mpango wa kujenga reli na mpango ule umeanza na reli ile itakuwa reli ya kisasa, reli ya kasi ambayo tayari imezinduliwa kwa awamu ya Morogoro - Dar es Salaam - Morogoro. Nimuombe Mheshimiwa Waziri, niwaombe na wataalam, reli ile inapoanza kazi kuja Morogoro na kwenda mikoa mingine, kwa kuwa itakuwa ni reli ya kasi, abiria wengi watapanda, ile miundombinu iliopo leo katika miji ya Morogoro na miji mingine haitoshelezi mahitaji ya kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wewe na wataalamu wako, jaribuni kubuni mkakati wa kuweka miundombinu mingine, tuseme mfano reli imepakia abiria 1000, abiria 1000 wanaoshuka katika reli ile katika kituo cha leo cha Morogoro kutakuwa na msongamano mkubwa, magari yatakuwa mengi kuwapeleka wale vituo vya mabasi na maeneo mengine. Jaribuni kujenga vituo vipya vitakavyokidhi mahitaji ya reli ya kisasa. Huo ni ushauri wangu kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi kwenye barabara ya lami inayojengwa kutoka Magole - Turiani - Mziha - Handeni. Barabara hii lengo lake kubwa ni kufungua milango ya uchumi kutoka Tanga - Mombasa - Arusha - Kilimanjaro na maeneo mengine. Na kwa lugha njema barabara hii ndiyo barabara mbadala kwa barabara ya Chalinze - Segera. Lolote litakalokea kwenye Daraja la Wami, ujue barabara

mbadala ni barabara hii ya Turiani - Mziha - Handeni. Kipande cha Magole - Turiani kinakaribia kukamilika, kipande cha kutoka Turiani - Mziha - Handeni, Mheshimiwa Waziri nikuombe mkandarasi yuko *site*, ana mitambo ya kisasa, ana uwezo mkubwa, na wewe kutambua uwezo wake na wataalam wako mkandarasi yule umempa kujenga *interchange* ile ya Ubungo. Mkandarasi huyu ndio anajenga pale Ubungo ambae leo anajenga lami Turiani, kwa sababu ana uwezo ana vifaa ana mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri, *Engineer Mfugale* na wengine wote wa *TANROADS*, kazi yake mmeionna, hebu muachieni amalize kile kipande kilichobaki, Serikali itaokoa mamilioni ya fedha. Hakuna *mobilization*, hakuna chochote zaidi ya yule kupewa kazi na kuendelea na barabara. Na barabara ile ndiyo itakuwa barabara mbadala kwa baadaye. Lakini leo Tanga tunajenga bomba la mafuta toka Uganda kuja Tanga, wenzetu wa Uganda watasafirisha mafuta yao kuititia kwenye meli. Tanzania tukinunua mafuta yale tutayasafirisha aidha kwa reli au kwa barabara. Barabara ya Segera - Chalinze ina msongamano. Mheshimiwa Waziri elekeza nguvu Handeni - Mziha - Turiani kuitia Dumila. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo naomba niseme suala la barabara za Halmashauri za Wilaya ya Mvomero ambazo tumeziomba zipandishwe daraja na ninaomba niseme kwamba taarifa nilizonazo kila Mkoa kuna barabara zimepandishwa daraja. Barabara iliyopandishwa daraja ya Mvomero kutoka Langali - Nyandila kwenda Kikeo, naomba sasa barabara ile itengewe fedha mwaka huu. Tusingubiri kwa sababu imepanda daraja mwaka huu isubiri bajeti ya mwakani. Na kila mkoa wamepata barabara, kila mkoa kuna barabara zimepanda daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mikoa yote na Wilaya zote fedha zianze mwaka huu. Kwa sababu tunakiu ya barabara hizi zipande daraja naomba fedha hizi sasa zitolewe mwaka huu na barabara zile zianze kazi mara moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, Meneja wa *TANROADS* Morogoro aliandika barua kwa Wizara yako kukumbushia ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipofanya ziara Mvomero katika tTarafa ya Mgeta, kwamba barabara ya kutoka Chuo Kikuu Mzumbe kwenda Mgeta itawekwa lami. Mheshimiwa Waziri, nakuomba wewe na timu yako tukumbukane katika ahadi ile ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye mawasiliano. Mheshimiwa Waziri wewe ni shahidi, nimekuja kwako mara nyngi, Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi tumezungumzia minara kwa ajili ya Mvomero. *Halotel* wamefanya kazi nzuri, wamejenga minara katika baadhi ya maeneo, lakini maeneo yafuatayo bado tuna upungufu wa minara. Maeneo ya kata za Pemba, Kinda, Mascut, Homboza pamoja na kata ya Kikeo pale Mgeta.

Mheshimiwa Waziri nakuomba sana waelekeze wenzetu wa *Halotel* na mitando mingine waweze kutukamilishia ahadi ya mitando hii ili wananchi waweze kufanya biashara zao, waweze kupata huduma mbalimbali kuititia simu za mkononi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho. Nimeona kuna bajeti imetengwa kwa ajili ya barabara ya Msamvu – Bigwa. Unapozungumza Msamvu – Bigwa unazungumzia Manispaa ya Morogoro, unazungumzia barabara ya Morogoro Mjini. barabara ya Morogoro Mjini sasa hivi ina msongamano mkubwa wa magari.

Nawaomba sana wenzetu wataalamu, barabara ile wachore ramani ya *two way*, kwa sababu ya reli inayokuja na kituo kile kilichopo barabara ile ina msongamano mkubwa. Fedha zilizotengwa wataalamu waelekeze kutoka Msamvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Ahmed Shabiby atafuatiwa na Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Hongoli Joram ajiandae.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake katika Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili ni kuhusu barabara zangu za jimbo la Gairo ambayo ni ahadi ya aliyekuwa Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ambayo alitoa tarehe 26 Juni, 2014 tarehe 26. Kwanza ni shukuru, maana usiposhukuru na kidogo basi ujue wewe shukrani huna tu hata ukienda mbinguni huko ni hivyo. Ukiangalia hata kwenye *youtube* ukiandika tu Magufuli Gairo au Magufuli aitwa jembe Gairo utaona hotuba yake inakuja pale. Alitoa ahadi ya barabara ya kutoka Gairo kwenda Chakwale kwenda Kilindi kwa kiwango cha lami. Alitoa ahadi ya kuweka Mji wa Gairo kilometa 5 za lami Gairo Mjini. Alitoa ahadi ya Gairo - Nongwe kilometa 76 kuchukuliwa au kukasimiwa na *TANROADS*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema hivyo kwanza na mpongeza Mheshimiwa Rais, na ninamshukuru Mheshimiwa Rais na ninamshukuru Waziri wa ujenzi kwamba; nikiangalia katika hotuba ya kitabu cha Waziri wa Ujenzi ukurasa wa 339 naiona barabara ya Nongwe imetengewa zaidi ya milioni 900 na kwa bahati nzuri mkandarasi wa kuweka lami Gairo Mjini tayari yupo kazini pale na anaendelea kazi ya kuweka zile kilometa tatu za lami.

Nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri, kwamba katika ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kilomita 5 zimebakia kilometa mbili, na wakati Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi anatupa ahadi ya unjezi wa kilometa tano alikuwa anaelewa matatizo yaliyopo pale. Kwa hiyo, tumepewa kilometa tatu lakini tunaomba hizi kilometa mbili zimaliziwe haraka, kwa sababu mwaka huu sijazona kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ukiacha hizi kilometra tatu peke yake ni sawa sawa na mtu kumvalisha koti la suti halafu chini umemvalisha kaptula. Kwa hiyo naomba tumalize hizi kilometra mbili. Vilevile nikiangalia ile barabara ya kutoka Gairo kwenda Kilindi kwa ndugu yangu Kigua, ambayo ingesaidia hata watu wanaotoka Iringa kupitia Dodoma, Zambia wapi kwenda bandari ya Tanga kwa sababu pale ni karibu sana kutoka Gairo mpaka Kilindi ni kilometra 100 tu nayo haimo kwenye bajeti. Kwa hiyo na washauri na najua hii Wizara ni sikivu mtaweka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha zaidi ambacho nilitaka kukiongea kwa leo ni kuhusu habari ya mashirika ya umma. Watu wengi wamepongeza sana mashirika yote ya umma ambayo yako chini ya Wizara hii ya Ujenzi. Wizara hii ya Ujenzi ni moyo wa nchi, Wizara hii ina taasisi 37, na moja ya hizo Taasisi kubwa nizitaje chache kuna *TTCL*, Posta, Bandari, *ATC*, *TRA*, hizo nikutajie tano ambazo zote ni kubwa kabisa. Nataka niseme kwamba namshukuru Mheshimiwa Rais, nimpongeze pamoja na Mheshimiwa Wazari na Mheshimiwa Naibu Waziri na Makatibu wa Wizara hii wote kwa kupata Bodi ambazo zinaongozwa na watu ambao wana weledi, wajumbe wenye weledi na ma-*CEO*. Ukichukua taasisi zote nilizozitaja ma-*CEO* *n/vijana* na ni wazuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu uko wapi? Haya mashirika ambayo yako kwenye hii Wizara ukiangalia sana ya natakiwa yaendee kibiashara. Shirika la Reli lazima liende kibiashara, *TTCL* lazima iende kibiashara, *ATCL* lazima iende kibiashara, Posta lazima iende kibiashara, bandari lazima iende kibiashara hata Mheshimiwa Rais wakati ananua ndege alijua kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika hakuna watu wanafiki kama baadhi ya sisi Wabunge. Miaka ya juma tunapiga kelele tunafananishwa na Rwanda. Rwanda wana ndege sisi hata kimoja hichi kibovu bovu, leo ndege zimekuja mnaanza kusema ndege sio kipaumbele cha kwanza. Mimi nasema vyote ni vipaumbele, lakini viongozwe kwa mujibu wa sheria za kibiashara, hicho ndio cha msingi. Kwa mfano, unaunda

Bodi, zina madaktari, zina maprofesa zina wajumbe safi halafu baadaye tena hapo hapo yanatoka maagizo, matamko kutoka huku ya naingilia kwenye ile Bodi. Sasa kuna faida gani ya kuweka Bodi mpya? Acheni watu wafanye kwa kutumia utaalamu wao. Kama mmeweka Bodi basi acheni Bodi pamoja na ma-CEO wao na Menejimenti zifanye kazi yake; lakini kutakuwa na faida gani ya kuweka bodi mpya halafu mnaziingilia ingilia? Hii ni biashara jamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni wapeni mfano mmoja hili shirika letu la *TTCL*; hili ni shirika ambalo lingekuwa linachangia uchumi wa Taifa. Tuchukue mfano wa shirika la simu la Ethopia, kwa mwaka wanatengeneza dola bilioni 3.3, ukitoa kodi wanabaki na dola bilioni 1.5. Kwenye mfuko wa Serikali wanachangia karibu dola milioni 300, hiyo ni sawa sawa na bilioni zaidi ya 700 za Tanzania. Sasa haya sio tunawategemea *TRA* lazima tuwe na mashirika ambayo yataingiza hela kwenye Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia uwekezaji wa *TTCL*, ili ifike Tanzania nzima itachukua zaidi ya miaka, na ikimaliza kufika huko vijijini na sehemu nydingine hawa Vodacom na kampuni zingine kama Tigo, watakuwa tayari wana mitandao mipyä. Wakati huko huko Serikali tena ina asilimia 40 kwenye Shirika la Airtel, kama Wabunge hawafahamu. Asilimia 40 ya Airtel ni hela ya Serikali ya Tanzania, lakini toka hizo asilimia 40 ziwekwe kwenye Airtel kila siku Airtel wanapata hasara hawaleti faida hata shilingi moja kwenye Serikali. Sasa kwa nini hizo hisa za kwo 60 zilizobakia tusizinunue ziwe za Serikali (*TTCL*) halafu tutakuwa tayari tumeshajigawanya, tumeshachukua mitambo ya Airtel tunakuwa tayari tuko Tanzania nzima na tunaingia kwenye *competintion*? Kuliko kuacha asilimia 40 wakati ilie asilimia 40 kila siku hawapati faida. Kwa hiyo, hela ya Serikali imekaa tu Airtel. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye shirika la ndege; uwekezaji wa ndege si mchezo. Ukiwa bilionea ukitaka kuwa milionea ingia kwenye biashara ya ndege. Inataka lazima muwe na mtaji na lazima uweke mtaji.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MBUNGE FULANI: Umemaliza muda wako.

AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, ila hilo shirika linatakiwa lipewe hela lijiendeshe, *TTCL*.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, ajiandae.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii, ya kuongea katika Bunge lako Tukufu. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu aliyeiwezesha kuongea sasa hivi katika Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefanya mambo mengi, mengi kweli. Katika kazi zake muda wake wote huu, ameweza kujenga barabara za lami mahali pote na kwenye majimbo yetu yote na hakuna mtu ye yote anayeuliza mwongozo, hayupo kwenye majimbo yote. Mheshimiwa Rais ameweza kuweka jiwe la msingi la reli na hiyo reli watu wote wataipanda, hakuna mtu atakayeuliza taarifa. Mheshimiwa Rais ameweza kununua ndege ambazo kila mmoja anazipanda, hakuna mtu anayesema mwongozo au taarifa. Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imefanya mambo mengi sana. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo mambo mazuri yanafanyika ni afadhali uponzeze kuliko kubeza kila kitu. Huko Dar es Salam kuna mabasi ya mwendo kasi, kila mmoja anaingia hakuna mtu anayeuliza mwongozo au taarifa au swali la nyongeza, hakuna, kila mmoja anaingia. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais wetu ni kweli anafanya kazi nzuri, ameibadilisha Tanzania kwa muda mfupi, barabara hizi tulikuwa tunaziona Ulaya, *flyover* zinajengwa aaah, tTunamuombea maisha marefu. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuongelea daraja la mto Kilombero. Wananchi wa Morogoro tunapongeza sana, tuliteseka sana kwa kusafiri kwa kivuko kwenye mto wa Kilombero, kiasi kwamba wengine walipata matatizo. Imekuwa ukombozi kwetu sisi kuona daraja limekamilika. Daraja hili ni kiungo cha Wilaya za Kilombero, Ulanga na Wilaya ya Malinyi. Enzi za kivuko kilikuwa kinafanya kazi kwa saa 12 tu. Kwa hiyo, ukiwa na mgonjwa baada ya saa 12 na ikishindikana kutibiwa kwenye hospitali za Malinyi na Ulanga huyo mgonjwa wako anaweza akafa. Sasa hivi kwa kupata daraja hili mgonjwa anasafirishwa na anakwenda Kilombero kwenye Hospitali ya *St. Francis* ambayo ndio hospitali kubwa na hasa akina mama wajawazito, na kwa kuwa akina mama wengi wanajifungua usiku, kwa hiyo kuwepo daraja letu la Mto Kilombero kwa kweli ni fahari na imerahisisha usafiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongeza tena hapo hapo, wakulima wengi kwa pande zote mbili, upande wa Kilombero/Ifakara na upande wa Ulanga/Minepa na Lupilo; wa Ifakara wanalima mpunga Lupilo na Minepa. Sasa wanawake ndio wanaolima, unaju asilimia 70 ya wanawake ndio wanalima chakula hasa. Kwa hiyo ni ukombozi wa usafirishaji wa vyakula na kwa mwanamke hasa wa mkoa wa Morogoro na mikoa mingine. Kwa sababu Ulanga kuna madini hata watu wengine watatumia daraja hilo la Mto wa Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba niongelee reli ya kati, ambapo kilometra 200 tayari Mheshimiwa Rais ameshaweka jiwe la msingi na mkataba umeshasainiwa. Na hiyo reli inaanzia Dar es Saalam kuja Morogoro, wana Morogoro tusime nini? Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu huu ni usafiri mbadala wa barabara, saa moja tu kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro. Naona hata magari yetu tutayaacha tutaanza kusafiri kwa reli. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mkoa wetu wa Morogoro ni wakulima, wakulima wa mboga, wakulima wa matunda, wa nafaka na kweli watafaidika kwa kusafirisha mazao yao kwa kutumia hii reli. Wananchi wa

Morogoro tunampenda sana na tunaishukuru Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais kwa kujenga reli ambayo itatumwa na watu wote bila kuuliza swali la nyongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongelea kuhusu barabara za mkoa wa Morogoro, napenda sana kuongelea barabara ya Dumila mpaka Kilosa. Barabara ya Dumila mpaka Kilosa kilometra 63, kuna sehemu imejengwa kwa kiwango cha lami kutoka Dumila mpaka Ludewa. Kwa kweli barabara hii ilikuwa mbaya sana, sasa hivi unaweza ukatembea usiku na gari lako dogo (*saloon*) ukafika mpaka Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipande cha barabara cha kuanzia Ludewa mpaka Kilosa Mheshimiwa Waziri ambaye na mpongeza na Makatibu wake na Mheshimiwa Naibu Waziri mnafanya kazi nzuri; mmesema kuwa mkandarasi tayali anatafutwa kwa hiyo naomba hiki kipande cha barabara cha kuanzia Ludewa mpaka Kilosa kiweze kujengwa kwa muda muafaka. Kitu ambacho sikuona kwa muendelezo wa barabara hii ya Dumila mpaka Mikumi ni kuanzia Kilosa mpaka Mikumi wananchi wa jimbo la Mikumi wanauliza tutafanyaje mpaka na sisi tuweze kuendana na barabara hii kwa sababu ni wakulima wazuri.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa muda umekwisha.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na namshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nakishukuru sana Chama cha Mapinduzi na nasema naunga hoja asilimia mia moja, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Hongoli Joram atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, ajiandae.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa kupata fursa ya kuweza kuchangi kwenye Wizara hii ya Miundombinu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, kwa uamuzi wake wa kununua ndege sita. Ni jambo lisilo la kawaida kwa nchi kama ya kwetu ambayo tumekuwa hatuna ndege na akaamua kununua ndege sita, kwa hiyo na mpongeza sana kwa uamuzi wake huo, ambo ni mzuri sana ambao utatusababishia Watanzania tuweze kuwa na ndege za kutosha na hatimaye kuweza kuboresha uchumi wetu wa Tanzania kwa haraka zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa hotoba yake nzuri ambayo inaleta matumaini katika kuboresha miundombinu. Nimpongezi Naibu wake Waziri, niwapongeze pia watendaji wa Wizara hii ya Miundombinu kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa kuhakikisha kwamba miundombinu kwa maana ya barabara, reli na bandari na pia mawasiliano yana boreshwa kwa ajili ya kuimarisha na kuchochea uchumi wetu wa Tanzania; niwapongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwa pongeze wajumbe wa kamati ya miundombinu kwa kutuletea taarifa nzuri na kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kushirikiana na Wizara katika kuandaa mipango na kuishauri vizuri Wizara ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii, niwapongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze kwa sababu katika taarifa yao wameeleza vizuri sana kwamba kuna baadhi ya mikoa ambayo bado haijaunganishwa na mikoa ile ya Njombe na Morogoro, mikoa ya Mbeya na Njombe, mikoa ya Katavi na Kigoma, mikoa ya Kigoma na Kagera, lindi na Ruvuma na mikoa mingine. Ukiangalia hii mikoa ambayo wameitaja ambayo haijaunganishwa ni mikoa ya uzalishaji. Ni mikoa ambayo tunaitegemea sana hasa katika kuzalisha mazao ya chakula lakini pia kuzalisha mazao ya biashara. Pia ni mikoa ambayo ina mvua nyingi sana, maana

kwa kuwa ni mikoa yenyewe mvua nyingi lakini pia ndiyo mikoa inayozalisha chakula kwa hiyo barabara zake sio nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe katika mipango na nimeona mmeeleza na mmeiandaa vizuri sana; katika mikoa hii mmeanza kutekeleza kuhakisha kwamba inapata barabara nzuri, moja wapo ikiwa ni barabara ile ya Lupembe, barabara ambayo inasaidia sana katika kuhakikisha kwamba mazao ya biashara na mazao ya chakula kama nilivyosema yanasa firishwa. Kwa hiyo, niwashukuru kwa hilo, kwa kuhakikisha kuwa barabara yetu pia ya Lupembe inaendelea kuwekwa katika Bajeti na kuongezewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii mwaka wa jana tulilingiza kwenye bajeti tulitengea fedha na mwaka huu pia imetengewa fedha. Sasa naomba kujua, pengine Mheshimiwa Waziri utakaposimama utatueleza vizuri, je, zile fedha ambazo zilitengwa kwenye Bunge la Bajeti mwaka jana ambapo unaishia mwaka huu, na hizi fedha ambazo zimetengwa mwaka huu je, zitajumlishwa pamoja au zile za mwaka huu ambao unaisha zimeshapitwa na wakati au hazitatumika au hazitajumuishwa na tutegemee kupata tu fedha hizi za mwaka huu?

Kwa hiyo, nitaomba utakapo kuja kufanya majumuisho basi nipewe ufanuzi wa juu ya zile fedha ambazo tulikuwa tumetenga mwaka jana na hizi fedha shilingi bilioni mbili ambazo zimetengwa mwaka huu kama zitakuwa zitajumuishwa kwa pamoja na barabara ile ianze kufanyiwa utengenezaji au ujenzi wa kiwango cha lami. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kupongeza, kama tulivyosema nimeangalia kwenye taarifa pia mmeweza kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara nyingine, ile barabara ya kutoka llunda mpaka kuelekea Igongolo, ni barabara ambayo ni ya muhimu sana katika uzalishaji wa mazao, kwa maana ya uzalishaji wa wananchi wa maeneo yale. Kwa hiyo nipongeze sana kwa fedha zile ambazo zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe badala ya kuendelea kutenga fedha kwa kiwango cha kokoto ni vizuri tuanze kujielekeza kutenga fedha kidogo kidogo kuanza kutengeneza kidogo kidogo lami na hatimaye barabara nzima zitakuwa zimekamilika au tuanze kutengeneza zile sehemu ambazo tunafikiri kwamba ni korofi, sehemu ambazo wakati wa kifuku wananchi/wakulima wetu wadogo wadogo hawawezi kupitisha mazao yao yakafikia kwenye masoko basi angalau zianze kujengwa maeneo hayo kwa kiwango cha lami na hatimaye tutaweza kumaliza barabara nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisubiri tu fedha itakuwa ni ngumu lakini tukianza na hiso fedha ndogo ambazo tunatengenezea vifusi nya kokoto, tukaanza kutengeneza kiwango cha lami kwenye maeneo yale ambayo ni korofi na hatimaye barabara zote zitatengenezwa kirahisi zaidi na zitawenza kuitika wakati wote hata wakati ule wa mvua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie pia kwenye upande wa mawasiliano. Imeelezwa hapa kwamba maeneo mengi ya vijiji bado mawasiliano ni shida, bado hayafikiki mawasiliano na maeneo haya ya vijiji ndiyo maeneo ambayo tunayategemea, kama tulivyosema, kwenye uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula; kwa kuwa maeneo haya hayana mitandao ya simu au hayajengwa minara ya simu. Kwa mfano katika Jimbo langu la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, kuna kata tano hazina mawasiliano. Kuna kata za Ikondo, Ninga, Mfiliga, Idamba na Ukalawa hazina mawasiliano, kwa hiyo vijiji vyote nya maeneo hayo simu hazipatikani kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri maeneo hayo tuweze kujengewa minara ili wananchi wale waweze kupata mawasiliano kirahisi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nichangie juu ya suala mtambuka. Niwapongeze Wizara kwa uamuzi wa kuanzisha mafunzo maalum kwa wakandarasi wa kike, mafunzo hasa yanayohusika na ukarabati na matengenezo

ya barabara na uandaaji wa zabuni. Hii itasaidia akina Mama wengi kujunga na ukandarasi au kusoma masomo ya ukandarasi, masomo ya sayansi, lakini pia itawasaidia wanafunzi wetu wa shule za sekondari kuanza kupenda masomo ya sayansi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilivyo sasa hivi wanafikiri kwamba ukandarasi au uhandisi au *u-engineer* ni kwa ajili ya wanaume tu. Kwa hiyo tukiawesha hawa na wanapoenda huko kwenye maeneo haya ya ujenzi wa barabara wakiwaona basi watahamasika kusoma masomo ya sayansi na kuhakikisha kwamba wanafaulu vizuri, na tutakuwa na wanawake wengi ambao wanakuwa ni *Ma-engineer* na hatimaye kuwa na *ma-engineer* wa kutosha kuliko ilivyo sasa hivi, *ma-engineer* wengi ni wa kiume kuliko *ma-engineer* wa kike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine nichangie juu ya ajira hasa ajira za vibarua, wale ambao *they are not trained* kwenye maeneo huko ambako shughuli za ujenzi wa barabara zinaendelea. Niombe tuweke utaratibu wa kuwaangalia wale watu wanaowekwa kwenye maeneo ambako miradi hii inatengenezwa. Tukifanya hivi itasaidia kuwapa ajira vijana wa maeneo husika ambako barabara zinajengwa, lakini pia itawafanya hawa vijana wasiharibu miundombinu ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwengine vijana au watu wa maeneo yale wanaharibu kwa sababu wanaona kama ile barabara kwao hawajanufaika, wanapoona wajenzi wa barabara au wanaoshiriki kutoa *labour force* ya zile ambazo hazihitaji wasomi wanatumika watu wa kutoka maeneo ya mbali. Na kuna maeneo mengine wamekuwa wakiiba vifaa vya ujenzi au waki-vandalize vifaa vya ujenzi kwa sababu tu wao hawajashirikishwa katika ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukiwatumia vijana wa maeneo husika, maeneo ambako mradi unafanyika itawasaidia vijana wenyewe kuanza kupenda

shughuli zile na kuhakikisha kwamba wanakuwa walinzi wa vifaa na mali zilizoko katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa atafuatiwa na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa kama muda utakuwa bado unaruhusu Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria atamalizia.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote ninamshukuru sana Jehova kwa kunifanya hivi nilivyo. Mimi nitachangia katika maeneo mawili tu kwa leo, katika eneo la uchukuzi pamoja na ujenzi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijamtendea haki Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, jemedari wetu na mtumishi wa Mungu huyu Dkt. John Pombe Magufuli kwa mara ya kwanza kabisa katika historia ya Tanzania tumeweza kuwa na *flyovers* Dar es Salaam na tutakuwa nayo, lakini pia Serikali imeweza kujenga *standard gauge* kwa upande wa reli ya kati. Ninaamini sasa na reli yetu ya TAZARA itaangaliwa upya ili iweze kuboreshwa zaidi kutokana na umuhimu wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Ndege la Taifa (ATCL). Sasa hivi tumeweza kuwa na *national carrier* yetu, ni jambo jema na shirika hilli limefuliwa. Napenda kutia mkazo kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamesema kabisa kwamba mashirika haya ambayo yako chini ya Wizara hii, yaweze kupewa *full autonomy* ili *marketing teams* zao ziwe na ubunifu zaidi. Kana kwamba hiyo haitoshi wajaribu kuangalia ni jinsi gani wanaweza wakawa wabunifu kimkakati zaidi kujaribu kwenda katika nchi ambazo zitakuwa zinatuletea mapato mengi zaidi kwa kuongoza utalii wa nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niende kwetu sasa kule katika uwanja wa kimataifa wa Songwe pale Mbeya. Katika ukurasa wa 169 tumeona Serikali imetenga milioni 1,530 kumalizia jengo na mambo mengine, lakini mimi nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa ku-*wind up* atueleze suala zima la taa za uwanja huo wa ndege wa Songwe kutokana na umuhimu wake. Kuna ndege mara kwa mara zimeshindwa kutua, wewe mwenyewe ni shahidi kutokana na kwamba uwanja huo hauna taa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba pesa ya dharura iweze kutolewa ili uwanja wa ndege wa Songwe tuweze kupata taa wakati wowote wananchi waweze kufurahia huduma hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia naamini wote watasema na Mheshimiwa Waziri anaelewa pale kwamba siwezi kukaa chini bila kuzungumzia barabara ya *by-pass*, barabara ya mchepuko kutoka Uyole hadi uwanja wa ndege wa kimataifa wa Songwe, na jambo la kusikitisha sijaona hata kwenye kitaba cha taarifa ya Mheshimiwa Waziri hapa, sijaona *commitment* ya Serikali. Hili jambo ni kizungumkuti, nimekuwa nikilipigia kelele mpaka Waziri aliyeppita wa Ujenzi ambaye ni Rais wetu mpendwa sasa hivi, hili jambo analijua na alishatuhidi. Vilevile kana kwamba haitoshi mpaka kwenye vikao vyetu vya *Road Board* vya Mkoa tulishakubaliana kwa pamoja, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze hapa wana Mbeya tusikie, kwa sababu foleni msongamano kutokea Uyole mpaka Mafati pale barabara haipitiki kabisa, dakika 10 inachukuwa saa tatu. Mimi bila kusita Mheshimiwa Waziri kaka yangu ninaekupenda na kukuheshimu sana nitashika shilingi mpaka kieleweke, maana hili jambo sasa hatuelewii sisi Wana-Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barabara hii ya mchepuko madhara yake ni mengi, inaleta ajali, inaharibuu barabara. Vilevile itakapokuwa ina mchepuko sisi wana Mbeya kwetu ni faida kwa sababu tunaweza tukawa pia tuna bandari kavu. Ninayoyazungumzia ni haya malori

makubwa katika hii barabara ya mchepuko, sijazungumzia magari madogo; kwa hiyo Mheshimiwa Waziri anaelewa na alishakuja Mbeya na tumezungumza sana hili jambo lifike muafaka na lifike mwisho, maana mambo haya ya upembuzi yakinifu hata Mheshimiwa Rais hataki kuyasikia, tunataka utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabla sijakaa ni barabara ile ya Isonje – Mbeya Vijiji hadi Makete kuitia Kitulo, hii barabara inaunganisha mikoa miwili. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, kwa sababu kule kuna Hospitali ya *Mission* ya Ikonda ambayo inasaidia wananchi wengi sana, *actually* wananchi wote wa Mikoa ya Nyanda za juu Kusini.

Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba barabara ya kuunganisha mkoa wa Mbeya na mkoa wa Njombe kwa maana ya kwamba Makete kuitia Kitulo kwa ajili ya wananchi wetu hawa wanokweda kwa wingi kuhudumiwa pale Ikonda basi Mheshimiwa Waziri atuletee majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache ninaomba kuunga mkono hoja bajeti hii, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa naamini Mheshimiwa Waziri amelisikia hilo la taa, japokuwa alikuwa anazungumza kidogo hapo, naamini Naibu Waziri na Waziri mmelisikia hilo la taa uwanja wa kimataifa wa Songwe. (*Makofii*)

Tunaendelea Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa kama muda utaruhusu Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria atamalizia.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa utendaji huu mzuri uliotukuka, naomba tuwapongeze sana. Naomba nichukue fursa hii

kumpongeza sana kaka yangu Profesa Mbarawa pamoja na Naibu wake Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii, pamoja na watendaji wote wa Wizara yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze sasa katika mchango wangu, nitaanza na barabara ya kutoka Kinyarambo A - Salavanu – Saadani - Madibila – Rujewa. Barabara hii inaunganisha Wilaya mbili, barabara hii inaunganisha mikoa miwili na inaunganisha Wilaya ya Mufindi na Wilaya ya Rujewa, Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kama tulivyoahidiwa katika llani ya Uchaguzi wa mwaka 2000, kwamba itajengwa kiwango cha lami, 2005 itajengwa kwa kiwango cha lami, 2010 itajengwa kwa kiwango cha lami, na 2015 itajengwa kwa kiwango cha lami; lakini hizo ahadi zimekuwa hewa mpaka leo hakuna hata kilometra moja iliyojengwa kwa kiwango cha lami, katika barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ikijengwa itasaidia kwa kiwango kikubwa sana kukuza uchumi katika eneo hili na barabara hii ni *shortcut* ya barabara ya kutoka Mbeya itapunguza zaidi ya kilometra 60, hii ni manufaa makubwa sana katika uchumi huu. Kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atueleze sababu zipo zimepelekea barabara hii inaonekana kwenye llani ya Uchaguzi kwa vipindi vitano, lakini mpaka leo haijajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwa vigumu sana kurudi kwa wananchi wetu kuwaambia kwamba mpaka leo hii hatuna hoja za msingi kama watu wa CCM, watu wa Serikali, kwa nini vipindi vitano mfululizo mpaka leo haijajengwa? Naamini kabisa kaka yangu Profesa Mbarawa atakuja kuniambia maneno haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi ya pili ninayotaka kuzungumzia ni barabara ya kutoka Mtili – Ifwagi – Mdaburo – Ihanu – Isipii – Tazara – Mlimba. Barabara hii inaunganisha

Wilaya mbili, inaunganisha Wilaya ya Mufindi na Wilaya ya Kilombero, ina urefu wa kilometra 116, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi haina uwezo wa kujenga barabara hii.

Mheshimia Naibu Spika, katika vikao vyetu nya mwaka 2013, 2014 na 2015 tulipitisha katika Wakala wa Barabara wa Mkoa wa Iringa na Mheshimiwa Rais ambaye alikuwa Waziri wakati uliopita alikubali kupeleka wataalam kwa ajili ya kufanya utafiti kuona kama ina hadhi ya kupandishwa kuwa barabara ya *TANROADS*, lakini mpaka leo hii Mheshimiwa Waziri hawajaleta wataalam wa aina yoyote katika hili eneo. Namuomba sana kaka yangu atakapo kuja atuambie ni lini atatuletea hao wataalam kwa ajili ya kuja kufanya upembuzi yakinifu na barabara hiyo iweze kupandishwa kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la barabara kutoka *Jets corner*- Kibao mpaka Mgololo, barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Mufindi na uchumi wa Mkoa wa Iringa kwa ujumla. Eneo hili lina viwanda vingi nya mbao pamoja na chai, lakini ni muda mrefu hakuna hata kilomita moja ya barabara ya lami iliyojengwa katika eneo hili, ukichukulia kuna makampuni ambayo yanalipa mabilioni ya pesa kwenye kodi ya Serikali katika nchi hii. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali itupie macho mawili eneo hili kusudi tuweze kupata barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la uwanja wa ndege wa Mkoa wa Iringa wa Nduli. Huu uwanja ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Iringa ukichukulia Iringa ni sehemu ambayo ina-base kubwa sana ya utalii. Kwenye eneo hili naomba niunganishe na barabara ya *Ruaha National Park*. *Ruaha National Park* ni mbuga ya pili kwa ukubwa katika Bara la Afrika, baada ya mbuga ya *Kruger* ya *South Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna haja ya kuukuza uchumi wa nchi hii katika eneo la *Ruaha National Park* kwa kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Kuna

watalii wengi sana wanapenda kutembelea katika maeneo haya, lakini tatizo kubwa linakuwa hatuna barabara ya lami na hakuna uhakika wa kuflikika kwenye hili eneo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama barabara hii itapata kiwango cha lami nina uhakika kabisa ile mbuga ya Kruger haina sifa ambazo *Ruaha National Park* inazo. *Automatically Ruaha National Park* inaweza kuwa mbuga ya namba one kwa ukubwa katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana kaka yangu Profesa Mbarawa kwa kufungua kituo cha reli pale Mpanga Tazara ambacho kilikuwa kimefungwa, sasa hivi kinafanya kazi. Ninachomuomba ndugu yangu wakifanyie ukarabati kile kituo cha reli pamoja na kukifanyia ukarabati kituo kidogo cha pale Kimbwe kusudi wananchi katika eneo hili waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa Sheria za Barabara zifanye kazi, kwa sababu uharibifu mwingu unatokana kwa sababu zile sheria watu hawaziangalii, watu wanaharibikiwa magari yao, wanaacha magogo matokeo yake barabara zinaendelea kuharibika; hata ile dhana bora ya kutaka tupate barabara nzuri katika nchi hii inakuwa haina maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye masuala ya mawasiliano, kuna maeneo matatu ni muhimu sana katika Jimbo langu ya Mufindi Kaskazini. Eneo la kwanza ni eneo la Ikwera, tayari mnara umeishajengwa, lakini kwa masikitiko makubwa huu mwezi wa sita sasa hivi ule mnara haufanyi kazi. Eneo la Mapanda mnara umeishajengwa lakini kwa masikitiko makubwa mpaka sasa hivi mnara haufanyi kazi. Eneo la Isipii mnara umeishajengwa lakini kwa masikitiko makubwa mpaka sasa hivi minara haifanyi kazi.

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba utakapokuja kuhitimisha bajeti yako, utuambie kwa nini mpaka leo minara hii haifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria.

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante umenipa nafasi Munguakuweke, nakupongeza sana. Naipongeza Kamati yangu ya Miundombinu, Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati yangu, kwa sababu tumetembea katika maeneo mbalimbali na nimefaidika, na sisi tumeona eneo lingine jipy. Vilevile Rais wangu Mheshimiwa John Pombe Magufuli amefanya kazi nzuri sana katika Tanzania yetu, Mungu amuweke maana yake ana mbinu ya Rais wetu Mheshimiwa Narendra Modi wa India, yaani Narendra Modi anafanya mambo yake na yeye anachukua mbinu hiyo hiyo, Mungu amsaidie. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wangu wa Miundombinu, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wake wanafanya kazi nzuri pamoja ofisi yake wanafanya kazi nzuri wanamsaidia sana, Mungu amuweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja katika mada yetu inayohusu Mkongo wa Taifa (*Data Centre*) yaani mitandao ya simu. Kamati yetu tumekwenda juzi kutembelea, nimeona mambo mazuri kabisa, yaani hiyo mitandao chini kwa chini (*underground*) imekuja kutoka India, *South Africa* na *Zambia* mpaka hapa Dar es Salaam, tumeona mitandao hiyo, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu Magufuli, amefanya mambo hayo, yaani nchi nyingine hakuna lakini hapa Tanzania ipo. Mitandao hiyo imegusa Dar es Salaam, Zanzibar lakini wale watu ambao ni washirika wa mtandao huo, Zantel, Airtel Tigo pamoja *TTCL* wamefanya mambo mazuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imetengeneza *database* ili hawa watu wa mitandao, wale wa Zantel na wengine wanunue hiyo *data* waje kutia katika mitandao yetu katika

database. Kampuni hizo waje watie katika biashara yetu katika database, yaani wao wasitumie yao watumie ya Tanzania, ili sisi tupate pesa. Mheshimiwa Magufuli amefanya mengi pamoja na Rais wetu wa zamani Mheshimiwa Jakaya Kikwete safi yaani wamefanya vitu vya kuleta baraka na Tanzania yetu tushinde. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja katika barabara, tumetembelea barabara nyingi sana na juzi tumetembelea barabara ambayo Mheshimiwa Rais amefanya kuwa barabara kubwa, ina watu wengi, amekatisha sasa, ameipeleka barabara hiyo mpaka Kiwanda cha Saruji cha Wazo pale. Halafu kutoka pale inakwenda moja moja mpaka bandari, inakwena uwanja wa ndege, amegawa sehemu mbalimbali, mjini pamoja na huko sehemu za Dar es Salaam. Barabara hiyo ina watu na magari mengi, kwa hivyo nampongeza Mheshimiwa Rais wangu Magufuli. Mimi naomba Rais wangu Mheshimiwa Magufuli asaidie kidogo barabara za Zanzibar. Uwezo wetu ni mdogo, lakini mimi naomba Mheshimiwa Rais wetu wa Muungano asaidie Zanzibar ili na sisi barabara zetu ziboreshwé.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja uwanja wa ndege. Kweli mimi nampongeza Mheshimiwa Rais amefanya maboresho mengi sana, ameleta ndege kubwa. Tunaona uwanja wa ndege wa Dar es Salaam umeboreshwa vizuri kabisa. Sisi tulikwenda kutembelea *Terminal B*, tumeona mambo mazuri, yaani watalii watakuja wengi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile naomba Serikali iboreshe uwanja wa ndege wa Zanzibar, sisi wote ni wa Muungano, ndugu mmoja hatuna ubaguzi, uwanja wetu wa Zanzibar na sisi tuboreshe kwa sababu *terminal* ipo na wanakuja watalii pesa zote zinaingia Tanzania tutaondosha umaskini wetu. Vilevile viwanja vya ndege vidogo vidogo Tabora, Mwanza, Moshi, Kilimanjaro jamani hivi viwanja vya ndege kama sisi wananchi tuvitumie tunaongeza mapato, tunaongeza vitu mbalimbali, tutaondosha umaskini, tunatafuta mapato tunaleta maendeleo. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umenipa nafasi nakushukuru sana Mungu akuweke. Tunakuja katika bandari na bandari yetu imeboreshwa na tumekwenda kutembea bandari ya Dar es Salaam, tunataka kupanua bandari, na kupanua kwake kwa sababu zitapita meli mbili pamoja. Mimi nampongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati, yaani mimi pia nimefaidika kwa kuingia ndani ya Bunge nafahamu nini maana ya Muungano na nini ni Serikali. Kumbe Serikali iko imara, na Marais wa awamu zote wamefanya kazi ya kuleta maendeleo katika nchi yetu kwa kuondoa umaskini wetu. Nampongeza na Mwenyezi Mungu aipe nchi yetu ya Tanzania ipate baraka na kila kheri. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari yetu ya Dar es Salaam tunapanua, lakini mimi ninaomba Serikali yetu vilevile, bandari ya Zanzibar tuko katika enzi yetu ya zamani, tunataka na sisi bandari yetu ya Zanzibar pia tuboreshe ili tupate kuweka makontena nydingi kuliko zile, ili pia watu mbalimbali waje. Vilevile mimi ninaiomba Serikali yangu, Waziri wangu, Rais wangu bandari ya Mwanza, Tabora, Bagamoyo, Tanga umenifahamu pale...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa. (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Muongezee! Mpe za kwangu!

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bhagwanji kwa maombi makali kabisa hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa siku yetu ya leo na shughuli zetu, lakini kabla sijaaihirisha Bunge, na kwa sababu tunaendelea na mijadala niwakumbushe

jambo moja, wakati mwagine Mbunge anachangia naamua Mbunge amalize hoja yake kama hakukutokea na Mbunge mwagine anayekuwa ameligundua jambo hilo.

Wiki iliyopita kuna mwananchi mahali fulani sitataja niliona kwenye taarifa ya habari akilizungumza hili, sasa na sisi tukilitilia mkazo humu ndani haliko sawa sawa kisheria na Kikatiba.

Kuna Mheshimiwa Mbunge amechangia, limeishawahi kuzungumzwa huko nyuma naweka tahadhari kwa sababu si jambo zuri kwamba sehemu ya nchi hii inaweza ikaamua kujiunga na nchi nyingine, hilo jambo haliko sawa sawa kikatiba na kisheria, kwa sababu ukisema hivyo maana yake unataka kujitenga na kwa hivyo unatangaza uasi ama kwa jina lingine utasema ni uhaini kwa sababu umesema kwa kinywa chako.

Sasa Waheshimiwa Wabunge tunapochangia tuangalie matumizi ya haya mambo hata kama tunayaona yanasisika vizuri, sisi wote hapa ni viongozi tusiwe sehemu ya kuutaarifu umma kwamba una uwezo wa kusema jambo kama hilo. Haliko sawa sawa kikatiba wala kisheria. (*Makof*)

Baada ya kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Ijumaa tarehe 28 Aprili, 2017 saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 28 Aprili, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*